

21 MEI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thelathini – Tarehe 21 Mei, 2013

(Mkutano Ulianiza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu tuendelee?

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):

Randama za Makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

21 MEI, 2013

MASWALI NA MAJIBU

Na. 243

Upotevu wa Fedha Kwenye Halmashauri Nchini

MHE. RAMADHAN HAJI SALEH aliuliza:-

Kumekuwa na upotevu wa fedha nyingi katika Halmashauri nyingi nchini, hali ambayo imesababisha miradi mingi isiweze kutekelezwa.

Je, Serikali, imechukua hatua gani dhidi ya Watendaji wanaobainika kuhusika na wizi huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa, kumekuwepo na matuimizi mabaya ya fedha katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Nchini. Katika kukabuliana na hali hiyo Serikali, imechukua hatua mbalimbali za kuboressha mfumo wa udhibiti wa fedha na kuwachukulia hatua watumishi wanaobainika kuhusika na ubadhirifu huo.

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa dhidi ya watumishi, zikiwemo kufikishwa katika vyombo vya dola, kuvuliwa madaraka, kushushiwa mishahara na kufukuzwa kazi. Kwa kipindi cha mwaka 2006 mpaka 2012 Wakurugenzi 24 walivuliwa madaraka, Wakurugenzi 24 mchakato wa hatua za nidhamu upo katika hatua mbalimbali, Mkurugenzi mmoja alishushiwa mshahara na Wakurugenzi 8 wamefikishwa Mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

21 MEI, 2013

Aidha, watumishi wengine 1,452 walichukuliwa hatua kutokana na kukiuka Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha Serikali, imefanya yafuatayo; kuanzisha Kanuni za Tozo za Adhabu ya Mwaka 2010, kubadili Muundo wa Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri ambapo sasa wanaripoti kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, kuanzishwa kwa Matumizi ya Viwango vya Kimataifa katika Uandaaji na Utunzaji wa Hesabu za Mwisho za Matumizi ya Mfumo Fungamanishi wa Usimamizi wa Fedha (*EP/COR*) ambao unakusudiwa kudhibiti matumizi ya fedha katika Halmashauri pamoja na kupunguza akaunti za Halmashauri kutoka 33 hadi 6. Aidha, msisitizo unatolewa hivi sasa na Serikali, katika ngazi ya ukaguzi, ambayo ni kuangalia thamani halisi ya fedha za Serikali, zinazotumika katika kutekeleza miradi mbalimbali katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ziomesaidia kuboresha matumizi ya fedha katika Halmashauri, kama ilivyodhihirishwa na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mwaka 2011/2012 ambapo Hati Safi zimeongezeka kutoka 72 za mwaka 2010/2011 kwa mwaka hadi 104,

Hati zisizoridhisha kupungua kutoka 5 za mwaka 2010/2011 hadi 0 na Hati Mbaya 1 katika Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kuendelea kushirikiana na Madiwani, kuhakikisha kuwa fedha na mali nyingine za umma katika Halmashauri zinatumiwa kama inavyopasa. Jukumu la kuhakikisha kuwa mifumo ya udhibiti iliypopo inafanya kazi ipasavyo, sio la Serikali peke yake, bali pia ni la wenye Halmashauri ambao ni wananchi wanaowakilishwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani. (*Makof*)

MHE. RAMADHAN HAJI SALEH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, adhabu ya baadhi ya watumishi hao imekuwa ni uhamisho. Je, Serikali, ni lini itatoa adhabu kali pamoja na kufilisiwa mali zao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua tulizochukua ni nyingi nimeeleza hapa, lakini hii Sheria ya Uhujumu wa Uchumi, Sheria ya Mwaka wa 1984, Namba 13, inazungumza kule ndani. Inakwenda, ukimpeleka Mahakamani, ikithibitika kwamba, amechukua mali ya umma, ameitumia vibaya ni pamoja na ku-*confiscate* kwa maana ya kuchukua mali yake yote ile kwa hiyo, ni suala la Mahakama hapa ndilo ambalo Mahakama ikishaamua hivyo tutafanya hivyo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, ubadhirifu wa fedha kwenye Halmashauri ni mwinci. Na kwa kuwa, ubadhirifu huu Waheshimiwa Madiwani, hucheleva kuufahamu kutokana na kutokuwa na elimu yakutosha kuhusu mambo ya fedha. Je, Serikali, itakuwa tayari kuongeza Semina mbalimbali kwa Waheshimiwa Madiwani, ili wapate elimu yakutosha na waweze kuugundua ubadhirifu huu mapema kuliko wanavyosubiri mpaka ukaguzi wa CAG ufanyike?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili hata juzi tulipokutana katika *Association of Local Authorities of Tanzania (ALAT)*, limesisitizwa sana hili analolisema Mheshimiwa Mbunge, Chilolo. Tunachoweza kusema tu hapa ni kwamba, tumefanya Semina nchi nzima na tumehakikisha kwamba,

21 MEI, 2013

Madiwani wetu wanajua jambo hili, lakini kama mmesikia katika jibu nililolitoa hapa, utaratibu umebadilika. Sasahivi tumeingiza *Internal Auditor*, ambaye hawajibiki kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, anawajibika kwa *Internal Auditor* yule wa Taifa; hilo moja.

Mheshimiwa Spika, lakini kila baada ya mkiezi 3 Halmashauri lazima isomewe Taarifa ya Mapato na Matumizi, ikiwepo pia Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani. Kitu hiki ndicho kitakachowafanya Madiwani wajue kwamba, kuna kitu kimetokea, lakini tunapokea mawazo yake na maoni yake yatasaidia. (*Makofii*)

MHE. CECILIA D. PARESO: Mheshimiwa Spika, mfumo mpya wa *EPICOR* unaotumika katika Halmashauri zetu umekuwa na changamoto nyingi kwa Watendaji. Je, Wizara imewaandaaje Watendaji wa Halmashauri, ili kuweza kuendana na huo Mfumo?

SPIKA: Changamoto, maana yake? Hawaelewi, au?

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, wengine hawaelewi na hawana ujuzi kwa sababu pia ni mfumo mpya.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (*TAMISEMI*): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa ufanuzi kwa Mheshimiwa Paresso:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa *EPICOR*, ambao unasihamiwa na *TAMISEMI* katika kila Halmashauri, tumetoa mafunzo kwa watumishi ambao wanautumia. Na Makao Makuu pia, tunao Wataalam ambao wanazifuatilia Halmashauri zote na wenyewe wanapopata tatizo lolote, wanapiga simu na wanapewa msaada kwenye simu na inaposhindikana huwa tunawatembelea.

Changamoto kubwa ambayo tunaiona ni baadhi ya Halmashauri, kutokontakte kutumia mfumo wa *EPICOR* kwa sababu, kwa kiasi kikubwa unawabana. (*Makofii*)

21 MEI, 2013

Na. 244

Uhitaji wa Walimu wa Shule za Msingi

MHE. PINDI H. CHANA aliuliza:-

Shule za Msingi za Ludewa, Makete, Masasi, Manda, Kilando, Ibumi, Kipagalo na Mfumbi, Ikuwo, zinahitaji kubwa la kupelekewa Walimu:-

Je, ni lini Shule hizo zitapelekewa Walimu wa kutosha?

Mheshimiwa Spika, kabla swali langu halijajibiwa, kuna marekebisho kidogo. Kuna majina ya Kata, sasa kuna Kata zimechanganywa. Swali linasema Shule za Msingi za Ludewa, Makete, Manda, Kilando, Ibumi, Kipagalo na Mfumbi, Ikuwo. Baada ya neno Mfumbi kuna Koma, Ikuwo; hizi ni Kata 2 tofauti, zina hitaji kubwa la kupelekewa Walimu.

Mhweshimiwa Spika, baada ya marekebisho hayo, sasa naomba swali langu Namba 244, lipatiwe majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali, imeendelea kuwaajiri na kuwapanga Walimu Wapya katika Shule za Msingi na Sekondari, kila mwaka kadiri wanavyohitim, uwezo wa Serikali na kulingana na uwiano wa mahitaji ya Walimu katika Halmashauri zetu. Hadi mwezi Disemba, 2012 katika Shule za Msingi walikuwemo Walimu 171,986 na katika Shule za Sekondari, walikuwemo Walimu 51,469. Hadi Aprili 30, tulipofanya ajira ya mwisho mwaka 2013, Serikali, imeajiri Walimu 27,585 wakiwemo wa Shule za Msingi 13,568 na wa Shule za Sekondari 14,017.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, ilipangiwa Walimu wa Shule za Msingi 42 na wa Shule za Sekondari 99. Shule ya Msingi Ibumi, ilipangiwa Walimu 2 na sasa inao Walimu 6 na Manda Mwalimu 1 na sasa inao Walimu 10. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete, Shule ya Msingi Ikuwo, ilipangiwa Walimu 2 na sasa inao Walimu 6. Shule ya Msingi Makete ilipangiwa Mwalimu 1 na sasa inao Walimu 20, wakati Shule ya Sekondari Kipagalo, ilipangiwa Walimu wapya 3 na sasa inao jumla ya Walimu 9.

Shule ya Msingi Ludewa Mjini yenyne Walimu 16, Ludewa Kijiji yenyne Walimu 11 na Shule ya Msingi Mfumbi (Makete) yenyne Walimu 10, hazikupangiwa Walimu kutokana na uwiano wa mahitaji ikilinganishwa na shule nyingine.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali, ni kuendelea kuajiri Walimu kadiri wanavyohitimu na kufaulu kwao na kuwapanga ili kuhakikisha shule zinakuwa na walimu wa kutosha. Aidha, ili kuwa na uwiano sawa katika shule zetu, Wakurugenzi wa Halmashauri nchini wameagizwa kuwapanga Walimu wapya katika maeneo ya pembezoni yenyne upungufu wa Walimu na kusawazisha ikama, ili kuondokana na mlundikano wa maeneo ya Mijini na katika shule zilizo kandokando ya njia kuu. (*Makof!*)

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, asante. Kwa kuwa, idadi ya Walimu waliopo hailingani na ikama.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taaluma kila Shule ya Msingi inapaswa kuwa na Walimu wangapi?

(b) Mheshimiwa Spika, Waziri atakubaliana na mimi kwamba, katika bajeti hii ambayo, tunakwenda kuipitisha sasa Wizara ya Elimu, maeneo haya ambayo yametajwa, Kata hizi, ninaomba yaongezewe Walimu kwa mujibu wa ikama inayopaswa Kitaalam maana ni maeneo ya pembezoni sana, maeneo ya Ludewa na Makete?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza anaomba kujuu Walimu wanaotakiwa kwenye shule zake ni wangapi; kwanza nataka nimwambie kwamba, utaratibu tunaoutumia sasa ni wa Mwalimu kuwa na wanafunzi 40 kwenye shule za msingi. Na hatua tulioifikia sasa kutokana na ajira mbalimbali tunazoajiri kwamba, sasahivi nchini tuko kwenye *ratio* ya Mwalimu 1 Wanafunzi 46. Na jitihada za Serikali, ni kuhakikisha kwamba, tunaendelea kuajiri, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, mpaka pale ambapo tutahakikishakwamba, Walimu hawa wanatosha.

Lakini si hilo tu, mkakati wa Serikali sasa, tutaachana na hii *ratio* ya Mwalimu na Wanafunzi, tunataka tuwe na Mwalimu katika kila mkondo, ili kutosheleza mahitaji ya Darasa na Walimu na masomo yaliyopo katika Mkondo, ili kuweza kupata Walimu wengi wa kutosha, kuweza kufundusha masomo yote ambayo wanayo.

Mheshimiwa Spika, ombi la pili la kutaka kuwapeleka Walimu kadiri ya mahitaji ya Wilaya; ombi hilo tunalichukua na kwa sababu, mahitaji haya yako nchi nzima kwamba, tunao upungufu huu mkubwa wa Walimu kwenye maeneo haya, bado Serikali, itaendelea kuajiri kadiri ambavyo, Wanavyuo hawa wanafaulu na ili tuweze kuwapanga kwenye maeneo yao. Na sio sababu Serikali, imeongeza udahili kwenye Vyuo Vikuu, kwenye Vyuo vya Ualimu, ili kupata idadi kubwa ya Wahitimu wa mafunzo ya Ualimu, kwa ajili ya kuwapeleka kwenye shule, ikiwemo na Wilayani kwa Mheshimiwa Pindi Chana.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hapa tatizo la msingi ni hiyo Sera ya Elimu ya Uwiano wa Mwalimu Mmoja kwa Wanafunzi 40 kwa Shule

zote katika nchi ya Tanzania. Mimi naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, ni lini Serikali, itaamua kuleta mabadiliko hayo, ili kuwafanya watoto wetu wa Vijijini waweze kupata Walimu inavyotakiwa? Kwa sababu, Sera hiyo, haiwezekaniki kabisa kwa maeneo ya Vijijini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeeleza vizuri hapa nilipokuwa najibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Pindi Chana, kwamba, hatua tulioiflikia sasa kwa Shule za Msingi na kwa mujibu wa Sera ambayo ameieleza ni kweli, kwamba, Sera inasema Mwalimu 1 wanafunzi 40. Jambo hili, tunataka tuliflikie kuwa na Mwalimu 1, Walimu watosheleze katika Mkondo badala ya kufuata kigezo cha Mwalimu mmoja, wanafunzi 40.

Mheshimiwa Spika, tukifuata hii tunakuwa na idadi ndogo sana ya Walimu na mahitaji kuwa ni makubwa zaidi, lakini mkakati wa Serikali, baada ya kuongeza udahili Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ualimu ni kupata Walimu wengi wakutosha, ili kila mkondo uweze kuwa na Walimu wa kutosha.

Lakini suala la mabadiliko ya Sera, Wizara ya Elimu, sasa iko kwenye utaratibu wa kuihuisha hiyo Sera, ili kupata mabadiliko. Na ninadhani kama si muda mfupi hapa, itakuwa imeshafika kwa ngazi ya Wabunge, kwa ajili ya kufanya mapitio. Na hili jambo lilishatangazwa na linaendelea vizuri. Kwa hiyo, Sera itafanyiwa mapitio na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, kwa maana ya wadau watapata nafasi ya kufanya mapitio ya Sera nzima ya Elimu, ili kupata Sera ya Elimu inayokidhi mahitaji ya Watanzania kwa sasa. (*Makofii*)

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa katika Wilaya ya Kasulu ziko shule ambazo ziko umbali wa kilomita 50, 40, 30, kutoka Makao Makuu ya Wilaya na shule hizo kila mara zinapopangiwa walimu, walimu hawaendi.

Je, Serikai inasema nini kuhusu kuziangalia shule ambazo zipo umbali wa kutoka makao makuu ya Wilaya ambazo zipo katika mazingira magumu kuwaongezea walimu posho ili walimu waweze kuhamasika kwenda katika shule hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Genzabuke kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kauli yake kwamba tunazo shule za pembezoni ambazo hazina walimu na shule nyingine ziko kule hazina idadi kubwa ya walimu kutokana na mazingira yake kuwa magumu na ambacho tunakifanya Serikali sasa kwanza kuhakikisha tu kwamba katika kila shule pamoja na ugumu uliopo kuwa tunapata walimu wanakwenda kwenye maeneo hayo na ndio cha kwanza tumeagiza na kwenye jibu la msingi nimeeleza kwamba tumewaaagiza Wakurugenzi wote nchini na Maafisa elimu wao kufanya mapitio ya ikama waliyonayo kuona kwamba katika kila shule kunakuwa na walimu wa kutosha ili kuwezesha shule ile kuwa na idadi ya walimu wanaoweza kutosha kuweza kufundisha vijana waliopo na vijana hawa waweze kupata taaluma iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini mpango gani tunao wa Serikali sasa wa kupeleka fedha ambazo zinaweza kuboresha mazingira yale?

Kwa upande wa Sekondari tulichokifanya sasa ni kupeleka fedha katika Halmashauri tumeanza na Wilaya 265 kuboresha shule zilizopo ili kuondoa ule ugumu wa mazingira ya shule hizo na shule 264 sasa zimeanza ujenzi wa kuongeza

miundombinu kwa maana ya vyumba nya madarasa, nyumba za walimu, maabara ili ziwe na mazingira ambayo mwalimu anaweza kukaa na kuweza kufanya kazi yake.

Upande wa shule za msingi pia nako tumepeleka fedha katika Halmashauri jumla ya bilioni 2.5 zimetumwa kwenye shule za msingi kwenye Halmashauri ili ziweze kuboresha ujenzi wa nyumba za walimu hiyo ndiyo katika kuondoa mazingira magumu yaliyopo, lakini kuongeza vyumba nya madarasa kwenye shule zile ili walimu wakienda wakute nyumba, wakute vyumba nya kutosha wafanye kazi yao kama inavyokusudiwa, huo ndiyo mkakati wa Serikali. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa naomba tuendelee na swalilinalofuata Mheshimiwa Moza Abeld Saidi.

Na. 245

Kuboresha Mazingira ya Elimu Kondoa

MHE. MOZA A. SAIDI aliuliza:-

Shule nyingi kwenye Halmashauri ziko kwenye mazingira magumu ikiwa ni pamoja na upungufu wa walimu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru elimu kwa kuboresha miundombinu ya kielimu kama vile fedha na vifaa nya kufundishia?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kutoa elimu kwa walimu na watendaji wa elimu juu ya maboresho katika sekta ya elimu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moza A. Saidi Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mipango mbalimbali katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Kupitia awamu ya pili ya mpango wa maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMSE II) ujenzi na ukamilishaji wa shule za Sekondari 264 kwa kiasi cha shilingi bilioni 56.5 umeanza ili kuzifanya kuwa na miundombinu yote muhimu ikiwemo maabara, maktaba, vyoo, umeme na maji.

Kupitia mipango, bajeti na vipaumbele vya Halmashauri, Serikali inatenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu mbalimbali ya shule. Shilingi bilioni 9.3 zimeshatumika kukarabati shule za Sekondari Kongwe ikiwemo Sekondari ya wasichana Kondoa iliyopata shilingi milioni 100 na kazi hiyo imefanywa vizuri. Pia Halmashauri zimepatiwa shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya ununuza wa maabara hamishika na shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ununuza wa wa vifaa vya elimu ya awali.

Serikali inatoa fedha za uendeshaji wa shule (*Capitation grant*) kwa ajili ya ununuza wa vifaa ikiwemo vitabu. Mwaka 2012/2013 shule za Sekondari zilitengewa shilingi bilioni 41.1 na shule za msingi shilingi bilioni 82.5. Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa hadi Machi, 2013 imeshapokea kwa Sekondari shilingi milioni 252 kati ya milioni 288 na kwa msingi imepokea shilingi milioni 797.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia MMEM na MMES inaendelea kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa kusimamia Elimu katika kada zote za Elimu kuanzia kamati za Shule za Msingi, Bodi za shule za Sekondari, Walimu Wakuu, Viongozi

21 MEI, 2013

wa Elimu wa Halmashauri, Mikoa na Wizara kupitia Vyuo vya Ualimu na ADEM Bagamoyo. (*Makofii*)

MHE. MOZA A. SAIDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru ningependa kumwuliza maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na majibu yake mazuri moja ya changamoto zinazowakabili walimu ni kupatiwa makazi na wanapofuata mishahara yao kwa eneo la mbali. Je, Mheshimiwa Waziri Serikali ina mpango gani kuwaboreshea miundombinu walimu hawa ili wasiweze kutaabika kwa umbali na kutafuta makazi?

Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya Serikali ya Mkaguzi Mkuu kumeonekana kuna ubadhilifu katika fedha za MMES na Serikali imejipanga kupeleka bilioni 56.5. Je, Serikali imejipangaje kudhibiti ubadhilifu wa fedha hizi?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri naona maswali mengine yanajirudia kwa hiyo na wewe usirudie kujibu, jibu *straight*.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza suala la umbali wa makazi ya walimu na maeneo ya kufuata mishahara lakini pia kupata huduma mbalimbali. Jambo hili nimelieleza katika eneo la jibu la msingi na namna ambavyo Serikali imejipanga kuboresha makazi ya walim. Lakini pia sasa tumeshapeleka shilingi milioni 500 zile tunazozzungumza za mazingira magumu kwenye Halmashauri na awamu ya kwanza tumepeleka katika kila Halmashauri katika shule mbili mbili ili kupata kujenga nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, tunaamini tukianza kujenga nyumba za walimu tutakuwa tumeanza kuondokana na tatizo la ugumu wa mazingira ya mwalimu kufanyia kazi, lakini

Mheshimiwa pia amezungumzia suala la mishahara. Suala la Mishahara bado mtumishi anapokelea kupitia benki lakini nashukuru mabenki mengi sasa yameanzisha *mobile bank* ambazo zinatembea kwenye maeneo yetu, lakini pia uko mfumo ambao sasa hivi umeanza wa namna ya kupata fedha kutoka M-pesa kwenda *NMB* na *NMB* ndiyo benki ambayo wateja wengi walimu tunayo. Kwa hiyo mfumo huu unaweza kutusaidia pia mwalimu kupata fedha yake ya mshahara hapo hapo alipo kwa kutumia M-pesa kupitia *NMB*. Kwa hiyo hili linaweza kutusaidia sana kuondoa ugumu wa walimu kusafiri kutoka makazi ya mbali mpaka ambako Makao Makuu ya benki ipo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili tumejipangaje kuondoa ubadhilifu wa matumizi ya fedha. Fedha hizi zimetolewa maelekezo kamili na fedha hizi zikifika kwenye Halmashauri Mkurugenzi anapaswa kuitangaza zabuni ya wajenzi ambao watajenga majengo hayo ambayo yanapitiwa na wataalam ili kupata mjenzi ambaye ametenderkwa gharama nafuu lakini kwa viwango na usimamizi utasimamiwa na wataalam wetu hili litasaidia sana kuondoa ubadhilifu wa fedha hizi katika utekelezaji wa miradi ambayo sisi tumeipanga.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru, Mheshimiwa naibu Waziri wakati anajibu swali lake amezungumzia kuhusiana na *Capitation Grants* lakini Mheshimiwa Naibu Waziri najua anajua kwamba haya mabilioni anayoyataja hayafiki kule chini na hata utekelezaji wa bajeti unaonyesha 2011/2012 tulitenga hamsini ikafika kumi, 2012/2013 tulitenga tena zaidi ya hamsini lakini fedha kule chini hazifiki. Sasa matokeo yake ni nini?

Matokeo yake ni kwamba wazazi kule chini wanalipishwa umeme, wanalipishwa maji, wanalipishwa mitihani, wanalipishwa *tuition*. Sasa Serikali imekuwa ikitoa kauli kila siku sasa mimi nilitaka nipate kauli ya Serikali kwa sababu tunavyozungumza sasa hivi shule za Serikali zimekuwa ghali kuliko shule binafsi kwa sababu mia mbili mia mbili, elfu moja moja kila siku.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nipate kauli ya Serikali ni michango ipi ili sahihi kutolewa na mzazi katika hizi shule zetu ambazo wanasoma watoto wa maskini, ni michango ipi, naomba kauli ya Serikali?

SPIKA: Sawa sawa tayari, Mheshimiwa Majaliwa na wewe jibu kwa kifupi sina muda nina maswali matatu nusu saa imeshafika.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la msingi ni michango ipi imetakiwa kuchangwa katika shule. Kimsingi maelekezo ya Serikali ni kwamba shule hizi kwanza ni za wananchi wenyewe. Maendeleo ya shule hizi yanaratibiwa na wananchi wenyewe na tumewapa nafasi pia wananchi hawa kuunda Kamati za shule na kule Sekondari ziko Bodii. Mipango yote ya maendeleo ya shule itaamriwa na hawa Kamati ya shule na Bodii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama kuna michango yoyote wanayoona wao inafaa ni wao ndiyo wataamua. Sasa matumizi ya fedha hizi bado yatasimamiwa na Kamati yenyewe na Kamati inawajibika kuwatangazia wazazi wa eneo hilo na siyo kazi ya Mwalimu Mkuu na tumeshaeleza hapa mara nyingi. Lakini pia niwasihii Waheshimiwa Wabunge tusaidiane katika hili kusimamia shule zilizopo katika maeneo yetu ili tuhakikishe kwamba wazazi na wananchi kule hawachangiwishwi michango mingi ambayo haina tija. Badala yake pia fedha hizi zinakuwa zinapotea tu bado sisi tunaweza kusimamia kama sehemu ya wazazi na wazazi hawa pia waendelee kuangalia wazazi wenao kutoratibu michango mingi ambayo itakuwa inaleta kero kwenye maeneo yao. (*Makofii*)

21 MEI, 2013

Na. 246

Ujenzi wa Barabara ya Nyololo – Mgololo

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 barabara ya Nyololo – Igowole – Mtwango – Mgololo ilitengewa shilingi 65,000,000.00 kwa ajili ya upembuzi yakinifu na kukubaliwa na Serikali kujengwa kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Je, baada ya upembuzi yakinifu, ni lini sasa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami utaanza katika barabara hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyololo – Igowole – Mtwango – Mgololo ilitengewa shilingi 65,000,000.00 katika mwaka wa fedha 2012/2013 kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya awali ya kujengwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Utaratibu wa manunuzi ili kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya kazi hii unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika, Wizara itapata makisio ya gharama ya mradi mzima ili Serikali ianze kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hiyo. Kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami itaanza baada ya fedha kupatikana.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza mwaka jana wakati nimeuliza swali hili wananchi walikuomba kwamba uende kule Mufindi ukakae nao ili uweze ukawaelimishe ile Sheria ya barabara ili wajue watu wanaolipwa na wale ambao hawalipwi na wewe uliahidi kwenda na hukwenda. Je, sasa leo unawaambiaje watu wa Mufindi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili hii barabara ina umuhimu wake na wewe unajua kabisa kwamba kule kuna viwanda vingi ambavyo vinasaidia kitaifa kwenye pato la Taifa na hapa umesema ujenzi utaanza pale fedha itakapopatikanika. Lakini najua kabisa fedha ipo kwa sababu sehemu kubwa viwanda vipo kule na tunachangia pato kubwa sana la Taifa. Sasa je, kwa bajeti inayokuja ya mwaka 2014/2015 barabara hii itaanza kujengwa kwenye kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kigola kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niombe radhi kwamba niliahidi nitaenda basi nikua hidi tena nitakwenda kuangalia barabara hiyo na kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria ya barabara. Kuhusu kama tutaweka kwenye mpango wa miaka 2014/2015 barabara hiyo kuanza kujengwa. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba barabara hizi tukishajua makisio yake tutaziwekea kwenye orodha ya barabara ambazo inabidi tuanze kujenga kulingana na fedha ambayo Wabunge mtatupa katika kujenga barabara hizi. (*Makof!*)

MHE. MWIGULU L. M. MADELU: Mheshimiwa Spika, asante sana barabara ya Singida, Sepuka, Ndago hadi Kizaga imekuwa na umuhimu mkubwa sana wa kusaidia punde inapotokea uharibifu kama mafuriko kwenye

21 MEI, 2013

barabara kuu na ilikuwepo kwenye ahadi ya Serikali ya kuwekewa lami. Je, ni lini Serikali itazitengeneza barabara zinazosaidia panapotokea mafuriko kote nchini kwa kupitisha kuwa *high way* ili ziweze kuwekewa lami?

SPIKA: Afadhali umechepuka, Mheshimiwa naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mcchemba, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, barabara zote hizi tutazijenga kulingana na mipango ambayo tunaiwasilisha Bungeni na ambayo ninyi mnakubali. Kwa hiyo, barabara hizo anazozizungumza kama ziko kwenye mpango ambazo tumepitisha juzi basi tutazijenga kulingana na mpango huu kama haipo itabidi tuitengenezee utaratibu wa kuifanyia upembuzi halafu baadae tuweze kuzijenga kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Ninaomba tuendelee na swal linalofuata Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, hayupo kwa niaba yake Mheshimiwa Nyangwine.

Na. 247

Ujenzi wa Barabara ya Makutano hadi Mto wa Mbu

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE (K.n.y. MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE) aliuliza:-

Barabara ya kutoka Makutano – Loliondo – Mto wa Mbu iko kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na ilipangiwa shilingi bilioni 3.8 katika Bajeti ya mwaka 2012/2013.

(a) Je, barabara hiyo itaanza kujengwa lini na ni fedha kiasi gani kimetengwa cha kuwalipa fidia wananchi waliohama ili kupisha ujenzi huo na wataanza kulipwa lini?

(b) Kwa nia ya kuimarisha utalii kwenye maeneo haya, Serikali haioni ni vyema kuweka lami katika Mji wa Mugumu ambako barabara hiyo inapita?

(c) Kama Serikali ikiafiki wazo la kujenga kipande cha barabara kilomita 41 kutoka Mugumu mjini kwenda lango kuu la Ikoma kupitia Hifadhi ya Taifa, kuna mpango gani wa maandalizi katika kipindi hiki?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibi swali la Dkt. Kebwe S. Kebwe Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami ya barabara ya kutoka Makutano kupitia Natta hadi Mugumu Tabora B hadi *Kleins gate* na Loliondo hadi Mto wa Mbu yalianza katika mwaka wa fedha wa 2006/07 kwa kazi za upembuzi yakinifu ambazo zilikamilika mwaka 2007.

Kazi ya usanifu wa kina ilikamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Ujenzi wa barabara hii utafanyika kwa awamu ukihusisha ujenzi wa kiwango cha lami sehemu ya barabara ya makutano Mugumu kilomita 130 na barabara ya mto wa Mbu – Loliondo kilomita 213. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu katika mwaka wa fedha 2012/2013 ni shilingi milioni 3,827 na katika mwaka 2013/2014 ni shilingi milioni 5,617. 63. Aidha, mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Makutano – Sanzate kilomita 50 kwa kiwango cha lami umesainiwa Aprili 2013. Wananchi watakahama ili kupisha ujenzi wa barabara hii watalipwa fidia kwa kuzingatia sheria kabla ya Mkandarasi hajaanza kazi.

Mheshimiwa Spika, (b) ujenzi kwa barabara ya lami kwa sehemu ya kutoka Makutano – Natta hadi Mugumu umelenga kuboresha pia barabara katika mji wa Mugumu.

Mheshimiwa Spika, (c) matokeo ya upembuzi yakinifu yameonyesha kuwa umuhimu wa kuepuka ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami karibu au ndani ya hifadhi ya Taifa ya Serengeti kutokana na athari za kimazingira ambazo zinaweza kutokea. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na matengenezo kwa kiwango cha changarawe ya barabara inayopita ndani ya hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, asante pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza hii barabara ina urefu wa kilomita karibu 450 mpaka 500 na inavyoonekana Serikali inatenga fedha kidogo sana katika ujenzi wa hii barabara na kwa muundo huu wa kutenga shilingi bilioni tatu na laki tano kwa mwaka kuna uwezekano kabisa ikachukua miaka 30 kuikamilisha. Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kujinga hii barabara haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili hii barabara ikikamilika itasaidia sana kuimarisha utalii katika Hifadhi ya Serengeti na maeneo ya jirani; na kwa kuwa watalii wengi wanaotoka Kenya hupitia Silari, Tarime mpaka Serengeti na kuna barabara inayotoka Tarime, Nyamwaga, Nyamongo mpaka Serengeti na hii barabara ikiwekewa lami na yenyewe inajengwa kwa kiwango kidogo kidogo, ni lini Serikali itatenga hela za kutosha kukamilisha ujenzi wa barabara hii?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyangwine kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza urefu wa barabara hii ni kilomita 343, fedha zilizotengwa zinatosha kuanza kujenga kwa sababu huwezi kutenga fedha zote za kilomita 343 kwa sababu hawesi kujenga kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, tunaweka fedha ambazo zinaweza kwanza kumlipa *advance mkandarasi* aweze kuanza kujenga, kwa hiyo nikuhakikishie kwamba barabara hii upande huu wa Loliondo – Mto wa Mbu tutaanza na Upande wa kutoka Makutano - Natta kwenda mpaka Mugumu tayari tumesha saini

21 MEI, 2013

mkataba. Kwa hiyo nikuhakikishie fedha hizi zitatosha na kazi itaanza na mradi mzima tutaukamilisha kama Serikali inavyoahidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara unayoizungumza ya kutoka Tarime – Nyamwaga mpaka Serengeti barabara hiyo tutaiangalia katika utaratibu kama nilivyosema barabara kwanza zifanyiwe usanifu, zikubalike ndani ya mpango baada ya hapo tutatafuta fedha tuweze kuzijenga. Siwezi kusema sasa hivi kama mwakani tutaanza kujenga barabara hiyo lakini tutazingatia ombi lako.

Na. 248

Mpango wa Kutembelea Wajawazito Majumbani

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA aliuliza:-

Mpango wa kutembelea wajawazito majumbani unatekelezwa na Wahudumu wa Afya Vijijiini (VHW) katika Wilaya za Bagamoyo, Temeke, Mtwara, Hai na Magu.

Je, Serikali ina mkakati gani endelevu wa kusambaza mpango huu katika Mkoa wa Rukwa na Wilaya nyingine zilizobaki?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa kutembelea wajawazito majumbani, ni njia mojawapo ya kusogezza huduma za afya karibu na wananchi. Mpango huu umekuwa unatekelezwa katika baadhi ya Wilaya hapa nchini, zikiwemo Bagamoyo, Temeke, Mtwara, Hai na Magu kuititia wadau mbalimbali wa afya ya uzazi na mtoto. Katika kuhakikisha kwamba mpango huu unasambaa nchini kote. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imeandaa mwongozo wa Taifa

kuhusu huduma jumuishi ya mama, mtoto mchanga na mtoto chini ya miaka mitano katika ngazi ya jamii (*National Integrated Community Maternal, Newborn and Child Health Guideline*), ambao unaoelekeza wadau wa watoa huduma jinsi ya kuendesha shughuli hizo nchini. Mwongozo ulizinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, tarehe 20 Novemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mwongozo huo Wizara imeandaa vitabu nya mafunzo (*Curriculum*) kwa wahudumu wa afya vijiji na mafunzo ya wiki tatu yameanza kutolewa kuhusu mambo muhimu yanayohusu Afya ya Mama na Mtoto. Jukumu la wahudumu hawa ni kutoa Elimu ya Afya, Ushauri na kuwapa rufaa wenye matatizo kwenda vituo nya kutolea huduma za afya. Aidha, wahudumu wa afya hutakiwa kutoa taarifa za afya katika kijiji, kwa msimamizi wa kituo cha kutolea huduma za Afya kilichopo karibu kijiji. Hadi sasa wahudumu wa afya katika jamii 169, wamekwishapata mafunzo mkoani Morogoro.

Mpango huu utawezesha kuwa na huduma endelevu, kwenye vituo nya kutolea huduma hadi kwenye jamii. Lengo la mpango huu ni kuboresha huduma kwa wanawake wajawazito hapa nchini, na hatimaye kuendelea kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Rukwa, mpango huu umeanza kutekelezwa na wadau wa *Plan International* kuanzia Desemba, 2012. (*Makofii*)

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana na ya kuridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Plan International sasa hivi wanatekeleza mpango huu mzuri sana kwa Mkoa wa Rukwa, lakini kwa usoefu ni kwamba, wadau au wafadhili wanapoijiondoa basi miradi hii aidha husimama au hufa kabisa na pengine huendelea kwa kususua.

21 MEI, 2013

Je, Serikali imejiandaaje kuendeleza huu mpango mzuri unaotekelawa na *Plan Interenational* kwa Mkoa wa Rukwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba wadau wanapojiondoa, Serikali inakuwa na mpango gani wa kuweza kuendeleza shughuli ambayo imekuwa ikifanywa na wadau. Katika mpango huu wa uwepo wa huduma ya afya vijijiini, ni mpango ambao kwa sasa Serikali inaufanya tafiti mbalimbali na kuangalia ili ushauri wa kuweza kuona manufaa yake na namna ambavyo wahudumu hawa wanaweza wakaingizwa katika ajira badala ya kuwa watu wa kujitolea na namna ambavyo gharama zinaweza kuwa, ili Serikali iweze kufanya maamuzi sahihi na kuanza kutumia Wahudumu hawa wa Afya vijijiini na kuweza kufanya kazi nchi nzima.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Tunajua sera ya Afya inasema matibabu kwa watoto chini ya miaka mitano, mama wajawazito na wazee ni bure. Hata hivyo kumekuwa na changamoto sana kwenye Vituo vya Afya na Zahanati zetu; hasa maeneo ya vijijiini tatizo la akina mama wajawazito kudaiwa vifaa wakati wa kujifungua linaendelea.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa wakina mama wa vijijiini wanaondoka katika hatari hiyo na kuhakikisha kwamba wanatekeleza Sera hiyo ya Afya kwa vitendo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Sera inasema watoto chini ya miaka mitano, wakina mama wajawazito wale wenye magonjwa ya kusendeka, yaani magonjwa ya muda mrefu, pamoja na wazee

21 MEI, 2013

wanatakiwa wapate huduma bure. Huu ni msingi mbao unatakiwa kutekelezwa na watoa huduma kote nchini. Pale ambapo kunakuwa na tatitizo la kutekeleza sera hii, hatua stahili zinatakiwa zichukuliwe na wasimamizi wa watoa huduma hizi katika kila ngazi husika.

Kwa wazazi Serikali imeweza kupunguza tatizo hili kwa kuweka mpango rasmi wa kuweza kununua zile *package* kwa ajili ya matumizi wakati wa uzazi, yaani *delivery kits* ambazo zinatolewa kwa mama mjamzito anapohudhulia *clinic* ili wakati wa kujifungua aende na *kit* yake pale na kuondoa usumbufu wa kulazimika kutakiwa kuchangia au kutoa fedha za ziada.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mhesmiwa Roman J. Selasini anaulliza swali hilo. Nimesahahu kuna swali jingine namba 249. Mheshimiwa Rita Kabati, atauliza kwa niaba ya Mheshimiwa Faida M. Bakar. *Aah upo!*

Hao wanaokuombea wanakutakia afya njema karibu.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa dhati!

Na. 249

Serikali Kupunguza Uwepo wa Maradhi ya Ukoma

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR aliuliza:-

Watu wenye maradhi ya ukoma wameonekana kutengwa na jamii na hivyo kunyimwa haki yao ya msingi ya kuishi kama binadamu wengine na kupendwa na jamii yao.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupunguza uwepo wa maradhi hayo ya ukoma?

21 MEI, 2013

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampa pole Mheshimiwa Faida kwa kuugua muda mrefu, pole na karibu sana.

Mheshimiwa Spika, watu wanaouguia ukoma wamekuwa wanatengwa na kunyanyapaliwa kutokana na imani, mila potofu na ukosefu wa uelewa kuhusu ugonjwa huu. Maambukizi huanza wakati mgonjwa wa ukoma hajagunduliwa wala kuanza matibabu. Mgonjwa ambaye tayari ameanza matibabu ya ukoma hawezi kuambukiza mwингine na ana haki ya kuishi katika jamii kama mtu mwингine.

Serikali inaendelea kutoa huduma kwa wote wanaogunduliwa kuwa na ugonjwa wa ukoma. Mkazo zaidi unawekwa kwenye utambuzi wa mapema na matibabu sahihi ili kutibu vimelea vya ukoma na kupunguza au kuondoa kabisa madhara yanayotokana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali katika kupunguza uwepo wa ugonjwa wa ukoma ni kama ifuatavyo:-

Moja, kutoa elimu kuhusu dalili za ukoma kwa kutumia njia mbalimbali kama vile redio, televisheni na vipeperushi ili wananchi waweze kujitokeza mapema kwa uchunguzi na matibabu.

Mbili, kutoa huduma za matibabu ya wagonjwa wa ukoma hutolewa bila malipo na Serikali.

Tatu, Serikali imepanga kufanya kampeni maalum za kutokomeza ukoma katika Wilaya zenye idadi kubwa ya ugunduzi wa wagonjwa. Tangu mwaka 2007, zimefanyika kampeni za kutokomeza ukoma katika Wilaya 7 na jumla ya wagonjwa wapya 523 waliogunduliwa.

Nne, Serikali inafuatilia na kutoa matibabu stahiki kutokana na mahitaji kwa wenyе ulemavu unaotokana na ukoma. Huduma hizi ni pamoja na dawa maalum za madhara ya ukoma (*reactions*), viatu maalum, upasuaji wa marekebisho (*rehabilitative surgery*) ya miguu bandia. Tangu mwaka 2007, jumla ya watu 3,259 wenyе ulemavu utokanao na ukoma walipatiwa huduma mbalimbali za mareklebisho ya viungo. Jozi 19,000 za viatu maalum zilizotolewa kwa waathirika wa ukoma wenyе ganzi miguuni.

Tano, Wizara hutoa miongozo, mafunzo kwa watumishi wa afya wa kada mbalimbali kwenye utaalim maalum kwa utabibu na madhara ya ukoma.

Sita, Idara ya Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali, imeendelea kuwajengea uwezo watu wenyе ulemavu utokanao na ukoma ili waweze kujitegemea katika nyanja mbalimbali za maisha yao.

Pia, inatoa mahitaji ya kijamii kwa watu walioathirika na ukoma na jamii zao kama vile kutoa, mavazi ya shule na ada kwa watoto wa watu walioathirika na ukoma, utengamao (*resettlement*) na Machangamano (*integration*). (*Makofii*)

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali yangu ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza.

(a) Je, maradhi haya ya Ukoma yana ukaribu gani na maradhi ya Mbalanga, yaani Maradhi ambayo mtu anapata rangi nyeupe mwili mzima?

(b) Suala la Ukoma mimi naona halizungumzwi kabisa katika nchi ya Tanzania na siyo sana kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Kampeni dhidi ya maradhi ya UKIMWI yamezagaa Dunia nzima na Tanzania nzima. Watu wenyе maradhi ya UKIMWI mwanzo walikuwa wanatengwa, lakini sasa *Alhamudullilah* afadhalii, lakini kwa watu wenyе

maradhi ya Ukoma wanaogopwa hata kuguswa. Kuna vituo vingi hapa Tanzania ambavyo vinalea watu hawa wenye maradhi ya Ukoma hususani wazee wasiojiweza. Juzi nimeangalia TV huko Tanga, nimeona wanalamika kwamba hawapelekewi chakula.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, unalieleza nini Bunge hili na Watanzania kwa ujumla kuhusu kuwahifadhi wagonjwa hawa wa maradhi ya Ukoma?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Spika, kwa Niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali, kama ifuatavyo:-

Maradhi hao ya Mbalanga ambayo anayafananisha na Ukoma, kwa hakika mimi siyafahamu vizuri, kwa sababu neno allotumia siyo neno la kitaalam, hivyo siwezi kujua hiyo Mbalanga ni ugonjwa gani. Hata hivyo, inawezekana anazungumzia ugonjwa wa Ngozi aina nyingine ambao labda unashabiana au kufanana kidogo na Ukoma. Ugonjwa wa Ukoma unasababisha kuwepo na mabaka au baka kwenye ngozi lakini pia baka hilo linakuwa tofauti na mabaka mengineyo, kwa sababu mgonjwa wa Ukoma baka lake linakuwa halina hisia, yaani hupati hisia ya mguso. Kwenye Ugonjwa wa Ukoma kunakuwa na mashambulizi katika nerve au mashipa ya fahamu, hivyo kupata dalili za mtu kupata ganzi kwenye mikono na miguu.

Sasa suala la matibabu na huduma zinazotolewa kwenye makambi, hilo ni suala lingine ambalo naamini kwenye maswali yaliyopita, tulieleza juu ya huduma zinazotolewa kwenye Makambi ya kutunza Wazee yakiwemo makambi ambayo yana wagonjwa wa Ukoma. Kutokana na ukweli kwamba Tanzania imepiga hatua sana na miongoni mwa nchi zinazoendelea kutokomeza ugonjwa wa Ukoma, kwa kufikia lengo la Kimataifa la kuwa na Mgonjwa mmoja katika kila watu 10000, tunakoelekea siyo kubaya. Dalili zinaonyesha tunakoelekea ni kuzuri na mazingira yanaonyesha tunatoa matibabu bora na sahihi na ugunduzi uko hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna waratibu wa huduma hizi za Kifua Kikuu na Ukoma nchi nzima na katika kila Wilaya ambaao wanazunguka na kufanya kazi hizi katika ngazi zetu za Vijiji na ngazi zetu za Kata.

Kwa hiyo, naamini katika eneo hili eneo la ufahamu pamoa na matangazo ambayo yanatolea kwenye TV basi naamini watendaji hawa wataongeza nguvu, ili angalau wagonjwa hawa waweze kugundulika zaidi kila mara wanapojoitokeza ili tuendelee kupiga hatua ya kutokomeza ugonjwa huu wa Ukoma. (*Makofii*)

Na. 250

Vumbi Litokanalo na Upasuaji Mbao

MHE. JOSEPH R. SELASINI aliuliza:-

Kwa miaka mingi Wilaya ya Rombo imekuwa ikivuna miti kwenye Msitu wa Rongai na kupasua mbao ambazo zimekuwa zikiwanufaisha wananchi na nchi jirani, lakini kwa kiasi kikubwa vumbi linalotokana na mbao hizo kutupwa au kuchomwa moto.

(a) Je, Serikali haiwezi kutumia vumbi hilo kutengeneza vifaa mbalimbali kama *chipboard*, vidonge vyaa mkaa kwa matumizi mbalimbali ya nyumbani na viwandani?

(b) Je, Serikali haioni ikianzisha viwanda vy a kutumia vumbi la mbao itasaidia kutoa ajira kwa vijana?

(c) Je, kupitia utafiti wa *SIDO* na kampuni nyingine nchini uanzishaji wa viwanda hivyo unawezakana hapa nchini au ni lazima kupata msaada kutoka nje?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selasini J. Roman, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu a, b na c, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuwa vumbi linalotokana na mbao linaweza kutumika kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa matumizi ya nyumbani pamoja na viwandani kwa kutegemea malighafi na bidhaa kama vile vidonge vy a mkaa (*Briquettes*), *chipboard*, samani, vizibo vy a chupa na vifaa vingine vy a nyumbani na viwandani.

(b) Mheshimiwa Spika, hivi sasa viwo viwanda kadhaa ambavyo vimekuwa vikitimua vumbi la mbao kama malighafi ya kutengeneza bidhaa mbalimbali, kwa mfano, kiwanda cha *Fiberboard* kilichoko Arusha, kiwanda cha Tanzania *Chipboard* kilichoko Tanga vinafanya kazi hii. Pia, viwo viwanda vidogo vinavyozalisha vidonge vy a mkaa kutokana na vumbi la mbao na mabaki ya mimea mingine.

Aidha, asasi nyingine kama *Kilimanjaro Industry Development Trust (KIDT)* ya Kilimanjaro, Nishati Poa Service ya Arusha na Mkaa Bora ya Tanga kwa kutumia huduma ya teknolojia ya kitimizi (*Incubator*) toka *TEMDO* ili kuzalisha vidonge nya mkaa pamoja na matumizi ya vumbi hilo. Matumizi haya yote katika viwanda vikubwa na vidogo yataongeza ajira kwa vijana wetu.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia utafiti unaofanywa na *SIDO* pamoja na kampuni nyingine hapa nchini itaendelea kuboresha na kuongeza uzalishaji wa viwanda vidogo ili kutumia vumbi hili la mbao kwa ajili ya matumizi mbali mbali. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Viwanda vilivytajwa katika jibu la swali la msingi, vinapatikana Arusha na Tanga ambako hakuna misitu.

Je, Serikali haioni kwamba ni vyema ikahamisisha *SIDO* ili iweze kuwashauri wenye viwanda kujenga viwanda hivyo katika Wilaya ya Rombo au maeneo mengine ya nchi hii ambako misitu ya Serikali ipo kwa wingi?

Pili, nilitembelea *TEMDO* Arusha, mtambo unaotengeneza vidonge nya kuni zinazotokana na vumbi hili ni ghali sana.

Je, Serikali iko tayari kuwasaidia wananchi wa Rongai na Tarakea ili kuweza kupata mtambo huo kwa ajili ya kusindika vumbi hili ili liweze kuwa mbao na kusaidia vijana wetu kupata ajira?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Joseph Selasini, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni ajira kwa upande wa Rongai na Tarakea kupitia *SIDO*. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, hii inawezekana na nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine kwamba, tunajaribu kutumia fursa ambazo ziko wazi za *SIDO* zinazoweza kupatikana Kilimanjaro na kwa Wabunge wengine kila Mkoa kuna *SIDO* ambayo ina uwezo wa kubuni mambo mbalimbali ya kuweza kusaidia ajira na kipato kwa vijana.

Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kupitia *SIDO* Kilimanjaro, na sisi tutaoa msaada wa kuweza kuwaunganisha wote waweze kupata msaada wa ushauri ili waweze kuwa na viwanda hivi vya vumbi la mbao.

Kuhusu mashine au mitambo ya kuweza kuwasaidia wananchi wa Longai na Tarakea ni kwamba mimi niko tayari na Wizara yangu iko tayari, itasaidia sana kuwaunganisha pamoja na taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara kama vile *TIRDO* inayofanya utafiti wa mambo kama hayo na *TEMDO* kwa maana ya ufundi ili kuweza kuwaunganisha na kupata mashine au mitambo mbalimbali ya kusaidia maeneo haya ya Rongai, Tarakea na sehemu mbalimbali nchini. (*Makofii*)

Wakulima wa Korosho Kutafutiwa Soko la Korosho

MHE. FAITH M. MITAMBO aliuliza:-

Kwa muda wa takribani miaka mitatu sasa wakulima wa korosho wameshindwa kuuza korosho zao wakati wa msimu:-

(a) Je, Serikali inawasaidiaje ili waweze kuuza korosho zao kwa wakati?

(b) Je, kama mfumo wa ununuzi wa korosho haufai, kwa nini Serikali isifikirie mfumo mwingine wa kuuza korosho za wananchi kwa haraka?

(c) Je, kwa nini Serikali inaendelea kutoa leseni kwa wafanyabiashara ambao wanagoma kununua korosho hizo na kuleta athari kubwa kwa wakulima?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faith M. Mitambo Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2012/2013, kiasi cha korosho Wilayani Liwale iliyofikishwa kwenye maghala, ni kilo 5,570,000, ambapo hadi kufikia tarehe 30 Machi, korosho yote ilikuwa imeuzwa kwa bei katika shilingi 1350 na 1435 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa changamoto mbalimbali, Serikali kuitia Bodi ya Korosho na Balozi zetu nje ya nchi, inaendelea na jithada za kutafuta wanunuzi wa korosho katika maeneo mbalimbali duniani ili kuondoa ukiritimba wa kuwa na soko moja tu la India.

(b) Mheshimiwa Spika, mfumo unaotumika katika kuuza korosho ni ule wa Stakabadhi Ghalani. Mfumo huu ulifanikiwa kumnufaisha mkulima katika miaka miwili ya kwanza lakini hivi sasa umekumbwa na matatizo, unapigwa vita na baadhi ya wanunuzi, watendaji wa vyama vya ushirika na maghala pamoja na wasafirishaji wa mazao ambao wanalenga kumlipa malipo madogo mkulima.

Mheshimiwa Spika, ili kurekebisha kasoro hizo, Serikali inakusudia kuleta marekebisho ya Sheria yatakayolenga kuondoa bugudha na kasoro hizi ndani ya mfumo wa Stakabadhi Ghalani ili kulejesha malipo mazuri zaidi kwa mkulima na pia kulejesha imani ya mkulima katika mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inafanya mapitio ya mjengeko wa bei ndani ya korosho (*price structure*) unaotumika sasa hivi wenyе makato mengi ambayo yanaweza kupunguzwa ili kumnufaisha mkulima.

(c) Mheshimiwa Spika, katika utaratibu huo uliopo, wanunuzi wanaotaka kununua korosho, ni sharti wapate leseni kutoka Bodi ya Korosho ya Tanzania kabla ya kushiriki kwenye mnada wa mauzo. Ni kweli wapo baadhi wanunuzi wenyе lengo la kulipa bei ndogo kama tulivyowataja, isiyomnufaisha mkulima na wakati mwingine, wanafanya hivyo kwa kushirikiana na watendaji wa vyama vya ushirika wasio waaminifu ili kutimiza azma yao. Wafanyabiashara wa aina hiyo hawatapewa tena leseni ya kushiriki katika biashara ya zao la korosho.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Siku za hivi karibuni, wakulima wa Wilaya ya Liwale wamelipwa shilingi 200/= badala ya shilingi 600/= walizoandikiwa kwenye stakabadhi zao. Kwa madai kwamba korosho zimeuzwa chini ya bei elekezi ya shilingi 1200/. Je, Serikali iko tayari sasa kuwafidia wakulima wa Liwale shilingi zao 400/= na hasa ukizingatia kwamba wamelipwa shilingi 200/= ambazo haziwezi kuwasaidia kutayarisha mashamba yao kwa msimu huu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari sasa kukaa na Chama cha Msingi cha llulu kufanya ukaguzi wa mahesabu upya na kuondoa makato yale yote yasiyo ya lazima ili kuweza kupata fedha za kuwafidia wakulima wa Liwale shilingi zao 400/=? (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi, jibu lenyewe ilikuwa refu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, hili la kufidia bei ya korosho kwa shilingi 400/= tumelisema katika nyakati mbalimbali na siyo tu kwa zao la korosho, ila ni kwa mazao yote ambayo yanategemea mwenendo wa soko.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni gumu sana kulitekeleza kwa sababu bajeti yake siyo kwa Liwale tu, lakini itajumuisha maeneo mengine, pamoja na wakulima wa Mkuranga wale ambao wakati wanauza mazao yao, bei ya korosho ilikuwa imeshuka kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nachelea kulichukulia ahadi kwa sababu ninajua ugumu wake wa kulitekeleza na *implications* zake kwa mazao mengine pia, lakini kama tulivyosema, tunachoweza kufanya, ni kuangalia ule mchakato wa bei, kwenye ile 1200/= bado kuna 292 ambazo ni makato kwa watu mbalimbali. Ile tunaweza tukapunguza ili katika ile 292 tukiangalia, sehemu ya hiyo, badala ya kwenda kwa vyama vyaya ushirika na vyama vikuu na kadhalika na Halmashauri, zikapunguzwa, zikaenda kwa mkulima moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la Chama cha Msingi cha llulu, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Faith, Mheshimiwa Mbunge wa Rwanwa na wa Nachingwea, wamefanya maamuzi ya makusudi watu wao ya kujitenga kwenye chama cha llulu na kutengeneza Chama chao cha Msingi. Sasa katika hili kwa sababu mtakapogawana chama cha msingi, pia mtatakiwa kutenga mahesabu yao, mimi naomba nikuhakikishie tu kwamba Idara ya Ushirika ya Wizara

21 MEI, 2013

ya Kilimo, Chakula na Ushirika, itasaidiana na ninyi katika kusimamia zoezi hili ili kila mtu apate haki yake stahili.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed swali linalofuata, kwa niaba yake Mheshimiwa Rashid Ali.

Na. 252

Uzalishaji wa Mchele na Mahindi Mwaka (2005-2010)

MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED aliuliza:-

(a) Je, katika kipindi cha mwaka 2005-2010 nchi yetu imezalisha nafaka ya mchele na mahindi kiasi gani?

(b) Je, Serikali ililagiza tani ngapi za mchele na mahindi kutoka nje kwa mwaka katika kipindi cha mwaka 2005-2010?

(c) Je, katika kipindi hicho Serikali imesamehe kodi kiasi gani kwa kila nafaka iliyouzwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005-2010, nchi yetu imezalisha jumla ya tani 5,900,000 hivi za nafaka ya mchele na tani 21,300,000 za mahindi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005-2010, uzalishaji wa nafaka nchini ulikuwa wa kutosheleza kwa kiwango cha kuridhisha, kiwango kikubwa tu. Hata hivyo,

mwaka 2008 kulitokea upungufu wa nafaka ya mahindi wa takribani tani 300,000, hali iliyofanya Serikali kuruhusu wafanyabiashara kuagiza mahindi nje ya nchi bila kulipia ushuru. Aidha, kutokana na bei ya mahindi nje ya nchi, katika masoko ya dunia kuwa kubwa, kwa maana ilipanda kwa wastani wa kutoka dola 200 hadi 240 kwa tani moja. Kiasi kilichoingizwa nchini, kilikuwa jumla ya tani 10,000 tu kwa sababu waagizaji walishindwa ku- *cope* na ile bei kubwa, katika kipindi hicho hakukuwa na upungufu mkubwa wa mchele.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 (*The East African Customs Management Act, 2004*), mahindi ni mojawapo ya bidhaa muhimu (*sensitive products*) ambayo hulipiwa ushuru wa asilimla 50. Kwa hilo, kutokana na zile tani 10,000 zilizoingizwa mwaka 2008, jumla ya shilingi 1,200,000/= zilisamehewa na Serikali kama kodi iliyostahili kulipwa.

(c) Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumiwa na Serikali katika kuagiza nafaka toka nje ni pamoja na uzalishaji wa nafaka unapokuwa mdogo humu ndani ikilinganishwa na mahitaji yetu, bei kubwa ya nafaka inayosababisha wananchi wengi wa kawaida kutokumudu bei ya soko na nafaka nyingi inayozalishwa nchini kuuzwa nje kwa kiasi kikubwa.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali madogo mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Naibu Waziri, anasema moja ya sababu kuu ya kuagiza nafaka nje ya nchi, ni nafaka nyingi ndani ya nchi kuuzwa nje ya nchi. Kwa nini Serikali inaacchia nafaka hizi ndani ya nchi ziuzwe na badala yake unaagiza nafaka nje ya nchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, dhana kuu ya Kilimo Kwanza ni kuhakikisha kwamba nchi inapata chakula cha kutosha, inapata chakula cha akiba na inapata chakula cha kuuza nchi za nje. Kwa nini leo Serikali inaangiza zaidi ya tani 300,000 nje ya nchi, haoni kwamba hii dhana ya Kilimo Kwanza inahitaji kufanyiwa marekebisho na *ime-fail* kwa wakati huu? (*Makofij*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, haukumwelewa sehemu ya pili?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza hili la nafaka kuuzwa nje, hili ni katika utaratibu wa kufungua masoko kwa ajili ya kumpa manufaa zaidi mkulima. Wakulima wa Tanzania kwa kiasi kikubwa, kama wale wa Rukwa, wao walikuwa wanazalisha mahindi, mnunuzi mkuu alikuwa *NFRA*, tunamlipa 350, wakitoka watu nje wanamlipa 500. Sasa tulichofanya ni kwamba tumefungua milango hiyo ili wale wakulima waliokuwa wanazalisha mahindi wanayauzu 350, wamepata motisha zaidi ya kuzalisha zaidi. Ni kweli kwamba mahindi ambayo tulikuwa tunazalisha tani milioni tatu mwaka 2007, leo tunazalisha tani milioni 5.2. Kwa hiyo, lile zoezi la kufungua milango limewapa hamasa zaidi wakulima pamoja na hatua zingine ambazo Serikali inachukua. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, hili la pili, kwamba dhana kuu ya Kilimo Kwanza sijui, kwanza hatujawahi kuagiza tani 300,000, ni kwamba tulifungua milango kwa sababu ndiyo ilikuwa *deficit* wakati huo, lakini tumesema kwamba zilizoingizwa ni tani 10,000. Katika hali hii, wakati wowote ule, kwa sababu kwenye mfumko wa bei, mambo mawili yanayopiga uchumi wa Tanzania ni mafuta na chakula, tukiona kwamba chakula kimezidi sana bei, wale Watanzania wanaotumia chakula kile kwa kukinunua, wanashindwa kukinunua. Kwa hiyo, kwa maana hiyo kama mchele ukifika 2800, mahindi yakifika 1500, bado tutalazimika kuleta mchele wa bei nafuu ili kushusha bei na uchumi wetu uweze kuhimili mfumko huo na ongezeko hilo la bei. (*Makofij*)

SPIKA: Ahsante sana. Muda wa maswali umekwisha. Naomba nizungumzie shughuli za kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Magreth Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa Saba mchana watakuana katika chumba Na. 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na Kikao chao chumba Na. 219.

Mheshimiwa Mnyika, lakini tusitumie muda mwingi kwa sababu tunatumia muda vizuri.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa idhini yako naomba kutoa hoja, kwa mujibu wa Kanuni ya 55(3)(a), juu ya hoja ambayo inaweza kutolewa bila taarifa ya kutengua Kanuni yoyote kati ya Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, Ibara ya 100(1), inatamka madaraka na haki za Bunge kwamba kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania au katika Mahakama au mahala pengine popote rje ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naamini hoja hii nitakayoitoa kwa maneno machache Wabunge wenzangu wataiunga mkono kwa kusimama, ili Bunge hili liweze kufanya vizuri zaidi kazi yake kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya nchi yetu ya kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuitoa hoja hii, ni yaliyojiri na yanayoendelea kujiri kwenye Bunge letu hili juu ya mjadala unaohusu Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, juu ya kukithiri kwa masuala ya matukio yanayowahusu wanahabari ya utekaji na utesaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya jambo hili kuwa muhimu sana, ninaomba nitoe hoja sasa, ili Bunge lako litengue Kanuni ya 64(1)(c), inayosema kwamba, Mbunge hatazungumza jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa uamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia, na ambalo halikuletwra rasmi kwa njia ya hoja mahsusni na vilevile hatapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge, isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahsusni inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja, Kanuni hii itenguliwe ili Wabunge waruhusiwe kuchangia katika mjadala kwa mambo yanayohusu kuihoji Serikali kutekeleza Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kuhakikisha Askari waliohusika na mauaji ya Ndugu Mwangosi, kwa maana ya Askari ambao hawako Mahakamani kama Kamanda Kamuhanda wanachukuliwa hatua, ili kuepusha vitendo vinavyoendelea vya utekaji na utesaji wa Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, ili matendo ya watu kama kutekwa, matukio ya watu kama Kibanda na matukio mengine yasiendelee, ni vizuri Bunge hili likajadili jambo hili. Naomba kutoa hoja na ninaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja za namna hii haziungwi mkono, kwa hiyo tunaendelea na kazi. (*Kicheko*)

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka
2013/2014 - Waziri Wa Habari, Vijana,
Utamaduni Na Michezo**

(Majadiliano yanaendelea)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu kuhusu hoja inayoendelea. Ninayo mambo machache, kwanza naiunga mkono hoja, lakini nina mawazo ambayo ninaweza kuyatoa katika kuboresha hoja yenyewe na nitazungumza mambo mawili au matatu.

Mheshimiwa Spika, moja ni juu ya uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kueneza habari. Kila mtu anaruhusiwa kutoa habari. Katiba ya Jamuhuri ya Muungano Ibara ya 18, inatoa uhuru huo wa kupokea na kusambaza habari, lakini Ibara ya 19(3), inaweka masharti juu ya jambo hilo. Inasema hifadhi ya haki zinazotajwa katika Ibara hii, itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria, ambazo ni muhimu katika jamii za kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa Taifa. Hilo ni sharti katika kueneza habari. Katika suala zima la demokrasia, suala kubwa ni habari, ni mtu kusikilizwa na kutoa habari au mawazo na kwamba wachache wanapewa haki ya kusikilizwa na mtu anasikilizwa bila kujali anapendwa au hapendwi, kinachomaanisha hapa ni kwamba wewe unachotakiwa ni kutoa habari, sura yako haiwezi kuwa habari, lakini maneno yako yanaweza kuwa habari. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini mjadala katika demokrasia, lazima uzingatie Kanuni na Sheria, kwa sababu kama uhuru tu utakuwa unakuwa uhuru bila Kanuni na bila Sheria, sasa ule uhuru hauwezi kuwa uhuru, utakuwa ghasia kwa sababu uhuru lazima uwe *managed*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunao uhuru wa kutoa mawazo, wa kusikilizwa, lakini lazima tuwe na uhuru vilevile wa kutekeleza maamuzi tunayoyafanya wenyewe. Nidhamu katika utekelezaji ni jambo la lazima katika demokrasia, demokrasia itakuwa haina maana tena na wala maendeleo hayawezi kupatikana chini ya mfumo wa demokrasia ambayo haina nidhamu.

Mheshimiwa Spika, nimeyasema hayo kwa sababu inaonekana kama tuna rudiarudia mambo yaleyale ambayo tunayasema, tunajiwekea Kanuni, tunavunja wenyewe. Tulipitisha juzi Azimio, zuri sana, tena liliungwa mkono na vyama vyote ndani ya Bunge letu, kwamba tuiongoze jamii yetu iondokane na mfumo unaoweza kuleta mfarakano katika jamii. Mimi nadhani tuki- *maintain* hapo, bila hata maelezo zaidi, inatosha kwa sababu lazima tuwe Taifa, lazima nchi yetu longozwe na lazima ikubali kusikilliza Bunge hili na liwe na mambo ambayo hayawezi kuvunjwa kwa sababu ambazo hazina msingi.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vyombo vyahabari na mara nyangi sana tunesikia malalamiko juu ya uhuru wa vyombo vyahabari. Mimi sina hakika sana, kama kweli Tanzania sisi tuko nyuma sana katika uhuru wa habari, mimi siamini sana maana sisi Tanzania ili uweze kutuhukumu lazima utulinganishe na nchi nyagine, unatulinganisha na nani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuko katika Jumuia ya Afrika Mashariki, tuko Afrika, labda tuache dunia, lakini Afrika tu hapa. Tanzania katika Afrika hii, ndiyo nchi peke yake ambayo ina magazeti 13 yanatoka kila siku na habari ni zilezile, kila mtu anaandika kichwa chake cha habari, maana haziwezi kuwa nyangi hivyo kila gazeti likawa na habari yake, lakini kila siku yanatoka magazeti 13, kati ya hayo matatu ya Kingereza na 10 ya Kiswahili. Vilevile kila wiki kuna magazeti siyo chini ya 62 na majorida kibao. Kuna magazeti 781 yameandikishwa, mengine hayatoki yanashubiri kutoka siku nyagine. Mimi nadhani, kama ingekuwa kuna kuminya uhuru wa habari, haya mambo yote yasingewezekana kuwepo.

Kwa hiyo, mimi nasema na naamini tunao uhuru wa habari.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini uhuru wa habari nao ni kipimo, ni *relative*, unalinganisha na nani, ukienda Muhimbili pale kila mtu ni mgonjwa lakini kuna wagonjwa zaidi, wengine mahtuti. Sasa ukitaka kulinganisha, unaweza ukalinganisha tu, ukasema huyu ni mgonjwa, lakini huyu ni mgonjwa zaidi. Sasa unaposema hapa hakuna uhuru wa habari, unalinganisha na nani.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kulisema hilo kwa sababu mimi nadhani tunajitahidi na niweze kuviasi tu vyombo vyaa habari vijitahidi kutumia weledi, kwa sababu ni *professionalism*, lazima ihakikishe inaonekana. Mimi nadhani wanajitahidi, lakini wakati mwingine wanaandika mambo nusunusu halafu wanafanya jamii inapata tabu kidogo kuelewa. Kwa mfano, juzi tarehe 19 Mei, Wabunge wa CCM wataniunga mkono tulikuwa na kikao, mambo mengi sana yamesemwa, lakini gazeti linaandika mambo ambayo hayakusemwa yaliyosemwa hayakuandikwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa siwezi kuwalaumu maana hawakuwemo, nadhani kuna mtu aliwapa taarifa nusunusu hivi, sasa wangefanya utafiti ili wajue zaidi, lakini nusu nusu ile haiwezi kutusaidia sana. Mimi nataka niseme kwamba, kwa sababu mimi siyo msemaji wa Chama cha Mapinduzi wa jambo hili, inawezekana Chama kitasema sasa, maana hatukufanya siri pale. Watanzania wanaweza kuelezwa tulisema nini ili tuelewe vizuri na waache kupokea habari ambayo ni nusunusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo ningewashauri vyombo vyaa habari, ni kuandika habari za kweli tu, ziwe mbaya, ziwe nzuri lakini ni za kweli, hakuna haja ya kuficha kama ukweli upo lakini kuandika tu habari ambazo siyo za kweli halafu ukaziiza, hiyo nayo vilevile nadhani siyo sawa. Mimi mwenyewe nimepata kuathirika na hili. Gazeti moja, sitaji leo gazeti kabisa liliwahi kuniandika

nimeenda Geita nikafukuzwa na siku hiyo wanaandika mimi nilikuwa kwenye ndege nikitokea Arusha kwenye mazishi ya Askofu wa KKKT. Sasa nikajiliza nimefukuzwa kwenye msiba wa Askofu au nimefukuzwa Geita? Baadaye asubuhi nadhani kwa sababu waliningizia mimi pamoja na *Inspector General*, wakaandika harakaharaka, kumradhi, kumradhi, nadhani waliogopa kofia ya *IGP*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo napenda kulisemea, linahusu ajira kwa vijana. Hapa kwenye Wizara hii wamesema kuna shilingi 3,000,000,000/= na kuna mtu anasema shilingi bilioni tatu haziwezi kuwaajiri vijana 16 milioni, mimi ninadhani hii siyo sawa. Vijana ni kweli hawana ajira lakini huwezi kusema Sh.3,000,000,000/= ndizo zitakazo-*solve problem* ya vijana 16 milioni, hii ni *exaggeration* ya ajabu kidogo. Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, umeweka *provision* ambayo itazalisha ajira katika sekta zote. Kuna sekta za viwanda, kuna sekta ya kilimo, kuna sekta ya ujenzi, kuna sekta ya uchukuzi, zote hizi zitazalisha ajira, haziwezi kuwaajiri vijana wote wa Tanzania. Hakuna nchi ambayo imeweza hiyo lakini jitihada zitaonekana siyo kwa shilingi bilioni tatu zilizotengwa katika Wizara hii lakini kwa sekta nzima na uchumi mzima wa nchi kadri unavyokuwa na mpango wetu unatekelezwa ajira kwa vijana lazima zitapatikana. Kiasi gani, zimewekwa kwenye Mpango wa Maendeleo, sina muda wa kueleza, lakini nina imani ziko huduma nydingine nydingi sana ambazo zitatolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi shilingi bilioni tatu ninavyojua mimi, ni za kusaidia vijana wanaoanzisha vikundi vya kujajiri, kwa mafunzo na mitaji. Vilevile Serikali iko tayari kuwasaidia na kuwawekea dhamana ya benki maana fedha za kuingiza watu katika ajira siyo lazima zote zitoke kwenye bajeti ya Serikali, nydingine lazima zitoke katika mabenki na kama ni vigumu kupata Serikali tuingie mle ndani tuhakikishe kwamba benki zinapata dhamana na vijana wetu wanakopeshwa na wanafanya kazi za kujajiri na kuajiri wenzao. Mimi nadhani hili ndiyo jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitegemea vilevile rafiki zangu wa CHADEMA watatupa mawazo basi hawa vijana tunawajirije maana ile ndiyo inaitwa *constructive opposition*. Unatuambia hili hamfanyi vizuri, vizuri ni hivi maana kulalamika vilevile siyo *solution*. Huwezi kulalamika tu halafu watu wakaajiriwa, watu hawawezi kuajiriwa kwa kulalamika, toa mawazo tufanye nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tutoe mawazo *constructive kwamba* sisi *government in the waiting* ingekuwa sisi sera yetu ni hii. Sera yenu haiwezi kuwa ni kulalamika peke yake, kulalamika haiwezi kuwa sera. Kwa hiyo, nawashauri lazima mtoe mawazo yanayosaidia nchi na msitoe mawazo ambayo yanaifanya nchi iwe inatetemeka, inagombana, kugombanisha nchi siyo sehemu ya sera. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi na atafuatiwa na Mheshimiwa Nassib Omar.

MHE. JADDY SIMAI JADDY: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mimi ninauelekeza katika mambo mawili tu yaani ajira kwa vijana pamoja na vyombo vyta habari. Ingawaje Mheshimiwa Wasira kwa kiasi fulani ameishanifilisi mawazo yangu lakini hata hivyo nami nitapata la kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana ni jambo la msingi sana. Tumekuwa kila mara tukisema kwamba vijana ndiyo Taifa la leo haidhuru zamani tulikuwa tukizungumza kwamba vijana ndiyo taifa la kesho lakini sasa hivi tumebadilisha na kusema kwamba vijana ndiyo taifa la leo. Hii ni kweli kabisa.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali itatoa kipaumbele kwa vijana, mimi naamini kabisa kwamba matatizo ya vijana kwa kiasi kikubwa tuyaweza kuyaondoa, ajira kwa vijana inaweza kupatikana. Iwapo Serikali itaweka kipaumbele kwa vijana na kuweka bajeti kubwa kwa vijana, naamini hiyo ajira itapatikana.

Mheshimiwa Spika, Nabii Suleiman alikuwa na miujiza fulani, mojawapo ni kutambua lugha za wanyama, wakiwemo ndege. Siku moja katika msafara wake Nabii Suleiman alifika sehemu akawakuta ndege wawili, moja jike na mwingine dume. Ndege dume alikuwa akimshawishi ndege jike kubali nikuo nitakujengea nyumba Syria. Nyumba yenyele ilikuwa ni ya nyasi. Maaskari walimuuliza Nabii Suleiman, kwa sababu walimuona Nabii Suleiman anacheka, mbona Nabii unachecha kuna nini? Akasema kama mngetambua wale ndege wawili wanazungumza kitu gani basi hata nanyi mngelicheka pia. Akawaambia yule ndege dume anamshawishi ndege jike, anamwambia amjengee nyumba Syria amkubali amuo. Hivyo ndivyo inavyotokezea kwa vijana. (*Makofii*)

Mheshimwia Spika, vijana wameahidiwa kupata ajira lakini mpaka leo vijana bado ajira yao imekuwa ni ngumu. Kila siku huwa tunapiga makelele kutengeneza mazingira mazuri ya kupata ajira vijana lakini imekuwa kila inapokuja bajeti, tunakuwa tunajadili vipaumbele ambavyo si vya kuwakomboa vijana. Iwapo tutakuja kukaa kitako kujadili vipaumbele vya kuwakomboa vijana, naamini kabisa ajira wataipata na hiki kishindo cha vijana kuingia mitaani na katika maandamano kitatoweka kwa sababu vijana wanataka ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi vipaumbele ambavyo tunakuwa tukivijadili humu Bungeni mara kwa mara haviwasaidii vijana. Kujenga miundombimu ya barabara, hospitali, vijana haya siyo hamu yao. Hamu ya vijana ni ajira kwa sababu hata ukijenga hizo barabara ambazo haziwasaidii vijana sijui itakuwa ni kipaumbele cha namna gani ambacho tumekifikiria, hakipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kujadili kipaumbe cha mwanzo kabisa kwamba iwe ni ajira kwa vijana. Kama tunakusudia kutengeneza miundombinu au kutengeneza mazingiza ya ajira kwa vijana basi iwe ni kweli kwamba tunataka kutengeneza mazingira ya ajira kwa vijana. Vinginevyo vijana siku zote wataendelea kulalamika hawana ajira na Serikali tutaendelea kuwalaumu vijana kwamba kuwa hawatulii wakati hatuwapatii ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo ninataka kulizungumza ni kuhusiana na vyombo vyahabari. Vyombo vyahabari haidhuru, baadhi yetu tumekuwa tukiteeta sana humu ndani lakini kwa kweli katika jambo ambalo linaipeleka pabaya nchi hii, ni baadhi ya vyombo vyahabari. (*Makofi*)

Mheshimwia Spika, imekuwa sasa hivi ni kawaida kwa vyombo vyahabari kuandika maovu tu, wanasema wao ndiyo kioo cha jamii lakini ni kioo cha jamii cha kuandika maovu, mazuri siyo kioo cha jamii, sasa nashindwa kuelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hakutakuwa na utaratibu wa kuweza kuvidhibiti baadhi ya vyombo vyahabari, nchi hii inaelekea kubaya. Nchi hii inaelekea kubaya na sote tunakumbuka yaliyotokea Rwanda. Tukiamini kabisa kwamba yaliyotokea Rwanda yalisababishwa na baadhi ya vyombo vyahabari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara ianzishe Sheria ya kujaribu kuvidhibiti baadhi ya vyombo vyahabari. Imekuwa kila wakati vyombo vyahabari vinadai uhuru, hatuwezi kutambua ni uhuru wa namna gani ambaovinadai. Kama imefika wakati vyombo vyahabari vinaandika maneno ya kashfa mpaka kwa Mkuu wa Nchi na Serikali imenyamaza kimya, hawaviingilii, wanandika watakavyo na bado wanaendelea kusema kwamba bado hawako huru. Sasa sijui wanataka uhuru wa namna gani?

Mheshimiwa Spika, mimi ni msomaji mzuri sana wa vitabu vya riwaya. Niliwahi kusoma kitabu kimoja kinachoitwa ‘Adili na Ndugu Zake.’ Mhusika mkuu alikuwa ni Adili. Adili alikuwa na ndugu zake wawili. Kuna wakati walimfanya maovu, wakaadhibiwa. Adhabu waliyopewa waligeuzwa maumbile. Akapewa kazi Adili sasa ya kuwashikisha adabu, ya kuwaadhibu ndugu zake. Aliwafungia katika chumba, ikawa kazi yake kubwa kwa kila siku anaenda akiwapiga mjeledi lakini kabla ya kuwapiga alikuwa akiwapelekea chakula na vinywaji mbalimbali na wakati akiwaadhibu alikuwa anatokwa na machozi. Maneno aliyokuwa akiyazungumza ninapenda kuyanukuu na kama itakuwa sivyo, Mheshimiwia Muhammed Seif Khatibu, aliyewahi kuwa Mwalimu wangu wa Kiswahili, atasema haya sivyo yalivyokuwa. Adili wakati akiwaadhibu ndugu zake wakiwa katika maumbile mengine, alikuwa akisema hivi. “Nala sumu ndugu zangu, msambe naona tamu. Takallfu kubwa kangu kudhulumu yangu damu. Sina raha ndugu zangu neno hili kwangu gumu.”

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari tunavihitaji lakini kwa kuviaachia vifanye wanavyotaka, vitatufikisha pabaya. Lazima vyombo vya habari vidhibitiwe. Wao habari ni za maovu tu, nzuri hakuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, humu Bungeni ni rahisi kutambua habari ya kesho ndani ya vyombo vya habari itakuwa namna gani. Tumeshazoea sisi wengine. Kwa mwenendo wa ndani ya Bunge unavyokwenda unajua kabisa kesho habari itakuwa ni hii kwa sababu tayari tunajua kabisa vyombo hivi vina mwelekeo wa namna gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni rahisi kulalama kusema kwamba sisi hatuna mwelekeo wowote wa kisiasa lakini ukweli wa mambo wakati unasoma habari zao, kuna haja ya kwenda shule kubwa sana, unatambua kabisa kuwa hivi ni vyombo vya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Waziri amesema kuna sheria inayotarajiwa kuletwa kuhusiana na vyombo vya habari.

Namwomba Waziri sheria iletwe, tujadili, kubwa likiwa ni kujaribu kuvidhibiti vyombo va habari. Rwanda baada ya yaliyowakuta pale, wameamua sasa kupeleka Muswada wa Sheria wa kudhibiti vyombo vya habari. Wakitaka kutambua sifa ya Mwandishi wa Habari iwe ya namna gani na habari ambazo zitakuwa zikiandikwa katika vyombo vya habari zижilikani zinatoka *sources* gani kwa sababu wameshaona yaliyotokea miaka ya 1990. Wametengeneza makumbusho pale kutohana na mauaji yaliyotokea kule na sisi kama hatutakuwa na tahadhari hiyo, tunaelekea kuja kutengeneza makumbusho yatakayotokea Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sina mengi zaidi isipokuwa ni hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilsemwa nitamwita Mheshimiwa Profesa Kahigi, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassib Omar na Mheshimiwa Sara Msafiri pia ajiandae.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja ya Wizara hii. Mengi yameshasemwa kuhusu mada nyingine, mimi nitachangia kuhusu utamaduni na lugha.

Mheshimiwa Spika, si mara yangu ya kwanza kuchangia mada hizi mbili, nimechangia huko nyuma na leo nitachangia tena kwa ajili ya kusisitiza lakini pia kwa ajili ya kutahadharisha. Nitaanza na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, ili nchi iendelee na kupata maendeleo ambayo ni endelevu lazima iwe na mkito imara wa kitamaduni. Nchi zote ambazo zimeendelea, ziwe nchi za Ulaya kama vile Uingereza, Norway, Finland hata nchi ndogo yenye watu 300,000 tu Iceland ina zina mkito imara wa kitamaduni.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere ambaye ni marehemu kwa hivi sasa kwa kulitambua hili alitamka kabisa toka mwanzo kwamba utamaduni ni roho ya Taifa. Miaka

mingi baadaye UNESCO katika Azimio lake la mwaka 2001 ambalo linahusu uanuwai wa kitamaduni duniani, nalo lilitambua umuhimu wa utamaduni. Nchi zote ambazo zimeendelea hivi karibuni ambazo ni pamoja na China, Malaysia ambayo sasa hivi tumeanza kuiiga na nchi nyingine za Mashariki ya mbali, nazo maendeleo yake yamejikita kwenye mkito imara wa kitamaduni. Mimi nataka kumuuliza Waziri, sisi Tanzania hali ya utamaduni wetu ikoje? Nasi tunao mkito imara wa kitamaduni au hatuna?

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuongezea hapo kudondoaa aya moja kutoka kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo, ambayo inasema kwamba kuna madhumuni ambayo yanapaswa kufikiwa, ukurasa wa tano. Taifa hili linapaswa kuwa na misingi ya kujitegemea inayotokana na mazingira ya ukombozi wa kisaikolojia, kifikra na kuweza kujiamini ili jamii iweze kuamua na kuliongoza gurudumu lake la maendeleo kwa lengo la kutosheleza mahitaji ya msingi ya watu wote, wanawake, wanaume na watoto. Je, jambo hili ambalo limetajwa katika Dira yetu, Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, inalitekelezaje? Kwa sababu limeachwa hivihivi tu. Bila kufanya hivyo huku kujiamini tunakokuzungumzia hapa, hakutatokea.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine mfano Uingereza, nchi zote za Ulaya na China, ambayo siku hizi tuiigalga, hata Malaysia, nimesomasoma kuhusu habari za Malaysia na utamaduni wake, zote zinatoa fedha nyingi sana katika kuendeleza utamaduni wake wa ndani lakini pia huko nje huwa zinaeneza utamaduni wake. Uingereza ina *British Council*, Ufaransa ina *Alliance France*, Ujerumanu ina *Goithe Institute*, Urusi ina Vituo vya Utamaduni vingi sana, hata Iran ina vituo vya utamaduni, kueneza utamaduni wake, nchini kwanza imeujenga ukawa imara lakini huko nje pia inataku kueneza. Hata India siku hizi, ukiangalia filamu nyingi sana ambazo watoto wetu wanaangalia ni za Kihindi. Siku hizi baadhi ya watoto wetu wanajifunza Kihindi kupitia filamu za Kihindi, sisi tumefanya nini? Kwa kutoa kasma ndogo kama hiyo sisi tutafanya nini? Hata Maafisa Utamaduni katika

Wilaya hawatambuliki. Idara ya Utamaduni katika Wilaya ilikuwepo zamani lakini siku hizi haipo, imeshafutwa kabisa. Naomba hilo Wizara ilichukue na ilifanyele kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Sera ya Utamaduni, kuna wakati kuliundwa Kamati ambayo ilikuwa inaandaa mpango wa utekelezaji wa yaliyokuwa kwenye Sera hiyo, huo Mpango Mkakati umefikia wapi na sasa hivi ni miaka zaidi ya miaka kumi? Halafu lile pendekezo letu kwamba Sera hiyo ifanyiwe marekebisho ikizingatia maendeleo ya baadaye ambayo yametokana na mazimio na matamko mbalimbali ya kimataifa, imefikia wapi katika uandaaji wake? Hilo la kwanza la utamaduni.

Mheshimiwa Spika, la pili nataka niongelee kuhusu lugha. Hili pia ni jambo ambalo kwa Serikali hii ni kwamba imekuwa iklenda mbele halafu inarudi nyuma, imekuwa ikiamua hili lakini inalitengua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni kama kwamba inachelea kuchukua hatua. Tumekuwa tukisema kwamba sababu za kielimu, sababu ya kiisumu na sababu mbalimbali za kizalendo zinatutaka tuanze sasa hivi kupanga mipango ya kuanza kutumia Kiswahili katika shule zetu kuanzia shule ya msingi mpaka chuo kikuu. Hiyo haimaanishi kwamba hapatakuwa na *International School*, zitakuwepo! Hizi ni za kimataifa zipo kila mahali, zitakuwepo! Hofu ambayo imekuwepo hata mionganoni mwa Wabunge wenzangu ni kwamba ukianza kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia basi utaua Kingereza na Watanzania tutakuwa nyuma ya Wakenya, Waganda na wengine, hapana!

Mheshimiwa Spika, tatizo la msingi ambalo nimeliona nilipokuwa Mwalimu kwa miaka hii yote ni kwamba Tanzania hatujui namna ya kufundisha lugha za kigeni. Mtu huwezi kumfundisha lugha kwa zaidi ya miaka 10 akawa hawezi hata kuandika sentensi sahihi, haiwezekani! Mimi nimesomea Marekani, watu wanajifunza lugha wanatoka Uarabuni, China, Japan na kwingineko wanajifunza Kingereza kwa

miezi minne wanaanza kusoma masomo kwa lugha hiyo, ni kwamba tupo nyuma sana katika mbinu za kufundishia lugha za kigeni. Hilo ndiyo tatizo la msingi. Kwa hiyo, tushughulikie tatizo hilo badala ya kukaa tu na hofu kuchukua hatua, hii hofu ndiyo inatufanya tubaki nyuma hata katika mambo mengine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Nassib Selement Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Sara Msafiri halafu Mheshimiwa Rebecca Mgodo atafuatia.

MHE. NASSIB SELEMAN OMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza tumshukuru Mungu sana kwa neema zake nydingi juu yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na tatu naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niungane na Serikali kwanza kusema kwamba Serikali haijashiriki kabisa kung'oa watu kucha, meno, kuwatoboa macho au kuua watu...

SPIKA: Naomba uondoe maneno hayo!

MHE. NASSIB SELEMAN OMAR: Mheshimiwa Spika, la pili, napenda sana kumpongeza Waziri kwa kuendeleza utamaduni wa Mtanzania na Waafrika na anatoa darasa tosha kwa akina mama wote wa Tanzania kwa kuendeleza hasa usukaji asilia wa akina mama. Akina mama wengi wameacha kabisa kufuata mila hii na utamaduni huu. Kwa

hiyo, tuna haki ya kumpongeza na yeye kweli ni Waziri wa Utamaduni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita zaidi kuzungumzia *TBC*. Tulipongeze sana Shirika la *TBC* kwa kutoa huduma ya utangazaji kwa nchi nzima lakini vilevile kwa ukweli na uhakika. Kazi wanayofanya ni kubwa, matatizo ni mengi lakini kwa juhudii yao wanayakabili matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, redio vilevile inafanya kazi nzuri na tukiangalia nyuma tutaona redio yetu imechangia sana katika kutoa elimu kwa wananchi na vilevile imechangia katika kukuza lugha ya Kiswahili na hali kadhalika zimesaidia sana katika ukombozi wa nchi za Kiafrika ambazo zilikuwa zikitawaliwa. Nchi kama Afrika Kusini, Mozambique na Zimbabwe, zote zilikuwa zikifuautilia sana matangazo ya redio Tanzania na zillhamasisha watu kugomboka katika ukoloni huo. Kwa hiyo, lazima tuienza sana na tuithamini kwa kazi kubwa ambayo imefanya.

Mheshimiwa Spika, lakini mbali ya hayo tulikuwa na Watangazaji wazuri katika miaka ya 1960, 1970 na 1980 ambaao walikuwa wakifanya kazi nzuri katika *TBC* na walipokuwa wakitoa matangazo au habari katika Tanzania na Afrika na Afrika Mashariki wote walikuwa wanapenda kuwasikiliza kutokana na lafudhi yao nzuri na namna walivyokuwa wakisoma vizuri taarifa zao. Kwa hiyo, ni vizuri leo tunapozungumzia redio Tanzania basi na wao tuwakumbuke. Baadhi yao ni Selemani Hega, David Wakati na wengine. Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Watangazaji hawa walitoa huduma kubwa kwa nchi yetu, sasa hivi ni muhimu vilevile katika kutafuta Watangazaji basi tutafute Watangazaji wenye vipaji kama hawa, wapewe mafunzo ili waendeleze kazi hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TBC* linakabiliwa na matatizo mengi sana, *TV*na redio zote zina mitambo ambayo

imechakaa, ni ya muda mrefu na kwa kweli sasa hivi haifanyi kazi vizuri. Kwa hiyo, inabidi tufanye juhudii sana ili tuhakikishe kwamba mitambo hii yote inabadiishwa ili radio na *TV ziweze* kufika kote ambapo sasa hivi hazifiki.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kwamba sasa hivi radio haifiki katika Mikoa tisa na Wilaya kama 82 na tatizo kubwa hasa ni uchakavu wa mitambo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itoe sasa hivi hizo shilingi bilioni 11.15 ili waweze kununua mitambo ya radio, mitambo ya *satellite* na waweze kuweka *studio* mpya yenyewe kutumia digitali ili waweze kututangazia vizuri.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo nakwenda katika madeni ya Shirika. Taasisi mbalimbali zinadaiwa na Shirika hili pamoja na Wizara za Serikali. Mwanzoni mwa mwaka Taasisi zilikuwa zinadaiwa shillingi milioni 845 katikati hapa zimelipa shillingi milioni 302 na sasa hivi zinadaiwa shillingi milioni 548. Wizara za Serikali mbalimbali zilikuwa zikidaiwa shillingi bilioni 1.9 lakini zimelipa shillingi milioni 135 tu ambayo ni sawasawa na 7% na hivi sasa Wizara zinadaiwa shillingi bilioni 1.672, jumla ya madeni yote ambayo Shirika hili linadai ni shillingi bilioni 2.216. Hizi ni pesa nyingi na lazima Taasisi na Wizara zilipe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri mimi namna ya kuzipata hizi pesa harakaharaka kwanza wadaiwa wote wachapishwe katika magazeti waonekane ili watu wote wajue kwamba wanadaiwa na hii itasaidia ulipaji. Aidha, baada ya bajeti, Wizara zote ambazo zinadaiwa zikatwe *OC* zao moja kwa moja na pesa hizi zipelekwe *TBC* ili *TBC* iweze kwenda mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *TBC* vilevile inadaiwa, hivi sasa inadaiwa zaidi ya shillingi bilioni tano, katika hizo milioni 300 ni *overdraft* za benki. Wakati Serikali inajitahidi kuwapatia shillingi bilioni 11.15 lazima *Management* ya *TBC* na *Board of Directors* wahakikishe wanabana matumizi ili kuwezesha Shirika hili liende vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu mchango mdogo wa Serikali kwa *TBC*. Mapato ya Shirika kwa mwaka 2013 yalikuwa ni shilingi bilioni tisa, mchango wa Serikali ulikuwa ni shilingi bilioni sita, kwa hiyo, utaona kwa hesabu za harakaharaka mchango wa Serikali ni takribani 40%. Uzoefu wa nchi mbalimbali kwa mfano Kenya - KBC, Zimbabwe - ZBC na Uingereza - BBC unaonyesha mchango wa Serikali katika mashirika kama haya ni mkubwa ambao unakaribia 60%. Kwa hiyo, bado mchango huu ni mdogo na Serikali lazima iongeze mchango wake katika Shirika hili ili kuhakikisha kazi zake zinaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Sara Msafiri na Mheshimiwa Rebecca Mgodo ajiandae, Mheshimiwa Iddi Azzan pia ajiandae.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Habari.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara ambapo kwa miaka mitatu mfululizo tulikuwa tunashuhudia bajeti ndogo sana ya Wizara hii ukilinganisha na majukumu ya Wizara na changamoto zinazowakabili vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu, Serikali imeweza kuongeza bajeti kutoka shilingi bilioni 19.3 mpaka shilingi bilioni 21.3. Tunaamini kwamba ni mwanzo mzuri lakini tunaomba Serikali iendelee kutufikiria sisi vijana ambapo Wizara hii ndiyo ina jukumu la kusimamia changamoto zote za vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana wa Taifa. Kwenye bajeti hii ya Wizara, Serikali imetenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya Mfuko

huu. Fedha hizi ni ndogo ukilinganisha na changamoto za vijana.

Mheshimiwa Spika, tunajua huu Mfuko upo kwenye kila Halmashauri zote kwenye nchi nzima, vijana wamejunga na vikundi vya ujasiriamali, vijana wamesoma na wengine mpaka vyuo vikuu. Kwa takwimu za sasa kila mwaka tunakuwa na wahitimu 1,200,000 lakini vijana 200,000 tu ndio wanamezwa kwenye soko la ajira, wengine wote wallobaki wanategemea kujajiri. Vijana hawa wametoka kwenye familia maskini, tunatambua kwamba 75% ya Watanzania wanaishi vijijiini na ni wakulima na wanategemea jembe la mkono na hawa ni watoto wao. Vijana hawa wanapohamasika kujunga na vikundi vya ujasiriamali hawakopesheki, mabenki yote siyo rafiki kwa vijana, vijana hawana dhamana ya kutoa ili wapewe mikopo. Tegemeo kubwa la vijana ni kwenye Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali tena kupitia bajeti hii itazame upya ili iweze kuongeza pesa, vijana ambao wamemaliza vyuo vikuu, wana makampuni wamejajiri hawawezi kushindana na soko, hawana mitaji, kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iangalie suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba Serikali imejipanga kuanzisha benki ya vijana, mimi nasema kwamba hili wazo ni zuri lakini huu mtandao wa benki utafika kwenye nchi yote hii na maeneo yetu? Mimi naona suluhisho kubwa lipo kwenye Mfuko wa vijana ambapo upo kwenye kila Halmashauri. Tunaunga juhudzi za Serikali kuanzisha benki ya vijana, hatukatai, lakini mfumo utakuwa ni uleule, unaanzisha benki leo, wadau wakubwa ni vijana, hawana pesa wala mitaji, hiyo benki inaanizisha na kukopwa mara moja? Lazima tuwaimarishe vijana kiuchumi kwanza kupitia mfuko wao ili fedha wanazowekeza ile faida wawe wadau na wana hisa kwenye hiyo benki lakini vinginevyo itaanizishwa benki ya vijana lakini wadau watakuwa siyo vijana ambapo itakuwa imekwenda kinyume na malengo ya kuanzishwa benki ya vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba Halmashauri zichangie 5% ya bajeti yao kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Naomba kwa zile Halmashauri ambazo hazitatao hii 5% zipewe adhabu ili hii asilimia iwafikie vijana. Kwa hiyo, ninaomba usimamizi wa sheria ufuatwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye Baraza la Vijana la Taifa. Sera ya Vijana ya Taifa ya mwaka 1996 inaeleza wazi kwamba kutaundwa Baraza la Vijana la Taifa ambalo litawakutanisha vijana wote bila itikadi zao za kisasa wala za kidini. Sera ya Vijana ya mwaka 2007 ambayo ni mwendelezo ya ile ya mwaka 1996 nayo inasisitiza kuwepo kwa Baraza la Vijana la Taifa lakini sasa ni miaka 17 tangu Sera itamke kuwepo kwa Baraza la Vijana la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimeona hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaeleza mchakato wa kuanzishwa kwa muundo wa Baraza umefikia kwenye Baraza la Mawaziri lakini naiomba Serikali yangu, kama kulikuwa na muda ambao kunahitajika Baraza la Vijana la Taifa basi ni sasa. Vijana wengi wamejiunga kwenye vyama vyaa siasa, vijana wengi wamejiunga kwenye taasisi za kidini kwa mfano *CASFETA* na asasi nytingine mbalimbali lakini kule hawafundishwi utaifa, wanafundishwa itikadi za vyama vyao na wanachofundishwa kule ni imani za dini zao, suala la utaifa lazima libaki ndani ya Serikali, Serikali ndiyo ina wajibu wa kuwaunganisha vijana wote nchi nzima waweze kuongelea masuala ya kitaifa, waweze kutoa maoni yao na waweze kuishauri Serikali. Vijana sasa hivi hawana sehemu ya kusemea mahitaji yao, wamemezwa na taasisi mbalimbali ambazo hazipo chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini kabisa kwamba ukiona vijana wanajitokeza kwenye maandamano au ukiona vijana wanajitokeza kwenye mikutano ambayo mingine siyo rasmi wanaamini kule ndiyo watakapoweza kutoa madukuduku yao labda watasikilizwa. Kwa hiyo, mimi ninaamini kuwepo kwa Baraza la Vijana la Taifa kwa sasa ni muda muafaka, naiomba Serikali yangu iharakishe huo mfumo ili vijana waweze kutoa maoni yao kwenye Baraza

21 MEI, 2013

na yaweze kufika Serikalini, kwa sababu hiki ndiyo kitakuwa chombo pekee, kitakuwepo kuanzia ngazi za Halmashauri na kupanda mpaka ngazi ya Taifa. Kwa hiyo, yale maoni yataweza kufikiwa na Serikali na kutolewa ufumbuzi siyo kama ilivyo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali yangu ijitahidi sana na hasa Wizara ya Vijana, ishiriki kwenye mchakato na mpango mzima wa kurasimisha ardhi. Ardhi zinapimwa na kugawiwa, tunaona wawekezaji wakubwa kwenye miradi mikubwa ya *SAGCOT* wanakuja, maeneo yale yatamilikishwa, yatakuwa kisheria, vijana watakuwa wanaishia kuwa wafanyakazi kwenye ile miradi au kwenye yale mashamba. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuitia Wizara hii, ishiriki mchakato wa kurasimisha ardhi, yatengwe maeneo ya vijana ya kujifunza killimo cha kisasa, miradi mikubwa kama ya *SAGCOT* inavyokuja vijana wawe na eneo lao la kujifunza ili hatimaye hawa wawekezaji wakubwa wakiondoka tubaki na vijana wetu amba ni wataalamu wetu watakaofaidika na uwekezaji wa miradi mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono bajeti hii, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Rebecca Mngodo, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Azzan na Mheshimiwa Albert Obama.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuanza napenda kusema kwamba nimekipitia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari na kwa masikitiko makubwa sijaona popote ambapo amezungumzia kuhusu kuteswa, kudhalilishwa na kuuawa kwa waandishi wa habari. Mazingira magumu ya waandishi wa habari hayajaandikwa popote katika kitabu hiki na sielewi ni kwa nini kwa sababu ni Wizara yake na waandishi wa habari kwa vyovoyote wako chini yake na wanastahili kuzungumziwa na yeeye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hotuba pia katika ukurasa wa tisa, imezungumzia kuhusu kufungiwa vyombo vya habari vya Neema *FM* na Iman *FM*, ambavyo vimeonekana vimekiuka maadili ya utangazaji. Lakini cha kushangaza sijaona mahali popote ambapo gazeti la Mwanahalisi ambalo limefungiwa kwa muda mrefu, limezungumziwa. Kwanza, ningeomba kujua katika majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kifungu gani cha sheria kilichotumika kulifungia gazeti la Mwahalisi pasipo kikomo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 12 wa kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna maelezo kuhusu ubia kati ya *TBC* na kampuni ya Kichina ya *Star Communication Network Technology* ambapo walianzisha Kampuni ya *Star Media*. Ninachopenda kuzungumzia hapa ni ving'amuzi vinavyoingizwa na *Star Media*. Ving'amuzi hivyo havilipiwi kodi, lakini vinauzwa kwa bei kubwa na wananchi wengi walioko vijijini na hata mijini wanashindwa kumudu bei ya ving'amuzi hivyo ambavyo Wachina wanaviingiza bila kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua kwanza ni kwa nini havilipiwi kodi, kwa sababu kuna ving'amuzi vingine ambavyo vinalipiwa kodi. Ni utaratibu gani ambaou umefuatwa ili hawa Wachina wao wasilipe kodi? Kama hawalipi kodi, ni kwa nini bei iko juu kiasi kwamba wananchi wa Tanzania wanashindwa kumudu bei hizo? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tujue kwamba, ni haki ya kila mtu kupata habari. Kuna mazingira magumu sana kwa waandishi wa habari. Tunafahamu vyombo vya habari vina nguvu ya kubomoa na nguvu ya kujenga, hivyo basi, tukivitumia vizuri tunaweza kujenga, lakini tukivitumia vibaya na kufanya uadui navyo tutakuwa hatujengi na badala yake tutakuwa tunabomoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana wengi hawaamini magazeti, lakini naamini vyombo vya habari kwa sababu ndivyo vimewekwa kutuhabarisha, kutufahamisha na kutuburudisha, lakini sasa inatufanya tuijulize ni kwa nini vipo

kama hatuwezi kuviamini? Nataka kuendelea kuviamini kwa sababu najua wanafanya utafiti, lakini mara nyingine wanakosa ushirikiano kutoka vyanzo ambavyo ni Serikali, sisi Wabunge wenyewe, pale tunapokuwa tumewanyima ushirikiano hapo ndiyo tunakuwa tumekwamisha kazi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini mauaji ya waandishi wa habari, mateso na manyanyaso yameendelea kwa wingi. Hapa Bungeni tumezungumzia tu kuhusu Absalom Kibanda na Daudi Mwangosi, lakini ukweli ni kwamba, kuna waandishi wengine wengi sana ambao wameteseka, wamenyanyasika na ambao mazingira yao magumu yamesababishwa na sisi wenyewe ambao tungeweza kurahisisha maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika gazeti la Tanzania Daima la tarehe 7 mwezi wa Tatu, mwaka huu kuna taarifa ya baadhi ya waandishi ambao ningependa kuwanukuu, ambao wameteseka, wameuawa na wengine kuwekewa mazingira magumu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Kwanza kabisa ni Mwandishi Fredrich Katulanda wa gazeti la Mwananchi anayeishi Mwanza. Mwandishi huyu alivamiwa nyumbani na wavamizi walikuwa na vipaza sauti na nyaraka za akaunti za benki za Halmashauri ya Jiji. Wavamizi hao walikuwa pia na mapanga, wakichangizana kusema...

SPIKA: Mheshimiwa Sabreena.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, naitwa Rebecca Mgodo.

SPIKA: Mheshimiwa Rebecca, katika maagizo yangu ambayo nilikataa mojawapo ni hilo. Sasa tusitafutane, naomba tutii maamuzi. Endelea na *discussion* yako.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nirudie, vyombo vya habari vina nguvu sana, tukivitumia vizuri tutaweza kuwaelimisha wananchi na

kuwafundisha. Kuna mambo mengi tunayazungumza humu ndani ambayo wananchi hawana habari hasa wale wanaoishi vijijiini. Kwa mfano, mambo ya Kilimo Kwanza, wananchi na vijana wengi hawaelewi.

Mheshimiwa Spika, kama tungekuwa tunavitumia vyombo vyahabari vizuri, nakumbuka wakati wa awamu ya kwanza ya hayati Baba wa Taifa, katika redio moja iliyokuwepo, Redio Tanzania, kuna kibwagizo cha wimbo kilikuwa kinarudiwa mara kwa mara juu ya habari ya kula chakula bora, mboga, samaki, watu walikuwa wanafundishwa, lakini sasa hivi tumeweka uadui na vyombo vyahabari, jambo ambalo ni tatizo kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haki ya kupata habari ni ya kila mwananchi na ni jambo muhimu katika kuendeleza jamii yetu. Waandishi wa habari wanaweza kukuza demokrasia na amani. Pale ambapo kuna amani, demokrasia inaendelezwa na Taifa zima pia litakuwa limeendelezwa, lakini pale ambapo tunawakwamisha waandishi wa habari kwa kuwanyima haki yao ya kupata ile habari na kuipeleka. Kimsingi hapa Tanzania sisi tunasema tuna uhuru wa habari, lakini ile haki ambayo iko katika Katiba haitekelezwi, ndiyo maana mtu anapotaka habari hapati habari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mdogo tu, mtu anaamka asubuhi anakuta nyumba yake imewekwa alama ya X. Hajui ni nani ameweka alama hiyo, akiuliza nani ameweka alama ya Xkwenye nyumba yake, hafahamishwi. Yaani inakuwa kama ni vitisho vitisho. Habari haitolewi kwa usahihi au kwa wakati muafaka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, wananchi wanabaki wakiishi kwa hofu wakati tungeweza kutumia vyombo vyahabari kuwahabarisha na kuwaeleza ili waweze kuishi kwa amani. Pia na wao wangeweza kuifanya Serikali iwe na uwazi pia iweze kuwajibika katika kuendesha shughuli zake za kila siku.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu siku ya uhuru wa vyombo nya habari ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe 2 mwezi wa Tano. Maadhimisho hayo kwa mwaka huu yalifanyika Mkoani Arusha na waandishi wa habari pamoja na wamiliki wa vyombo nya habari walikutana mjini Arusha na walizungumzia kuhusu mazingira magumu ambayo waandishi wa habari wanakumbana nayo, hasa wale wanaofanya *investigative reporting* ambao wanapata matatizo sana wanapokwenda kutafuta habari.

Mheshimiwa Spika, taarifa mojawapo iliyotolewa ni kuhusu mwandishi mmoja wa habari ambaye sitamtaja jina, alikwenda huko Mwanza kufanya utafiti ili kujua ni kwa kiwango gani, njia zipi na sababu zinazopelekea watu wenye ulemavu wa ngozi kuuawa. Mwandishi huyo wa habari alipata hali ngumu sana, ushirikiano ulikuwa ni mgumu, lakini alijitahidi kufa na kupona mpaka akapata taarifa ambazo zilisababisha kutumiwa ujumbe wa vitisho. Hii ni hali halisi ambayo wanakumbana nayo waandishi wengi wanaofanya *investigative reporting*. Waandishi hao wanapata vitisho, wanazuiwa kwa kuambiwa kwa nini wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni shahidi mmojawapo ambaye nilikwenda huko Arusha kutaka kujua ni kwa nini wanawake katika lile eneo la Simithi walitolewa nje na eneo lao la ardhi akapewa mwekezaji. Mwandishi niliyekwenda naye ambaye naye pia sitamtaja jina nikihofia asipate vitisho, alipata vitisho kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, akimuuliza ni kwa nini amekwenda kuandika taarifa kuhusu wanawake ambao waliondolewa katika eneo lao la ardhi na ardhi ile kupewa wawekezaji?

Mheshimiwa Spika, hiyo ni mifano michache tu ya jinsi ambavyo waandishi wa habari wananyanyasika na kukosa ushirikiano. Hata hivyo, waandishi walijiwekea azimio katika mukutano ule wa Arusha kwamba, wangependa kabisa haki za msingi za kupata habari na uhuru wa habari, vitekelezwe sasa katika nchi yetu. Hata lile Azimio la Windhoek la mwaka 1991 la Haki ya Uhuru wa Habari kwa kila Mwananchi, litekelezwe katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia walizungumzia jambo ambalo naona ni muhimu Serikali ikaangalia jinsi ambavyo inapaswa kuwawezesha waandishi wa kujitegemea. Waandishi wa kujitegemea wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wengi hawana vitambulisho na kimsingi wanafanya kazi kwa ajili ya nchi yao. Wanaipenda nchi yao na wanajiedeleza wenyewe. Hata katika jua kali au mvua, pamoja na kukosa fedha za kutosha, lakini wanafanya kazi kwa sababu wanaipenda nchi yao. Hivyo, ni muhimu mamlaka husika pia ikaangalia ni jinsi gani waandishi wa kujitegemea wakapata unafuu katika yale ambayo wanayafanya.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema nchi ya Tanzania imewekewa kiwango kwamba, ni ya tatu barani Afrika kwa kunyanyasa waandishi wa habari kwa kuwaua na kuwatesa. Nchi ya kwanza ni Somalia, ikifuatiwa na Eritrea, Tanzania ambayo ilikuwa ni kisiwa cha amani katika bara la Afrika, sasa tumewekwa katika nafasi ya tatu kwa kuwasababishia mazingira magumu waandishi wa habari na kuwanyima haki zao katika kuwapa taarifa.

Mheshimiwa Spika, pia waandishi wa habari wengi hawana bima ya maisha. Huo pia ulikuwa ni wito wao kwa vyombo na wamiliki wa vyombo vya habari kwamba, waweze kuwakatia bima ya maisha hasa pale wanapokuwa katika mazingira magumu ya kazi na wanapokutwa na mauti kule au tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu *trade unions*, vyombo vingi vya habari havina *trade unions*. Kwa hiyo, ni wito wa waandishi wa habari kwamba *trade unions* zianzishwe katika vyombo vya habari.

*(Hapa kengele ya pili illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makof*)

SPIKA: Nilisema namwita Mheshimiwa Iddi Azzan, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati kama yupo, Mheshimiwa Amina Mwidau na Mheshimiwa Murtaza Mangungu wajiandae.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nichangie Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kabisa nachukua nafasi kuwapongeza sana waandishi wa habari wa vyombo vyote vya habari kwa kazi nzuri wanazozifanya za kutuhabarisha. Nafahamu mionganoni mwao wapo ambao wana jina lile la makanjanja, lakini hao ni wachache na wanashughulikiwa, lakini walio wengi wanafanya kazi zao vizuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuwafahamisha Wabunge na wananchi kwamba, mionganoni mwa magazeti ambayo yapo muda mrefu na yamekuwa yakitoa habari zake vizuri na yameelimisha sana jamii yetu ni gazeti la Nipashe pamoja na mengine na ndiyo maana likaitwa mwanga wa jamii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilisikitishwa sana na Mheshimiwa mmoja ambaye alichangia hapa Bungeni akasema, Nipashe ni giza la jamii. Nafikiri alikuwa na jambo lake kwani gazeti hili ni mwanga wa jamii, limefanya kazi vizuri sana, hivyo, ni lazima tuwape moyo ili waendelee kufanya kazi hiyo vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kazi kubwa iliyotuleta hapa ni kuja kuwawakilisha wananchi wetu na kueleza matatizo yao na si kuja kumsafisha mke wangu au mume wangu ndani ya ukumbi huu. Kwa hiyo, niwaombe wale ambao wana tabia hiyo waialche. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo iko mbele yetu. Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la Jela Mtagwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kulizungumza jambo lile siku ile, Serikali wamekwenda kumuona na kwa kweli nashukuru kwa sababu kile kitendo cha kumpa pole peke yake kimempa faraja sana. Kwa hiyo, niwapongeze kwa hilo na moyo huu uendelee hata kwa wanamichezo wengine ambaao wameiletea sifa nchi yetu. Si lazima upeleke kitu, lakini kumtembelea mgonjwa na kumpa pole pia ni faraja kubwa sana. Kwa hiyo, nawapongezeni sana kwa hilo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa bajeti hii sikuiunga mkono na nilikuwa na sababu, kubwa lilikuwa ni Sera ya Michezo pamoja na Sheria ile ya Baraza la Michezo ambavyo vyote viwili vimepitwa na wakati kupita maelezo au vimepitwa na wakati sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nikilizungumza hili tangu mwaka 2006 na kila mwaka unaofuata Serikali imekuwa ikisema tuko kwenye mchakato, mambo yanaendelea, lakini hadi leo hii tunapozungumza hakuna chochote ambacho kimefanyika zaidi ya kuoneshwa kwenye hotuba hii ya Waziri ambayo mara hii kidogo amekuja na maneno mengine na siyo yale ya kwamba tuko kwenye mchakato.

Mheshimiwa Spika, safari hii amekuja na maneno kwamba, rasimu imewasilishwa ngazi za juu, rasimu ya sera za michezo iko ngazi za juu. Sasa hatujui rasimu hiyo imapelekwa lini, ngazi hizo za juu ni zipi na lini itakuwa tayari? Bado mnatuweka kwenye kiza wanamichezo wa nchi hii na ndiyo maana migogoro inazidi kuwa mingi kwa sababu sheria mnazotumia zimepitwa na wakati. Vyama vya Michezo vina sheria ambazo zinaendana na wakati, ninyi bado mmeendelea kuwa na sheria zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri kwenye majibu yake alieleze Bunge hili ni lini rasimu hiyo ya sera za michezo itakuwa tayari ili baadaye ije kuwa sera na kisha tutengeneze sheria kwa ajili ya michezo yetu. Kinyume

cha hivyo, ni kuendelea kuwa na migogoro isiyokuwa na sababu. Tumeona migogoro ambayo imejitokeza juzi tu hapa kwenye uchaguzi wa Shirikisho la Soka Tanzania (*TFF*).

Mheshimiwa Spika, Sheria ambayo inatumiwa na Baraza la Michezo ya mwaka 1967 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1971, haiendani kabisa na sheria ambazo ziko kwenye Vyama vya Michezo. Vyama vya Michezo vime-*advance* zaidi, viko mbele, lakini ninyi bado mko nyuma na matokeo yake sasa kunakuwa na migogoro ambayo Serikali mkiingilia kati, mwisho wa siku mtakuja kupata aibu tu, kwa sababu mnazungumzia sheria ambayo imeshapitwa na wakati, wenzenu wako mbele. Kwa hiyo, niombe sana hili tuhakikishe tunalikamilisha ili mambo yaende vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Sera ya Michezo ikiundwa tutakuwa na Sheria ya Michezo. Juzi wakati Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, anajibu swali langu hapa Bungeni, pamoja na mambo mengine alieleza kwamba, wachezaji hawa wameajiriwa na ajira ziko kwenye vilabu vyao na wana mikataba na vilabu hivyo ndiyo vinahusika kwa kila kitu kwa wachezaji hawa.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni tofauti kabisa na sheria kwani haisemi hivyo, sheria inasema michezo Tanzania ni ridhaa. Kwa hiyo, suala la wachezaji kuajiriwa Serikalini halipo, sasa Waziri akilisema hivyo anzidi kuwachanganya. Niseme kwa wachezaji ambao wameajiriwa hakuna ajira ya maana kwa sababu anaweza akapewa mikataba wa leo na kesho akaambiwa ondoka, hana haki yoyote anayopata. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama kungekuwa na sheria nzuri ambayo inalinda tusingekuwa na matatizo kwa wachezaji wetu, tungekuwa na mikataba mizuri ambayo inaeleweka. Lakini kwa sababu hakuna ndiyo maana unaona wachezaji wanaondolewa kadri viongozi wa vilabu wanavyotaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia suala la matibabu au kuwasaidia wachezaji wanapokuwa wamestaafu mpira. Majibu ya Waziri ni kwamba, suala hilo liko kwa vilabu. Vilabu havifanyi hivyo kwa sababu hakuna sheria inayovitaka vilabu vifanye hivyo. Kwa hiyo, hakuna bima ya wachezaji kama anavyosema Mheshimiwa Waziri, kama ukikuta bima kwa wachezaji basi labda ni Simba na Yanga tu, lakini vilabu vilivyobakia vyote hakuna bima za wachezaji, mchezaji akiumia ni lwake. Mchezaji akistaafu ameshalitumikia Taifa kwa muda mrefu, mwisho wa siku anajikuta hana mtu wa kumhudumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tuwe na sheria ambayo itawalinda wachezaji wetu, hawa wa vilabu, lakini na wale wanaochezea timu za Taifa ili kuondokana na haya ambayo yamejitokeza kwa Jela Mtagwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati Waziri anajibu hapa alielezea kwamba, mengi ambayo tulimpa wakati ule, yeye ndiyo kwanza alikuwa ameingia madarakani, karibu miezi mitatu au minne tu, hivyo tuendelee kumpa muda. Sasa anataka tumpe muda mpaka lini ili sheria hizi ziwe zimekamilika? Kama hivi sasa ni zaidi ya mwaka na mambo hayaendi, tunajuliza tumpe muda wa miaka mingapi? Anataka tumpe muda wa miaka mingapi ili akamilishe haya mambo? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, alisema kuhusu wizi wa kazi za wasanii. Wasanii wanaibiwa sana kazi zao, akasema yeye mtoto wa mjini. Nakubali kweli Naibu Waziri ni mtoto wa mjini, kitovu kiko *Ocean Road* kweli, kweli kakulia Kawe sawa tena *Police line*, kwa hiyo, mbinu za kipolisi anazo. Alisema kwa sababu yeye ni mtoto wa mjini na wizi wa kazi hizi unafanywa na watoto wa mjini pia, atapambana nao ili kuhakikisha kazi za wasanii hazitaibiwa tena.

Mheshimiwa Spika, walianza vizuri, kuna watu walikamatwa mwanzo mwanzo, lakini hivi tunavyozungumza wizi wa kazi za wasanii unaendelea tena kwa kasi kubwa sana na Serikali imeendelea kukaa kimya. Sasa tunajuliza zilikuwa

ni nguvu za soda? Mheshimiwa Waziri yupo, Naibu Waziri yupo, najua ni mtoto wa mjini, hebu wahakikishe wasanii hawa wanapata haki zao kwa sababu kelele zimekuwa ni nygingi na wamekuwa wakilalamika kila kukicha na ukiangalia ni kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina hakika kwa utoto wake wa mjini na kazi aliyoifanya kwa kipindi hiki atawea kupambana kuhakikisha wasanii wanapata haki ya kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kwenye michezo na hasa kwenye mpira huu wa miguu. *TRA* wamekuwa wakiwakata *TFF* kodi kwa ajili ya mishahara ya Walimu wa timu za Taifa; Maxio Maximo na Paulsen. Juzi tu hapa walichukua karibu shilingi milioni 150...

SPIKA: Ahsante, naona...

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofî*)

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami naomba nianze kwa kuungana na Wabunge wenzangu kuwapa pole waandishi wote ambao walipatwa na matatizo wakiwa kazini na kwa wale ambao wametangulia mbele ya haki Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi na wale ambao wamenusurika, basi Mwenyezi Mungu awape afya na awaongezee umri.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze hotuba yangu kwa kumrukku Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa katika sherehe za siku ya Uhuru wa Habari Duniani ambayo ni *World Press Freedom Day*. Mheshimiwa Rais aliongea vizuri sana kwa siku hiyo na naomba nimrukku machache katika yale aliyosema:

"Napenda kuwapongezeni Wanahabari wote nchini na wadau wenzenu duniani katika siku hii ya kuadhimisha

miaka 20 ya siku ya uhuru wa habari duniani. Aidha, kama ambavyo tumekuwa tukifanya, napenda kuwahakikishieni, hii *promise*, napenda kuwahakikishieni kuwa, mimi binafsi na Serikali yangu ninayoongoza, nitaendelea kushirikiana nanyi katika kupanua, kulea, kulinda na kutetea uhuru wa habari nchini ikiwa ni haki ya waandishi kufanya kazi yao kwa mazingira muafaka ya kisiasa, kiuchumi, kisheria na kijamii.

Vilevile napenda kuwahakikishieni tutaendelea kushirikiana nanyi katika kuulinda uhuru wa wapata habari nchini amba ni muhimu kama ilivyo uhuru wa vyombo vya habari." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais hapa alikuwa muwazi kabisa katika hili na nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu aliposema kuwa mimi na Serikali yangu Mheshimiwa Waziri na watendaji kwenye hiyo Wilaya wana jukumu kubwa la kuyatekeleza kwa sababu Rais ni kiongozi Mkuu katika nchi hii, Amiri Jeshi Mkuu, kauli yake inakuwa ni ahadi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ana kazi kubwa ya kuyatekeleza haya. Kwa sababu sote tunajua umuhimu wa vyombo vya habari. Wachangiaji wengi sana hapa wamechangia kwa sababu tangu jana ni malalamiko ya vyombo vya habari na matatizo ambayo yaliwapata na malalamiko yaliyotokea.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amejaribu kugusia suala ambalo ni muhimu kuwa, ataleta Muswada wa Habari hapa Bungoni jambo ambalo ni muhimu kabisa na ameahidi kuwa mwaka huu atauleta. Kwa sababu hiyo itatusaidia kuweza kuchangia, lakini ningewomba awashirikishe wadau wa habari katika huo Muswada kwa sababu wao ndiyo wahusika wakuu na watasaidia.

Mheshimiwa Spika, pia kuna marekebisho kwa sababu kuna Sheria ile ya Magazeti ya mwaka 1979 ambayo inampa mamlaka Waziri kufungia gazeti pale ambapo

limefanya makosa na Waziri naye ni binadamu inawezekana likawa limemkera ye ye binafsi akalifungia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuifanyia marekebisho hii sheria ni kandamizi itasaidia vile vile. Pia kuwasaidia waandishi wengi ambao wameajiriwa kwenye *private company* ambapo wanapata matatizo sana kwenye malipo na mafao. Mheshimiwa Waziri kwa kufanya hivyo, basi utakuwa umeanza.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningeomba ndugu zangu, waandishi wa habari wanatusaidia sana kwa sababu mwandishi anamwinua mwanasiasa kutoka chini kabisa mpaka anakuwa maarufu. Kwa hiyo, tujaribu kuwapongeza waandishi wa habari pale ambapo wanafanya vizuri. Wao ni binadamu wanakosea wakati mwingine, lakini pale ambapo basi wanafanya yale mazuri tuoneshe kuwapongeza waandishi wa habari. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tukichukulia mfano, hivi juzi kulikuwepo na tatizo la mpaka katika Tanzania na Malawi walionyesha uzalendo wa hali ya juu. Kwa sababu waandishi wote waliungana na kuwa na kauli moja kwa nchi. Kwa hiyo, yale machache ambao wanayafanya vizuri au mengi ambayo wanayafanya vizuri na machache wanayoyafanya vibaya, basi tusichukulie kauli zao moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee juu ya michezo. Kabla suaanza hotuba yangu kwanza niwape pole watani wetu wa Yanga kwa sababu magoli mawili hayajamtingisha mnyama. Kuna bao tano ambazo bado hamjavunja rekodi yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielekee Tanga. Tanga tuna ahadi ya uwanja wa michezo wa Kimataifa ambapo eneo lipo Kata ya Mzingani maeneo ya Minjani na *TFF* wameshawalipa Halmashauri ya Tanga na wao wamewalipa wananchi eneo lipo tangu mwaka 2009/2010. Lakini bado tunaona mpaka leo hakuna mwendelezo

wowote, na hii ni *complex stadium*, ni uwanja mkubwa ungekuwa wa Kimataifa, tukiacha uwanja ambao tunao Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja yake atwambie, huo mradi upo kwa sababu ni mwakilishi wa *FIFA* Kusini mwa Afrika ndio alikuja nao na akashirikiana na *TFF*. Eneo likatafutwa na wale watu wamelipwa na sasa hivi hakuna shughuli za kimaendeleo zinaendelea pale, lakini tunaona kimya.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake hapa mbele atwambie, huu mradi upo au umeishahamishwa nao angalau tujue kwa sababu tuna bahati ya kupata miradi, lakini baadaye inapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu uwanja ni muhimu kwa Tanga kwa sababu ungeweza kufungua fursa nydingi sana za kiuchumi, lakini pia kwa nchi kwa ujumla wake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri suala hili ni muhimu kweli kwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie kwenye *Olympic*. Kama ninavyojua, najua tuna Kamati ya *Olympic* ya Kitaifa, sijui inafanya kazi gani. Kwa kweli nasikitika sana na nadhani wenzangu wapo wanaoguswa. Mwaka 2012 tulishuhudia mashindano ya *Olympic* huko London, lakini Tanzania kama alivyosema jana Mheshimiwa Mbilinyi tulishiriki kwa uchache mno.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli inasikitisha kwa sababu mimi nilivyoangalia kuna michezo mingi sana ambayo tungeweza kushiriki na kuiletea sifa nchi yetu na sisi tungeweza kuingia kwenye ramani ya michezo ya kidunia, tungeweza kutambulika Tanzania, siyo lazima Kenya na South Africa kila siku. Tanzania tupo wapi?

Mheshimiwa Spika, ningeomba hii Kamati basi ifanye kazi yake. Siyo lazima michezo yote lakini ile michezo michache ambayo tunaimudu kwa sababu nina uhakika

kwa upande wa Tanga, kuna mashindano yale ya majahazi, niliona mashindano ya mashua ambayo Tanga sisi ni wataalam, wangeweza kwenda kwenye maeneo machache ambayo tungeweza kuanza kuonesha mfano.

Mheshimiwa Spika, pia baiskeli watu wanaendesha kwenye *rough road*, je, kama wangeshindana kwenye maeneo ambayo ni mazuri. Nitoe wito kuwa, Kamati hii basi ikafanye majukumu yake na kama hawawezi wabadilishwe. Halafu pia mashindano yanakuja yale tumeshayakosa, lakini mwaka 2016 yanafanya Brazil, maandalizi yaanze sasa hivi. Kwa kweli tunakuwa tunapeleka Mabalozi tunaitangaza nchi yetu, siyo kila siku kuwashangilia wenzetu tu wakati Wizara nzima ipo. Ningeomba Mheshimiwa Waziri hili alifanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nielekee kwenye suala la utamaduni. Katika utamaduni bado tuna utamaduni ule ule wa *hardware*, utamaduni ule wa kuonekana ambayo ni mavazi, ngoma, nyimbo. Lakini ningependekeza tukawa na utamaduni wa *software*, tukawa na siku ya kufikiria duniani ambayo ni utamaduni wa *software*, Watanzania wengi ni wavuvi wa kufikiri. Hawapendi kufikiri, wanapenda ku-copy na ku-paste.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiwa na siku ya kufikiri duniani. Kwa mfano, kama hivi juzi Mheshimiwa Rais alienda kwenye sherehe ambapo kulikuwa na mkakati wa lishe, ni suala ambalo ni muhimu kwa sababu utamaduni wa lishe ni muhimu kwa maisha ya Mtanzania. Kwa hiyo, tukiwa na utamaduni wa aina hiyo ni sawa sawa na kuwa na utamaduni tulio nao wa kuleta amani na utulivu na tuna balozi wa amani.

Mheshimiwa Spika, basi tuwe na utamaduni wa kufikiri ili kuweza kutengeneza *ma-think tankers*, tuhamie kwenye *software* sasa. Mheshimiwa Waziri ana Wizara nzima, kuna suala la utamaduni, siyo kila siku hizo hizo nyimbo, ngoma tuwe na utamaduni sasa wa kuwafanya Watanzania wafikiri ili tuweze kuwa *creative* na ili tuweze kusonga mbele kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nigosie kwa vijana, watu wengi sana wameongelea suala la vijana. Vijana hapo zamani tulikuwa tukisema ni Taifa la kesho, hiyo imepitwa na wakati kabisa. Vijana sasa hivi ni Taifa la leo, lile suala la Taifa la kesho limekwisha.

*(Hapa Kengele ya pili illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Sabreena Sungura atafuatiwa na Dkt. Hamisi Kigwangallah, atafutia Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba halafu nitaona mbele.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nami nataka kuhoji Wizara kwamba ni miaka 17 sasa toka sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ilipoahidi kuundwa Baraza la Vijana, lakini mpaka leo hii Baraza la Vijana bado halijaundwa. Je, ni kitu gani ambacho kinakwamisha Baraza hili kuundwa? Tumeona hapa kwenye hotuba kwamba zimetengwa bilioni 6.1 kwa ajili ya Mfuko wa Vijana. Sasa kama Baraza la Vijana halipo, je, tuna uhakika nani anakwenda kusimamia maslahi haya ya vijana? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vijana wa Afrika wanaunda asilimia 40 ya watu wote wa Afrika na mwaka jana hapa mwezi Februari, tulipitisha Mkataba wa Vijana wa Afrika, lakini mpaka dakika hii wala kwenye mipango ya Serikali hazoneshi jitihada zozote za kuhakikisha kwamba, ni vi pi tunaenda kutekeleza mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, tulitegemea labda Serikali kwa mwaka huu ingeweza kuleta mapendekezo aidha wanatunga sheria mpya ama kama kuna *amendment*,

regulations ama wenyе sera zetu ni vipi tuna-*domesticate* Mkataba huu ili kuhakikisha kwamba haki za vijana zinalindwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba, vijana wa Kitanzania wanapata ajira kuna mambo ya msingi ambayo ni lazima tuyaimarishe. Kuna sekta ya kilimo na kilimo pekee hakitoshi kwa sababu kilimo lazima kiendane sambamba na miundombinu. Kama unalima matunda kijijini, lakini unakosa barabara ya kuyafikisha kwenye maeneo husika hasa masoko, hatuwezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna suala nzima la Vyuo vya Ufundı, lazima tuzingatie na nishukuru kwamba kuna programu mpya ya kupeleka Vyuo vya VETA hususan kwenye makambi yetu ya JKT na hii programu mpya iliyoanza ya vijana wallomalliza *form six* kwenda JKT itasaidia vijana wengi kupata Elimu ya Ufundı ambayo ndio itasaidia kuokoa Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna kuimarisha Mfumo wa Elimu, tumeona jinsi mfumo wetu wa Elimu wa Tanzania hauwasaidii vijana kujajiri. Kwa hiyo, lazima Waziri husika akae na wenzetu wa Wizara ya Elimu waaangalia ni jinsi gani wanabadilisha mfumo wa elimu Tanzania ili vijana wetu wawe na sifa ya kujajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia bado tuna changamoto ya lugha za Kimataifa. Vijana wa Kitanzania wengi wetu hatujui lugha za Kimataifa. Ningependa tu kujua hivi Baraza la Kiswahili la Taifa huwa lina Wakalimani wa kutafsiri lugha, kwa sababu sasa hivi dunia tunapoelekea lugha mbalimbali zinatafsiriwa. Ukienda kwenye *google translate* ukisema *translate* Spanish labda kwenda kwenye Kirusi unapata. Je, katika Kiswahili tuna mkakati gani na hii itakuwa ni njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba lugha yetu ya Kiswahili inakua.

Mhehimwa Spika, lakini ningependa moja kwa moja sasa niende kwenye suala nzima la michezo. Tuna haja sasa ya kuhakikisha kwamba michezo inakuwa *promoted* katika

nchi yetu. Tuache siasa kwenye michezo kwa sababu lazima tuwe na *think tank* ambayo itaangalia miaka 10 ijayo Tanzania Sekta ya Michezo inapelekwa namna gani?

Mheshimiwa Spika, lakini tunalala, tunaamka, anakuja Waziri anasema leo tunafuta UMISETA, kesho anakuja mwingine anasema tunaanzisha UMITASHUTA. Kwa hiyo, tunakosa *direction* kama Taifa la kuhakikisha kwamba michezo tunaipeleka katika maeneo gani? Michezo imekuwa *promoted* Tanzania lakini katika *level* za juu, tunaangalia tu Simba, Yanga, Azam. Lakini kwa nini tunasahau huku chini ambapo ndiko kuna vyanzo vya kuibua.

Mheshimiwa Spika, ningependa tu kuishauri Serikali kwamba turudishe ule mfumo wa zamani. Mashirika ya Umma, Idara Binafsi, Taasisi za Serikali zilikuwa zinamiliki timu za mipira. Hii inapelekea kwamba klubu zetu nyngi za mipira sasa hivi watu wanaozientesha hawana fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini tutakaposema kwamba na Mashirika yaweze kudhamini ama kuwa timu za michezo, itasaidia sana kwa sababu watu hawa watakuwa na fedha, wataweza kuandaa viwanja vizuri, wataweza kuandaa vifaa vizuri vya michezo, lakini hata lishe. Kwa sababu michezo bila chakula ni kitu ambacho hakiwezekaniki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vyema sasa tukaangalia utaratibu wa zamani, zamani tulikuwa na timu nzuri Idara ya Maji ilikuwa na timu yake, tulikuwa na wenzetu Pamba Mwanza, Magereza, Reli Morogoro, tulikuwa tuna Bandari Mtwara. Hizi ni Taasisi ambazo zilikuwa zinajitegemea, lakini zilisaidia kukuza sekta ya michezo. Lakini sasa hivi michezo imekuwa kama yatima, michezo haina mwangalizi, michezo imekuwa haina nini.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama tunaweza tukawa na timu bora ya Taifa bila kuwa na vilabu bora ambavyo vitaibua wachezaji kuweza kuwafikisha katika *level* hii. Kuna wachezaji wazuri ambao zamani walitoka katika hizi timu ambazo zilikuwa zinafadhiliwa na Mashirika ya Umma.

Kulikuwa na mchezaji kama Mohamed Hussein Mmachinga kutoka Lindi au huko Mtwarara, tulikuwa tuna Bea Simba, Kitwana Sulemani, Mau Mkami, lakini walikuwa ni wachezaji ambao walikuja kuchezea Timu ya Taifa ambao waliibuka kutoka huko mwanzo.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukaangalia mfano wa wenzetu wa Uganda, wana Uganda *Revenue Authority* ina timu, wenzetu wa Zambia, Migodi ya Shaba inafadhili timu, timu kama *Kabwe Warriors* ni timu ambayo inafadhiliwa na mgodi wa shaba. Kwa hiyo, tunasema kwamba vifaa vyatia michezo, viwanja vizuri, mazingira ya watu kuchenza ndani na nje ya timu yanawezekana kwa sababu kuna watu ambao ni wafadhili wana fedha ya kuhudumia michezo yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna timu kama *ZANACO*, hii ni timu ya Benki ya Wananchi wa Zambia na inafanya vizuri na imewahi kushindana klabu bingwa Afrika. Sasa sisi tuna mpango gani na Wizara ina mpango gani kuhakikisha kwamba, michezo tunarudisha kwenye Mashirika ya Umma ambayo yataweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaweza kuona kwamba, timu ya Simba na Yanga ndiyo zinacheza zinakuja kushirikishwa na klabu hizi ndogo ndogo za Mikoani, klabu ambayo haiwezi kuingiza hata laki sita kwa mwezi, lakini inashindanishwa na timu ambayo inaweza ikapata kwa mwaka *one billion* au milioni 800 au milioni 500.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, hapa hata ule uwiano unakosekana. Kwa hiyo, ni vema sasa Wizara ikachukua suala hili ikalirudisha nyuma kama utaratibu wa zamani ulivyokuwepo ili Mashirika, Idara na Taasisi nyingine za Serikali ziweze kushika michezo na hivyo michezo itaweba kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Okay, ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangallah.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nianze kwanza kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanafanya, lakini niwapongeze zaidi kwa namna ambavyo wameamua kutekeleza kwa dhati Azimio la Bunge lilitopitishwa hapa kutokana na hoja binafsi ambayo mimi mwenyewe niliwasilisha.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ilihuiana na Kukuza Ajira kwa Vijana kupitia Kilimo na Sekta nyingine mbalimbali ikiwemo uvuvi na biashara ndogo ndogo. Kutokana na Azimio hilo la Bunge mwaka huu nimesoma vitabu na nimeona kwamba, Wizara imeamua kutenga kiasi cha shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya Kukuza Ajira kwa Vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze kwa kuchukua hatua hizo, lakini niwashauri wajikite zaidi kwenye kulenga sekta mahsus, lakini pia kwenye kulenga maeneo mahsus ili basi fedha hizo ziweze kuwa na tija, lakini pia maeneo ambapo watafanya uwekezaji pawe kama *case study*, pawe kama maeneo ya mfano ili Mikoa mingine pia iende kujifunza hapo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia uwekezaji wa namna hiyo ukifanikiwa utatuwezesha sasa mwakani tuweze kuitaka Serikali itenye fedha nyingi zaidi ili kuongeza wigo wa kuwawezesha vijana katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitumie fursa hii kuwataka vijana wa Kitanzania badala ya kulalamika, badala ya kusikitika na kunyongea kwamba, wametengwa na Serikali yao waanze kutambua kwamba fursa zipo na tayari sisi Wabunge ambao tupo hapa tunawawakilisha, tunafanya kazi yetu ipasavyo na ndiyo maana tulileta hoja binafsi na hoja ikapitishwa na Bunge na sasa utekelezaji unaanza. Hivyo basi, waendelee kujishughulisha wasikatishwe tamaa na wala wasirubuniwe na watu wenye maslahi binafsi ya kisiasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri ndugu yangu komredi

Makala, Mbunge wa Mvomero, kwa jitihada alizozifanya kutatua mgogoro wa uchaguzi wa uongozi wa *TFF*. Hapa niwashauri wenzetu katika Shirikisho la Mpira wa Miguu, Tanzania watambue kwamba, mchezo huu unapendwa na Watanzania wengi na ni muhimu sana katika maisha ya kila siku ya jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hivyo, unapoongelea uchaguzi ndani ya *TFF*, ni siasa kubwa na tusileté mzaha. Tusimame kwenye sheria na Kanuni ambazo zinatambulika ili haki itendeke. Kama wagombea wamejitokeza kanuni zifuatwe, wasikatwe bila kufuata misingi ya sheria na kanuni ambazo zipo ili mchezo huu uweze kupata viongozi wanaopatikana kidemokrasia na wanaokubalika na watu.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo napenda kulizungumzia linahusiana moja kwa moja na uhuru wa vyombo vy'a habari, lakini pia haki ambazo zinalindwa na sheria na Katiba ya Taifa letu. Haki za binadamu na uhuru wa kusema unachukua msingi wake toka mwaka 1948 kutokana na Azimio la Haki za Binadamu liliolujikana kama *The Universal Declaration of Human Rights* na baadaye Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ambayo ilikuja kusainiwa na nchi mbalimbali zika-ratify katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, mfano, ni ule wa *The International Covenant on the Protection of Civil and Political Rights* na *The International Covenant on the Protection of Economic, Social and Cultural Rights*. Maazimio yote haya na Mikataba yote hii ya Kimataifa ililenga kutoa haki zaidi kwa binadamu na ililenga kuzitaka nchi wanachama wa Umoja wa Kimataifa kufuata misingi ya haki ambazo zinatambulika kama haki za misingi za binadamu.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi Tanzania tumesaini mikataba yote hii na pia tume-ratify Azimio la Haki za Binadamu la Mwaka 1948. Lakini leo hii tunaongelea uhuru wa vyombo vy'a habari. Kwa tafsiri ninayoifahamu ya uhuru,

hakuna uhuru utakaokuwepo bila ya kuwepo kwa mipaka, hakuna haki itakuwepo ya kwako wewe bila kuwepo haki ya watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima uhuru, ni lazima na haki pia viwekewe mipaka na vilindwe na sheria zinazoongoza nchi yetu. Sasa leo hii sisi tunatoa uhuru wa vyombo vyahabari, lakini badala ya uhuru huu kutumika vizuri tumekuta sasa uhuru umekuwa unakuwa *abused*, watu wanasema wanayoyataka na magazeti yanaandika wanayoyataka, uhuru umevuka mipaka, haki imepita kipimo na matokeo yake nchi yetu inaelekea kubaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa uchungu mkubwa sana nikizingatia kwamba, Taifa hili ni la kwetu sote na sisi leo hii wengine tuna watoto wachanga na tungependa warithi Taifa hili na tungependa kesho kutwa waje kuwa viongozi wa Taifa hili hali ya kuwa likiwa katika hali ya kutulia, hali ya kuwa Taifa likiwa katika umoja, upendo na mshikamano. Sasa kumekuwa na vitendo vyta uvunjifu wa haki, kumekuwa na vitendo vyta watu kutukana hata ndani ya Bunge wakidai tu kwamba wanatumia uhuru wao wa kusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa uhuru wa kusema hauwezi kuwa uhuru usiokuwa na mipaka. Haki ya kuongea haiwezi kuwa haki bila ya kutazama haki ya wengine pia kusikiliza, kwa sababu pia hata kusikiliza ni haki ya binadamu. Kuna watu wanaskiliza tunapoongea hapa, unapokuja hapa na kutukana, unapokuja hapa na kutoa maneno ya kejeli, unapokuja hapa na kudharau watu wengine, kuna watu wengine unawa-*offend*. Sasa pale ile haki ya watu wanaotusikiliza tunakuwa tumei-*abuse* na hilo sio jambo la haki na sio jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, leo hii yanaandikwa mambo kwenye magazeti, mambo ambayo yanalenga katika uchochezi, mambo ambayo yanalenga katika kutugawa

Watanzania katika matabaka, aidha ya makabila yetu ama ya dini zetu na magazeti yanashabikia, yana-*glorify*, yanaandika mambo ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, Uhuru huu wa vyombo vya habari sio uhuru unaozungumziwa katika Azimio la Haki za Binadamu, sio uhuru unaozungumziwa katika mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ambayo nimei-refer hapo mwanzoni, lakini pia haya mambo ya namna hiyo hayaruhusiwi hata na Katiba na Sheria ambazo zimebekwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, niombe hapa na nishauri sana kwamba, Wizara itakapoleta hiyo sheria ya uhuru wa vyombo vya habari muweke vipengele vya kuweka mipaka ambayo iko wazi kwamba, uhuru unaanza hapa na unaishia hapa. Kwa mfano, gazeti limetukana, gazeti linapotukana biashara ya gazeti ni matangazo, lakini matangazo hayo yanapelekwa kwenye gazeti husika kama gazeti lenyewe lina wasomaji wengi.

Mheshimiwa Spika, sasa ili kumdhiliti mwenye gazeti ambaye ametukana au ameandika habari ya uongo, ama ameandika habari ya uchochezi, ama ameandika habari ya uzushi ili kumdhiliti mmiliki wa gazeti hilo ni kumpunguzia kopi za magazeti ambayo anaweza kutoa kwa muda fulani. Tukifanya hivyo, mara mbili au mara tatu, tutaona vyombo vya habari vikiwa na nidhamu na vikiandika mambo ya ukweli.

Mheshimiwa Spika, Ndugu Charles Mulinda leo hii amehukumiwa na wenzake kwenye *Tanzania Editors Forum* na amesimamishwa kwa kuandika tu habari ambayo ye ye aliona kwamba ameitafsiri vizuri amefanya utafiti wa kutosha akaiveka kwenye *front page* ya gazeti lake inayohusu ugaidi na namna ambavyo wahariri mbalimbali wameshiriki katika ugaidi wa kumng'oa kucha ndugu Absalom Kibanda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuandika habari ile wenzake wamemfukuza wamesema habari ile ni

inappropriate na ni ya kichochezi. Kuna habari nyingi zinazoandikwa zinazofanana na hizo na zinahaririwa na Wahariri hao hao. Sasa kwa sababu hawa wana uhuru wa kuandika na kufanya wanachokitaka wamemuadhibu leo mwenzao, lakini pia wiki hiyo hiyo waliandika habari kwenye gazeti lingine moja la kunichafua mimi binafsi. Nikashangaa kwa nini Mhariri yule ambaye amekiuka pia maadili naye hakuadhibiwa na Tanzania Editors Forum. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, huu ni mfano mmoja tu, hivyo, napendekeza sasa Wizara muanzishe kitengo maalum cha kufanya *censorship* ya habari ambazo zinatolewa na cha kuadhibu magazeti ambayo yanakiuka misingi ya haki za binadamu kwa kuwaonea wengine na kuwaadhibu wengine. Kwa mfano, hiyo nchi ya Singapore, kule kuna bwana mmoja anaitwa Lee Kuan Yew, aliwahi kuwa Waziri Mkuu wa nchi ile, alitengeneza kitengo hicho na alikiweka lkulu.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo aliweza *ku-control western medias* ambazo zilikuwa zinaleta propaganda katika nchi yake na naamini hilo tunaliweza hapa. Leo kuna propaganda za kuangusha dola, kuna propaganda za uchochezi wa udini ama wa ukabila ama wa ukanda.

Mheshimiwa Spika, propaganda za namna hiyo zisiandikwe kwenye magazeti yetu na kama gazeti likiandika habari za namna hiyo lichukuliwe hatua ikiwa ni pamoja na kufungiwa. Rais Museveni juzi amelifungia *The Monitor* Uganda pamoja na redio zake zote na TV zake zote. Amelifungia kwa sababu lilikuwa linafanya kazi ya kuangusha dola, hivi tumerogwa na nani? Jamani, tuanze kutawala, tuanze kuongoza hii nchi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLAH: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante muda umekwisha. Sasa nitamwita Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Clara Mwatuka na Mheshimiwa Ritta Kabati wajilanda.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii ambayo imeshika nguzo za ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na ambalo Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla amelizungumza hapa kwamba, ni lazima tuweke mfumo na tuwasaidie wenzetu wa vyombo vyahabari kuweza kuzingatia na kusimamia maslahi yanayohusu ustawi wa nchi yetu. Si jambo zuri sana kwamba vyombo vyahabari kuwa ni chanzo cha kuweza kuamsha ari ya watu *ku destabilize* usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wakati wanachangia hapa, walisema jambo moja ambalo Waandishi walizungumza kiuzalendo sana, ni mgogoro baina ya Tanzania na Malawi. Lakini naomba niwakumbushe Waandishi wa Habari wa nchi nydingine jinsi ambavyo wanasisimama na kutetea na kusimamia ustawi wa nchi zao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 pale Tottenham, London, Uingereza zilitokea vurugu vijana wali-*riot* wakachoma magari, wakavamia maduka na wakawa wanahatarisha usalama wa nchi ile, lakini vyombo vyahabari vyote siku iliyofuata magazeti na televesheni na vituo vyadio vilandika kichwa cha habari kimoja kwamba wahuni wametaka kuvuruga amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini leo hii inapotokea tatizo la aina yoyote vyombo vyahabari ndio vinawekwa uzito wa lile jambo na kulitafsiri kila mtu ambavyo anaelewa. Hii haiweki sana ustawi wa nchi yetu. Naomba wazingatie weledi na taaluma yao kama vile ambavyo inawaelekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vipo vyombo vyabari vyakuchukulia mfano, si vyote ambavyo vinafanya vibaya. Nawenza nikachukulia mfano chombo cha habari cha *Clouds Media*. Wenzetu wa *Cloud Media* wanafanya vitu vingi sana vyatya ku-advocate na kujenga umoja mionganoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Wamekuwa ni wabunifu, wanatengeneza mambo mengi kuwasaidia vijana pamoja na changamoto nyingine ambazo wanazipata kuna wengi ambaao wamejitetahidi kuwakuza na sasa wanawageuka, ndio maisha ya binadamu, huwezi kuacha kuzaa kwa kuogopa kulea, endeleeni tu kulea na kuweni wabunifu kuweza kujenga nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika uhuru wa vyombo vyahabari, linalonikera sana, sasa umezuka mtindo wa ajabu kabisa na lazima Serikali mchukue hatua zinazotakiwa. Mwaka huu kuna magazeti katika kipindi cha mwezi wa Nne na hilo gazeti niko nalo hapa nitakuletea nakala yake. Wametoa picha Kiongozi wa Dini ambaye ameingia kwenye matatizo na mtu mwingine, unamchukua Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki unamweka pale picha yake.

Mheshimiwa Spika, hii jamani tunavunja taswira, viongozi hao lazima waheshimike, wanaoongoza watu, huwezi ukatoka ukamchukua Askofu Mkuu au Sheikh Mkuu ukaenda kumfananisha na mambo mengine ya mitaani, hili jambo tunavuka mipaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la *TBC*. Wabunge wengi wanailalamika *TBC* haipewi mitaji, *TBC* haiwezeshehi, wafanyakazi na watumishi wa *TBC* zamani ndio ilikuwa kimbilio, ilikuwa ukiajiriwa *TBC* ulikuwa unapata maslahi mazuri, lakini leo ndio wamekuwa duni sana. Kila siku tunakuja hapa tunapanga mipango mikakati, isiyokwisha.

Mheshimiwa Spika, tunataka sasa mtuletee mkakati wa kuweza kuimarisha *TBC* iweze kusikika nchi nzima, *TV* ya

Taifa isikike kote, Redio ya Taifa isikike kote. Mnasema mikoa 11, tuna mikoa 25 ukijumlisha na Zanzibar mitano mikoa 30 mnasikika 11, huu Utaifa huko wapi hapa? Hakuna Utaifa.

Pia nataka wakati mnajumuisha mtueleze nini kilichopelekea mitambo ya *medium wave* iliyozimwa pale Kunduchi na Nachingwea. Leo hii hatusikii Redio Tanzania kwenda katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, tunasikia sauti ya Tanzania Zanzibar. Sasa kama mnataka habari zetu tutazihamishia Zanzibar tuweze kusikia na tuweze kushirikiana nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nije katika michezo. Hapa watu wengi wanachangia, lakini wanazungumza hili jambo katika hali ya wepesi sana, hivi tuiulize Serikali imewekeza nini katika michezo. Rais ni kweli tunampongeza na tunamsifu sana kwa moyo wake wa kizalendo anamlipia kocha. Lakini huwezi ukazungumzia suala la kumlipia kocha ndiyo jitihada za Serikali, hizi ni jitihada zake yeye binafsi, Serikali haijawekeza hata kidogo kwenye michezo.

Mheshimiwa Spika, angalieni kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo, hakuna kiwanja hata kimoja ambacho mmeweza kujenga na wala kusaldia. Walimu wa shule za msingi na sekondari hawana mafunzo yoyote ya ukocha na ndio ambao wanawakuza watoto katika ngazi ya chini. Hamjawekeza kutoa mafunzo kwa Walimu wa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunatumia fedha nyingi kuweza kuendesha programu ambazo hazina manufaa. Wachezaji wetu ambao wamechezea timu za Taifa kina Edgar Fongo, Abeid Muziba, Malota Soma, Kaingila Maufi, Kipenga, tungeweza kuwatumia hawa wangekwenda kupata mafunzo kwa kutumia *Cultural Exchange Programme* ambazo nchi zingine wanazifanya.

Mheshimiwa Spika, tuwapeleke wakapate mafunzo, wajifunze waje kuwa makocha kufundisha katika nchi yetu, lakini tumekaa hapa tunalaumu *TFF*, Serikali imetoa kiasi gani kuwasaidia *TFF*, hakuna hata senti moja ambayo imepewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilzungumzie ni kuhusiana na suala la Mashindano ya Olympiki. Suala la Olympiki ni aibu sana. Kuna nchi moja inaitwa Kiribati, raia wa nchi nzima ile wako 14,000, lakini kwenye mashindano ya Olympiki walipeleka wanamichezo zaidi ya 60. Sisi tuko zaidi ya milioni 48,000,000, tunapeleka wachezaji wangapi? Wachezaji saba, halafu tunajisifu kwamba sisi tumefanya vizuri. Hatujafanya vizuri, lazima tuwe wabunifu.

Mheshimiwa Spika, mathalani ukichukua maeneo ambayo sisi tunaweza tukafanya vizuri zaidi ni masuala ya kuogelea. Ukienda Kilwa, Tanga, Kigoma, ukiona watoto jinsi ambavyo wanapiga mbizi na kuogelea, wanahitaji kuongezewa *skills* ndogo ndogo tu na wanaweza wakaingia kushindana.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuthibitisha hilo, watu tunaotoka maeneo hayo ya ukanda wa Pwani ya Maziwa na Bahari hata Mheshimiwa Komba au ukimchukua Mheshimiwa Zitto, ukiwapeleka kwenda kuwashindanisha kwenye kuogelea, utaona jinsi wanavyofanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilzungumzie ni usimamizi wa filamu. Nchi zote duniani zinaweka usimamizi wa filamu. Angalia nchi kama Marekani ambayo tumeisifu kuwa ndiyo inaongoza katika utandawazi wanaweka *PG 13, PG 11, PG 7* kwamba, *Parents guardians* kwamba, hawesi kutazama bila uangalizi wa mzazi.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa mtoto wa miaka mitatu au minne anakwenda kuangalia jinsi watu wanavyocheza muziki, wanavyotongozana mitaani huko, wanavyokimbizana vichochoroni huu utamaduni ambao tunaulinda kwa nchi

yetu ni utamaduni wa aina gani? Lazima tuweke misingi ya kusimamia utamaduni na taratibu ambazo zimekuwa zinatukuza na zinaendeleza nchi yetu katika nyanja ya ustaarabu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa nataka kuzungumzia suala la *TVIman*. Waziri lazima atupe majibu ni sababu zipo zinazopelekea *TVIman* isipewe leseni ya kurusha matangazo. Wamelipa *TCRA* imewapa kibali, taratibu zote zimekubaliwa na pia wameshalipa ada zinazotakikana, lakini mpaka leo haijapewa ruhusa ya kurusha matangazo yake. Hii ni *double standard* na haiwezi kukubalika na haya ndio matatizo ambayo yanachangia kuleta shida katika nchi yetu, tusilete *double standard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: *Okay, ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Albert Obama wajiandae.*

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kufikia asubuhi hii kuweza kuchangia katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile nimpongeze Waziri ambaye kweli ameonesha kwamba, yeye ni Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa jinsi alivyojiweka na kwa kweli anasema kiongozi ni wa kuongoza njia. Sasa lazima kiongozi aoneshe mfano wa lile analoliongoza. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni ya wakulima na wafanyakazi. Kila kukicha asubuhi wakulima wanachukua majembe wanakwenda mashambani na wafanyakazi wanakwenda makazini kwao. Sasa kwa kipindi hiki cha Bunge la Bajeti, wengi walikuwa wanapenda wasikie nini kinazungumzwa Bungeni kulingana na Wizara zinazowahu, nini

lakini wanakosa kusikiliza kwa sababu ya kule waliko makazini na hata sisi wenyewe hapa ndani ukiangalia hivi sasa, wengine wengi wapo kwenye Kamati, wengine wapo kwenye Maktaba kwa shughuli mbalimbali, yale yanayozungumzwa hapa nyuma hawawi na habari nayo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wakati gani hawa wangeweza kupata. Zamani kulikuwa na kipindi cha usiku *Star TV*, wale walikuwa wanaonesha Bunge na kwamba hasa walikuwa wanawapatia nafasi wale waliokosa mchana, wakati huu ndio walikuwa wanaona. Sasa kile kipindi hakipo kulikoni? Naomba Waziri atueleze kwa nini kipindi hiki kimeondolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna Mfuko wa Utamaduni, huu Mfuko umetengewa fedha kidogo ambazo ni shilingi milioni 100 na hizo ni kwa ajili ya mishahara tu, hakuna hata senti iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo. Sasa tamaduni hizi tutaziendeze kivipi kwa sababu watalii wengi wanakuja nchini kuangalia tamaduni zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sehemu kubwa ya vifaa vya tamaduni au vitu vya utamaduni vinahitaji fedha. Ukienda kwa wasusi kama alivyosuka Mheshimiwa Waziri pale, kunahitajika fedha, ukienda kwa wasusi wanaosuka kili au milala, wanahitaji fedha pia kwa sababu maliasili huwezi kwenda ukakata milala, wakakuachia hivi hivi, lazima ulipie.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati Mfuko huu haukutengewa fedha kwenye maendeleo, utamaduni huu utakwenda vipi? Kwa kukosekana fedha namna hii, ndiyo maana vijana wetu hivi sasa au wengi tunajua tamaduni zilizopo ni kwenye mavazi. Tunapenda sana kuiga tamaduni za kigeni ambazo hivi sasa kwa kweli nchi yetu inakokwenda tunaharibikiwa mno. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vijana wanapenda kuiga kila wanachokiona kutoka nje, cha kigeni, wanaona hapa ndiyo mahali pake tunakwenda na wakati, tumefika hapa.

Unamkuta kijana wa kiume siku hizi wanasema kuna kata 'K'. Suruali inaishia humu, nguo ya ndani ambayo haikustahili ioneckane nje, yeye ndiyo anafanya hasa ya kuonesha nje.

Mheshimiwa Spika, kuna aina mbalimbali za kunyoa nywele kwa watoto wa kiume. Utakuta amevaa hereni, utafiriki yuko India ambao wanavaa hereni na shanga wanaume. Sasa na sisi tumeiga hiyo kitu ambacho hakipendezi, mpaka nywele vijana wa kiume wanasuka siku hizi, wanasema wanakwenda na wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukienda kwa vijana akinamama huko ndiyo hatusemi. Kumeharibika kiasi kwamba Taifa letu linaaibika kwa ajili hiyo. Inafikia mahali sasa baba na mama kuangalia *TV*mbele ya mtoto au watoto haipendezi.

Mheshimiwa Spika, michezo inayoonekana kwenye *TV* ni ile michezo ya ajabu ajabu. Wanacheza michezo ile, watoto wa kike wanajua kazi ya kukata viuno tu. Sijui hawajui ni wapi inapofanyika kazi hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni vema wakaenda kuonesha ufundu wao kule sirini, lakini si sehemu za wazi, wanaharibu utamaduni wetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza vijana wanaocheza nao huko kwenye miziki wanajiheshimu, wanavaa suruali nzuri, shati zuri na hakuna anayeonesha tumbo au kitovu kwa watoto wa kiume. Lakini watoto wetu wa kike hawathamini miili yao, wamefanya miili yao maonesho kwa akinababa. Kwa kweli hali hii inasikitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mbunge mmoja juzi hapa anasema kwamba, kuna ukumbi mmoja ambao wanakwenda kucheza muziki uchi wa mnyama. Tunakwenda wapi? Tunaipeleka nchi hii wapi? Sisi wazazi tunawaona watoto wetu, unamwona mtoto wako anatoka ndani kavaa nguo pengine nyepesi inaonesha kila sehemu unamwangalia

tu. Wala huna cha kumwonya kwamba, wewe nguo hii vipi? Hakuna. Anakwenda nje. Aibu ile si ya yule tu mpaka wewe mzazi unayemwacha mtoto wako katika hali ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, wala si ajabu akinababa hapa wengine ndani wanawaacha wake zao wamevaa suruali ambayo ni kitambaa chepesi kinaonesha mpaka nguo ya ndani na isitoshe huku nyuma blauzi imeishia juu, akiinama kidogo, hapa mambo yameharibika. Lakini mwenyewe anaona ni vizuri tu. Wewe huyo ni mkeo, unataka aone nani sasa uzuri unaouona wewe mwenyewe? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nasema kwa uchungu, Serikali iangalie hili, hakuna heshima yoyote ya kuruhusu mambo haya ya michezo ambayo inachezwu kwenye majumba ya starehe na baadhi yetu tunakwenda kuburudika, unaona yale. Sasa unapomwona mtoto wa mwenzio vile na wa kwako unalinganishaje? Serikali ichukue hatua, ikomeshe mambo haya, sio mazuri. Tuige mambo mazuri, lakini si haya yasiyoelewaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwa vijana maana haya yanajulikana kwa kila mmoja. Mtwara pale mwaka juzi kulikuwa na uvumi kwamba, Rais amekataza akinamama wasivae suruali. Kwa hiyo, kuna vijana wadogo wadogo walikaa kwenye kona ya uwanja wa mpira wa Shule ya Rahaleo pale Mtwara wakiwa na fimbo zao. Walikuwa wakimwona msichana anapita amevaa vile wanamtandika mikwaju mwisho wakaacha kupita njia ile na wote wakaanza kujirekebisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, amri ikitoka mivao isiyoelewaka itakoma. Mheshimiwa Waziri nakuheshimu, nakuelewa na nakuamini kwamba utalifanya hili. Niombe Serikali ikusaidie kukomesha kitu hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la vijana. Vijana wengi siku hizi wameacha uvivu, wanajiunga kwenye vikundi ambavyo ni vya uzalishaji. Wengine wanakwenda kwenye

vikundi nya ufugaji, wengine kwenye mabustani, wengine kwenye uvuvi na mambo mbalimbali tu vijana wanajishughulisha siku hizi. Tatizo kubwa ni kwamba hawana mitaji. Watafanya kitu gani ambacho hakitahitaji pesa.

Mheshimiwa Spika, wanaolima bustani kuna mbegu za nyanya, vitunguu na mbogamboga zinahitaji pesa. Sasa hawa wanashindwa kupata vitu hivyo kwa sababu hawana pesa. Hivyo, naiomba Serikali iwaangalie vijana wapatiwe mikopo kwa ajili ya mitaji ili waweze kuijendeleza, waache na uzururaji. Tukiwapa mikopo hiyo, hawa wanaoitwa Wamachinga watakoma, watakuwepo wale tu ambaa ni wa zamani tu, lakini walioko vijijiini, hawatakuja mjini watajua kwamba, hakuna kitu kule, kitu kipo huku.

Mheshimiwa Spika, kumbuka Nanganga, kijiji ninachokaa mimi. Vijana wanajenga majumba kwa kuuza maji, sasa kupata baiskeli ni kazi. Wakipata mikopo wengi watanunua baiskeli ili waweze kupakia madumu kwa wingi ili wauze maji vijijiini waweze kuijendeleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wengine hawa wa vitunguu, wakipata mkopo watanunua mbegu, watanunua mashine za kumwagilia, badala ya kuchukua *cankwenda* kuzunguka mle itasaidia sana. Hivyo, Serikali izingatie. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante. Ila tu ulivyokuwa unafanya kwenye *Hansard* hata haikuonekana. Kwenye *Hansard* ulikuwa huonekani na vituko vyako. Sasa namwita Mheshimiwa Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Obama na Mheshimiwa Kapteni Komba.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa nianze kuwapongeza Mawaziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya kwa ajili ya taaluma ya vijana, habari na michezo.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Serikali kwa kuongeza pesa katika Mfuko wa Vijana. Lakini kwanza kabisa

nilishasema kwamba, katika hotuba zangu zote lazima nianze na walemavu, kwa sababu walemavu wamekuwa hawakumbukwi katika Wizara nyingi.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali iniambie, je, kuna juhudzi gani zimefanyika katika kuweka vyombo vyaa watafsiri kwenye vyombo vyaa habari kwa walemavu? Kwa sababu na wao wana haki ya kupata habari na kujua nini kinaendelea katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika michezo ya walemavu mmetenga kiasi gani ili kusaidia hii michezo iweze kuendelea? Kwa sababu hawa walemavu wamekuwa wakituletea medani mara nyingi sana. Nakumbuka Bunge hili lilishawahi kufanya michezo na Mabalozi kwa ajili ya kuwachangia walemavu. Je, Serikali hii inawawekea kiasi gani ili wafanikishe michezo yao Kimataifa?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwakumbuka walemavu, sasa nichangie kuhusu vijana. Kabla sijachangia kuhusu vijana kwanza nitumie nafasi hii kuwapa pole sana wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini kwa matatizo waliyoyapata siku ya Jumapili. Vijana wetu waliowekwa ndani, vijana waliopotoshwa kwa kukiuka ile Sheria ambayo tulikuwa tumeitunga kwenye Halmashauri na Mbunge wetu Mchungaji akafanya vurugu kiasi kwamba, hata wananchi wakakosa haki yao ya msingi ya kwenda kusali. Poleni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niulize kwamba, je, hii mikopo kwenye Halmashauri hawa vijana wanauelewa kiasi gani? Kwa sababu tumeona kwamba, vijana wengi sana hawana uelewa wa kuifikia hiyo fursa iliyoko kwenye Halmashauri. Pesa nyingi zinatengwa kwenye Halmashauri, lakini vijana hawaelewi wataifikiaje hiyo fursa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najua kwamba, katika ile asilimia kwa Halmashauri ile ya akinamama kwenye Jimbo la Iringa Mjini, mimi na mwenzangu Mheshimiwa Chiku Abwao na

Madiwani ndiyo tunauratibu ule Mfuko kuhakikisha kwamba kila Kata inafikiwa kwenye ile mikopo. Sasa je, hii mikopo ya vijana inaratibiwa na nani?

Mheshimiwa Spika, naomba hii iangaliwe ili vijana waweze kupata haki. Kuna vikundi vingi na vijana wengi wamekuwa wakijitahidi kuanzisha vikundi vyao, lakini hawapati hii mikopo na utakuta Halmashauri zetu zina uwezo mkubwa sana za kuwasaidia vijana hata kuwapatia mitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Halmashauri zetu zina *tender* za madawati, zina-*tender* za chaki na tuna vyuo vya VETA, lakini kwa nini *tender* zote za Halmashauri zisiende kwenye hivi vyuo ili zile faida ziweze kuwasaidia kama mitaji hawa vijana wanapomaliza hivi vyuo. Naomba Serikali iliangularie jambo hili kwa umakini ili vijana wetu wasiweze kuzurura hovyo au kuhangaika mpaka kuichuklia Serikali yao kwa ajili ya kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, Chama chetu cha Mapinduzi kinasema kwamba, watu wote wanatakiwa waishi maisha bora. Sasa naomba Wabunge wote, viongozi wote na watendaji wote tuhakikishe kwamba tunawapa maisha bora vijana wetu. Sisi wanasiasa tumekuwa tukiwatumia vijana katika kutatufa umaarufu wa kisasia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba muwatumikie hawa vijana, mmewaaahidi ahadi, lakini badala ya kutimiza ahadi mnawachochaea, mnawapa maneno makali ya kuichuklia Serikali yao na kuvunja Sheria za nchi hii. Naomba mkome kabisa. Hawa vijana wamezaliwa na akinamama, hawa vijana ni wetu wenyewe, wanapopata ulemavu mnatuachia sisi ndiyo tunapata matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba Vyama vingine viwaelimishe vijana, viwape yale waliyokuwa wametegemea kwa sababu walikuwa wametegemea kupata maisha bora. Kama mmeputa Majimbo wekeni mikakati, lakini msianze kuwapa vijana mambo mazito au mambo magumu.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu badala ya kusoma shule, mnakwenda kuwadanganya, wanakuja kwenye maandamano, juzi vijana 72 wamewekwa ndani kwa ajili ya kudanganywa. Naomba Sheria ije, wanasiasa wasiwapotoshe vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la michezo. Vijana wetu wana haki kabisa ya kucheza katika Halmashauri zao. Kuna viwanja vya michezo vya wazi vilitengwa kwa ajili ya michezo, vikavamiwa, wale waliovamia mmewafanyaje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa kwamba, wale ambao wamevamia wangeweza hata kubomolewa nyumba zao ili hata vijana waweze kupata haki. Je, ni lini wale waliovamia watabomolewa ili vijana wale waweze kupata haki zao?

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna hii michezo katika shule za msingi, mbona imesahaulika? Hii michezo sasa hivi Walimu wa shule za msingi wamekuwa wakihangaika. Kuna mkakati gani wa kuwawekea fungu? Maana tunajua kwamba, tukitaka wachezaji wazuri lazima tutengeneze vipaji kutoka shule za msingi ili viweze kuboreka.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaona kwamba kule ambako tungepata msingi bora hakuna fungu lolote. Mnategemea tutapata wachezaji wa aina gani? Najua hata kwenye nchi zilizoendelea, wenzetu wamekuwa wakiwaandaa watoto wakiwa bado wadogo kabisa. Sasa na sisi tunaomba Serikali irudi nyuma hili somo lifundishwe kuanzia shule za msingi na pesa iwekwe ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru wale wanaosaidia Serikali yetu kuleta vifaa vya michezo. Kama *Vodacom*, *TBL* na mashirika mbalimbali, basi tunaomba waangalie na hawa watoto wadogo wa shule za msingi ili waweze kufanya kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna majumba mengine ya starehe yamekuwa yakiweka kanda mbaya, watoto wetu

badala ya kwenda shule wanaishia kwenye hayo majumba. Naomba hilo liangaliwe na majumba mengine pia watoto badala ya kujifunza *tuition* na kufanya nini, jioni wanaangalia mipira mpaka saa sita hadi saa saba za usiku. Naomba pia haya majumba yaangaliwe na hili jambo likomeshwe.

Mheshimiwa Spika, vile vile niongelee kuhusu waandishi wa habari. Kwanza kabisa kama wenzangu walivyosema, hii *TBC* iongezewe fedha za kutosha kwa sababu yenye we inatakiwa ifike mpaka vijijiini. *TBC* ni chombo cha Serikali, naomba iangaliwe. Wenzangu wamesema kwamba, waboreshewe mambo yao mengi ili hata wanahabari wenye we waweeze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaomba Serikali iangalie hawa wamiliki wa vyombo vyahabari, wamekuwa wakiwanyanya sana wanahabari. Hawana mikataba, wengi wanafanya kazi za kujitolea na wapewe bima za afya na bima za maisha. Pia niwape pole wale waliopoteza maisha wakati wanatimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie kuhusu vazi la Taifa. Kunakuwa na fahari kubwa sana mtu anapovaa vazi la Taifa lake. Kuna wakati kulikuwa na mchakato mkubwa sana na ulianza kwa kasi kubwa. Sasa ile kasi imeishia wapi? Tunasikia raha tunapokwenda kwenye nchi za wenzetu, unamtambua huyu ni Mnaigeria, huyu ni Mhindi, huyu ni nani?

Mheshimiwa Spika, kwa nini hata tusivae Kimasai kwa sababu ni vazi la Tanzania hapa hapa. Hebu tunaomba kasi iongezeke na sisi tueleweke kwamba Mtanzania akiwa sehemu, unamtambua huyu ni Mtanzania. Pengine hata humu Bungeni tuvae Kitanzania zaidi kama nilivyo vaa mimi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Haya ahsante. Hatuna uhakika kama ni Kitanzania au vipi. Sasa namwita Mheshimiwa Albert Ntabaliba na Mheshimiwa Komba ajiandae.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii. Kwanza kabisa naunga mkono hoja. Nina mambo machache. La kwanza, nataka niongelee mwenge kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwenye ripoti ya Kambi ya Upinzani wamejaribu kusema kwamba mwenge hauna maana yoyote. Lakini wengine tumezaliwa tumekuta mwenge upo, mwenge umeasisiwa miaka ya sitini na mpaka sasa upo. Wito wangu wangu nataka tuendelee kuuenzi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tuliwasha mwenge na kuuweka Mlima wa Kilimanjaro ili uweze kumulika maadui wa ndani na nje. Kama Mwenge umeanza kukumulika ndani ukiwa ni adui, basi tulia. Tuliwasha Mwenge ili ulete mshikamano, Mwenge hauruki kijiji. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwanza una faida ya kuimarisha mshikamano, kijiji hiki kinaupokea mwenge kinawapa kijiji kingine kuonesha kwamba ni *chain* ambayo inaonesha kabisa kuna mshikamano. Lakini vile vile mwenge huu umepambana na ukabila kutoka kijiji kwa kijiji hadi Mkoa kwa Mkoa, hii ni moja ya kuua ukabila. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile umeweza kupambana na koo ambazo zinajitokeza kati ya koo moja hadi koo nyengine. Kwa hiyo, mwenge una faida nyengi na mwenge tulisema kwamba ulete matumaini pale ambapo pana mafarakano. Ndiyo faida yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwenge umekuwa na faida nyengi. Kwenye Majimbo yetu umehamasisha miradi, umekosoa pale ambapo watendaji wamefanya vibaya, wananchi wametoa maoni yao. Kwa hiyo, mwenge ni kitu ambacho lazima kiendelee kuenziwa.

Mheshimiwa Spika, wakati ule tulipoanza ulikuwa chini ya Chama cha Mapinduzi na mwaka 1992 tuliamua kwamba mwenge uwe chini ya Serikali. Kwa hiyo, sasa hivi ni jukumu la Serikali kukimbiza mwenge. Mwaka jana nilisikia katika Kambi ya Upinzani hawapendi mwenge na mwaka huu tena nimesikia. Nafikiri ni kitu ambacho ni lazima na hao vijana waanze kujifunza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili niipongeze Serikali. Nimesikia kilio cha *TBC*, *TBC* bajeti yao ya kufufua mitambo yao ili isikike nchi nzima ni bilioni 34, lakini kwa mwaka huu ili waweze kuanza walikuwa wameomba bilioni 11. Tunashukuru Serikali imeweza kuwasogezea na kuwapa hizi bilioni sita kama zilivyooneshwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mwanzo mzuri, tunaomba Serikali iendelee kusukuma. Mawaziri mnaosimamia dhamana hii kwa uchungu mlionao wa kutaka kweli *TBC* iwepo, nawapongeza na tumeshirikiana na nyie kwenye Kamati. Hii ni *achievement* kubwa. Kwa hiyo, songeni mbele twende mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba tena niipongeze Serikali kwa kuongeza fedha kwenye Mfuko wa Vijana. Mfuko wa Vijana unaongozwa na Profesa pale kwenye Wizara ile na anafanya kazi nzuri. Tumpe nguvu sasa hii mikakaki iweze kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niongelee ving'amuvi. *Startime* ilipoanza kuuza ving'amuvi ilianza kuuza kwa bei ndogo. Sasa hivi ving'amuvi vimepanda bei ambayo inawafanya watu wa kawaida washindwe kupata habari.

Mheshimiwa Spika, tulipowaita wakasema bei ile ndogo ilitokana na sababu kuwa walismehewa kodi na Serikali. Mkiona bei imepanda ni kwamba Serikali haikusamehe kodi.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali iendelee kuwasamehe kodi ili watu wengi waweze kupata ving'amuzi. Sasa hivi watu wengi wana TV lakini hawaoni habari, kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kuwapa ruzuku *Star Times* ili ving'amuzi viwe na bei ambayo watu wengi wanaweza kupata. Lingine, siku kama tatu niliona kipindi kile cha *Star Times* kikawa kinasema kwa nini Wabunge wanaotokea katika vyombo nya habari ni walewale! Waliongea mengi na mimi sitaki kwenda huko na nawapongeza hawa wanaotoka kila siku, lakin wazo langu ni moja, imefikia mahali ambapo sasa tunatetea wasanii kwamba kazi zao zinanyonywa hawapati faida ya wao kujishughulisha na ule usanii.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Wabunge ambao wanatoka kila siku na wanaaidia kuuza magazeti ya vyombo nya habari na wao waweze kulipwa. Kwa sababu wanaaidla kuleta mauzo kwenye magazeti ya vyombo nya habari. Kwa hiyo, hao Wabunge wanaotoka kila siku, ninawaombea na wao waanze kulipwa. (*Kicheko*)

SPIKA: Kama Spika hivi. (*Kicheko*)

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Sawa kabisa, hilo lilikuwa ni ombi kwa wale wanaotoka kila siku, kwa sababu sura zao zinatoka kila siku, familia zao zinawasoma kila siku na mambo yao yanasmwa kila siku, ni lazima walipwe sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuongelea suala la michezo kuhusu bajeti. Katika Wizara hii, tumeiangalia fedha inayowekwa kwenye maendeleo ya michezo ni kidogo sana na hasa mashulenzi kwenye Halmashauri zetu, kwenye bajeti hakuna fedha zinazotengwa kwenye bajeti zao. Kwa hiyo, ningombaa ishinikize TAMISEMI wanapokuwa wanapanga bajeti zao, fedha nazo ziweze kutengwa, ili michezo kwenye Halmashauri zetu, kwenye vijiji vyetu, zipatikane waweze kusaidiwa. Timu ya Wilaya inaenda kushindana Mkoani, inakwenda kwenye Halmashauri kuomba fedha angalau za kujikimu wanakosa. Kwa hiyo, ningetua wito kuwa tushuke

21 MEI, 2013

hii Wizara ya Habari na Michezo, michezo iende mpaka chini
isiwe kwenye Sera tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tuna Wilaya mpya ambazo
zimeanzishwa, tutahitaji Maafisa Utamaduni wapya na Ofisi
zao, tunaomba bajeti za Ofisi hizo ziweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa
kuheshimu kuwa wengi wamesema mengi, ninaomba niishie
hapo. Ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kateni Komba,
atafauatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Majaliwa.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika,
ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, nawapongeza
Viongozi wa Wizara hii; Mheshimiwa Mukangara na
Mheshimiwa Pedeshee Makalla. Mheshimiwa Mukangara,
ninampongeza kwa kudumisha utamaduni wa Mwafrika.
Tangu nimeanza kumwona huyu mama yeye kwenye kichwa
chake ni twende kilioni kila siku. Habandiki nywele, habandiki
nini, twende kilioni. Huo ndiyo utamaduni na ninadhani hilo
sasa lingekuwa ndiyo vazi la kwanza la Kitanzania kwa
Mwanamke wa Kitanzania. Inaitwa Utii wa Rodha. Kwa hiyo,
mama endelea kuwa mtii. (*Kicheko*)

Mchango wa pili ni kuhusu hii Sera ya Habari.
Ninataka kukwambia ukweli Mheshimiwa Spika, nchi hii kama
itaingia kwenye machafuko wakulaumiwa wa kwanza ni
Vyombo vyta Habari, Magazeti na TV Binafsi; wanachochaea
kwa nguvu kubwa na wenyewe wanajitahidi wauingize uwe Mhimili
usio rasmi na wanajitahidi wauingize uwe Mhimili wa Nne.
Sijui wataingiza kwa njia gani; *I don't know*, lakini Mhimili huu
ndiyo ambao utatuingiza kwenye machafuko; kwa nini?

Mheshimiwa Spika, tangu Wizara zimetoa Hotuba za
Wizara zao hapa, magazeti karibu mengi ukiondoa ya Serikali,
utakuta yanazungumzia vioja tu, hayazungumzii bajeti
inayotolewa kwa Wananchi. Hawazungumzii mantiki ya

bajeti Mwananchi anafaidika nayo vipi, ama Serikali iongeze nini. Hawazungumzii hilo, wao wanazungumzia vioja tu huyu kafanya hivi, huyu kamchambua huyu na huyu kafanya hivi na hasa Wapinzani na hasa hizi sura mnazoona zinauzwa hizi sura za kuuza hizi zinatoka upande huo. Mimi ninamuunga mkono Mheshimiwa Obama, walipwe pesa maana ni biashara. Nikwambie kuwa, magazeti ndiyo yanatureleka huko, wanatuambia tufuate mfano wa Kenya wanatuambia sisi.

Sisi Tanzania tufuate mfano wa Kenya kwa lipi katika amani? Wasifikirie kitakachotokea Kenya kitatokea kwetu, sisi tulishakaa na amani miaka mingi. Wakenya wanagombana katika makabila, wanagombana katika usomi, wengine wasomi na wengine siyo wasomi, maskini maskini kweli na tajiri tajiri kweli. Katika nchi yetu, mambo hayo mengi hayapo, lakini siku tutakapoingia katika machafuko kama wa mwaka ule wa Kenya, nchi hii haitarudi tena, itabaki kuwa na tabu mpaka Yesu arudi tena Duniani. Ninaomba sana Sera hiyo ije, lakini halahala tuzingatia kuimarisha amani ambayo tumewekewa urithi na wazazi wetu na Mungu mwenyewe miaka hamsini tumekaa kwa amani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na hii ina vionyesho tu, hebu fikiria sasa hivi *giants* wako wawili tu Duniani; Wachina na Wamarekani. Mchina anaona hawezi kukaa nchini kwake mpaka afike Tanzania, amefika Rais yule. Mmarekani amesema hawezi kukaa nyumbani kwake mpaka afike Tanzania, anafika Obama keshokutwa, haendi sehemu nyingine katika Afrika ni nchi mbili tu na hii ni ya tatu anafika kwetu sisi katika Afrika ya Mashariki na Kati. Kwa hiyo, hiyo ni ishara kuwa, amani hii tusiichezee. Kuna watu wengine wamezoea kujidharau wenyewe, sisi tunapendwa nje kwa sababu ya amani yetu, lakini magazeti mengi na watu wengine wanaopenda fujo, kila wakati amani hii wanaibeza tu. Ninafikiri hawa siku nyingine utakapochagua watu wengine kwenda Jeshini, wapeleke Jeshini wakanyooshwe kule maana wengi hawajaenda Jeshini wote hawa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia wale waliokuwa wanaleta leta maneno zamani walivyokwenda Jeshini wamerudi hapa wametulia, lakini hawa wanaofanya fujo hapa hawajajua Jeshi, kushoto kulia, geuka kulia, lala chini kwenda juu. Hawa akina Tundu Lissu waende Jeshini, safari ijayo waende Jeshini. (*Kicheko*)

SPIKA: Tena mwaka mzima.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Tena huyu Tundu apewe miaka miwili siyo mwaka mmoja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie habari ya *TBC*; kwa masikitiko makubwa sana *TBC* ni maskini. *TBC* ninayojua mimi ambayo ya zamani baadaye ikaja kuitwa *Radio Tanzania*, baadae imerudi tena *TBC*; haifanani kabisa na ile ya zamani. Angalia *Radio Tanzania* ya wakati ule ilivyojua imejengewa vituo vyake, kila mahala; Dar es Salaam, Arusha, Songea, sijui wapi Lindi, kila mahala na kila mahala tulikuwa tunapata *medium wave* vizuri kabisa. Leo ukienda kwenye vituo vile, *TBC* imekufa kabisa, *TBC* mitambo wanatembea buibui, wametanda maeneo yale yote na mitambo ile ni *analog*, ya zamani sana. Ninaomba sana Serikali, pamoja na kusema *TBC* ianze kujitegemea, lakini Serikali yenyewe kwanza ianze kuimarisha mitambo ya *TBC* kila mahali ilipowekeza.

Mheshimiwa Spika, bila *TBC* nchi hii hatutakwenda pazuri, kwa sababu vyombo vya habari hivi vingine vya watu binafsi, ataamua ye ye wakati wa kutoa taarifa atoe taarifa gani na aifiche taarifa gani, lakini kwa *TBC* atatoa taarifa ambayo Mwananchi atafaidika. Sasa leo hii inasikika Mikoa kumi na moja tu; ina faida gani hii? Ninaomba sana kila wakati tuangalie *TBC*, ipate pesa ya kutosha. Tunashukuru Serikali inaongeza bilioni sita, sawa wao waliomba bilioni 11, mwakani tena bilioni sita, saba, nane, mwaka mwingine bilioni sita, saba, nane, kwa maana hiyo tutaimarisha *TBC*.

Wengine hawajatembelea maeneo hayo, mimi nimefika maeneo hayo, kama msanii nimefika huko, lakini pia kama Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo. Ukienda kule

Nyerere Road, utaona huruma kabisa, Mtangazaji anapokwenda kutangaza kwenye chumba chake kile cha studio kama ni wakati wa mvua ni lazima awe na ndoo pembeni, ambayo atakingia maji yanayotoka juu yanaingia studio ili maji yale ama yasimchafue yeye lakini pia yasiingie katika vyombo ambavyo anatangazia. Anapata shoti hiyo, ndiyo hali ya TBC iliyoko sasa, ni hali mbaya sana. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amsikilize sana Mama yule wa utii wa Rhoda, ana matataizo makubwa, amwongezee bajeti yake. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, mwisho, michezo. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuimarisha michezo wa mpira na tumeona matunda yake. Ninampongeza sana Mheshimiwa Makalla, kwa kuimarisha michezo wa mpira na kuunganisha wale waliokuwa wanagombana. Ninawaomba Mheshimiwa Makalla na Mama Mukangara, tuinue michezo mingine. Zamani sisi tulikuwa ni kioo kwa riadha Duniani, leo Riadha imekufa.

Tulikuwa kioo kwa *basket ball*, Mheshimiwa Rais wetu alikuwa anacheza *basket ball* zamani, tuinue upande huo na tukienda *basket ball* ni gharama ndogo sana, tukiimarisha hiyo tutakuwa watu waangavu katika Dunia hii katika upande wa michezo. Tusifuate michezo wa mpira tu peke yake, mpira uko Dunia nzima, lakini watu wana sehemu ya kupitia kama hupitii kwenye mpira pitia kwenye riadha, kama hupitii kwenye riadha pitia kwenye ngoma, kama hupitii kwenye ngoma pitia ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana muda umeisha.

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza sana Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Fenella E. Mukangara (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Amos Makalla (Mb), Katibu Mkuu, Wakurugenzi Wakuu wote, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri ambayo imeonesha nia thabiti ya kuendeleza Watanzania kwa ujumla hususan vijana.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali ya CCM, kwa kukubali maombi ya Watanzania ya Lugha ya Kiswahili kuwa Lugha ya Kimataifa. Hivyo, ninazidi kuisihi Serikali kutumia Lugha ya Kiswahili kwenye maeneo yote ya kazi; mfano, Mashulen, Mahakamani na hata kwenye ziara za nje kuwe na wakalimani ili Viongozi wetu wahutubie kwa Kiswahili wanapokuwa na ziara kwenye nchi mbalimbali. Ikiwezekana, vijana wengi wajifunze lugha mbalimbali ili wawe wakalimani kusaidia Viongozi wetu kuzungumza Lugha ya Kiswahili ili Wananchi wawe wanasikiliza kujua Kiongozi anaongea nini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, Mahakama zetu kuendeshwa kwa kiingereza watuhumiwa na watuhumu wengi wanapoteza haki zao. Vilevile nakala za hukumu kuandikwa kwa kiingereza nazo hazikuwasaidia Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Vijana, nimepokea mabadiliko ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya vijana kuwa shilingi bilioni 6.1 kwa furaha kubwa sana, kwani awali zilitengwa shilingi bilioni 3.1. Inaonesha jinsi gani Serikali inasikiliza mawazo na ushauri wa Wabunge kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali igawe fedha hizi kwa uwiano unaozingatia usawa kwa nchi nzima tena zipelekwe kwenye Halmashauri zetu zisibaki Wizarani. Vilevile ziwe na usimamizi madhubuti ili vijana wote wenye nia ya

kujajiri wapewe. Fedha hizi zigawiwe kidogo kidogo siyo vikundi viwili vinapata milioni kumi, yaani milioni tano tano. Kuwe na sheria za kuwabana vijana ili wale wanaokopeshwa wawe wanarejesha kwani Mfuko huu ni wa kuzunguka.

Mheshimiwa Spika, ni faraja ya pekee *TBC* kuongezwa fedha hadi kufikia shilingi bilioni sita kwa ajili ya *expansion of TBC coverage*. Pamoja na kazi iliyokusudiwa ya kupanua upatikanaji wa masafa ya *TBC* ambalo ni jambo jema sana maeneo mengi nchini kupata televisheni hii, lakini pia ni vyema Serikali imalizie kazi ya kukarabati majengo ya Makao Makuu ya *TBC*, ambayo zimekuwa zikitengwa fedha bajeti mbili zilizopita lakini bado ukarabati huu haujamalizika. Naomba majibu ya Serikali wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika napenda kuishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Kuimarissha Michezo kila Halmashauri ili kuimarissha michezo kwa lengo la kufufua vipaji vipyta vya vijana wachezaji huko vijijini. Endapo Serikali itakuwa inatenga fedha na kupeleka kila Halmashauri, itawatia moyo sana wadau wa michezo kuiunga mkono Serikali kwa kuchangia Mfuko huo kwenye Halmashauri. Hii itasaidia sana wachezaji wanaotoka Wilayani kwenda Mkoani au Taifani kwenda bila shida, tofauti na sasa wanakuwa ombaomba sana, wanawategemea wanasiasia. Nitashukuru Serikali itakapotoa majibu kesho, hili pia litolewe maelezo kwani ni ombi la vijana huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa kipaumbele sana mpira wa mguu kwa kutoa michango mbalimbali pamoja na kutafuta kocha kutoka nje ya nchi. Ninaishauri Serikali kutoa ushirikiano wa juu pia kwenye mpira wa pete (*Netball*) ili kuwatia moyo wanawake kuendelea kujitokeza kwa lengo la kujajiri kama wanavyojajiri vijana wengine. Napenda kutoa mfano, Timu ya Mpira wa Pete ya Twiga ilifikia hatua nzuri, sasa hivi haisikiki tena. Nasubiri maelezo ya Serikali kesho wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zangu zinanipa kuwa, kuna kipindi Serikali iliunda Kamati ya Kulibuni Vazi la

Taifa, sijui Kamati hiyo ilienda wapi na matokeo yake hayajulikani. Kuwa na vazi ni jambo muhimu sana. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii na kuwatakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu ya Serikali kwa manufaa ya Watanzania. Nawapongeza sana Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Dkt. Mukangara (Mb) na Naibu Waziri, Mheshimiwa Amosi Makalla, kwa ushirikiano wao mzuri sana, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Ninapenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kuendelea kuwashaa Mwenge wa Uhuru kila mwaka, kwani unafanya kazi kubwa ya kuhamasisha maendeleo kwenye Halmashauri zetu. Kwa sababu ya Halmashauri kushindanishwa, zitaendelea kuibua Miradi ya Maendeleo kwa masilahi ya Watanzania. Hivyo, Mwenge wa Uhuru uendelee daima milele.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa changamoto wanazokabiliana nazo. Napenda kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, napendekeza Kitengo cha Utamaduni kipewe ruzuku, hapa namaanisha Kitengo cha Utamaduni katika Halmashauri za Wilaya zetu. Vitengo vyote vya Halmashauri hupata ruzuku isipokuwa Kitengo cha Utamaduni pekee. Ni vyema Kitengo hiki nacho kikaangaliwa. Ikumbukwe Kitengo cha Utamaduni ndicho kwa sasa kinatumika na kutegemewa katika Halmashauri kuleta mabadiliko chanya ya michezo, sanaa, pamoja na maswala mbalimbali ya kijamii. Mabadiliko yatapatikanaje bila kutengewa fedha au kasma kwa ajili ya uendeshaji? Aidha, Maafisa Utamaduni hapa nchini ni kama yatima, kwani hawajaliwi ukilinganisha na watumishi wengine. Kwa mfano, TAMISEMI hawawazungumzii kwa stahili stahiki

watumishi hawa na hata Wizara yenyewe ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, haina mawaidha nao ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda Wizara iweke utaratibu maalum kuhusu mavazi yanayoaliwa na wasanii. Baadhi ya mavazi hasa yanayoaliwa na wasanii wa kike ni kinyume na maadili ya Taifa letu. Ni vyema basi utaratibu wa kimaadili ukawekwa ili kudhibiti maadili ya kimavazi.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kiswahili kinafundishwa sana na Vyuo Vikuu vingi Duniani na nchi jirani kama Kenya wametokea kujipatia ajira. Hivi ni mkakati upi kama nchi na kama utamaduni na asili yetu tumejipanga ili Kiswahili kitoe ajira kwa Watanzania kwa wingi?

Mheshimiwa Spika, nne, tuangalie upya namna bora ya kuwapata wachezaji wetu wa Timu ya Taifa. Wapo vijana wengi wazuri walioko Mkoani ambao wakitumika wanaweza kutuletea heshima kubwa. Tabia ya kupata wachezaji kutoka Yanga na Simba zaidi inauwa na kukatisha tamaa wenye vipaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, hivi sasa Duniani, Kiswahili kinafundishwa kwenye Vyuo Vikuu mbalimbali na kinazungumzwa katika redio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, inaeleweka Tanzania ndiyo ina wataalam wakubwa wa Kiswahili hapa Afrika ya Mashariki na Duniani kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, ni kwa kiasi gani Wizara imewasaidia wazawa wetu wa Kiswahili hapa nchini kupata ajira nchi za nje za kufundisha Kiswahili? Kama Serikali haikuwa makini katika suala hili, siyo ajabu hata kidogo vyuo na redio zinazotangaza kwa Lughya ya Kiswahili ikawa walimu hao wanatoka katika nchi jirani ambaou uelewa wao wa Kiswahili ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) ni Shirika la Umma, linalomiliki mitambo ya radio na *television*. Kwa kuwa ni Shirika la Umma, uendeshaji wake katika suala la gharama unatokana na fedha ya umma inayochangiwa na Wananchi wote. Kwa sababu hiyo, kwa nini *TBC* karibu wakati wote wanashindwa kuzitangaza na kuziendesha mechii za mpira wa miguu hususan zile mechii kubwa, badala yake mara nyingi inaonekana ni *Star TV* ndiyo wanaozidesha mechii hizo? Je, ni lini *TBC* watazionesha moja kwa moja mechii zile kubwa na wakati mwingine za kimataifa? Haifanani hata kidogo; kwa mfano, mechii ya tarehe 18 Mei, 2013 baina ya Simba na Yanga kuoneshwa na *Super Sport* wakati *television* yetu ya *TBC* haikufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, *Taifa Star* ni Timu ya Taifa ya Nchi yetu na kwa maana hiyo ni Timu ya Muungano, inayohusu nchi mbili. Licha ya Timu hiyo kuwa na uwakilishi kutoka Zanzibar katika suala la wachezaji, lakini benchi la ufundi haliashiri huleta sura ya Muungano. Je, Wizara italirekebisha lini hili suala?

Mheshimiwa Spika, licha ya ongezeko la fedha za kuwaendeleza vijana kiuchumi kutoka shilingi 3.1 bilioni mpaka shilingi 6.1 bilioni, bado fedha hiyo ni kidogo, ukilinganisha na ukosefu wa ajira kwa vijana unaolikabili Taifa letu. Je, fedha hiyo inakopeshwa kwa vijana wawe wachuuzi au kwenye kilimo? Nchi hii haitaendelea kwa kuhimiza wachuuzi (wauza biashara ndogo ndogo). Ni kiasi gani fedha hiyo imewasaidia vijana kwa kuwa na ajira? Je fedha hizo zinazolipwa zinarejeshwa?

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono Hotuba ya Kambi ya Upinzani iliyowasilishwa na Waziri Kivuli, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Kilombero, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu fedha zilizopelekwa mashulenii kwa ajili ya michezo tangu Serikali iliporudisha UMISHUTA.

21 MEI, 2013

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kujenga Uwanja wa Michezo wa Wilaya ya Kilombero?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuinua michezo nchini kwa kuibua vipaji mashulenii na kuwapima kwa mitihani na kuendeleza vipaji hivyo kwa kujenga vyuo vya michezo kila Mkoa kwa kuanzia?

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuperomoka maadili nchini, Serikali haioni ni vyema kuanzisha na kuimarisha na kuendeleza ngoma za asili mashulenii sambamba na michezo mingine kwa kuwa ngoma hizo za asili huimarisha umoja na mshikamano?

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina viwanja vya michezo vingapi na viro maeneo yapi Mikoani na Wilayani? Je, vinatosha kwa sasa na kama havitoshi ni lini Serikali itaongeza kujenga?

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Wananchi kupata habari za uhakika ni jambo muhimu kwa ustawi wa Taifa lolote kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Ni kutokana na ukweli huu, naiomba sana Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha kuwa, Wananchi wanapata habari za uhakika. Kwa muda mrefu sasa Wananchi wa maeneo ya mipakani wamekuwa wakitegemea sana vyombo vya habari vya nchi jirani kutokana na usikivu mbaya wa vyombo vyetu hususan *TBC*. Hali hii inawaathiri sana Wananchi wa Wilaya ya Mkinga katika maeneo ya Daluni Mwakijembe, Ng'ombeni, Mayomboni na Kigongozi, ambao hawapati matangazo ya Televisheni na Radio. Tunaomba jitihada zifanyike kurekebisha kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Lugha wanatanabaisha kuwa, ili lugha ikue, hutumia vilahaja vya lugha nyingine kwa kuvikopa. Hata hivyo, ili lugha iwe na

ustaarabu, lazima jitihada za makusudi zifanyike kulinda utamaduni na stara za jamii husika. Inasikitisha kuona sasa vyombo vyetu vya utangazaji vya Taifa vimekumbwa na tatizo la kuruhusu matumizi ya lugha zisizo rasmi. Weledi wa uhifadhi wa stara ya Lugha ya Kiswahili na matamshi murua ya lugha yetu, yameathirika kwa kiasi kikubwa katika vyombo vyetu. Lazima turejee Katika maadili ya matumizi fasaha ya Lugha ya Kiswahili kama tulivyokuwa tukifanya wakati wa Redio Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tunashuhudia wimbi la makocha wa kigeni wa nchi mbalimbali kutumika nchini na nchi kadhaa za Kiafrika, Ulaya na kadhalika. Wimbi hili lazima litufundishe kuwa kuna fursa ya kiuchumi kwa Taifa na Wananchi kwa ujumla. Ni vyema kama Taifa tukawa na mikakati ya kuwaandaa makocha wa nchini ili nasi tuweze kufaidika, siyo tu na fursa hii ya kiuchumi, bali pia kuinua viwango vya michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la ajira kwa vijana, tunayo fursa kubwa ya kutatua tatizo hili endapo tutaipa umuhimu mkubwa Sekta ya Ufugaji wa Samaki Baharini, kuchimba mabwawa na kufuga samaki kwenye maeneo yote yenye mifumo ya kilimo cha umwagiliaji. Nchi kama Vietnam, Uganda, Kenya, Nigeria, Malawi, Msumbiji na Namibia, zimefanikiwa sana katika kukuza ajira kupitia Sekta hii ya Ufugaji wa Samaki.

Mheshimiwa Spika, mbona Kenya wameweza kuhakikisha kuwa wamechimba mabwawa 200 kwa kila Jimbo na hivyo kuwezesha vijana kujilajiri? Tuache kutumia nguvu kubwa za kuendesha *operation* za kuwachomea Wananchi nyavyo zao za uvuvi, bali tutumie nguvu hiyo na rasilimali zilizopo kuwawezesha Wananchi kumiliki mabwawa yao wenyewe ili waweze kuondokana na umaskini.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vya Serikali na vya Umma, vinaweza kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi na haki za Wananchi kupata na kutoa habari.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vya Serikali na vya Umma vinapaswa kuwa na sera ambazo haziashirii ubaguzi wala upendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imechukua hatua gani kufuatia malalamiko yaliyotolewa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wadau wengine, juu ya *TBC* kuonesha mwelekeo wa ubaguzi na upendeleo?

Mheshimiwa Spika, naomba kutangaza maslahi (ingawa si ya kifedha) katika suala hili kuwa nimewahi kufanya kazi kwa muda *Radio Tanzania (PRT)*, sasa *TBC Radio (TBC FM)*. Aidha, kwa sasa ni Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa CHADEMA. Hivyo, naelewa undani wa mawasiliano kati ya *TBC* na baadhi ya wadau kwa miaka mbalimbali; na ushauri kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ni kusimamia Sera ambayo itafanya *TBC* siyo tu itende haki, bali haki ionekane ikitendeka.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Wizara ya Fedha kufanya marekebisho ya Bajeti ya Maendeleo kwa kuongeza shilingi bilioni sita kwa *TBC* kwa Ofisi ya Mradi wa *Expansion of TBC Coverage (Project Code 4279)*, unapaswa kuambatana na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika majumuisho kueleza kazi mahususi zitakazofanywa chini ya Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zisiende hata shilingi moja katika kulipa madeni ambayo *TBC* inadaiwa sasa kufikia zaidi ya bilioni tano ukijumuisha na na madeni ya kulipia huduma ya kukodi mitambo. Ulipaji wa madeni ya *TBC* ufanyike kwa *TBC* kuweka mkazo katika kukusanya madeni; hivyo, katika majumuisho Wizara ieleze mkakati wa ukusanyaji madeni. Aidha, mikataba yenye kuipa mzigo *TBC* na hivyo kuongeza gharama kwa walipa kodi na Wananchi kwa ujumla, mathalani ya kukodi mitambo ya *satellite segment*, inayotolewa na Kampuni ya Marekani ya *INTELSAT* kuititia Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*). Hatua hiyo ichukuliwe

kwenye mikataba kati ya *TBC* na Kampuni ya *Star Times* kutoka China.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*), ni vizuri ikakamilisha mapema mazungumzo ya kutafuta fedha kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji. Mkakati uwe kufanya *TSN* itoe magazeti yake kwa gharama ambazo pamoja na kumudu kuendelea kufanya uzalishaji, iwezeshe Wananchi wengi zaidi kupata haki ya habari. Sera ya Makampuni ya Magazeti ya Serikali iwe ni kutoa huduma badala ya kuweka kipaumbele katika faida pekee. Mkakati uwe kuondoa utegemezi kwenye ruzuku ya Serikali, lakini wakati huo huo kutoongeza mzigo mkubwa kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuchangia katika kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri, lenye vijana wenyewe uwezo na malezi bora, linalothamini utamaduni wake na lenye umakini katika michezo, masuala yafuatayo ya nyongeza ni muhimu yakazingatiwa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana: Wizara ilitenga katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, shilingi bilioni 3.1. na Waziri wa Fedha amewasilisha marekebisho ya Bajeti kuongeza bilioni tatu kufikia bilioni 6.1. Pamoja na kuwa fedha hizi zimeongezeka, bado kiasi hakilingani na mahitaji. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, ifanye uamuvi kama ilivyofanya juu ya fedha chache zilizorejeshwa na mafisadi kwenye Akaunti ya Madeni ya Nje (*EPA*) kwenda Benki ya Rasilimali (TIB). Hivyo hivyo ifanyike kwa fedha za kutoka marejesho ya mpango wa kunusuru uchumi (*stimulus* na *package*) na madeni ya waagizaji bidhaa toka nje (*Commodity Import Support*). Wakati hatua hiyo ikitabuhiwa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha awezeshe kuongezwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, aidha, badala ya Mfuko kuwa kwenye Idara ya Vijana au kuwa kama Mradi tu ndani ya

Wizara, Mfuko huu uwe chini ya Baraza la Vijana la Taifa kama nilivyopendekeza kwenye kifungu cha 31 cha Muswada Binafsi niliouwasilisha kwa Katibu wa Bunge. Pia, katika kujibu hoja ya Kambi ya Upinzani, juu ya Muswada huo; Mwanasheria Mkuu wa Serikali aeleze iwapo katika kutoa ushauri juu ya Muswada Binafsi niliouwasilisha, alizingatia kuwa katika Muswada huo nilipendekeza Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuanzishwa kwa mujibu wa Sheria, kwa kuzingatia Ibara ya 135(2) ya Katiba ya nchi. Wizara izingatie kuwa toka mwaka 1993, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umekuwa ukiendeshwa Wizarani na kwenye Halmashauri bila kuwa na mfumo thabiti wa kisheria, kitaasisi na kiuongozi na matokeo yake ni kuwa kwa miaka 20 pamoja na tatizo la kutengwa fedha kidogo, pamekuwepo pia na ujisadi wa marejesho kutokuwasilishwa.

Wizara iwasilishe Bungeni tathminni ya Mifuko hiyo kwa miaka 20 na pia kuhakikisha kila Halmashauri inatenga asilimia tano kwa ajili ya vijana. Mpango wa kukopesha vijana kwa dhamana ya vyeti ulioanzishwa na Benki ya *CRDB* upanuliwe wigo wake na kuhusisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*UDSM*), kwa wahitimu wenye fani ambazo zinaweza kuwa na mchango kwenye uzalishaji na ajira. Aidha, mikakati mikubwa ya kandarasi inayogharamiwa na Umma iwe na kigezo cha mkandarasi kuonesha mchango wake kwenye ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, inapaswa kuondoa udhaifu uliojitokeza katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, ambao umechelewesha kazi na miradi ya kuchangia katika kuendeleza utambulisho wa Taifa, kwa kuwezesha upatikanaji mzuri wa habari, kuwezesha vijana kiuchumi na kukuza utamaduni na michezo kwa Umma kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Kusimamia Vyombo vya Habari uletwe katika mukutano wa kumi na mbili. Muswada wa Sheria ya Haki ya Kupata Habari usisubiri mpaka kufungwa kwa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari

kwani Miswada yote tayari wadau walishaandaa Rasimu zake na kuikabidhi kwa Serikali. Naomba kupewa nakala ya Ripoti ya Mkutano wa Maafisa Mawasiliano wa Serikali, uliofanyika Dodoma, tarehe 4 – 9 Februari, 2013, kwa kuwa kuna masuala yanayohitaji usimamizi wa Kibunge kuwezesha utekelezaji. Wizara iweke mfumo wa Bunge na Wabunge kupewa nakala ya uchambuzi wa kero za Wananchi zilizotolewa kwenye tovuti ya Wananchi ili yale yenyе kuhitaji usimamizi wa Kibunge, hatua zikachukuliwa. Uhamaji kutoka mfumo wa analogia kwenda dijitali haukufanyika kwa mafanikio Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine na unaathari haki ya Wananchi kupata habari; ni hatua gani zimeshukuliwa kurekebisha hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mkakati wa kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, naomba Wizara yenyе dhamana ya Vijana Ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara, ahadi iliyotolewa na Wizara hiyo kupeleka Waraka kwenye Baraza la Mawaziri kuhusu mapitio ya mikataba ya ubinafsishaji eneo la viwanda Ubungo. Wizara hiyo ilikubaliana na ushauri wangu wa kutenga eneo kwa ajili ya wazalishaji na wafanyabiashara wadogo vijana, hivyo ufuatiliaji ufanyike, ahadi hiyo itekelezwe. Naomba maelezo iwapo mpango wa kazi nje nje (KNN) kama umetekelawa katika Jimbo la Ubungo. Pia Wabunge tushirikishwe kutoa mchango wetu katika utayarishaji wa awamu ya pili ya KNN. Wizara irejee mchango wangu Bungeni tarehe 3 na 4 Februari, 2013 na kueleza hatua zilizochukuliwa tangu wakati huo. Aidha, naunga mkono maoni yaliyotolewa na Kambi Rasmi kuhusu Muswada Binafsi wa Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa niliouwasilisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa Waraka wa Vazi la Taifa, Wizara iweke wazi ripoti ya maoni yaliyokusanywa, kwa kuwa kazi hiyo ilitumia fedha za Umma na za watu binafsi. Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), likutane na Taasisi za Kiswahili za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*UDSM*), kuhamasisha kamusi za kwenye simu zilizoandalishi. Kamusi hiyo ya kwenye simu inaweza kuwa bidhaa itakayoendeleza Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Baraza la Taifa

(BASATA), lihusishe pia wasanii toka Jimbo la Ubungo katika mafunzo maalum yanayotarajiwa kufanyika Mkoani Dar es Salaam katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naomba Baraza la Taifa la Michezo (BMT), katika kuimarishe shughuli za michezo kwa wanawake kwa kushirikiana na *UK Sport International, Anita White Foundation* na Taasisi zingine, ihusishwe pia wachezaji toka Timu ya *Mburahati Queens* ya Manispaa ya Kinondoni. Aidha, Mradi wa *International Inspiration* uhamasishe pia Vijana wa Jimbo la Ubungo kushiriki kwenye michezo.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Vijana wa Kata Kumi Jimboni Igalula baada ya *Mfutakamba Igalula Super League Cup 2011/2012 Kata Kumi*, wachezaji kwenye mabano walichaguliwa kuja Timu B za Ligi Kuu za Taifa Goweko (3), Nsololo (3), Kigwa (3), Loya (3), Lutende (3), Miswaki (3), Miyenze (3), Tura (3), Kizengi (3) na Igalula (3). Wizara iliandikia Timu za Yanga, Simba, Azam, Mtibwa na Afrika Lyon ili kuwaingiza kwenye majaribio na kuchagua wanaofaa kujunga na timu hizi kubwa. Naishukuru Wizara kwa jithada hii. Ninajipanga tukishirikiana na Wizara ili vijana hawa wawasili Dar es Salaam kwa majaribio haya muhimu.

Mheshimiwa Spika, nilipata habari kuwa *EU* inatoa msaaada wa kutusaidia nchini rasilimali fedha za kusaidia utamaduni uimarike hapa. Je, tumejipangaje katika kulinda taswira, mustakabali na uhimilivu (*sustainability*) wa mila, desturi na utamaduni wa nchi yetu kwa misaada tunayopata kutoka nje?

Mheshimiwa Spika, kujenga uwezo katika tasnia za filamu, uigizaji na michezo kunahitaji ubunifu. Pia kuunganisha uzoefu wa ndani na nje (*Networking*). Je, Wizara imeweka mkakati gani ili kuviiuba vipaji vyta ndani, kuvikuza na kuvipatia viunganishi (*Linkages*) na nchi nyingine bila kuathiri mila, desturi na tamaduni zetu na kulinda vizazi vyta sasa na vijavyo?

Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kuunganisha Sekta za Michezo, Filamu, Kujihami, *Marshal Arts* na *Karetee* hasa wasichana na nchi kama India (Bollywood), Marekani (*Hollywood Universal Studio*) na nchi nyngine kama Brazil (mpira wa miguu chipukizi), Italy, Spain na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wizara iboreshe michezo tangu *Kindergarten* (Chekechea), Shule ya Msingi na Sekondari, kwa kuwa na makocha na walimu wa michezo na mazoezi (P.E.) muhimu sana kwa nchi yetu.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuweza kutoa mawazo yangu kwa njia ya maandishi. Pamoja na kuchangia kwa kuzungumza jana, lakini nina ya kuongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyosema kuwa, mimi ndiye mwanzilishi wa kuleta hoja ya kusaidia wasanii ndani ya Bunge; hivyo, najua tulikotoka na tulipo. Ninaweza kusema kuwa, hatua iliyochukuliwa na Serikali ni kubwa na mafanikio ni makubwa, kwani hatimaye wasanii wanaongelewa sasa ndani ya Bunge na kutambulika hata kuingia kwa kusikiliza mjadala. Kwani kabla ya pale, walikuwa wakihangaika kuunda vikundi tu visivyo halali au kutambulika popote na havikuleta tija. Hivyo, naipongeza Serikali kwa hatua hii.

Shida yangu ni moja tu; hebu Serikali iondoe tabaka zilizopo kwa wasanii ambazo zinawagawa wasanii, kuna kundi la wasanii wa juu na wa chini na mgawanyiko huu unaletwa na watu au vyombo ambavyo wanadai kuwa-*promote* wasanii au kuingia nao mikataba isiyo na tija kwa wasanii, maana hata mikataba hiyo hakuna anayewasimamia kisheria. Hali hiyo inasababisha baadhi ya wasanii kutojiunga na mashirikisho ambayo yapo kisheria na ambayo wangeweza kuwa msaada mkubwa kwa wasanii na Serikali kwani mambo yote yan gepitia pale. Hivyo, naomba Wizara mtangaze rasmi kwamba, wadau wote wa sanaa zozote, wawe wanachama kwenye mashirikisho ya

sanaa zote. Pia mashirkisho yawezeshwe, Serikali kupitia BASATA iyasimamie kwa ukamilifu na kanuni ziwe wazi. Hapo itaondoa matabaka na migogoro inayotokea kama ya kina Lady JD, kwani kama wangkuwa ndani ya mashirkisho, haya yote yasingetokea.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; naomba sana suala la Vyombo vyta Habari vinavyotumia kazi za wasanii, ikabidhiwe *TCRA* kwa kushirikiana na *COSOTA*, waweze kuwahimiza kulipa mrabaha kwa kila kazi wanayotumia. Naiamini *TCRA* kwani wapo makini katika kazi zao na ndiyo wanaotoa vibali au leseni ya vyombo vyta habari vyta utangazaji; hivyo, wao itakuwa rahisi kuwasimamia. Tafadhali narudia, *TCRA* wakabidhiwe jukumu hilo pamoja na kusimamia nyimbo zinazotumika kama milio kwenye simu. Naomba majibu ya hili ama nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, Maafisa Utamaduni wa Wilaya na Manispaa wako chini ya TAMISEMI na pia hakuna Maafisa Utamaduni wa Mikoa. Sasa naomba kujua; Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nao? Maagizo na mipango ya Wizara inafanikiwa vipi? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, suala la nne, bado narudia suala la stika siyo suluhisho la kumaliza tatizo la wizi wa kazi za sanaa. Bado Kanuni na Sheria havijakaa sawa. Tafadhali mpango huo usitishwe ili tukae na wadau na kuweka Kanuni kwa ajili ya kumnufaisha msanii.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Njombe na hasa Wilaya ya Wanging'ombe hatusikii Redio (*TBC*) na wala Televisheni hakuna. Je, Bajeti hii ya 2013/2014 na hasa baada ya miaka 51 ya Uhuru sisi Wanajombe itatuletea majibu yoyote?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo Maafisa Michezo kwenye Mikoa na Wilaya zetu, naona kama hawana mikakati yoyote ya kuendeleza michezo zaidi ya kusimamia mchezo wa mpira wa miguu. Naomba sana Maafisa hawa wasimamiwe na kuwajibishwa pale wanapokuwa wameshindwa kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, mapato ya viingilio kwenye michezo yawe kwa uwiano wa 60:40, yaani asilimia sitini zipewe timu na asilimia arobaini iwe kwa maeneo mengine ili kuinua viwango vya wanamichezo.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vina umuhimu wa pekee katika kuleta upashanaji habari katika jamii hapa nchini. Hata hivyo, kama vikitumika vibaya vyawenza kuiangamiza jamii badala ya kuisaldla.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) ni Chombo muhimu cha Umma katika kuelimisha, kutangaza Sera na Mikakati mbalimbali ya Serikali na pia kuuelezea Umma Programu mbalimbali ambazo Serikali imepanga na hivyo Umma wa Watanzania kuunga mkono Mipango yote ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili haya yawenze kufanyika, Serikali ni lazima iongeze bajeti kwa *TBC* ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba, nchi yetu inalinda tasnia ya habari, lakini uhuru huo umeanza kutumiwa vibaya na baadhi ya vyombo vya habari. Mfano, Redio Imani na Adhana, zilitumia vibaya uhuru huo kwa kuanza kukashfu Dini ya Kikristu na Viongozi wake.

Mheshimiwa Spika, cha kuchangaza ni kwamba, *coverage* ya vyombo hivyo ilikuwa takribani nchi nzima, ingawa Sheria hairuhusu chombo cha habari cha binafsi kuwa mawimbi yake kusikika nchi nzima. Naomba Serikali

ichunguze ni nani alitoa kibali kwa vyombo hivyo kuwa na *coverage* ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana hautoshelezi na hata mgawanyo wake haueleweki kwani usimamizi wake siyo mzuri.

Mheshimiwa Spika, Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu (*Taifa Stars*) inaelekea kutuondolea aibu ya miaka mingei. Naomba ipewe kila aina ya msaada ili wachezaji wetu na viongozi wawewe kusimamia mazoezi ili mechi zote zilizobakia ipate kushinda. Naishauri Serikali ianzishe *Sports Academy* hapa nchini ili tuandae vijana wetu katika michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utamaduni inapaswa kujengewa uwezo ili Sekta hilipate kuchangia katika uchumi wa nchi yetu. Uhifadhi wa makumbusho ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nchi nyngi duniani zimefanikiwa kwa kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wao. Naomba juhudzi zifanywe kuhakikisha tunahifadhi utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba *TCRA* na Idara ya Habari Maelezo wawe makini katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuepusha madhara yanayotokana na Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, hakuna uhuru usio na mipaka; siku zote *TCRA* na Idara ya Maelezo wafuatilie mwenendo wa Vyombo vya Habari na wachukue hatua kali vinapokiuka mipaka yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. NAMELOK E. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza Wizara, kwa kazi nzuri inayofanya, pamoja na kuwa na changamoto nyngi ambazo mnakutana nazo. Pamoja na hayo, ningependa kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ijitahidi kujenga vyuo vya michezo zaidi hapa nchini hata kwa kutafuta mbia, lakini pia Wizara ihamasishe zaidi wawekezaji katika sekta hii. Kuna aina nyngi sana za michezo, ambayo hapa nchini haifahamiki, watafutwe wataalamu wa kuja kuelezea michezo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia iwasimamie waandishi wa habari hasa hao wanaoandika habari ambazo hazina ukweli na pia hawaandiki majina yao. Je, Wizara ina mpango au mkakati gani wa kuhakikisha mambo kama hayo yanakomeshwa mara moja?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa vijana wengi wamejunga katika *SACCOS* na kununua pikipiki. Kama tunavyofahamu, vijana ndiyo Taifa la kesho; je, Wizara ina takwimu sahihi za kujua ni vijana wangapi hivi sasa wamepoteza maisha au kupata ulemavu kwa ajili ya bodaboda hizo? Zipo Hospitali ambazo hivi sasa ukifika wakijua chanzo cha ajali ni bodaboda, hawahangaiki zaidi ya kuamua kukukata miguu au mkono. Je, Wizara ina mpango gani na vijana wetu hawa? Tusipoangalia hili tutakuwa na Taifa la Vijana walemovu wengi. Ni bora vijana wakapata Elimu ya Usalama Barabarani na Wizara ikisaidia.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa tumekuwa tukizungumzia Vazi la Taifa, Wizara iharakishe mchakato huu tupate Vazi la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. VICKY P. KAMATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi nichangie kwa maandishi juu ya hoja ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Kwanza kabisa, napenda kuunga mkono hoja hii na kutoa ushauri kidogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kubwa sana, inabeba habari kwa upana wake, vijana kwa upana wake, utamaduni na michezo. Kwa kweli naona ni Wizara kubwa mno, kiasi

kwamba, kuona ufanisi wa Watendaji katika Wizara hii ni kazi sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itoe vijana ipeleke Wizara ya Kazi na Ajira ili iunde Wizara ya Vijana, Kazi na Ajira, kisha Habari ihamie Wizara ya Sayansi na Teknolojia. Hapa ibaki Utamaduni na Michezo tu. Itasaidia sana kuona ufanisi kwani watendaji watajikita kwenye michezo na utamaduni tu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nilete kwenu maombi ya Vijana wa Geita. Kwanza, wanaomba mfike na kuzungumza nao juu ya kero zao mbalimbali kuhusiana na suala zima la michezo. Pili, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri, mfike Geita ili kutoa zawadi kwa watakaoshinda kwenye Finali ya Kombe la Vicky Kamata.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Spika, nimeipitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Dkt. Fenella Mukangara (Mb) na ningependa kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matangazo ya kutoka mfumo wa analogia kwenda dijitali yalikuwa na lengo la kuboresha matangazo na kuyafanya yawafikie Watanzania wengi huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzima mtambo wa analogia na kubakiza dijitali peke yake, kusema ukweli utaleta madhara na hasa kwa upande wa watumiaji wa Televisheni huko vijijini, kwani matangazo ya dijitali, yana-*involve* malipo ya kila mwezi yanayoanza shilingi 9,000 kwa mwezi na kuendelea mpaka 160,000.

Mheshimiwa Spika, tuchukulie kiwango ni shilingi 9,000; je, ni Watanzania wangapi wataweza kumudu kulipa shilingi 9,000 kila mwezi huko vijijini? Pengine ningependekeza kwamba, stesheni zote za TV za Taifa (kwa maana za

Kitanzania), kama vile *TBC, ITV, DTV, Channel Ten, Star Times* na kadhalika, ziendelee kuwepo na zioneshwe bila malipo ili Watanzania waweze kupata fursa ya kupata taarifa na matangazo na mambo mbalimbali yanayoendelea ndani na nje ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu huu mpya wa kupeleka matangazo kwa mfumo wa dijitali, bado matangazo hayo hayajawa safi, mara nydingi Televisheni zimekuwa zikonesha matangazo yake kwa kukwamakwama na wakati mwingine matangazo hayo huganda kwenye TV kwa muda. Serikali iendelee kuboresha mfumo huo wa matangazo kwa njia ya dijitali ili kasoro hizo ndogondogo ziondoke.

Mheshimiwa Spika, Televisheni ya *TBC* inaongoza kwa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Redio yetu ya *TBC* ndiyo Redio pekee ambayo Watanzania wengi wanaitegemea kupata taarifa mbalimbali. Malalamiko kuhusu *Radio TBC*, kutosikika hasa huko vijijini ni mengi mno, unaweza kufungua redio yako kwa huku Mikoa ya Kusini ukapata *Radio Free* iliyoko Mwanza, lakini huwezi kusikia matangazo ya *TBC* ambayo mitambo yake ipo Dar es Salaam. Ukimfungua redio, unaweza kupata *Radio Msumbiji* na *Radio Malawi*, badala ya *TBC* iliyoko humu humu Tanzania; tatizo ni nini? Wananchi wengi wamekuwa wakituagiza kila mara tunapokuja katika Vikao vya Bunge, nendeni mkawaambie kwamba, sisi huku sasa *TBC* hatuipati kabisa! Je, kwa nini Televisheni na Redio za watu binafsi zinafanya kazi yake vyema, huku TV na Redio ambayo Watanzania wengi wanaitegemea inaendelea kuchechemea?

Mheshimiwa Spika, maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Habari katika Hotuba yake hii ya Bajeti, tunatarajia yatafanyiwa kazi ili kuboresha huduma za vyombo hivi kwa maana ya *TBC₁*, *TBC₂* na *Radio TBC*. Kwa manufaa yetu sisi Watanzania wengi tulioko huko vijijini, ni matarafjio ya wengi kwamba, mipango na mikakati iliyopangwa itafanyiwa kazi

na tunategemea kwamba, mwaka ujao (2014), *complains* hizi hazitakuwepo kabisa au zitakuwa zimepungua sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuelekeza mchango wangu kwenye suala la utamaduni wetu. Ni hakika mpaka sasa hakuna mipango madhubuti ya kulinda na kuhifadhi tamaduni zetu. Leo hii Tanzania ina takribani makabila zaidi ya 120 na kila kabila lilikuwa na tamaduni zake au marithisho ya asili katika makabila yetu. Hakika sasa suala la uhifadhi wa tamaduni zetu haupo kabisa, kwa sasa unakuta hata mtoto au kijana wa chuo hawezি kuongea lugha yake ya asili ukiachia mbali Lugha ya Kiswahili ambayo ni Lugha ya Taifa. Hakika, kuwepo kwa utandawazi kumechangia kupoteza ile maana na uadilifu katika kutunza utamaduni wetu. Suala la mavazi ya tamuduni zetu, leo hii mavazi ya asili hayavaliwi na yamepoteza kabisa maana yake, ukiachia mbali baadhi ya makabila machache mfano Wamasai, Wanyaturu, lakini sehemu nyingi sasa tunaiga mitindo ya Kimagharibi zaidi kuliko kulinda utamaduni.

Mheshimiwa Spika, suala la uhifadhi wa nyimbo, hadithi, vitendawili na kadhalika halijafanyiwa kazi kabisa. Pale inapotokea kazi hiyo imefanywa inakuwa si kwa ukamilifu mkubwa. Hivyo, natoa rai kwa Wizara kuliona suala hili kwa ukaribu sana na kulifanya kazi. Tunaweza kutumia nguvu na pesa nyingi kuhangaika na tabaka la juu kwa kuangalia yaliyopo mitaani, lakini tunasahau ngazi ya chini kwenye familia zetu, koo na tamaduni. Hakika tukikazia hapo, tutaweza kutunza tamaduni zetu na hivyo kuwa na Taifa lenye utamaduni wa dhati na imara.

Mheshimiwa Spika, suala la michezo; katika nchi yetu mchezo unaofahamika ni mpira wa miguu tu. Kuna idadi kubwa ya michezo ambayo haipewi kipaumbele, kuna

michezo ya asili mfano kulenga shabaha, mchezo wa bao, mieleka na kadhalika. Leo hii katika mashindano yoyote yawayo, michezo hii haipewi kipaumbele. Ni wakati sasa kuona umuhimu wa kuhuisha na kuimarisha michezo hii ya asili, kwani ina mafunzo muhimu kwenye jamii. Suala la utafutaji vipaji halipewi umuhimu wowote! Leo vijana wengi wanaocheza mpira ni wale walioko mjini tu, wakati vijana tele wenye uwezo na nidhamu wanaachwa vijiji. Ni wakati sasa kuangalia vipaji kutokea vijiji kuliko kujikita kwenye masuala ya Kimaghribi zaidi; mfano, mashindano ya urembo yanavyopewa umuhimu na msisitizo mkubwa, ukijiliza katika makabila yetu ya asili ni wapi suala hilo liliibuliwa na kuasiwa? Je, katika makabila yetu zaidi ya 120 ni wapi utamaduni huo umehifadhiwa?

Mheshimiwa Spika, suala la makumbusho na hifadhi ya mambo ya kale; leo hii hakuna taarifa za dhati kuhusu makumbusho haya. Vijana waliozaliwa au wanaozaliwa sasa hawana kabisa taarifa za nini makumbusho hayo yamehifadhi. Sasa ni jukumu la Wizara, kupitia Maafisa Utamaduni ngazi ya Mikoa na Wilaya kuhakikisha kuwa, wanatoka ofisini na kufanya kazi yao katika jamii. Leo hii kazi ya Afisa Utamaduni na Michezo sana sana ni kuratibu vikundi vya nyimbo na maigizo wakati wa mbio za mwenge. Je, mwenge ukishapita wanafanya kazi gani? Hawaendi kwenye jamii walau kuzijengea uwezo wa kutunza hizi tamaduni, hakuna mpango mkakati walau wa kuwatambua watu mashuhuri ambao ni kumbukumbu na hifadhi ya hizi tamaduni, ikiwa ni pamoja na hifadhi ya mali kale.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara iyafanyie kazi masuala haya kwa ukaribu sana.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, michezo ni afya, burudani, ajira na kadhalika, inapaswa kuimarishwa kwa Watanzania wote lakini muhimu sana ni katika shule na vyuo vyetu. Kuna shule, hasa binafsi wanapewa vibali kuanzisha shule au vyuo bila kuwa na maeneo ya kutosha au viwanja vya michezo. *Confined spaces* au maeneo makubwa bila viwanja vya michezo

kunaathiri hata taaluma za vijana wetu. Nashauri Serikali itunge sheria kupiga marufuku uanzishajji wa shule au vyuo vinyavokosa mahitaji haya muhimu. Hiki kiwe mojawapo ya vigezo nya kusajili shule au chuo.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Watanzania maskini ambao wengine hupata habari kuptitia Redio hususan *TBC* pamoja na usikivu wake hafifu, wangependa hasa vijjini kupata majadiliano ya Bunge kama wenye kipato wenye *TV* wanavyopata fursa hiyo. Idadi kubwa ya wananchi vijjini wanategemea radio, *TBC* Chukatisha kipindi cha Bunge Mara baada ya maswali, wangependa kusikia nao majadiliano ya Bunge kwa ukamilifu wake kama wanavyopata katika *TV*.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, naomba kutumla fursa hili kuchangia hoja ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tabia ya wafanyabiashara mbalimbali mfano kwenye *disco*, baa au *promotion* ya bidhaa mbalimbali kuwaruhusu vijana haswa wa kike kucheza wakiwa wamevaa nguo fupi sana au gauni zinazoonyesha viungo au sehemu nyeti za miili yao. Jambo hili ni kinyume na utamaduni wetu. Nashauri Wizara hii kukemea jambo hili ili kuweza kuheshimu na kuendeleza utamaduni na heshima ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kundi kubwa la vijana haswa katika Jiji la Dar es Salaam wamekuwa wanatumia muda wao mwingi vijiweni. Pamoja na kuwa kuna tatizo kubwa la ajira kwa vijana hawa lakini katika hali halisia wengi wamekuwa hawajishughulishi na kutafuta ajira au kujiajiri, kundi hili limekuwa linajishughulisha zaidi na siasa za vijiweni na ni hatari kwa mustakabali wa nchi yetu. Nashauri Serikali yetu na Wizara kutoa elimu ya kutafuta ajira na kujiajiri katika biashara ndogondogo badala ya kukaa tu huku wakiwa na maisha magumu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

21 MEI, 2013

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, nashauri na kupendekeza Wizara iweke mkazo michezo mingine na siyo michezo wa mpira wa miguu (*football*) tu.

Mheshimiwa Spika, michezo ya akinamama, napendekeza na kushauri kwamba pamoja na michezo ya wanaume, michezo ya akina mama nayo ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, hoja naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD ABUU JUMAA: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunipa nafasi hii nichangie bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake nzuri yenye mikakati mizuri na dhahiri ya kutatua matatizo ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo hapa nchini. Bajeti pia imelenga kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, imeweka mikakati mizuri ya nchi katika kukuza utamaduni, michezo na kuboresha sekta ya habari na vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa Wizara hii, napenda kuanza kuchangia katika sekta ya utamaduni. Nchi hii tumejaliwa kuwa na makabila mengi tofauti na kila kabilalina tamaduni zake lakini tumekuwa wa mwisho katika kuzienzi tamaduni zetu, imefikia mahali sasa hivi hata huko vijijini ambako ndiko walikuwa wamebakia pekee kuzienzi tamaduni zetu na wao sasa wameanza kuacha kufanya hivyo. Cha kushangaza mpaka leo Taifa letu hatuna hata vazi la taifa, hii ni aibu kwa Taifa kwani hatuna utambulisho wowote tukienda huko nchi za nje zaidi ya utambulisho wa kusema kuwa mimi ni Mtanzania, haipendezi hata kidogo kwani wenzetu wamekuwa wana utambulisho wa mavazi na

vitu vyao. Kama sijakosea, nakumbuka kulikuwa na mchakato wa kutafuta vazi la Taifa na uliachwa kwa wabunifu kufanya ubunifu wao na kupata vazi moja ambalo litatutambulisha, lakini mpaka leo sijui huo mchakato umefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, pia tungetilia mkazo kwenye lugha yetu ya Kiswahili kwani mpaka sasa imekuwa ni utambulisho mzuri, mahali popote pale ukienda na kusikika ukizungumza Kiswahili unajulikana kuwa umetokea Tanzania. Naiomba Serikali kuendelea kutilia mkazo katika hilo ili lugha yetu ya Kiswahili izidi kukua kwani mpaka sasa Mataifa jirani yanayozungumza Kiswahili yanazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna vitu vingi sana ambavyo vingeweza kututambulisha kwa kuamua kuvitangaza, mfano Taifa letu tumejaliwa kuwa na wabunifu wa sanaa za uchongaji yaani vinyago na kadhalika, hakika kutumia sanaa hizo pia ingesaidia kwa kiwango kikubwa kututangaza na kupata utambulisho wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo kuna baadhi ya makabila bado yanaendeleza mila potofu ambazo zimepitwa na wakati, mfano ukeketaji ambao huchangia kwa kiwango kikubwa maambukizi ya UKIMWI, ndoa za kurithi pia ni mila hatari kwa jamii ya sasa. Nashukuru tumevida hatua kubwa sana kwa baadhi ya makabila kuelimika na kuacha mila hizo lakini kuna angalizo kwani kuna baadhi ya makabila yamekuwa bado magumu kubadilika. Mpaka leo kuna maeneo bado wamekuwa na tabia ya kuwaozesha watoto wa umri mdogo na kuwaachisha shule. Naiomba Serikali na asasi zisizo za Kiserikali na taasisi za kidini kuendelea na mikakati ya uelimishaji kwa jamii zote ambazo bado zimekuwa na ugumu wa kubadilika.

Mheshimiwa Spika, michezo hivi sasa imekuwa ni ajira kwani watu kuititia michezo wanalipwa fedha nyangi na kuendesha maisha yao ya kila siku. Taifa letu bado changa ila kuititia michezo tungeweza kultangaza zaidi likajulikana. Hapo awali tulikuwa tuna utaratibu mzuri sana tokea ngazi ya chini kielimu kuanzia shule zetu za msingi, sekondari

tuliweka utaratibu wa michezo na mashindano mashulenii, lakini miaka ya karibuni huo utaratibu ulifutwa bila kuangalia athari zake. Leo hii tunakosa na kupoteza vipaji vingi sana ambavyo tungeweza kuvipata tokea mashulenii na kuvikuza ili vije kusaidia Taifa letu, kwani kurudisha michezo, mashindano mashulenii kutasaidia sana kukuza vipaji mbalimbali. Naishauri Serikali kurudisha michezo mashulenii na kuboresha zaidi ili kupata vipaji mbalimbali vitakavyokuja kusaidia Taifa letu hapo baadaye na kutoa mwanya wa vijana kupata ajira kipitia michezo.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa pia tuna matatizo ya viwanja vya mipira, hili ni tatizo kwani maafisa wetu wa Serikali wamekuwa wakiuba kiholela maeneo ya wazi yaliyotengwa na Serikali kwa ajili ya michezo. Kufanya hivi ni kosa na kukosesha mahali ambapo vijana watafanya mazoezi na kukuza vipaji vyao. Ikumbukwe kwamba ufanyaji wa mazoezi unamweka kijana busy ukiachilia kukuza kipaji chake. Kutokana na hilo hata ile tabia ya ukaaji vijiweni na kufanya uhalifu inapungua kwa kiasi kikubwa. Naishauri Serikali kuweka mkakati wa kuwa na maeneo mengi ya viwanja vya michezo na kuviboresha ili vijana wengi waweze kufanya mazoezi na kukuza vipaji vyao. Naipongeza Serikali kwa kuzidi kuboresha na kulinda maeneo ya wazi yaliyotengwa kwa ajili ya michezo.

Mheshimiwa Spika, ila pia pato linalopatikana katika uwanja wetu mpya wa Taifa ni ndogo sana ukilinganisha na ubora wa huo uwanja. Jitihada zifanyike kuutangaza uwanja huo ili uzidi kujulikana zaidi. Kufanya hivyo kutasaidia pato lake kupanda. Vilevile mchakato wa kujenga viwanja vingine kama ule uwanja mpya ufanyike ili tuwe na viwanja vingi vya kisasa nchi nzima. Pia kuboresha usimamizi wa kiwanja chetu cha kisasa kwani kumekuwa na uharibifu mkubwa hufanyika baada ya kutumiwa, napendekeza elimu kutolewa kwa wananchi juu ya kupenda na kutunza vitu vyao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiweka nguvu zaidi kwenye michezo wa mpira wa miguu na kusahau michezo mingine. Kufanya hivyo ni makosa kwani kila michezo

una umuhimu wake. Naishauri Serikali kutilia mkazo michezo mingine na kuwekeza huko kama ilivyofanya kwenye mpira wa miguu kwani itawapa moyo wachezaji wa michezo hiyo na kuongeza juhudhi katika mazoezi. Pia Serikali isisahau michezo ya asili kuiweshesha na kuitangaza kwani michezo hiyo ni kivutio pia kwa Taifa letu. Pia tuisahau kuwapa Walimu wetu wa michezo mafunzo ya mara kwa mara ili waendane na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini bado ni changa ila lina maeneo makubwa ya ardhi. Kwa hali hiyo, naiomba Serikali kututafutia wawekezaji katika michezo kuja kuwekeza katika eneo letu kwa kuwa linaflikika kirahisi sana. Tukiamua kufanya hivyo kuwekeza katika maeneo ya Ruvu au Mlandizi itasaidia pia kukuza uchumi na kutengeneza ajira ambazo zitawasaidia watu wetu wa Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya habari imekuwa ikilaumiwa sana katika upotoshaji wa habari ambaao ni hatari sana. Imefikia mahali wenye vyombo vya habari wamekuwa wakijali kupotosha taarifa ili wauze kwa kiwango kikubwa magazeti yao ama televisheni zao kupata waangaliaji wengi bila kujali athari zinazoweza kujitekeza hapo baadaye. Uhuru wa Habari umewafanya baadhi ya Waandishi wa Habari kuutumia vibaya na kusababisha upotoshaji wa habari ama kutoa habari za uchochezi, pia baadhi yao wamekuwa wakinunuliwa na viongozi fulani fulani ama wa kislasa au Serikali, kuwatetea na kuwasafisha pale wapatwapo na kashfa. Naomba niwashauri Wandishi wa Habari kuwa wafuate miiko ya habari na kutii sheria zake kwani kufanya hivyo kutajenga hali ya wandishi kuaminika zaidi kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa ya kuendeleza michezo hapa nchini. Nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna matangazo mengi katika TV ambayo yanachangia kuperomosha maadili ya

Mtanzania. Naomba Wizara iweke utaratibu wa kuchuja habari zinazotoka katika vyombo vyahabari ili kuepusha mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Spika, vijana ndiyo nguvu kazi ya maendeleo hapa nchini kwetu lakini kuna wimbi kubwa la vijana wanaojihusisha na utumiaji wa madawa ya kulevyta. Naomba Wizara ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu kuweka mpango mzuri wa kuwalinda vijana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iweke kipaumbele kwa kusimamia masilahi ya Waandishi wa Habari kwani wengi wao hawana uhakika wa masilahi yao katika ofisi zao hivyo kushawishika katika kujihusisha na masuala ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuiongezea *TBC* fedha ili iweze kuboresha chombo hiki muhimu kinachohabarisha Watanzania katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naomba maslahi ya waandishi wa habari yaboreshwé.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kubadilisha muda wa kipindi cha leo katika Bunge kinachoanza kutangazwa baada ya saa nne usiku, kianze mapema na mimi napendekeza kianze baada ya saa mbili usiku kwani muda wa saa nne wananchi wakulima wa vijijini wanakuwa wamechoka na hivyo wanakuwa wamepumzika na kutokana na kazi yao ngumu wanakuwa wamelala. Hivyo, naomba Serikali iangalie muda mzuri wa leo katika Bunge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, Wizara hii inapangiwa muda wa siku moja, hautoshi na bajeti yake

pia ni ndogo, wapunguze masuala ya chai yaani takrima ili pesa zifanye kazi za jamii, hata ikibidi kuongeza pesa maana kuna mambo ya vijana mengi hayajafanyiwa kazi ukizingatia kuwa vijana waliopo katika jamii ni 50/50 kwa hiyo bajeti iongezwe.

Mheshimiwa Spika, tunaomba viwanja vya michezo vijengwe hasa kiwanja cha Lindi ambacho ni cha asili. Hapo zamani kiwanja hiki kilikuwa kinatumika wakati wa michezo ya Afrika Mashariki, pia ukizingatia kuwa wachezaji wengi wa zamani hapa Tanzania walikuwa wanatoka Lindi. Kwa kuwaenzi hawa wachezaji maarufu basi kiwanja cha Lindi kifufuliwe.

Mheshimiwa Spika, vijana tunaomba watazamwe kwa jicho la huruma kwa kuendeleza Baraza la Vijana. Kuna maeneo mengine Mikano hakuna Baraza la Vijana, nchi mzima iwe na Baraza la Vijana kwani vijana sasa ni asilimia 50 ya jamii.

Mheshimiwa Spika, mipira ya wanawake iendelezwe kwani ni kivutio kikubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, tunaomba mitambo ya Redio Tanzania iendelezwe ili huko vijijini tuweze kupata habari hasa wakati huu ambao tunatangaza Katiba ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa Hotuba nzuri na umahiri katika utendaji wa kazi zao za kila siku. Aidha, nawapongeza Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kutayarisha Hotuba hii nzuri. Nawatakia utekelezaji wenye mafanikio wa bajeti ya 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara kwamba waangalie uwezekano wa kushirikiana na *NGOs* zinazotoa huduma kwa vijana hususan katika nyanja za

mafunko ya stadi za maisha, michezo na uwezeshaji wa miradi midogo na uundaji wa vikundi vya kujisaidia kiuchumi. Mfano wa kuigwa ni ule wa Shirika la *Faraja Trust Fund* ya Morogoro wakishirikiana na Shirika la *Right to Play, ICT* na Mradi wa Zinduka. Ni vyema Serikali ikatambua juhudzi za wadau kama hao ambao wanawahudumia vijana vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Wizara sasa iuangalie Mkoa wa Morogoro kwani fursa za kilimo, ufgajji wa nyuki na ujenzi wa mabwawa ya samaki pamoja na usindikaji wa mbogamboga na matunda zipo katika Wilaya zote. Aidha, vijana wa wafugaji kama watawezeshwa, watasaidia sana kuchochea mabadiliko ya mtindo wa ufgajji wa ng'ombe wengi wa kienyeji ambao hawana tija. Mfano hai ni Ndugu Lucas Lemomo wa Kijiji cha Diguzi ambaye ameanza mradi wa kusindika maziwa ila changamoto yake ni miundombinu na vitendea kazi. Naomba Wizara imsaidie mjasiriamali huyu ili awe mfano wa kuigwa kwa wafugaji katika Wilaya ya Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara hii katika nyanja zifuatazo kwa mategemeo ya kwamba Waziri husika atatoa majibu ama ufanuzi kwa yale yote ambayo yanatupa mkanganyiko.

Mheshimiwa Spika, utoaji vibali kwa vyombo vya Habari (*TV Imani*). Wananchi, viongozi wa vyama na viongozi wa Kitaifa walitoa michango yao ya kifedha pale katika uwanja wa Taifa kuitikia harambee ya kuchangia uanzishwaji wa *TV Iman*. Uongozi wa *TV Imani* umekamilisha taratibu zote zinazotakiwa pamoja na kufanya malipo stahiki *TCRA*, la kushangaza kwa sababu zisizoelewaka bayana hadi leo hii *TV Imani* hajapatiwa ruhusa kutoka kwa Waziri ili kuanza kurusha vipindi na matangazo yake. Tayari baadhi ya wananchi wameanza kupoteza imani na uongozi wa *TV Imani* na hata kwa Serikali kwa kudhani fedha zao zimeliwa ama kutapeliwa, baadhi yao wamelenga shutuma kwa Serikali

kwa kujua Waziri husika ameamua kwa makusudi kuzorotesha mchakato wao.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri atoe maelezo na ufanuzi wa kina ni kwa nini hadi leo hii ameshindwa kuwapatia kibali cha kurusha matangazo na kuanza kuoneshwa *TV Imani*. Faili la maombi ya *TV Imani* liko kwake likingoja maamuzi na baraka zake.

Je, ni lini *TV Iman* itapewa kibali hicho kutoka kwa Waziri? Kwa kuwa *TV* hii ina eneo pana la kuelimisha waumini wenye itikadi ya Uislam, ili kuепusha vijisababu vyta kuona labda Serikali ama Waziri anafanya makusudi kuwanyima wananchi hawa haki yao ya msingi ya kupata habari na kuondokana na dhana ya ubaguzi wa kidini, nataka Waziri atoe ufanuzi ili isije ikaleta taswira mbaya kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Utamaduni. Tanzania kuna Mfuko wa Utamaduni ambapo wengi wetu hatuna uelewa nao. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi wa kina juu ya Mfuko huu umewezaje kuwasaidia wale wanaojihusisha na tasnia hii, una uwezo gani na ni nani wanaofaidika na Mfuko huu pamoja na hali halisi ya huu Mfuko.

Mheshimiwa Spika, matangazo ya *Star TV*. Tulizoea kuona matangazo ya Bunge nyakati za usiku kupitia *Star TV* ila kwa sasa si vipindi vyta asubuhi wala usiku havionyeshi Bunge. Waziri kama mlezi wa vyombo hivi tunataka kujua kulikoni hata ikawa *Star TV* haioneshi vipindi vyta Bunge kama tulivyozoea?

Mheshimiwa Spika, jukwaa la Wahariri Tanzania. Jukwaa hili limekuwa likifadhiliwa na Mashirika mbalimbali ya kifedha, ya kijamii na makampuni makubwa nchini. Kwa sasa limekuwa ni jukwaa la kibiashara zaidi na kuweka maslahi yao binafsi mbele, huku kazi yao kubwa ni kukusanya fedha na kuanzisha *SACCOS* ambayo ni kwa maslahi yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, Wahariri wa Tanzania wamekuwa kama vile waungu watu katika sekta hii ya habari. Kazi yao kubwa mbali na kujipatia fedha kusiko halali pia ni kuhudhuria semina na makongamano tu. Imefikia hatua hakuna anayeweza kulihoji Jukwaa hili na kupelekea Jukwaa hili kuwa watumwa wa makampuni fulani na baadhi ya taasisi kuficha maovu yao. Jukwaa hili limejitenga na baadhi ya Waandishi wa Habari, halijihuishi kwa namna yoyote ile na matatizo yanayowakabili Waandishi wa Habari, wakati linaelewa kwamba wao Jukwaa ndio viongozi wa Waandishi hao na ndio nyumba tegemezi ya tasnia nzima ya habari nchini.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari ndio chanzo cha habari. Ni watu muhimu sana hapa nchini na ni watu wa kupata hadhi na heshima zote zinazowastahili mbele ya Jukwaa hili la Wahariri. Namwomba Waziri atupatia maelezo ya kina ni kwa nini pengo hili linaendelea kukua na ni hatua zipi attachukua juu ya kadhia hii?

Mheshimiwa Spika, nina dhamira ya kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri iwapo sitopata majibu ya kuridhishwa kuhusu *TV Imani* na Jukwaa la Wahariri.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, baadhi ya wasanii wamekata tamaa kutokana na kazi wanayoifanya kutoendana na kipato wanachopata hii ni kutokana na kutokuwa na udhibiti wa kazi za wasanii. Aidha, ni jukumu ambalo linatakiwa lifanywe na chama cha wasanii BASATA. Ni watuhumiwa wangapi ambaao wamekamatwa katika wizi wa kazi za wasanii na ni wangapi ambaao wamechukuliwa hatua za kisheria mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, usumbufu wa soko la sanaa, baadhi ya wasanii wamekuwa hawanufaiki na soko la sanaa, hasa wasanii wanaochipukia, wanaopata manufaa ya sanaa hii ni wagavi (*distributers*) na hawa wagavi wamekuwa wakiwasumbua sana hawa wasanii chipukizi katika suala la malipo. Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia hawa wasanii walipwe kwa wakati ili wasidhulumiwe haki zao? Je, Serikali

itahakikisha vipi wasanii wanalipwa malipo ya kazi zao kwa wakati muafaka na hawa wagavi *distributers*?

Mheshimiwa Spika, suala la wasanii ambao wamekuwa, kwa mfano nchi za wenzetu wasanii wananaufaika wakiwa hai na wakiwa wamekuwa, kazi zile walizoziacha zinanufaisha familia zao. Kwa mfano, wasanii wa nje Michael Jackson familia yake inanufaika kwa kazi alizoziacha (alizofanya). Ni kwa nini wasanii wetu wa Tanzania wanapokuwa wamefariki kazi zao hazinufaishi familia zao kwa mfano Kanumba, Omari Kopa, Bi Kidude na kadhalika, kazi zao walizoziacha zinawanufaisha watu wengine. Ni kwa nini Serikali isiwadhibiti hawa wanaojinufaisha kupitia nguvu za marehemu na kuacha ndugu wa marehemu wakiwa katika hali ya umaskini?

Mheshimiwa Spika, suala la wachezaji mpira, kuna wachezaji wa mpira ambao wameipatia sifa Tanzania kwa kucheza mpira nje ya nchi na kuingizia Serikali pato la Taifa na baadhi ya picha zao zimetumika kwenye stempu za Tanzania, lakini Serikali imewasahau wachezaji hawa na wengine wanasumbuliwa na maradhi mpaka leo, Serikali inashindwa kuwapa msaada wachezaji hawa. Je, Serikali itawasaidia vipi wachezaji ambao wanaosumbuliwa na maradhi ili wapate matibabu *either* nje ya nchi au ndani ya nchi?

Mheshimiwa Spika, suala la waandishi wa habari, waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu na wengine kuhatarisha maisha yao na kupoteza uhai wao. Vilevile waandishi wa habari ni kioo cha jamii hata habari zilizofichika vijijini za jamii wamekuwa wakizifuatilia huko vijijini na kuzitoa katika magazeti na kutoa habari za viongozi ndani ya Serikali ambao si waadilifu. Cha kushangaza wanapotoa habari za viongozi na kama viongozi nao hawajavutiwa na hiso habari, waandishi wa habari hao wanahatarishiwa maisha yao. Ni lini waandishi wa habari watapatiwa bima ya maisha? Ni lini Serikali itawajali na kuwathamini waandishi wa habari na kuwapa uhuru wa

kutosha wa kuandika habari kama ilivyo kwa nchi za wenzetu?

Mheshimiwa Spika, suala la *TBC* (Shirika la Utangazaji), Shirika hili ni chombo cha habari cha umma. Chombo hiki katika utoaji wa habari kimekuwa kikilalamikiwa na wananchi na wanasiasa. Chombo hiki cha utangazaji kinatoa habari kwa upendeleo. Naishauri *TBC* itoe habari za wananchi na viongozi wote wa kisiasa bila kupendelea upande mmoja ili wananchi na wanasiasa wawe na imani nao.

Mheshimiwa Spika, suala la Baraza la Kiswahili, lugha ni sehemu ya utamaduni wa Taifa. Nchi zote zenye maendeleo wanatumia lugha yao kwa mfano Korea, Japan, Ujeruman, China na kadhalika. Mataifa haya yametoa kipaumbele kwa lugha yao na ndio maana zimekuwa na maendeleo lakini Tanzania tunapenda kuiga lugha za watu, kwenye Kiswahili hatumo wala kwenye Kiingereza. Ndio maana wenzetu Wakenya wamejua udhaifu wetu na kutubia ajira. Walimu wengi wa Kiswahili wanaofundisha nchi za nje kwa mfano Marekani, Rwanda wanatoka Kenya. Vilevile viongozi wetu wa nchi wanapohudhuria kwenye mikutano ya Kimataifa wanakuwa hawana wakalimani wa Kiswahili. Hii inachangia kudhoofisha lugha ya Kiswahili cha kushangaza kwa mfano viongozi wa Kijeruman, viongozi wa Kichina wanakuwa na wakalimani wao. Serikali haioni sasa kuna umuhimu viongozi wetu wa nchi wanaposafiri watumie Balozi kutangaza lugha ya Kiswahili ili tuweze kupata soko la ajira kwa Walimu wetu wa Kiswahili Tanzania kama wenzetu wa Kenya wanavyofanya kutafuta ajira ya lugha ya Kiswahili nchi za nje?

MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, Serikali itenye fedha ya kutosha katika bajeti ya Wizara hii, kwani tukiangalia bajeti waliyotengewa mwaka jana na hii ya mwaka huu haipishani kitu kilichoongezwa ni shilingi billioni mbili tu na haitaweza kutimiza matakwa na malengo walijojiwekea. Ni vyema Serikali ibadilishe mwenendo wake wa kuipa Wizara fedha

chache na hasa ikiwa kweli wanataka kuleta maendeleo katika nchi ili kukuza uchumi wake na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo yenyeye jukumu la kuandaa mazingira mazuri kwa vijana ili waweze kujajiri wenyewe na hasa ukizingatia kuna wimbi kubwa la vijana waliomaliza shule na vyuo ambaao hawana kazi wala maisha ya uhakika ya kula ya siku moja. Asilimia kubwa katika Tanzania ni vijana na wengi wao hubabaishababaisha katika kujitafutia kazi au ajira ambayo haipo lakini vijana hawa wanawenza kuwezesha ili waweze kujikimu na kujajiri kwa kupewa mikopo ingawa Wizara mnawapatia stadi za maisha na stadi za kazi ili waweze kujitambua, kujitegemea na kujajiri na wengine kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri utakapokuja kuhitimisha, anifafanulie mpaka sasa ni asilimia ngapi ya vijana waliopewa stadi hizo za maisha ambaao wamekwishakujajiri? Ni kwa nini Serikali inawaachia Askari wa Jiji au Halmashauri kuwanyang'anya Wamachinga bidhaa zao ambaao wengi wao wamejajiri na wengine kuajiriwa?

Mheshimiwa Spika, kati ya vijana 8743 mliowapa mafunzo ya stadi za maisha na maarifa ya ujasiriamali kutoka Mikoa 23 na Zanzibar, ni wangapi kwa ujumla wake walitoka Zanzibar na katika Mikoa ipi? Naomba ufanuzi?

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya utamaduni wa Kitanzania. Unapotoka hasa unapoangalia filamu na michezo ya Kitanzania, wanafuata mila na tamaduni za Magharibi. Inashangaza kuona kuna Bodi na pia hufanya sensa za filamu na michezo hiyo, hivi hawaoni kwamba wanakwenda kinyume na maadili? Hasa nguo wanazovaa wasanii wa kike ni uchi mtupu, kuanzia juu hadi chini, matiti yanaonekana, nguo chini ya makalio, kama suruali imembana mbele na nyuma, hivi huu ndio ustaarabu wa Kitanzania, kubusiana na kujifunika mashuka nalo ni mashaka pia. Je, wasanii hawa wanaifundisha nini jamii ya Kitanzania au haya ndio mafunzo wanayopewa na Bodi ya kuboresha

tashia ya filamu? Ni vizuri Wizara na Bodi iangalie michezo ya jirani zetu Kenya, nguo wanazovaa ni za kistaarabu na heshima, kwa nini na sisi hatufuati maadili au *CDS* zitakuwa hazinunuliwi? Ili Bodi ijisafishe na shughuli zake zionekane ni vizuri kabla ya filamu, *CDS/DVD* kutoka waziangalie na kama kuna upotoshaji wa maadili wasiziruhusu kutoka na kama zikitoka kikundi kifungiwe au kuwe na sheria itakayowabana.

Mheshimiwa Spika, taarab, utamaduni wa taarab nao umepotoka kuanzia waimbaji hadi watazamaji. Tabia mbaya inayojitokeza na kuendelea kujonesha, ni aibu wanawake kucheza mauno, wanaume kubanana na wanawake si vizuri. Haya mambo ya jando na unyago yana sheria zake na mahali pake maalum.

Mheshimiwa Spika, lugha nayo inayotumika katika mashairi ni mbaya au ya waziwazi kulinganisha na taarabu asilia ambayo kila kitu washairi wake walikuwa wakiweka kwenye mafumbo, huwa ni kazi yako wewe mwenyewe kulifumbua fumbo hilo, ambayo kwa upande mwingine hiyo ni fasihi simulizi au andishi. Je, Waziri haoni kwamba anaweka hali tete katika maonesho ya taarab, hasa kwa vijana wa leo ambaao wanawenza kujitia katika dimbwi la UKIMWI? Ni vizuri Wizara itoe maelekezo hasa kwa washairi na wale wanaohudhuria taarab.

Mheshimiwa Spika, michezo ni moja kati ya shughuli muhimu kwa kila mtu ambaye anataka kuujenga mwili wake. Michezo pia ni ajira kwa vijana. Ukiangalia nchi zilizoendelea, michezo ni kipaumbele katika shule zote, kwani huwajengea uwezo watoto wa kujajiri na kuajiriwa. Michezo hutoa vijana ambaao wana vipaji vizuri na kwenda nchi nyingine kwa kulipwa na hivyo husaidia nchi yake, klabu, familia na hata Taifa lake kulipa umaarufu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya timu zetu za mpira hupata wafadhili wazuri, hasa timu za mpira wa miguu za wanaume, lakini timu ya mpira wa wanawake ya *Twiga Stars* ipo mashakani katika kupata wafadhili. Je, kama Wizara ina mchango gani au mikakati gani ya kuisaidia timu hii

(ambayo inacheza vizuri na kuleta umaarufu wa Taifa katika mchezo huu) hasa pale wanapokuwa katika maandalizi ya kuiwakilisha nchi katika mashindano ya Kimataifa? Naomba Waziri anipe ufanuzi wa hili.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, tatizo la timu ya Taifa ya wanawake, bado hawajathaminiwa vya kutosha, wanapata tabu wanapokuwa kambini, hawana mdhamini lakini Serikali haina jithada za kusaidia timu hii mbali na kuliletea Taifa heshima, imekuwa ikiipa kisogo.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali ya kukarabati viwanja vya mpira wa miguu, ujenzi wa viwanja vya *netball*, navyo ni vichache sana. Bado kuna uhaba wa Maafisa Vijana na michezo kwenye Halmashauri zetu wao ndiyo wangekuwa na jukumu la kuibua vipaji vitakavyosaidia kupata timu madhubuti za Taifa kwa mpira wa pete, mpira wa miguu kwa wanawake na wanaume.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Spika, nianze na kauli mbiu ya *TBC* inayosema TBC ni ya ukweli na uhakika. Mimi naona *TBC* ni ya ukweli isyo na uhakika. Ina uhakika gani wakati haina vitendea kazi vinavyoendana na wakati. Ina mitambo chakavu kiasi kwamba inapelekea matangazo yake kutosikika maeneo mengi katika nchi yetu, *TV* inawagandisha watangazaji na kukatisha matangazo mara kwa mara, je, huo ni uhakika? Naishauri Serikali chombo hiki ni cha umma na wananchi wengi wanapenda kusikiliza na kuangalia *TV* hii. *TBC* iwezeshwe kwa kupewa bajeti ya kutosha kwenye fungu la maendeleo ili waweze kununua mitambo mipya, vitendea kazi vya uhakika ili kuwatendea haki wananchi wanaoipenda *TBC* kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, *TBC* inalo jengo kule Mikocheni ambalo limetelekezwa kwa kutokamilishwa kwa miaka kumi sasa. Wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira magumu. Niombe Serikali ikubaliane na maoni na ushauri wa Kamati kwa Serikali kutoa dhamana ya asilimia 100 ili Mfuko wa Jamii (*NSSF*) ambao upo tayari kukamilisha ujenzi wa jengo hilo uweze kuanza utekelezaji ambapo kukamilika kwa

jengo hilo kutaifanya *TBC* kuwa na heshima na mahali pa uhakika pa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W.*) kwa neema na rehema zake nyingi kwangu na familia yangu na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina umuhimu wa kipekee katika nchi yetu, kwani inabeba heshima katika nchi yetu kwa kiasi kikubwa. Habari, mila, silka na utamaduni ni vazi la sitara la nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo linaloendelea kukua na kuharibu mila, silka na utamaduni wetu ni Wizara hii kutokutoa umuhimu wa kuendeleza mila na utamaduni wetu na kuachia kila kikundi kikifanya kipendavyo tu na huko huwa ni kuharibu utamaduni badala ya kuuimarisha.

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni pamoja na lugha ambayo inachukua sehemu kubwa ya utamaduni wetu. Jambo la aibu hapa ni kuiachia lugha yetu nzuri ya Kiswahili ikiharibiwa na Serikali ikifurahia. Mfano wa hili ni nyimbo zinazotungwa na kuimbwa na vijana wa *Bongo Flever*. Nyimbo hizo hazina kabisa maudhui ya Kiswahili sanifu japokuwa zinainmbwa kwa Kiswahili na hii ni kwa sababu vijana wengi hawajui lugha yao ya Kiswahili, hii ni aibu na fedheha kubwa kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza na kufedhehesha zaidi ni kuwa hata mshindi wa Miss Tanzania wa mwaka huu hajui hata kuzungumza Kiswahili, lugha yake ya kuzaliwa, hii ni fedheha, fedheha, fedheha. Naomba Serikali ilione hili na illi kuijengea hadhi lugha yetu ya Kiswahili, Serikali imvue Taji la Ushindi Mrembo huyo na avalishwe anayejua Kiswahili kwa ufasaha akiwa ni mshindi wa pili au wa tatu kwani lugha ndiyo utambulisho wa kwanza wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vina wajibu na jukumu kubwa la kusaidia kuendeleza mila, silka, desturi na utamaduni wetu. Vyombo vya habari ni kama moto. Moto ukutumika vizuri utapikia chakula na kurutubisha afya ya kimwili na ukutumika vibaya, moto unaweza kuunguza nyuma, mtu na hata mji mzima, vivyo hivyo vyombo vya habari vinaweza kuwa moto. Serikali lazima isimamie maadili ya vyombo vya habari ili vifanye kazi kwa maslahi ya Taifa na sio kwa kurubuniwa na kupewa rushwa ili vifanye kazi kwa maslahi binafsi, ya mtu au kikundi fulani.

Mheshimiwa Spika, Serikali isimamie maadili, mila, silka na desturi za Kitanzania katika michezo ya sinema za kuigiza. Michezo hii ni michafu sana kiasi ambacho mtu hawezi kukaa na mama yake au mtoto wake na kuangalia. Mbona tumezidi kuiga mila na desturi za kimagharibi? Mila na desturi ambazo hazina macho?

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, uhuru wa habari ni haki ya kila mtu lakini ni jambo la ajabu kuona kuwa haki hii ya msingi ikipokonywa kwa kisingizo kuwa tuna magazeti mengi na vyombo vingi vya habari. Unaweza kuwa na magazeti mengi sana lakini hayako huru. Wote tunajua ni jinsi gani magazeti yetu hasa yale yanayoandika habari za viongozi (ufisadi) yakifungiwa kwa kisingizio cha uchochezi.

Mheshimiwa Spika, lugha ni kigezo kizuri sana cha kutangaza nchi lakini bado haitangazwi pamoja na kuwa lugha ya kumi duniani. Bado kitengo cha ukalimali (*translation*) hakipo na kama kipo basi hakifanyi kazi. Tumeshuhudia makongamano ya kimataifa wenzetu wanaongea lugha zao na zinatafsiriwa lakini Kiswahili hakitumiki matokeo yake tunaongea lugha ya Kingereza (*official language*) lakini bay a zaidi lugha hii haiongelewi vizuri.

Mheshimiwa Spika, vazi la Taifa limeongelewa kwa muda mrefu sana lakini mchakato wake hajulikani umeishia wapi. Ni jambo la kusikitisha kuona nchi nyngi za Afrika zimebuni mavazi yao na umekuwa ni utambulisho wao.

Watanzania ni vema sasa tuambiwe mchakato huu wa vazi la Taifa umefikia wapi kama imeshindikana basi tuambiwe zoezi lisimame.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Tanzania wamekuwa na mazingira magumu sana ya kujajiri na kuajiriwa na hivyo kujingiza kwenye makundi mabaya. Ni matumaini yangu kuwa Mfuko wa Vijana utawasaidia sana.

MHE. MUNDET ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, Serikali pamoja na shilingi bilioni tatu zilizotolewa, naishukuru sana Serikali lakini hazitoshelezi na ni vema wale wenye uwezo wa kufanya kazi wasaidiwe na kupata mkopo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wengi hawakoposheki, nashauri Wizara ikae na Wizara ya Fedha pamoja na Waziri wa Vijana na Wakurugenzi wa Mabenki ili vijana wanaoendesha bodaboda (pikipiki), bajaji, wakopeshwe na kadi ya pikipiki hizo ndiyo iwe dhamana yao. Kwa kufanya hivyo, naamini vijana wengi watajikomboa kimaisha na kuwainua kiuchumi na watalipa kodi za Serikali. Mfano Tabora hakuna viwanda, naamini hili litasaidia sana kuwatafutia ajira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, nomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wa Mtanzania unamomonyoka siku hadi siku kutokana na Serikali kutokuwa na sheria madhubuti. Mavazi wanayovaa watoto wetu wa kiume, wanavaa suruali ambazo wenyewe wanaita 'Kata K', mtoto wa kiume anavaa herein, anavaa bangili, huo si utamaduni wetu Watanzania. Pia tumuangalie kijana wa kike wakati wa mashindano ya warembo, hivi ni kwa nini Serikali inaruhusu mashindano haya vijana wetu kuvalishwa nguo zisizokuwa na heshima, huku sio tu kuvuruga utamaduni bali

pia ni kumdhalilisha mwanamke. Naiomba Serikali kuchukua hatua ili kukomesha hali hii.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili ni lugha ya Taifa lakini kwa kuzungumza tu, kiutekelezaji sio kweli kwani hadi leo sheria bado zinaandikwa kwa Kiingereza na kwa nini tunatumia lugha za kigeni katika mikutano? Naiomba Serikali isimamie kwa umakini utunzaji na uendelezaji wa lugha yetu ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha tamu ambayo hata wageni wanaipenda na ndio maana mataifa mengi sana wanajifuna Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, *Star TV* ilikuwa ikionyesha kipindi cha Bunge kila siku kuanzia saa tano usiku wakionyesha Bunge kipindi cha siku nzima, je, kulikoni? Wengi tulizoea kuangalia kipindi hicho muda huu. Naomba majibu.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kazi kubwa katika kuendeleza mipango mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, natambua rasilimali zote za Taifa ni za Watanzania wote lakini narudia tena, Serikali itoe jicho la huruma kwa waathirika, mfano Uwanja wa Taifa Dar es Salaam – Halmashauri ya Temeke iangaliwe kwa jicho la huruma kutohana na uharibifu wa mazingira pale zinaptokea mechii kubwa.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana, Serikali iweke mpango mkakati wa kuungana na Wizara ya Ajira na Utamaduni kuondoa tatizo la kipengele cha uzoefu kazini katika maombi ya ajira mpya. Kazi inafanywa na yeoyote hakuna haja ya uzoefu. Uzoefu wa kazi unaupata unapofanya kazi yenyewe. Kwani hata sisi Wabunge tumeingia Bungeni mara ya kwanza mbona tunatimiza wajibu wetu? Kipengele cha uzoefu kinawanyima haki vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu uendelezwe kuimarishwa kwa kuenzi na kuendeleza makumbusho na vitengo vya utamaduni asilia.

Mheshimiwa Spika, habari na vyombo vyoma habari, *TBC* iendelezwe kwa kupatiwa mitambo na vitendea kazi ili matangazo yafike mbali na wale wa vijijiini yawafikie. Hii ndio redio na televisheni ya Taifa tuiboreshe.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji. Wizara ni kubwa, wajitahidi kufanya kazi kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, nianze na sekta ya maendeleo ya utamaduni. Utamaduni ni sehemu inayowakilishwa na makabila yote nchini kuititia mila na desturi lakini kutokana na utandawazi, utamaduni umeanza kusahaulika na Serikali isiposimama imara, utamaduni utapotea kabisa kwani kizazi cha sasa asilimia kubwa hawashirikishwi kuutambua utamaduni wa nchi yao na kuiga mambo ya Mataifa mengine hasa kwenye mavazi, lugha na vyakula.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kutilia mkazo, kupinga au kukataza mambo ya kuiga yasiyofaa kwanza kama kuvala mavazi yasiyositiri mwili na ya ajabu. Pili, kuzungumza lugha na kuchanganya na isiyoleta maana halisi, mfano, nina kiasi cha Jello huko ni kupotea. Tatu, vyakula; Watanzania wengi wamekuwa wakidharau kula vyakula vyoma asili na badala yake wanaona kuwa ni umaskini au kuishiwa kama mboga za majani, viazi, maboga, mihogo na kadhalika. Watanzania hasa wakaao mijini, wanaona kuwa ni umaskini kutumia vyakula kama hivyo na badala yake wanaona kula chipsi au soda ndiyo chakula cha kutumia mtu mwenye fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vazi la Taifa; limekuwa kitendawili nchini ambacho hakijulikani kitateguliwa lini pamoja na kuandaa makundi maalumu wakiwemo wasanii, waandishi wa habari, vijana, wanawake lakini mpaka hivi leo ni hadithi inayojadiliwa. Naishauri Serikali sasa kwa kuwa

vazi hili la Taifa ni faida kwa Taifa zima kupata vazi litakaloitangaza Tanzania na liwe vazi la heshima litakalovaliwa na rika zote, naiomba Serikali ikae na Kamati iliyoandalialiwa, itangaze kwa kila Mkoa, wanawake washirikishwe na kuwe na mashindano ya Mikoa kuwasilisha vazi lao wakishirikiana na Wabunge wao wa Viti Maalum kuwakilisha Mikoa yao kwa kubuni vazi la heshima na Taifa likubaliane.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi ukiangalia bado hakuna ubunifu wa mavazi. Ukienda madukani, nguo tunazoletewa wanawake ni zile zinazoonesha migongo au mapaja na mikono ya shimizi, nguo ambazo hazimpi mwanamke heshima kutokana na hadhi ya mwanamke. Hivyo tunapaswa kuwa wabunifu wa mavazi kwa uangalifu na siyo kuiga mavazi ya nje. Hivyo, nashauri Serikali katika Kamati hii ya Mavazi, Wabunge wanawake tushirikishwe ili tulirekebishe Taifa letu na Tanzania yetu ambayo inakwenda ambako siko.

MHE. JITU VRAJLAL SONI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa kuchangia leo kwa kunipa afya njema.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Sekta ya michezo. Kwanza kabisa, naomba Serikali iangalie upya Sekta hii, ni muhimu Kwa maendeleo ya Nchi yetu na pia kwa maendeleo ya vijana na afya zetu pamoja na kuongeza ajira. Tunashauri Serikali iangalie upya Sheria zilizopo na kuziboresha. Pia kutoa elimu kwa wananchi juu ya utaratibu na kanuni na Sheria mbalimbali za michezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wizara hii, ichunguze Vyama vya michezo vya Taifa na Mikoa pamoja na Wilaya juu ya uendeshaji wa kazi zao na ushiriki hadi ngazi ya chini. Sehemu kubwa ya Viongozi hawa huangalia maslahi yao binafsi na kutozingatia uboreshaji wa michezo katika maeneo yao. Mfano TFF, Vyama vya Michezo au Mpira za Mkoa wa Wilaya, kwa sasa vyama hivi vya Wilaya na Mkoa vingi vimebakilishi kufanya siasa na kutafuta Uongozi wa Kitaifa

bila kuzingatia kazi yao na kuhudumia vilabu vyao na kuboresha mchezo wa mpira wa miguu (soka).

Mheshimiwa Spika, msimu huu Timu ya *Magogo Rangers* ya Magugu Wilaya ya Babati ilishinda klabu bingwa wa Mkoa na kutarajia kucheza ligi ya Kanda. Cha kushangaza ni *team* hiyo kutolewa katika mashindano kwa kigezo cha kuwa nyuma ya ratiba, na Chama cha Mpira cha Mkoa hakikutoa taarifa kwa *TFF* kwa wakati, jina la kbalu na hakukuwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, *team* zote za Mkoa Manyara walicheza kwa mazingira magumu ya uwezeshaji, usafiri na malazi, ukizingatia umbali wa vituo vya Mbulu na Samanjiro. Chama cha mpira Mkoa kudai walitoa taarifa na kuomba kusogeza mbele ratiba: Je, uzembe uliofanywa na Viongozi hao wa Mkoa na Taifa kutokujibu barua zao na kutoa taarifa kwa vyombo vya habari (*Press Release*) je, ni njia sahihi ya mawasilianao?

Je, gharama zote za timu zilizoshiriki zitalipwa na nani wakati hawakujua ratiba sahihi na kuchezeshwa nyuma ya ratiba na Viongozi hao? Inakatisha tamaa wadau wa michezo na wanamichezo wenyewe. Je, wakienda Mahakamani kudai haki yao, itakuwa kosa? Je, Wizara itachukua hatua gani kuwajibisha viongozi hao wazembe ili kurudisha imani kwa wadau wa michezo? Pia suala la kutoa ratiba na matamko mbalimbali kwa njia ya vyombo vya habari (*Press Release*) maeneo mengi hapa nchini vyombo hivyo havifiki wananchi wote. Iwe Radio, TV au Magazeti. Njia ya barua na mawasiliano rasmi yaendelee kuwepo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iangalie Mikoa yote Tanzania kwa kufanya uchunguzi namna walivyoendesha ligi za Wilaya na Mikoa. Kuna taarifa kuwa Mikoa mingi imeendesha ligi bila kuzingatia Sheria, kanuni na utaratibu. Kuna baadhi za timu zilipendelewa na timu chache kuchezeshwa. Hakukuwa na uwazi katika mashindano hayo. Je, kwa wale wataobainika kufanya hivyo (Vyama vya Mkoa) ni hatua zippi zitachukuliwa? Mfano, Mkoa

wa Manyara, Pwani, ambao walitoa timu kutoka Mkoa mwingine: Je, *team* za Mkoa wa Pwani wana kosa gani? Viongozi wabaya wenyе lengo binafsi walifanya hivyo? Je, kwa nini hao viongozi wasiwajibishwe na kufikishwa Mahakamni na kulipa gharama zote za timu za Mkoa wa Pwani? Tunasema kwenda Mahakamani itatutoa katika mashindano yote ya Kimataifa: Je, si Sheria mbovu na unalea Viongozi wasiokuwa waadilifu kufanya maamuzi wanayopenda wao? Wadau hasa vijiji ni wamekata tamaa kuchangia mpira na michezo kwa ajili ya Viongozi wabovu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe tamko leo juu ya namna itakavyotoa haki kwa timu zinazoshinda bila upendeleo na kuwajibisha viongozi wote wabadhirifu na wenyе malengo binafsi. Leo sitaunga mkono hoja bila kupata majibu sahihi. Pia ahadi ya kufanya uchunguzi wa kina katika Mikoa yote kwa namna ligi ilivyoendeshwa.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na kuweka mkakati wa kufundisha michezo katika Vyuo vyote vya Elimu, iwe katika mitaala yetu. Itakuwa na gharama nafuu pa kuanzia hadi tutakapokuwa na Chuo cha Michezo. Walimu wakipata mafunzo ya michezo, kanuni na Sheria za Michezo, Watanzania kutoa elimu hiyo kwa watoto wa shule za awali, Msingi na Sekondari kwa vijana ambao tunaona wana vipaji, ndiyo wapelekwe katika Chuo Maalum cha Michezo. Pia Serikali itoe elimu kwa wanamichezo.

Vilevile nashauri Wasanii lazima wawe na kazi nyingine mbadala ya kuingiza mapato ili wasipofanikiwa katika fani zao, wasibaki kulalamika na kuomba. Pia Serikali iwe na mpango maalum wa kutoa ushauri nasaha kwa wasanii na wanamichezo kwa namna ya kuweka akiba, kuweka vitega uchumi vingine ili wakati umri ukienda na wakistaifu wasibaki kuwa katika mazingira magumu ya kimaisha. Huwezi kucheza na kuwa maarufu miaka yote.

Mheshimiwa Spika, pia wanamichezo wote wangeingia mkataba ambao watakatwa fedha na mwajiri

kuchangia ili wawe katika mifuko ya akiba za pensheni. Hii itasaidia wakati hawana ajira au wanapostafu wapate msaada. Kingine ni wasanii na wanamichezo wote wapatiwe elimu juu ya faida ya Mfuko wa Afya ya Jamii ili waweze kungia katika mifuko hiyo na wapate matibabu wanapougua na familia zao kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie suala la habari. Tunaomba Serikali iangalie namna ya kuongeza vifaa na kuboresha miundobinu za *TBCTaifa*. Katika sehemu nyingi *TBC* haisikiki vizuri. Hiki ni chombo cha Serikali cha kutoa habari mbalimbali kwa wananchi. Chombo hiki kingeboreshwa ili huduma ya habari kwa kupita tu redio ziwafikie wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara hii iangalie namna ya kushirikiana na Wizara ya Sayansi na Teknoloja ili maeneo yote ambako hakuna mawasiliano wajitahidi kuweka minara ili habari kutoka vijijini ifike katika vyombo vya habari. Habari nyingi kutoka vijijini hazifiki kwa wakati katika vyombo kutokana na mawasiliano. Pia waandishi wawe na mkataba wa kazi pamoja na Bima za Afya na wawe katika mifuko ya akiba ya pensheni. Waandishi wakiwa na uhakika wa maisha na mazingira mazuri ya kazi, wataweza kufanya kazi kwa ufanisi na wa haki. Kutakuwa hakuna ushawishi mbaya wa kutoa habari kwa ajili ya kulipwa na mwenye kutoa habari.

Mheshimiwa Spika, kwa bajeti hii ndogo, Wizara haiwezi kuendeleza Sekta ya Vijana na Utamaduni. Naishauri Serikali iangalie namna ya kuongeza bajeti katika Wizara hii nyeti na pia iangalie namna ya kutoa elimu kwa vijana ya ufundishaji na namna ya kupata mkopo kutoka Taasisi ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nashauri Maafisa Utamaduni wetu watengewe bajeti katika Halmashauri zote ili waweze kutekeleza kazi yao vizuri. Halmashauri nyingi hawatengewi fedha ya kutosha, hawa Maafisa wetu wafanye kazi vizuri.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu Utamaduni katika nchi yetu. Kwa miaka ya hivi karibuni nchi yetu imegubikwa na mmomonyoko wa maadili na upotofu mkubwa wa maadili. Utamaduni wetu unatoweka kutohana na kuiga mambo mengi ya Magharibi ikiwemo mavazi, vyakula na hata miziki. Kuiga mitindo ya maisha ya nchi za Magharibi kama vyakula, kupuuza na kutothamini vyakula vya asili kumeleta magonjwa mengi yasiyoambukiza mfano, Presha, Kisukari, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mavazi tumeshuhudia watoto wetu wakivaa mavazi yasiyo na staha. Ni wakati muafaka sasa Serikali kuliona na kutoa elimu kwa Watanzania kuitia programu mashulenii na vikundi mbalimbali ili Watanzania wavitambue kama ilivyokuwa zamani. Uzalendo wa wananchi hujengwa na Serikali. Ni vyema turudi nyuma, Wizara ifanye utafiti, ni jambo lipi au yeti hadi hali ya uzalendo kufilia nchini hasa awamu ya kwanza na ya pili ya utawala katika nchi hii?

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu michezo mashulenii. Kipindi cha michezo mashulenii hakitiliwi mkazo. Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu kuhakikisha angalau vipindi viwili kwa wiki vinawekwa kwenye ratiba, lakini pia wawepo Walimu wa Michezo mashulenii. Wizara hii wanakuwepo na wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara, licha ya michezo kujenga afya lakini pia michezo hujenga akili na vipaji hutambuliwa katika umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupata wimbo wa Afrika Mashariki ulihusisha Watanzania ambao waliweza kuonyesha vipaji na kufikia hatua ya juu ya mchakato. Lakini hadi sasa wimbo huu umetoka na kuanza kutumika bila washiriki kujua hatima yao kimalipo. Je, Wizara inasemaje kuhusu hili? Je, katika mchakato wa kupata wimbo huu Wizara iliusika vipi?

Mheshimiwa Spika, Shirika la TBC kama ilivyotolewa maoni, Serikali ilisaidie liweze kupata fedha za kulisaidia kutoa matangazo, pia kuweza kuandaa *program* zinazovutia

watazamaji. Mara nyingi huonesha jambo moja hadi watazamaji hukinai. Nafikiri ni kwa vile hawana fedha kufuutilia matukio mbalimbali. Matangazo yao yanachosha, yamezeeka kama chombo chenyewe kilivyo. Ni vigumu kwenda na wakati kama hawaweki matanganzo au progamu mpya kama hawana fedha. Wangeiga *TV*nyingine kama *ITV* na *STAR TV* ambao wanafanya vizuri na *TV* zao zinavutia watazamaji, lakini pia hawafanyi upendeleo wa kisiasa na hivyo vinaheshimika. Serikali iache chombo hiki kijiendeshe kibashara, lakini pia kujenga hadhi ya kupendwa na Watanzania badala ya kukidharau.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nianze na Shirika la Habari la Taifa (*TBC*), kuendelea kupata ruzuku toka Serikalini ikiwa linajidesha kibashara.

Mheshimiwa Spika, inasemekana *TBC* inapata takriban Shilingi bilioni 20 kwa mwaka, lakini bado linapata ruzuku toka Serikalini. Hivyo basi, tunaomba ufanuzi kama taarifa hizo ni sahihi au la, na kama ni sahihi, kwa nini wanaendelea kupata ruzuku ikiwa wanaweza kujidesha. Vilevile tungeomba kupata ufanuzi kama Shirika la Habari la Taifa *TBC* linapata hasara ama faida?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkakati wa Serikali kulinda Waandishi wa Habari, kwa sababu ya matukio ya kuhatarisha usalama wao katika kipindi cha hivi karibuni, hivyo basi, tunaomba Serikali ielete ni namna gani itawalinda Waandishi wa Habari ili kunusuru demokrasia iendelee kufanya kazi? Kwa kuwazuia Waandishi wa Habari kufanya kazi, ni kuzuia demokrasia nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, Sekta ya Habari na Utangazaji, ni moja ya sekta za huduma za jamii nchini, huduma ambayo ni haki ya msingi ya raia kama ilivyo kwenye Katiba ibara ya 18 na ibara ya 19 ya tamko la Umoja wa Mataifa la haki za binadamu. Hivyo,

21 MEI, 2013

Serikali inatakiwa kulinda haki ya misingi ya mwananchi ya kupata habari.

Mheshimiwa Spika, kwakuwa teknolojia sasa hivi imekua na utandawazi hauzuiliki, hivyo Serikali na Taasisi zake kisekta kwa mfano ulinzi na usalama wa Taifa, wanatakiwa kuwekeza katika kujenga uwezo wa uchambuzi wa teknolojia ya habari badala ya kutumia nguvu kudhibiti, kwa kuwa teknolojia na *content* havidhibitiki.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatakiwa kuwekeza katika Sekta ya Habari katika uandishi wa kizalendo kwa kuwaendeleza waandishi kitaaluma badala ya kuwalaumu pale wanapoharibu na hata kutumia nguvu kutaka kuwadhibiti. Mfano mzuri ni suala la Marehemu Daud Mwangosi na Absalom Kibanda. Naiomba Serikali ilete huo Muswada wa Habari Bungeni ambao utazingatia maoni ya wadau wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeambiwa kwamba katika maadhisho ya mwaka huu, kumezinduliwa mfuko maalumu utakaosaidia waandishi watakaopata matatizo yakiwemo ya kuhatarisha maisha yao wawapo kazini.

Mheshimiwa Spika, ningeomba nichangie kwenye michezo. Tanzania tuna uhaba mkubwa wa *foot ball academy*, kwani mpaka sasa ipo ya Azam ambayo ni chamazi *football academy*. Nakuomba Mheshimiwa Waziri hili mlifanyie kazi, kwani ni muhimu sana kuwa na *academy* ili kupika vipaji. Michezo ni ajira na ni biashara, badala ya kugombea wachezaji wa kulipwa nje, *let say* kama Rwanda mfano Mbonyu Twite, Tanzania tuna uwezo wa kutengeneza akina Mbonyu Twite hata 1000 na kuweza kupata pesa za kigeni na kuitangaza nchi yetu duniani.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuwe na mkakati wa *ku-promote* utamaduni wa kufikiri, ni muhimu sana.

MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Spika, kabla na mara baada ya uhuru Mamlaka za Serikali za Mitaa

zilikuwa zinajenga na kusimamia viwanja vya michezo. Baadaye jukumu hili lilichukuliwa na Chama Tawala wakati wa Chama kimoja na kimeacha baada ya ujlo wa Vyama vingi. Nashauri Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ihamasishe Mamlaka za Serikali za Mitaa kujenga viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, matangazo ya biashara kama vile ya Kampuni za simu na kadhalika zinapotosha sana matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili, kwa mfano kutumia maneno masaa badala ya saa au lisaa limoja badala ya saa moja na kadhalika. Kuna umuhimu wa Wizara kuhakikisha matangazo yanayopelekwa katika vyombo vya habari yanahaririwa vizuri ili mafunzo ya lugha wanayopata vijana wetu shulenii yafanane na matangazo wanayoyasikia.

Mheshimiwa Spika, kuna ongezeko kubwa la mahitaji ya usimamizi wa ludha ya Kiwahili. Usimamizi wa lugha ya Kiswahili yanayotendwa kwa ajili ya BAKITA hayatoshelezi. Wakati mwagine hata vikao vya Baraza havifanyiki kwa ukosefu wa fedha. Wanahitaji kuwasaidiwa. Aidha, kuna haja ya kuangalia upya Sheria iliyoanzisha BAKITA ili kuipa meno zaidi, maana hivi sasa ni katika masuala ya ushauri tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALUM KHALFAN BARWANY: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutounga mkono hoja mpaka pale Mheshimiwa Waziri atakapotoa maeleo ya kina kwa yale yote niliyoyatolea taarifa kupitia mchango wa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu usajili wa vyombo vya habari. Inaonesha kuwa kuna upendeleo au rushwa kwenye utoaji wa vibali kwa Taasisi ya kidini, *Islamic Foundation* yenye makao yake pale Morogoro. Taasisi hii ya Kiislam imekusudia kuwa na *TV* baada ya kuwa na *Radio Imani*, inahitaji kuwa na *TVImani*. Pamoja na kutimiza masharti yote, bado kuna urasimu usiokuwa na lazima katika upatikanaji kibali. Kwa Wakrito, haraka; kwa Waslam, taratibu.

Kuna nini? Naomba maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo, namwomba Mheshimiwa Waziri aandae mpango kabambe wa kuwa na michezo yenye tija mashulenii.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 60 - 70 kulikuwa na michezo ya Shule za Msingi na Sekondari kwenye ngazi ya Sekondari za Tanzania ambayo ilikuwa inacheza na timu ya Taifa ya Zambia hadi mwaka 1978 ilipositishwa kutokana na vita vya Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana, kuanzisha michezo ya timu za Taifa na nchi za Afrika Mashariki. Hyo itasababisha kuwa na timu nzuri zenye washiriki wazuri kwenye michezo tofauti.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, magazeti, *TV*, na Redio ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya watu, lakini kuweka amani na utulivu. Hali ya magazeti sasa hivi ni mbaya. Ukishika gazeti, kwanza ujiulize ni gazeti la nini, kabla hujaanza kusoma ili uelewe nimesema uongo kwa kiasi gani? Haya magazeti yanayosema uongo, uzushi na ugombanishi yanaachiwa bila kuchukuliwa hatua. Baraza la habari sijui linafanya kazi gani, maana nadhani wangeweza kuchukua hatua, lakini hata wakichukua hatua ni baada ya miezi kadhaa. Ikiwa kweli inataka kuweka amani kwenye nchi yetu ni lazima ichukue hatua sasa.

Mheshimiwa Spika, vijana ni kada muhimu sana. Mimi naomba Serikali itoe kauli mbiu kwamba "Ajira ya Vijana Wote Tanzania Inawezekana." Ajira ya vijana ni suala mtambuka, Serikali imejitahi sana kuandaa ajira mbalimbali, lakini bado itatuchukua muda mrefu sana kuajiriwa vijana wengi. Kwa nini kama vile Serikali ilivyaoanda sera kama "Kilimo Kwanza,"

"Tanzania Bila Malaria Inawezekana," "Tanzania Bila UKIMWI Inawezekana"; Kaulimbiu hizo zimesaidia sana kuleta mwamko kwa Watanzania kuhusu kilimo, Malaria, UKIMWI na kufanya shughuli ya Malaria, UKIMWI na Kilimo kuwa mtambuka na kutengewa fedha za kutosha za ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa vijana ni mtambuka. Kwa hiyo, likiwekewa kauli mbiu, itahamasisha Wizara zote, siyo tu kwa vijana, bali pia kilimo, viwanda, michezo yote inaweza kutoa ajira tena nyingi za kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba Sheria ya Habari ije ili vyomo vya habari viweze kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, nasema tena, naunga mkono hoja.

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Spika, matangazo ya *TBC*, radio hayasikiki katika Wilaya ya Nkasi hasa mwambao mwa Ziwa Tanganyika. Sasa ni hatari, maana hawapati kabisa matangazo na kujua Tanzania au dunia inakwendaje. Karibu vijiji vyote vya mwambao mwa Ziwa upande wa Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika, wanasikia matangazo ya Redio Mobamoba, ni Mji uliopo katika Jamhuri ya *DRC-Congo* na hata kutuma ujumbe au salaam kwa kutumia hiyo *radio Moba*. Tafadhalii sana, tena sana, nataka uhakika wa kupata usikivu wa *radio* ya *TBC*, isikike kwa ufasaha kwa Wilaya ya Nkasi Rukwa.

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Nampongeza Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia Sekta ya Maendeleo ya Michezo. Sekta hii ni muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa jamii zetu. Wananchi wengi mpaka vijijini wanapenda sana michezo, hivyo naishauri Serikali kuimarisha miundombinu muhimu ya michezo. Mfano uimarishaji wa viwanja vya michezo, hii itasaidia kuwajengea

uwezo watoto wa kitanzania na hatimaye kupitia michezo wataweza kunufaika kiuchumi na kiafya. Shule nyingi za Msingi na Sekondari hazina viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuimarisha viwanja katika Wilaya na Mkoa. Nikiangalia katika Wilaya na Mkoa mpya wa Geita, hakuna viwanja vya michezo. Hata kama ukikuta kiwanja ni cha mpira wa miguu tu. Kama kuna nia ya dhati ya kuendeleza michezo, Serikali ijenge miundombinu katika Wilaya na Mikoa ili wananchi washiriki shughuli za michezo kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze Wataalam (Walimu) wa michezo ili fani hii iweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nailaani hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa kuandika uchochezi na wanapoelekezwa na Kiti wamekataa kuitikia agizo la Kiti cha Spika. Hii ni nidhamu mbovu na siyo mfano wa Serikali mbadala. Kambi ya Upinzani imeshindwa kutimiza wajibu wake kwa umma kwa kuendekeza maneno yasiyo na mapokeo ya heshima kwa umma.

Mheshimiwa Spika, (*TBC*) *Radio Tanzania* haisikiki kwa wananchi wa mwambao mwa Ziwa Tanganyika. Naomba tuwezeshwe kuisikia Radio ya Taifa. Inakuwaje *Radio Free Africa* inakuwa na nguvu kuliko Redio ya umma? Ni aibu! Iboreshwe!

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TV* ya Taifa, naomba mtandao wa *TV* hii ambayo ina vipindi elimishi isambae nchi yote ili twende kwa pamoja katika agenda zenyenye kuhitaji umoja wa kitaifa. Waongezewe fedha katika bajeti (nafurahi kuona wameongezewa fedha).

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara kuongeza fedha za vijana ili kuboresha miradi itakayowezesha vijana kupata ajira na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina kazi kubwa ya kuwaumba kimaadili waandishi wa habari. Habari wanazotoa wengi wao ni za ubabaishaji, na ukiwa na fedha unaweza kulazimisha habari iandikwe kama unavyotaka. Haya siyo maadili kabisa ya uandishi wa habari kama 'kioo cha jamii.'

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iache kigugumizi katika kufikia maamuzi ya kukienzi Kiswahili. Tusipoamua sisi, wenzetu wataamua na itakuwa aibu kubwa. Kiswahili kimekuwa na kupea karibu katika mabara yote duniani na chimbuko lake ni Tanzania. Hebu tuamue haraka Kiswahili kitumike katika kufundishia na kujifunzia katika masomo ya Elimu ya Sekondari na Vytho Vikuu. Lughya ya kigeni haiwezi kulikomboa Taifa, kwani wananchi wengi wanakwamisha kupata taaluma muhimu kwa maendeleo yao na Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipango ya kuanzisha makazi au makambi ya vijana, tutumie miradi ya kilimo kwanza kuanzisha makambiya mfano ya kuwa-reform vijana wanaopoteza mwelekeo kwa kuwachanganya na vijana *smart* kuanzisha mashamba ya uzalishaji mali na baadaye wakifanikiwa wapatiwe mikopo. Ardhi ni kubwa na ni *productive*.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMER: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa hotuba yao nzuri na yenye matumaini na mwelekeo wa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na wasemaji wa Wizara zote za Serikali yetu. Kwa kweli kila Wizara inaweza bajeti ya Idara ya Habari na Mawasiliano. Ningombaa sana kila Wizara iwatumie hawa kutoa habari au taarifa kwa niaba ya

Wizara husika. Siyo lazima waajiri au Katibu wa Wizara husika aongee. Naomba Waziri aliangalie suala hili kwa undani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kuweza kuongeza pesa kwa ajili ya *TBC*. Kwa kweli jengo lao ni aibu sana kwa Taifa. *TBC* ni Taasisi inayojitegemea, lakini naomba Wizara iwaangalie kwa macho mawili. Tukubali kuwa asilimia 90 ya mazuri inayofanya Serikali yetu ya CCM hutolewa na kuwahabarisha Watanzania, kupata taarifa au habari kuititia chombo chetu cha habari.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni aibu kwa Taifa letu ni mavazi wanayovaa wasanii wetu. Ni aibu sana kwa wazazi wanaopenda muziki kuangalia kwenye runinga au katika sherehe za kitaifa, kimkoa au kiwilaya. Ningombaa Wizara basi angalau kwenye sherehe za kitaifa au sherehe mbele ya jamii iweze kuzuua mbele ya hadhara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa vijana, napenda kusema kwamba pamoja na dhamira nzuri ya Mheshimiwa Waziri kutaka kuwawezesha vijana, lakini bado nasisitiza bajeti ni kidogo. Dhamira ya Mheshimiwa Waziri ya kuwasaidia vijana ningependa angetoa kauli kwa Maafisa Utamaduni kwenye Halmashauri zote nchini waweze kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge katika kupewa hizo pesa ili ziweze kuwafikia vijana walengwa.

Mheshimiwa Spika, shukurani.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa bajeti na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi tunakosa habari kutokana na ving'amuvi kwenye *Television* zetu. Tumenunua ving'amuvi kwa gharama kubwa lakini *TV* hazioneishi muda wote. Taarifa zinakatika kila wakati. Ni kero kubwa sana! Serikali ina mpango gani kuhakikisha ving'amuvi

vinavyouzwa ni vya uhakika *TV* zioneshe habari kwa uwazi na uhakika?

Mheshimiwa Spika, *TBC1* ndiyo tatizo kubwa kuliko. Taarifa ya habari unaangalia robo tu, robo tatu haioneshi.

Mheshimiwa Spika, tangu mchakato wa Vazi la Taifa uanze mpaka leo ni miaka minne. Ni kwa nini vazi hilo linachelewa? Hatua zimefikia wapi hata vazi la Taifa tunachukua miaka?

Mheshimiwa Spika, Serikali na Watanzania wote ni muhimu sana kutunza, kulinda na kuhifadhi utamaduni wetu na maadili yetu. Wasanii wa kiume wanavaa vizuri kwa heshima wakati wa kucheza, lakini wasanii wa kike baadhi wanavaa nusu uchi! Wanapocheza sehemu za maungo yao yanadhalilisha wanawake. Serikali inaona, hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, wapo wasanii wanatumia watoto kuigiza filamu sehemu mbalimbali. Filamu nyingine zinatisha sana, hawa watoto tunawafundisha nini? Tunawaharibu kimaadili, lakini pia tunawatoa kwenye mlango wa kusoma na kuelekeza mawazo yao kwenye filamu. Hivyo, hawawezi kufanya vizuri kwenye masomo. Serikali inatoa tamko hapa Bungeni kuzuia hili lakini linafanyika. Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Vyombo vya Habari ni muhimu sana ifanyiwe marekebisho ili kutobinya uhuru wa vyombo vya habari. Sheria iliyopo ina Upungufu sana.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuendelea kufungia Gazeti la Mwanahalisi kwa muda sasa kwa madai kwamba liliandika habari za uchochezi, siyo haki hata kidogo. Yapo magazeti mengi hayafungiwi? Serikali lazima ikubali kukosolewa na kuambiwa ukweli ili waweze kujirekebisha. Vyombo vya habari pia vinakosoa, vinarekebisha na vinaelimisha. Hivyo viachwe viwe huru. Wasifungwe pingu!

Mheshimiwa Spika, Watanzania na hasa vijana wamekuwa wanalamikia utaratibu unaotumika kukatisha tiketi za kuingia kwenye Uwanja wa Taifa wenye ukiritimba wa hali ya juu na wizi pia. Tiketi zinauzwa kwa uwezo mbalimbali kuendana na sehemu na viti 5,000, 7,000, 15,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi uwezo wao kiuchumi ni mdogo, hivyo wanategemea *ticket* za 5,000 na 7,000; wauzaji wanunua wao *then* wanaanza kuzuza kwa bei ya kuruka. Hili linakatisha tamaa, ambao wana moyo wa kuangalia mpira na wanashangilia wachezaji kuwapa nguvu.

Mheshimiwa Spika, suala la michezo mashulenii muhimu sana kuimarisha akili na kujenga milli ya watoto mashulenii. Serikali ihakikishe vitendea kazi na vifaa vya michezo mashulenii vinakuwepo na viwanja vinatengwa kila shule tena kwa michezo yote, siyo *football* tu.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari wafuate maadili ya uandishi wa habari na wasipendeele upande wowote. Wasiandike kile kinachowafurahisha wao wakasahau kuwa wanaandika kwa ajili ya jamii.

Mheshimiwa Spika, waandishi watambue heshima yao inapimwa kwa umahiri wao wa kuandika habari muhimu na siyo vituko vinavyotokea. Zipo tetesi kwamba waandishi wanachukua rushwa kwa Waheshimiwa Wabunge na hata Waheshimiwa Mawaziri na wafanyabishara ili waandike habari zao. Kama hili ni kweli, hii ni hatari kubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana na ajira ni tatizo kubwa hapa nchini. Hata kile kidogo kinachotengwa kwenye mfuko wa vijana kwenda Halmashauri ya Wilaya ni kidogo sana, hakiwezi kuwawezesha kujajiri kwa vijana. Ni lazima Wizara hii iandae mikakati na mipango makini ya kuwesesha vijana wapate mikopo nafuu ili wajajiri kwenye sekta mbalimbali.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Spika, kazi nzuri imefanywa na Wizara, ila fedha zinazotengwa kwa Wizara hii ni chache na hazitoshelezi utekelezaji wa majukumu. Ni vyema fedha zilizobakia Serikali izitoe mapema zisaidie.

Mheshimiwa Spika, *TBC* bado ina udhaifu wa usikivu katika maeneo mengi. Bajeti yake ni finyu sana, Serikali inaipa majukumu makubwa na huku ikiifunga mikono kwa Wizara na Taasisi zake kutolipa huduma wanazopata toka *TBC*. Madeni inayodai ni mengi, lazima Serikali isimamie ili *TBC* ilipwe fedha hizo na waweze kufanya kazi zao. *Management* ya *TBC* iwe *creative* na *innovative* ili waweze kuhimili ushindani wafanyakazi wake watizamwe kimaslahi wasomeshwe njia mpya za mawasiliano zenye kuleta mvuto kwa wasikilizaji na pia wawe na *succession plan* kwa kuajiri vijana kuwasomesha ili wazee waklondoka waweze kushika nafasi.

Mheshimiwa Spika, uchakavu wa mitambo ya *TBC – TV* na *radio* utazidi kuendelea iwapo bajeti ya *TBC* haitoongezwa ili waweze kubadili mitambo ya kizamani na kuweka ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mfumo wa dijiti ni lazima, hivyo vifaa vya *TBC – TV* na redio lazima viendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, majengo ya *TBC* yamechakaa, hayana mvuto na yanakimbiza wateja. Ukumbi wa maelezo umepitwa na wakati, unahitaji kukarabatiwa sana na kuweka vifaa vya kisasa ili uendane na hali ya ushindani wa leo. Serikali lazima isaidie fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sanaa, inasaidia sana wananchi kupunguza *pressure*, wasanii wapewe *priority* na kazi zao zithaminiwe na ziwalettee tija.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya. Hongera Mheshimiwa Rais kwa kusaidia kocha wa *football*. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri amwombe Mheshimiwa Rais

atulipie kocha wa *netball* ili tuweze kuinua kiwango cha mchezo huu. Wanariadha waonwe, watafutwe na wapewe uzito, nasi Tanzania tuwe kama Kenya na Ethiopia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwa kuwa Wizara hii ni muhimu kwa nchi yetu, nami naomba kufahamu, hivi ni lini sisi kama Watanzania tutatumia lugha yetu ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, huko vijijini kuna watoto wenye ubunifu na ambao hawafahamiki kwa Wizara, lakini ni wabunifu wa vifaa vya utamaduni. Ni vyema kuwatumia Maafisa Utamaduni ili kuibua vipaji kutoka hapa chini, kwani kuna baadhi ya watoto ambao hawana hamu ya masomo, lakini ni wabunifu wa vifaa vya kuitamaduni. Pili, baadhi yao hata Kiswahili hawajui na wanatumia lugha yao ya asili. Ni vyema tukawaibua kutoka huko waliko.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa hili, lakini cha ajabu, angalia *BBC Swahili* watangazaji wake kwa asilimia kubwa ni Wakenya na Watanzania ni wachache. Ni vyema sasa tukaamua kuitangaza lugha yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata Miswada humu Bungeni bado inakuja kwa Lugha ya Kiingereza. Kama Muswada wa uundwaji wa Tume ya Katiba ulikuja kwa Kiswahili, ni kwanini Miswada mingine iwe haiwezekani? Huu ni wakati mwafaka kwa Wizara kuvalia njuga kuhusu lugha ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu mavazi ya vijana wetu. Ni vyema sasa (KK) ambalo ni vazi la vijana wa kiume kuvala suruali chini ya makalio lipigwe marufuku, kwani inakuaje mtu kuonyesha nguo ya ndani alioivaa nusu inakuwa nje? Ni vyema kutafuta dawa ya kukemea hilo hata kama ni kwa viboko, lakini likomeshwe kabisa. Siyo vazi la adabu hata kidogo! Cha ajabu, hata

wanafunzi wa Vyuo nao baadhi yao huvaahivyo. Hawa ni wasomi sana na tegemeo la nchi lakini wanavyaa kk.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mavazi ya waimbaji wa kiume ni tofauti kabisa na vazi la waimbaji wa kike. Kwanini basi hawa wanawake wanavaa nusu uchi? Chukueni hatua sasa! Hatuhitaji kanga ndembe ndembe, huu nao ni uchafu, kwani ni aibu kwa mwanamke wa kitanzania. Ongeeni na wasanii hawa kuhusu kulinda utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa kazi ngumu ya kuendeleza kulinda na kuwaokoa vijana kwa mambo tofauti. Kazi kubwa mnayo, kazeni buti kazi bado mbichi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana katika kizazi hiki kwa kuwa ni wakati mzuri wa vijana kufanya kazi ili kukuza uchumi wa nchi yetu. Ili Taifa liendelee, ni lazima tuweke mazingira mazuri katika eneo la habari. Habari ni muhimu sana katika kuboresha utamaduni na michezo katika nchi yoyote duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa njia ya habari unaweza kujifunza mambo mengi sana. Napendekeza kitengo cha habari kipewe umuhimu wake. Kwa mfano waandishi wa habari wapewe ujuzi zaidi ili waweze kutoa habari kwa ufundi zaidi, Waandishi wa Habari walipwe posho kutoka katika mfuko wa Serikali ili wasiingie katika tamaa ya kupokea fedha kutoka kwa mtoa habari, pia mishahara yao iwe ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu uheshimiwe, wala usidharauliwe na Mataifa yaliyoendelea. Tuna utamaduni wa kujivunia ambao tumerithi kutoka kwa mababu zetu. Tudumishe utamaduni wetu wa mavazi pia vyakula vyetu tunavyokula ili kulinda afya zetu.

21 MEI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo, bado sana Watanzania hasa vijana wajitume katika kufanya mazoezi ya michezo wowote ule, kwa mfano michezo wa mpira, dansi uimbaji (*music*) na kadhalika. Michezo ni ajira. Kwa hiyo, vijana wajitume na waone kama ni ajira ambayo inaweza kuwaingizia kipato katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja.

MHE. CLARA DIANA MWATUKA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi yake ambayo inaleta matumaini, vilevile kwa Naibu wake pamoja na Kamati.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie kwa machache juu ya bajeti ya Wizara hii. Kwanza, nianze na utamaduni kwa upande wa mavazi. Vijana wetu wanapenda sana mambo ya kuiga hasa mavazi. Mavazi wanayovaa vijana wetu ni ya kusikitisha hasa kwa wasichana, sina haja ya kueleza kirefu kwa vile yanaonekana. Ukienda kwenye miziki ndiyo balaa! Ajabu ni kwamba, vijana wa kiume wanavaa nguo za heshima, wanacheza vizuri tofauti na wasichana kazi ya kukata viuno. Sisemi bila kukata viuno ndiyo kusema bila hivyo michezo labda haipendezi, sjui. Naiomba Serikali pamoja na Mheshimiwa Waziri waone haja ya kukomesha tamaduni hizi. Ikitolewa amri, ni wazi kwamba itatekelezwa tu bila kusita.

Mheshimiwa Spika, naomba Waandishi wa Habari wawe wanaandika habari za kweli, waache kuandika habari zisizo na ukweli. Wakati mwengine huwa wanaandika kichwa cha habari ambacho ukienda kuangalia ndani, tofauti na kichwa cha habari. Pia inawezekana isiwepo pale ndani.

Mheshimiwa Spika, waandishi wengine ni ukweli usiopingika kwamba wanununuliwa ili waandike habari za wale wanunuvi.

Mheshimiwa Spika, inafahamika wazi kwamba lugha yetu ya Taifa ni Kiswahili, lakini lugha hii haithaminiwi vilivyo.

Imeelezwa umuhimu wake ili kuikuza kwamba kitumike mashulen na sehemu mbalimbali. Pamoja na kwamba Kiingereza ni muhimu, lakini Kiswahili ni lazima kipewe kipaumbele. Inashangaza kuona hata kwenye Semina hata kwenye taarifa zetu hapa baadhi yake hutolewa kwa Kiingereza wakati Bunge letu ni la wananchi tupu. Wakati huo huo wananchi wanapenda kusoma taarifa hizi. Wakati huo huo sio wote wanaelewa. Hayati Baba wa Taifa aliusia ya kwamba, wakati wa kuchangia Wabunge Bungeni isiwe wanachanganya lugha kwa manufaa ya wananchi ambao wanasikiliza, wajue nini kinazungumzwa Bungeni. Kwenye semina pia taarifa inaanidikwa kwa Kiingereza, baadhi, lakini maelezo hutolewa kwa Kiswahili. Sasa kuna faida au maana gani ya kufanya hivyo? Ni vyema msisitizo ukatolewa, iwe ni ya Kiswahili moja kwa moja, labda pale inapotakiwa kupelekwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wengi wanazurura Mijini na hata Vijiini. Hii ni kutokana na kukosa ajira. Wengine wanakuwa na nia ya kujihangaisha ila wanakosa mitaji. Kama kule Masasi, vijana wengi wanajishughulisha na kilimo cha bustani kwa wale ambao wapo karibu na mito ya kudumu. Changamoto wanazokumbana nazo ni pamoja na kukosa mitaji. Kama wangkuwa wanapewa mitaji, wangeweza kununua mbegu pamoja na madawa. Kule wanalima zaidi nyanya, vitunguu na mboga mboga. Pia wanahitaji mashine za kumwagilia. Hivyo, naiomba Serikali iwasaidee kuwakopesha fedha, wajiedeleze.

Mheshimiwa Spika, vile vile vijana wengi wanapenda sana michezo, hasa mpira. Kama inavyojulikana juu ya ukata, uwezo wa kupata mpira na jezi ni taabu. Hata mashulen pia zamani vifaa vya michezo vilikuwa vinapatikana Wizara ya Elimu. Hii ilikuwa inakuza vipaji vya watoto. Hivyo ni vyema Serikali itilie mkazo suala hili la michezo.

Mheshimiwa Spika, kuna vijana ambao hivi sasa wanaamua kuunda vikundi ambavyo hujishughulisha na mambo ya usanii, wanafanya mambo ya uigizaji, kwaya na ngoma. Hawa wana nia ya kuendeleza vipaji, pia

wanatafuta ajira binafsi. Hivyo ni vyema ivione vikundi hivi na Masasi Vijijiini (Nanganga Kata) na kuwatia moyo kwa kuwapa mitaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nianze hotuba yangu kwa kuiomba Serikali kutokana na umuhimu na Wizara hizi na huduma inayotegemea kutolewa katika jamii, Bajeti yao ni finyu sana.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa nne umezungumzia majukumu ya Wizara kwamba ni pamoja na kuratibu na kusimamia masuala ya maendeleo ya vijana ili kuwawezesha vijana kujiajiri, kuajirika na kujitegemea. Je, Wizara hii inasimamia vipi ile mikopo inayotolewa katika Halmashauri zetu kama ni kweli mikopo ile vijana wanayo elimu ya kutosha ya kujua jinsi ya kuifkia fursa hiyo? Kwa kuwa wapo vijana wengi wenyewe taaluma mbalimbali na wengine wamehitimu katika Vyuo vyetu vya VETA, lakini tatizo lao kubwa, hawana mitaji.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara imefanya jitihada gani kuhakikisha haya Mashirika na *NGO* zinazoshughulika na mambo ya vijana, zinatimiza wajibu wao? Je, ni Taasisi gani za fedha zinatenga mafungu kwa ajili ya maendeleo ya vijana?

Je, nini mkakati wa Serikali kusaidia vijana wa kimachinga kwa kuwa vijana hawa kutokana na kutokuwa na maeneo maalum ya biashara zao wamekuwa wakitumika na baadhi ya wanasiasa kujipatia umaarufu kisiasa?

Mheshimiwa Spika, ni vyema Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, atueleze ni mkakati gani umewekwa na Wizara wa kupata taarifa ya vijana na vikundi vyao kwenye Halmashauri? Je, ni mkakati gani uliowekwa kwa ajili ya kuboresha mwongozo uliokuwepo katika mfuko wa maendeleo ya vijana ili kuongeza tija ya ufanisi wa mfuko huo kwa vijana?

Mheshimiwa Spika, ukisoma pia ukurasa wa nne wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, unazungumza uratibu wa kusimamia maendeleo ya michezo nchini. Naomba Wizara ituambie mkakati wa wavamizi wa viwanja vyta wazi vivilvyotengwa kwa ajili ya michezo katika Halmashauri zetu. Tulisikia kuwa wale wavamizi wangebomolewa. Je, maazimio hayo yalifanyika na hatua gani ilichukuliwa kwa Watendaji wa Halmashauri waliohusika na tuhuma hizo?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kurudisha michezo ya mashindano ya shule za msingi (UMISHUMTA).

Mheshimiwa Spika, michezo ile ndiyo ilikuwa inaibua vipaji vyta watoto wetu na kuvienda. Waalimu wa Shule za Msingi hawana mafungu kwa ajili ya michezo. Naomba Serikali itenye fungu kwa ajili ya michezo hiyo ili ilete tija kwa Taifa. Nyumba nzuri hujengwa na msingi imara, hivyo kuimarisha michezo. Tutapata wanamichezo bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Timu ya Taifa ya Wanawake, ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha timu hii inasonga mbele, kwa kuwa imekuwa inajitahidi sana kupeperusha Bendera ya Taifa hili vizuri sana. Tunasikitika kuona mashindano yakianza, bakuli linatembezwa kama watoto yatima. Ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya timu hiyo na jinsi ya kupatiwa kocha wa kigeni?

Mheshimiwa Spika, ni lini Sheria ya Uhuru wa Vyombo vyta Habari italetwa? Ni imani yangu itaongeza uwajibikaji wa vyombo hivyo. Je, Serikali inaweza sheria gani kuwabana wamiliki wa vyombo vyta habari kuboresha ajira ya wanahabari katika utendaji wao? Wengi hawana ajira ya uhakika, hawapati mishahara, hawana hata Bima ya Afya na mbaya zaidi hawana hata Bima za Maisha. Wakipata matatizo kazini, ndiyo ukomo wa ajira zao. Tunaomba Serikali iwasaidie ili waitendee haki tasinia hii ya habari, matokeo yake wanununuliwa na Vyama na baadhi ya Viongozi na

kusababisha kutotenda haki na kuangalia maslahi ya mtu binafsi.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu mfululizo Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo sana kwa ajili ya Wizara hii. Mwaka huu tunaishukuru Serikali kwa kuongeza Bajeti kutoka bilioni 19.3 hadi bilioni 21.3. Japo kiasi hicho Mheshimiwa Spika, bado hakitoshi ikilinganishwa na majukumu ya Wizara na mahitaji ya vijana ambao wanakabiliwa na changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo wa Vijana wa Taifa (*YDF*), Serikali imetenga bilioni tatu tu. Fedha hizi ni ndogo sana hazitoshi. Vijana hawana ajira wameamua kujunga na kujajiri kupitia vikundi mbalimbali vyta ujasiriamali, lakini mabenki hayako rafiki kwa vijana kwani hawana mali za kuweka dhamana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mfuko huu ndio ukombozi kwa vijana. Hivyo Serikali iweke fedha za kutosha kwenye Mfuko huu ambao kwanza mtandao wake uko katika kila Halmashauri kwani itasaidia kufikia vijana wengi nchini.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi hazichangii asilimia tano ya mapato yake kwenye Mfuko huu kama vile Sheria ya Mfuko inavyoelekeza. Naomba Halmashauri zote zitekeleze na adhabu zitolewe kwa zile Halmashauri zitakazokiuka.

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji wa vijana kujunga na vikundi vyta ujasiriamali bado hautoshi. Mfano *SACCOS* na *VICOBA*, taswira iliyopo ni kama kwa ajili ya akinamama tu. Tusipofanya hivyo umaskini hautakwisha katika jamii, utakuta kwenye familia mama amejinga na *SACCOS* anafanya shughuli za kujiongeza kipato, lakini ana jukumu la kuhudumia watoto wake watatu ambao ni vijana wenye nguvu na uwezo wa kufanya kazi. Matokeo yake mama

anaishia kulea watoto na wajukuu kupitia kipato chake kidogo anachopata.

Mheshimiwa Spika, Wizara ishiriki kikamilifu kwenye mpango mzima wa kurasimisha ardhi ili vijana wapewe kipaumbele, waweze kutengewa maeneo ya kutosha kwa ajili ya michezo na maeneo ya kufanya biashara ndogondogo ili vijana wenzetu Wamachinga wasisumbuliwe tena. Miradi mikubwa kama *SAGCOT*itengewe mashamba kwa vijana kujifunza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Baraza la Vijana la Taifa; ni miaka 17 sasa tangu Sera ya vijana ya Taifa ilipoelekeza kuundwa kwa Baraza la Vijana la Taifa mwaka 1996, sera ambayo baadaye iliundwa upya mwaka 2007, Mheshimiwa Spika, sera zote mbili zinaelekeza kuundwa kwa Baraza la Vijana la Taifa.

Mheshimiwa Spika, vijana hawana mfumo wowote unaowakutanisha na kuweza kujadili mambo yao na kutoa maoni yao na kuyafikisha Serikalini.

Mheshimiwa Spika, vijana kwa sasa wamejiunga na mifumo iliyopo kwenye Vyama vya Siasa, Madhehebu ya Dini na Asasi zingine mbalimbali. Lakini kule wanafundishwa itikadi za kisiasa na masuala ya imani, hivyo Serikali ndio yenyewe wajibu wa kuunganisha vijana tuweze kujadili masuala ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa tisa kuna maelezo ya vyombo vya Habari vilivyofungiwa kurusha matangazo yake kutokana na kukiuka kanuni za utangazaji. Vyombo hivyo vya habari ni Neema FM na Imani FM. Hata hivyo, hotuba ya Mheshimiwa Waziri haielezei chochote kuhusu kufungiwa kwa gazeti la Mwanahalisi ambalo ni muda mrefu tangu gazeti hilo lifungiwe.

21 MEI, 2013

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri katika majibu yake anieleze ni kifungu gani cha Sheria kilitumika kulifungia gazeti hilo la Mwanahalisi bila kikomo?

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 12 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna maelezo ya makubaliano kati ya TBC na Kampuni ya China iitwayo *Star Communication Network Technolgy* na kuanzishwa Kampuni ya ubia iitwayo *Star Media Limited*. Hata hivyo, ving'amuzi vinavyoingizwa nchini na *Star Media* havilipipi ushuru na ingetegemewa kwamba ving'amuzi hivyo viuzwe kwa bei nafuu ili Watanzania wengi zaidi waweze kumudu bei na hivyo kupata haki yao ya msingi ya kupata habari.

Mheshimiwa Spika, mamlaka husika iangalie namna ya kupunguza bei ya ving'amuzi hivyo kwani wananchi wengi wanashindwa kumudu bei ya ving'amuzi hivyo.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana litasaidia sana katika kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za maendeleo yao. Serikali iharakishe uundwaji huo wa Baraza la Vijana ili vijana wetu waweze kufaidika na Baraza lao.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Vijana bado hatujaona mafanikio yoyote. Ni muda mrefu sasa tangu tuambiwe hapa Bungeni kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi hawana mitaji kwa ajili ya kuanzisha biashara na hivyo kujikimu maisha. Vijana wengi wamezagaa mitaani kwa kutokuwa na shughuli rasmi za kufanya. Benki ya vijana itasadia sana vijana katika kujikwamua kiuchumi kwa kupata mikopo na kuijendeleza na hivyo kuondokana na umaskini kwa kufanya kazi na kuwajibika katika kujenga Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia katika Sekta ya Habari. Taifa hili lichukue hatua za dharura za kudhibiti vyombo vyahabari ambavyo vinachochaea uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Spika, hakuna Demokrasia isiyokuwa na mipaka. Leo waandishi wa habari wanaandika habari za kuchochaea wananchi na kuhamasisha wananchi waichukie Serikali, vilevile kutoa habari zenyenye kuashiria udini.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara husika haitawachukulia hatua wamiliki wa vyombo hivi, Taifa hili litaangamia mara moja. Naomba Serikali ichukue hatua mara moja.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana ni muhimu sana katika maendeleo ya ustawi wa jamii na Taifa letu. Naishauri Serikali iandae mpango mkakati wa kuwawezesha kupata mitaji na kuwapa elimu ya ujasiriamali utakaowasaidia katika maisha yao. Kama tutawapa elimu ya ujasiriamali tutawasaidia vijana walio wengi ambao watachangia uchumi katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, suala la michezo; naishauri Serikali ikuze michezo mashulenii na isiwe mpira wa miguu pekee, ni vyema tukajenga mfumo wa kuandaa watoto kwa kujenga vituo vyaa michezo ambazo vitakuza sekta ya michezo na kuibua vipaji vyaa michezo ambavyo vitaibua Watanzania watakaoleta sifa kwa Taifa letu. Ni vyema Serikali ije na mkakati mpya ambao utawasaidia vijana walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Lugha ya Kiswahili; tunaomba Serikali iandae na kusimamia kwa dhati Lugha hii. Inashangaza sana kuona Lugha ya Kiswahili ikibezwa sana na kuiharibu bila kuwa na usimamizi. Naiomba Serikali itenye fedha za kutosha ili ziendeletezeli Lugha ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kuhusu Chama cha Mpira (*TFF*), kiangalie kuwaenzi wanamichezo walioilitetea sifa Taifa letu. Inasikitisha sana kuona wanamichezo kama Peter Tino,

Jella Mtagwa, Zamoyoni Mogella na wengineo wengi hawawandalii mpango mahususi wa kuwaenzi kwa kuandaa michezo ya hisani itakayowasaidia kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana bado haujatengewa fedha za kutosha ambapo tunafahamu kwamba, wimbi la vijana amba ni wengi sana nchini, lakini hawana ajira na haiwezekani wote kuajiriwa na Serikali au Taasisi Binafsi.

Mheshimiwa Spika, ni muda sasa Serikali iwatendee haki kwa kuwawekea mazingira rafiki ya kuweza kupata mikopo, lakini pia Serikali iangalie uwezekano wa kutambua vyeti nya wanavyuo kwa ajili ya kuwawezesha kupata mikopo. Kama vijana wamesoma na vyeti wanavyo lakini hawana ajira au mikopo ya kujidendeza; tujiulize hiyo elimu ina manufaa gani kwao? Tutumie nguvu hii kubwa ya rasilimali vijana, lazima itumike kujenga Taifa na si kuvunja Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione uwezekano wa kuwaendeleza vijana katika sekta ya kilimo ikiwezekana kila Serikali ya kijiji itenye maeneo kwa ajili ya kuwapa vijana kuendeleza kilimo katika maeneo mengi nchini yanamiliikiwa na wazee amba hawawezi kulima eneo lote, lakini vijana wapo wamekosa maeneo ya kulimia.

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu ya mwakani "kilimo ni ajira kubwa kwa vijana".

MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa afya. Sasa naomba nichangie kwa kuanza na vijana.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea vijana ni kwamba, tunaongelea nguvukazi ya Taifa. Leo hii nikisema nimuulize Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kuwa Serikali

imewasaidia vipi vijana katika kujikwamua na umaskini. Majibu yake yatakuwa na utata tu.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa hatuwezi kuumaliza umaskini kama tutawasahau vijana ambao ndilo kundi kubwa katika rasilimali watu hapa nchini.

- (i) Kuna vijana waliosoma mpaka vyuo, lakini hawana ajira wala mikopo.
- (ii) Kuna vijana waliosoma mpaka kidato cha nne hawakufanikiwa kuendelea ambao ni wakulima tu na wengine wapo mtaani.
- (iii) Wapo vijana ambao wamesoma mpaka darasa la saba na wasiosoma kabisa na wameishia kufanya biashara ndogondogo, kilimo, uchimbaji madini na uzururaji wa kukaa vijiweni. Hili kundi ndilo litalitesa Taifa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Serikali na vijana lipohapa. Mfano:-

- (i) Vijana Wamachinga wananyanyaswa na Serikali yao na ugomvi mkubwa ni maeneo ya kufanya biashara zao. Serikali imekuwa ikiwatoa katika maeneo yao na kuwapeleka sehemu nyngine ambayo unakuta haina huduma ya maji au vyoo vya kutumia hawa wafanyabiashara.
- (ii) Mheshimiwa Spika, sehemu nyngine ni vijana wanaofanya shughuli ya uchimbaji madini. Wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakinyanyaswa kwa kukosa maeneo na kuchimba katika maeneo ya wachimbaji wakubwa na kuuza kwa bei ya hasara na wenye maeneo hayo huku Serikali yao inaona. Je, kijana anaendelea vipi?

- (iii) Mheshimiwa Spika, vijana wanaoshughulika na kilimo wanalima katika mazingira ya kimaskini. Mikopo hakuna, ardhi ni ya migogoro, hivyo unafuu wa maisha kwa vijana ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwaangalie vijana sana na iwaangalie kwa jicho la *Gender*. Naishauri Serikali ifanye utafiti katika maeneo ya machimbo ya madini, kisha iwagawie maeneo vijana wa kike na wa kiume katika maeneo ya kuchimba madini angalau kwa vikundi, vivyo hivyo hata katika kilimo, vijana wajiveke katika vikundi. Serikali iwagawie maeneo vijana na kwa vikundi itaraphisisha kuaminipa katika mikopo ya zana za kilimo ili wajkwamue na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanatumia ardhi vibaya kwa kuwanyima wenzao nafasi wakijilimbikizla maeneo makubwa ambayo hawana uwezo wa kuyalima yote na badala yake wanafanya biashara ya kuwakodishia wananchi wengine kwa riba kubwa ya fedha au chakula mara tu atakapovuna mwananchi analipa magunia kama ni mpunga au mahindi ambao labda ndiyo amepata kwa matumizi ya chakula. Je, huu siyo ubepari?

Mheshimiwa Spika, haya mambo ndiyo yanayoididimiza nchi kwa umaskini na kuigawa mafungu ya tajiri na maskini. Serikali ifanye ukaguzi na iwanayang'anyo maeneo mengine na kuwapatia wasio na maeneo kama vijana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akihitimisha, napenda anieleze kuhusu vijana. Serikali kuitia bajeti hii inakwenda kuwasaidia vipi vijana kujkwamua na umaskini na kupata angalau unafuu wa maisha?

Mheshimiwa Spika, utamaduni unawakilishwa na mila na desturi kutoka katika makabila mbalimbali yaliyopo nchini. Mila na desturi za:-

- (i) Mavazi;
- (ii) Vyakula; na
- (iii) Lugha.

Mheshimiwa Spika, mfano, mavazi, makabila mengi yana utamaduni wa kuvaa nguo za heshima zinazositiri maumbo. Lakini kuna watu wanaopenda mambo ya kuiga kutoka Mataifa ya wageni ambao kwao kuvaa chupi mbele ya watu ni sawa, tofauti na sisi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mfano mwagine ni vyakula. Utamaduni wa Mtanzania, wengi hupenda kupika viazi vitamu vikiwa kwenye maganda yake kiafya zaidi. Lakini kwa wale wanaopenda kuiga atasema kwamba kula viazi kama hivyo ni umaskini au kuishiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo. Serikali isisitize vipindi vya michezo virudishwe mashulen, kuwe na mazoezi ya michezo mingi na siyo mpira wa miguu tu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia hoja kadhaa katika wizara hii.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya kwanza ni umuhimu wa Serikali kufuatilia kwa karibu taratibu za chaguzi za Vyama vya Mpira wa Miguu ili kuhakikisha kuwa ni chaguzi za haki na huru.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tulishuhudia utata mkubwa katika uchaguzi wa *TFF*, ngazi ya Taifa uliovnjika na kulazimika kusimamishwa na *TFF* na Serikali lakini hata na *FIFA*.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa hapa lilikuwa ni jitihada za makusudi zilizokuwa zinalazimishwa na kundi la

watu waliokuwa wakitaka watu maalum wanaowataka ndiyo wawe viongozi.

Mheshimiwa Spika, tulishuhudia haki za Wagombea zikikiukwa waziwazi, baadhi ya wagombea wakiambiwa hawana uzoefu wa uongozi, wakati ni viongozi wa vyama vyaa soka wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia baadhi ya viongozi kila wanapotaka kugombea, huambiwa wamefanya kosa linalokatazwa na *FIFA* hata kama kosa hilo liliifanyika zaidi ya miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika hili ni kwamba, ili haki itendeke, ni vema wagombea wote wa nafasi za *TFF* Taifa wafikishwe kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa *TFF* ndiyo uwapigie kura.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja. Hata hivyo, haya yafuatayo yazingatiwe na nahitaji ufanuzi (majibu).

Mheshimiwa Spika, Tasnia ya habari ni muhimu sana kila mahali hususani katika karne hii ya 21. Lakini badala ya kuelimisha, kuhabarisha na kuburudisha, imekuwa ndio sehemu ya uchochezi. Hii ni kwa vyombo vyaa habari na waandishi, ukiukwaji wa maadili ya habari umekithiri sana kama vile kuchafua viongozi, ushabiki mwangi na kadhalika. Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti hilo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la michezo; ni kweli michezo ni afya na hamasa ni kubwa sana kwa Watanzania katika michezo yote na kiwango kinapanda. Hongera. Hata hivyo, Walimu (Makocha) wa kigeni licha ya kuwa wanalipwa mishahara kwa kiwango cha juu sana (*expatriates*) lakini:-

(a) Kwa nini hawalipishwi kodi i.e *P.A.Y.E*?

- (b) Mishahara yao inapitia Hazina - sawa ingawa mikataba yao ipo baina yao na *TFF*, lakini kwa nini *TFF* wadaiwe kodi hiyo na *TRA* wakati mishahara, malipo yanafanywa huko huko Hazina? Hii ni kuwaonea *TFF*. Mwaka jana tu Milioni 157 zilikatwa *TFF*, kweli itajiendeshaje? Zaidi ya Milioni 570 zinatakiwa kukatwa kwa *expatriates* hawa kwa nini wasikatwe wao wenyewe?

Mheshimiwa Spika, lini sera ya michezo itakamilika? Vijana ni Taifa la leo. Zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania ni vijana. Ajira hakuna. Nini mkakati wa Serikali katika kusaidia vijana hawa mitaji ili waweze kujajiri?

Mheshimiwa Spika, kwa nini wasanii wa kike wanadhalillika na uvaaji wa nguo ambazo ni kinyume na maadili ya Kitanzania? Nini mkakati wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, Redio zilizofungwa kwa ajili ya uchochezi, zilikuwa ni za dini gani na uchochezi gani ulikuwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Waziri; Mheshimiwa Amos Makalla, Naibu Waziri; Ndugu Seth Kamhanda, Katibu Mkuu; Bibi Sihaba Nkinga, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi/Kamishna wa Idara za Wizara, Watumishi wote na Wenyevitini na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ingawa wengi katika mazingira yasiyokidhi sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utangazaji: Nalipongeza kwa dhati Shirika la Utangazaji (*TBC*) kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhabarisha Watanzania hadi vijijini. Katika ziara zangu vijijini nimebaini kuwa yako maeneo ya nchi ambayo matangazo ya Shirika hili hayafiki. Nashauri kuwa

booster ziongezwe na pia mkongo wa mawasiliano wa Taifa utumike ili kufikisha matangazo ya *TBC* maeneo yote ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ili shirika litimize matarajio hayo na kwa kuzingatia kuwa chombo cha utangazaji kinatoa huduma kwa umma, hivyo kutoruhusiwa kuwa na vipindi vingi vyta matangazo kama vilivyo vyombo binafsi, nashauri kuwa Serikali itoe ruzuku ya kutosha kwa *TBC*. Kanuni za utangazaji zirekebishwe ili kufanya makampuni yanayomiliki *multiplex* watoe sehemu ya mapato wanayokusanya kwa *TBC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhamiaji toka Analojia kwenda Dijitali; tunatambua umuhimu wa teknolojia ya dijitali katika utangazaji hususani katika kuboresha picha na sauti. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mdhibiti wa mawasiliano nchini yako makampuni matatu yaliyopewa leseni za kuendesha *multiplex*. Tokea teknolojia hiyo ilipoanza kutumika ubora wa huduma uboreshwe vilivyo.

Hata hivyo, yako makampuni matatu ya *TV* ambayo yamekuwa yakitoa matangazo yao kwa majoribio (*Test*) kwa muda mrefu. Naomba maelezo ya kuwa ni lini makampuni hayo yatakamilisha ujenzi wa mtandao na kuanza kutoa matangazo kikamilifu. Ili Watanzania wote wafaidi matangazo ya Dijitali, nashauri kuwa *TBC* ipewe fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ili ijenge mtandao na kufikisha matangazo yake hadi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Habari; Watanzania wamekuwa wakipewa taarifa zisizo sahihi kupitia magazeti na mitandao ya kijamii ikiwemo blogu. Baadhi ya magazeti na blogu imekuwa ikichapisha taarifa zenye kukiuka maadili ya Taifa letu. Nashauri kuwa ili kudhibiti hali hiyo, nashauri kuwa Serikali kupitia Wizara hii itafakari na kuona namna ya kudhibiti vyombo hivyo ili kupusha jamii yetu na upotoshaji unaofanywa kwa jamii yetu. Tuangalie namna ambayo Kamati ya maudhui inaweza ikapanua wigo wa kazi zake kujumuisha maudhui ya magazeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waandishi wa Habari; katika miji karibu yote Tanzania wako watu wanajiita Waandishi wa Habari ingawa kitaaluma hawajafuzu. Wengi kati ya hawa ndio wanaoandika habari za kupotosha jamii. Kwa bahati mbaya wamiliki wa vyombo vyta habari huwatumia hawa kupata habari na huzichapisha bila kwanza kuzihakiki. Nashauri kuwa ziwepo kanuni zitakazozua wamiliki wa vyombo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya vijana; tunalo jeshi kubwa sana la vijana nchini lisilo na ajira. Wengi wamekuwa wakitegemea kuajiriwa kwenye sekta rasmi jambo ambalo uwezekano haupo. Kwa kuzingatia kuwa mahitaji ya vijana ni suala mtambuka, nashauri kuwa sera ya vijana ipitiwe upya ili kuzitaka Wizara zote kujumuisha katika mpango wao mkakati namna watakavyosaidia vijana kutumia fursa zilizo kwenye sekta zao kuwezesha vijana kujajiri.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa kuzingatia kuwa vijana hufanya asilimia kubwa ya jamii yetu, Mfuko wa Vijana utengewe fedha za kutosha ili vijana wakopeshwe, watekeleze miradi iliyohakikiwa na kuthibitika kuwa inatekelezwa kwa faida. Kwenye Jimbo langu ninalo jeshi kubwa ambalo hakika linahitaji kuungwa mkono ili kuwapa mafunzo ya ujasiriamali na mbinu za kuanza na kufanikisha biashara na miradi mingine ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi na ufugaji nyuki. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie ili idara ya vijana inisaidie kutekeleza jukumu hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mwenge wa Uhuru; Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ameshauri kuwa Mwenge wa Uhuru upelekwe Makumbusho ya Taifa utumike kama kumbukumbu na kivutio cha utalii. Ingawa sipendi kusema kuwa mhusika ana uelewa mdogo, nadiriki kusema kuwa anajitia hamnazo.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Wizara ikaandaa semina juu ya alama za Taifa (*national symbols*) ili hata wale ambao hawakubahatika kupata elimu ya uraia wasije wakaonekana

vituko mbele za wageni au na wenyeji wao watakaposafiri nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mwenge ni alama muhimu ya umoja wa Taifa letu na ni lazima tuulinde kwa gharama zote. Hao wanaoudhihaki mbona walishabikia mwenge wa Olimpiki na ule wa Malkia wa Uingereza ulipoingia na kukimbizwa hapa nchini? Tuwaelimishe ili wajitambue. Ili kulinda alama za Taifa letu ukiwemo Mwenge alama hizo ziorodheshwe kwenye Katiba Mpya na watu wote kutakiwa kuziheshimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya utamaduni; Tanzania ndiyo kitovu cha Kiswahili duniani. Kila mwaka vijana wengi wanahitimu shahada ya Kiswahili kwenye vyuo vikuu. Wachache huingia kwenye ualimu, lakini baadhi hubaki mitaani bila ajira. Kwa bahati nzuri ziko fursa zinazojitokeza hapa Afrika na maeneo mengine duniani za ajira kwa wataalam wa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni Umoja wa Afrika; hata hivyo, wakalimani wengi kwenye maeneo hayo ni wageni wa Kiswahili ikimaanisha nchi nyingine na si Tanzania. Nashauri kuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo isimamie maslahi ya vijana kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhakikisha kuwa vijana wetu wanashawishiwa na kuandaliwa kuchukua fursa zinazojitokeza ndani na nje ya nchi. Aidha, viongozi wetu washawishiwe wakubali kutumia Kiswahili kwenye hotuba zao ndani na nje ya nchi na wawe na wasaidizi wa lugha (wakalimani) kama ilivyo kwa fani nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Michezo; hivi sasa ni dhahiri kuwa michezo si burudani tu bali ni ajira. Kama ambavyo tunawekeza kwenye viwanda, kilimo na madini, tuwekeze kwenye maendeleo ya michezo ikiwa ni pamoja na kujenga na kuimarisha vyuo vya michezo na kuwezesha vijana wenye vipaji vya michezo ili waweze kushindana kwenye soko la ajira ya michezo ndani na nje ya nchi. Katika tasnia hii tuwekeze

kwenye mafunzo ya Walimu wa michezo ili kupunguza kiasi cha fedha za nchi zinazopotea kila mwaka kwa kuajiri Walimu wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari; *Right to Information* ni haki za binadamu. Sijaona Wizara ikiweka jitihada katika suala la *Information* kupatikana bure. Kwani magazeti yanauzwa, ipo haja baadhi ya taarifa zikawa *accessible* kwa wananchi kama wazee, vijana, vijijiini bure mfano, Matangazo ya ajira kwa vijana (Habari).

Habari za Masoko/Habari za hali ya hewa, *Right to information*, Wizara iwe na mabango pale ofisini kuonesha habari mbalimbali bure kwenye *website* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Vijana ni asilimia 60 ya idadi ya watu. Sijaona *Proper Management* ya vijana. *Caucus* za vijana au *counseling* kwani changamoto ni nydingi, vijana wanahitaji *counselling*, vyuo vikuu vina vijana wengi / Sekondari mahusiano ya Wizara na *Clubs* za vijana, *clubs* za *Sports* mashulenii. Wizara ipange *Open Sports area Garden* kama Uingereza *Leicester Square* matokeo yake kama hakuna *Open space* za *sports* vijana wanakaa kwenye magenje na kudanganyana.

Mheshimiwa Spika, Wizara igawe mipira ya kike/kiume kwa kila Kata mbona siyo hela nydingi, vifaa vya michezo kupitia Halmashauri kwani tunao Maafisa Michezo kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu BASATA; ni mwaka mmoja sasa Bodi haijateuliwa; kwa nini? Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, Wizara iweke *job centers* kila mkoa na kila Wilaya *part time job*, kazi za *shift*, Wizara i-coordinate,

coordination kati ya private sector na wananchi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba maswali yote yajibiwe.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja na pia kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya nchi katika sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na michezo.

Mheshimiwa Spika, nina hoja mbili ambazo ningependa kupata ufanuzi au maelezo ya Waziri.

- (1) Je, Wizara ina mikakati gani mahsusni ya kupambana na udhaililishwaji wa wanawake hasa unaofanywa na magazeti (ya udaku!)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi inayodai na kuthamini utu na hadhi ya wanawake. Tumetunga sera na sheria mahsusni kwa ajili ya kulinda haki za wanawake. Hata hivyo, inasikitisha kuona taarifa na picha nyingi kwenye vyombo vya habari hasa magazeti ya udaku zenye kudhalilisha wanawake. Nipatiwe majibu, ni mikakati gani ipo/au imewekwa na Wizara katika kupambana na vitendo hivi?

- (2) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya Elimu ya stadi za maisha kwa vijana kwa mwaka 2013/2014?

Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada za Wizara kwa kutekeleza programu ya mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule. Ni kweli kuwa mafunzo haya yana mchango mkubwa katika

kuwawezesha vijana hasa walio nje ya shule kupambana na changamoto mbalimbali za maisha kama vile maambukizi ya VVU/UKIMWI, mimba za utotoni na matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Tanzania *HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey (THMIS)* ya 2011/2012, zinaonesha kuwa maambukizi ya UKIMWI kwa vijana wa kike wa umri wa miaka 23 – 24 ni asilimia 6.6 wakati kwa vijana wa kiume ni asilimia 2.6.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu hii kwa kiasi kikubwa utachangia kuwaokoa mamia ya vijana wa kike kupata maambukizi ya UKIMWI kwa wasichana. Hii ni kutokana na sababu kuwa vijana hawa wengi hawana elimu ya stadi za maisha na hivyo kujilingiza katika ngono zembe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata maelezo ni kiasi gani cha fedha za ndani kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, wafanyakazi katika vyombo vya habari maslahi yao ni duni sana. Jambo hili linasababisha waandishi wa habari kukosa ujasiri wa kujizuia na vishawishi vya rushwa. Hivyo, naiomba Wizara hii ivisimamie vyombo vya habari ili kujenga maslahi mazuri kwa waandishi wa habari na hivyo kulinda Tasnia ya habari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa hapa nchini mwetu tumekumbwa na tatizo kubwa la mmomonyoko wa maadili kwa vijana wetu. Mmomonyoko huu umechangiwa sana na utandawazi tulionao. Kuna baadhi ya vyombo vya habari vinaonesha picha na matangazo yanayochangia sana katika mmomonyoko wa tabia za vijana wetu. Naiomba Serikali isimamie vyema vyombo vya habari ili visije vikaleta athari kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vijana ndio chachu ya maendeleo. Naiomba Serikali ipambane ipasavyo na mtandao wote unaojihusisha na madawa ya kulevyia ili kulinda afya za vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa vijana wetu. Naiomba Serikali zile fedha za Mfuko wa JK ziende moja kwa moja kwa vijana na wanawake ili kuwasaidia vijana kujajiri na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Timu ya *Twiga Starimeiletea Taifa* letu heshima kubwa. Nasikitika sana kwani timu hii haipewi kipaumbele licha ya kazi nzuri inayofanya katika soka. Naiomba Serikali iwekeze ipasavyo kwa Timu ya *Twiga Star* ili kujenga hamasa kwa vijana wa timu hii, hivyo iweze kufanya vizuri zaldi.

Mheshimiwa Spika, uzalendo kwa vijana unazidi kuporomoka kwa vijana wetu wa sasa juu ya kuthamini nchi yao. Naiomba Wizara iweke utaratibu wa kutoa elimu ya uraia kupitia vipindi vya *Television* na *Radio* ili Taifa liwe na vijana waliojaa uzalendo wa nchi yao na hivyo kutokuwa tayari kurubuniwa na yeote asienteakia mema nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

- (1) Kuhusu Lugha ya Kiswahili: chimbuko la lugha ya Kiswahili ni Afrika Mashariki na ilienea mpaka Afrika ya Kati. Lugha hii adhimu imetuunganisha Watanzania wa makabila yote bila kujali mila zetu. Ni vizuri sasa pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kukikuza, bado Serikali haijaonesha jitihada za makusudi kukithamini Kiswahili hasa pale kunapokuwa na mikutano ya Kimataifa ambapo ndio sehemu pekee ya kukifanya Kiswahili kisikike ulimwenguni. Ni kwa nini viongozi wetu wa juu pamoja na Mawaziri huwa

hawapendi kutumia Kiswahili wanapohutubia hadhara ya Kimataifa? Ni kwa nini wanapenda kutumia Kiingereza hata kama hawakwezi sawasawa na hivyo kulitia aibu Taifa? Ifike wakati sasa iwe sheria kwamba, ni marufuku kutumia Kiingereza kwenye mikutano yoyote ile ila Kiswahili kitumike pamoja na wakalimani wa kutafsiri kwa Kiingereza.

- (2) Kuhusu Vazi la Taifa; imekuwa ni muda mrefu sasa tumekuwa tukipigia kelele nchi yetu kuwa na vazi la Taifa. Ni nini kinakwamisha kupata vazi la Taifa? Kama Mataifa mengine ya Kiafrika yameweza ni kwa nini sisi tushindwe? Ifike muda sasa Wizara hii ifanye kila iwezalo ili nchi yetu iwe na vazi la Taifa ili kututambulisha mbele ya Mataifa mengine.
- (3) Kuhusu Wasanii wa kike na mavazi ya aibu; kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu toka kwa wananchi kwamba wasanii wa kike huva mavazi yasiyositiri maungo yao ya siri na hivyo kuwaabisha wanawake wote. Wasanii wa filamu na muziki wa dansi ndio wanaongoza kwa aibu hii. Ni kwa nini sasa Wizara isichukue jukumu la kuwafungia wanawake hawa hasa wasichana endapo watakaidi amri au agizo la kuva nguo za staha? Siyo kweli kwamba wanavalishwa ila ni wao ndio wanapenda kuva hivyo. Sasa ni lazima Wizara itoe maelekezo ya makusudi ili kuondoa aibu hii inayofanywa na wasanii wa kike kwa makusudi.
- (4) Kuhusu Waandishi wa Habari na vyombo vyahabari; Waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana na yanayohatarisha maisha yao. Pamoja na wimbi lililoitokeza hivi karibuni la Waandishi wa habari kuuawa wanapokuwa kwenye majukumu yao, bado maslahi yao ni madogo sana na hivyo kuwakatisha tamaa kwenye utendaji wao wa kazi. Ni muhimu sasa Serikali ikaona umuhimu wa kuongeza maslahi ya Waandishi wa habari na itoe maelekezo kwa vyombo binafsi vyahabari navyo

viboreshe maslahi ya waandishi ikiwemo pia kuwapa fursa za kujiendeleza kielimu.

Vyombo vya habari vya Serikali hususani *Television na Radio (TBC)* vimekuwa vikikabiliwa na tatizo kubwa sana la ukosefu wa fedha. Pamoja na udhaifu mkubwa wa viongozi kwenye Shirika la *TBC*, bado shirika hili lina matatizo makubwa ya kuwa na bajeti finyu na hivyo kushindwa kufanya kazi yake sawasawa. Tumeshuhudia kukatikakatika kwa matangazo ya *TBC* na pia picha ambazo zinakuwa haziko katika mpangilio mzuri wa matukio na habari.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo la kibajeti na hivyo Wizara ifanye juhudzi za makusudi kuinusuru *TBC* kwani ndio jicho la habari la nchi na ni aibu kwa nchi kuwa na Shirika la Habari lisilofanya kazi zake kwa ufanisi tena likiwa linaendeshwa na kodi za wananchi.

- (5) Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkataba wa *TBC* na *Startimes*; ni muda mrefu tumekuwa tukiishauri Serikali kuititia upya mkataba wake (*TBC*) na *Startimes* kwani unatia shaka. Imeonekana kwamba *TBC* imekuwa hainufaiki ipasavyo na mkataba huo na hivyo kupoteza mapato yake mengi.

Kamati ya *POAC* ilishauri kwamba angalau kwa kila Sh. 1,000 inayopatikana kwenye malipo ya ving'amuvi (*air time*) iwe inakatwa ili kuisaidia *TBC* katika utendaji kazi wake. Ni kwa nini hili halioneckani kwamba ni muhimu na kwamba litainusuru *TBC* katika aibu ya kutokufanya kazi zake kwa ufanisi?

Ushauri huu ni muhimu na una nia njema na Shirika letu hili ambalo ni muhimu kwa mustakabali wa uchumi, ustawi na amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii. Nina mchango ufuatao:-

- (a) TBC haisikiki kabisa Jimboni au sehemu karibu yote ya Wilaya ya Manyoni. Ni Redio Mwangaza tu ndiyo inayotegemewa na wananchi wa maeneo haya. Kwa miaka yote tangu uhuru (1961) wananchi walipata habari kuitia *Radio ya Serikali TBC (Tanganyika Broadcasting Corporation)* na baadaye RTD (Redio Tanzania Dar es Salaam). Lakini kuanzia miaka ya 2000, *Radio Tanzania*, Dar es Salaam ikaacha kusikika kwa kile kinachoelezwa matatizo ya mitambo ya kurushia matangazo katika baadhi ya maeneo nchini. Je, ni lini maeneo ya Wilaya ya Manyoni yataanza kupata matangazo ya *TBC* ili wananchi wapate taarifa rasmi (*first hand information*) kuliko kudoweya taarifa kuitia *radio zingine* za Taasisi binafsi?

Naomba majibu wakati wa *ku-wind-up* ili wananchi waskie from the horses mouth maana maelezo yetu Wabunge wa eneo hilo hayaingii akilini mwa wananchi, kwamba karne hii ya 21 Radio ya Taifa haisikiki kwa wananchi.

- (b) Mheshimiwa Spika, mara nyngi Mipira ya Michezo (*Football*) ndiyo inayopatikana katika maduka ya vifaa vyta michezo, lakini mipira ya *netball* na *basketball* ni adimu kwenye maduka ya vifaa vyta michezo na tunapotembelea maeneo yetu katika ziara tunaulizwa sana na vijana kuhusu mipira hiyo adimu na hata kupelekea kuonekana kwamba tunawapendelea vijana wa kiume wanaocheza zaidi mipira ya miguu (*football*).

Je, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha mipira yote inapatikana ili kuhamasisha ukuaji wa michezo yote hapa nchini na kuibua vipaji vyta vijana nchini? Naomba kupata maelezo na ufanuzi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja ila nipatiwe majibu. Badala ya kuwajibu Wapinzani tu naomba na sisi Wabunge wa Chama Tawala tupatiwe majibu wakati Mheshimiwa Waziri anapohitimisha.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Spika, Michezo ni afya, michezo ni ajira na michezo inaweza kuchangia katika Pato la Taifa. Kwa sasa hivi hapa Tanzania magonjwa ya shinikizo la damu la kupanda/ kushuka na sukari ya kupanda/kushuka kwa kiasi kikubwa kinachangiwa na mtindo wa kula na kwa kutofanya mazoezi au michezo. Cha kusikitisha, viwanja vingi vya michezo havipo, tena vingine vimegeuzwa, maduka, malisho ya mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesisitiza michezo kurudi mashulenii, lakini shule nydingi pia hazina viwanja vya michezo. Je, Serikali ina mikakati gani hasa kwa kuanzia kuhakikisha kila Wilaya kuna viwanja vya michezo? Kwa sasa hivi kama nchi imejikita zaidi katika michezo ya Soka na kusahau kabisa aina nydingine za michezo kama kuruka, kukimbia, kuogelea na kadhalika. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha michezo mingine inafufuliwa na kupewa uwezo wa kuicheza ikiwa ni pamoja na kutafuta Walimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni, ningependa kujua kutoka kwa Waziri utamaduni wa Mtanzania ni upi? Sababu kwa sasa hivi kitu pekee kinachoonesha utamaduni wetu ni lugha ya Kiswahili ambayo sasa inatumika nchi za Afrika Mashariki na karibu Bara la Afrika wengi wanajifunza Kiswahili. Je, kuna mkakati wowote wa kuanzisha utamaduni wa Kitanzania? Miaka ya sabini kama nchi ilipigwa marufuku kwa wanawake kuвая nguo fupi au nguo zisizokuwa na heshima. Je, ni lini Serikali ilitoa ruhusa kwa nguo hizi fupi kuvaliwa tena.

Mpaka sasa hivi mkakati wa kutafuta vazi la Taifa umefikia wapi na ni kiasi gani cha fedha kilichokwishakutumika mpaka sasa hivi? Je, inachukua muda gani kupata vazi hilo la Taifa?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, Tanzania tunajulikana kwa kuvaan Khanga kwa nini sasa tusitumie Khanga kama Vazi la Taifa. Wanaume washone mashati wanawake washone magauni, *Skirt, Blouse* na kadhalika badala ya kutumia zaidi ya miaka miwili wakitafuta Vazi la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari; ni haki ya kila Mtanzania kupata habari kama Katiba ilivyoainisha katika Ibara ya 18, lakini kwa sasa hivi siyo watu wote wanaopata habari hata kwa kuanzia kwa kutumia vyombo vyaa Serikali vya habari kama *TBC*. Yamekuwepo malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa watu wenye ulemavu wa kusikia, *TBC* awepo mkalimani wa ishara ili kuwasaidia watu hawa na wao waweze kupata habari. Je, ni lini *TBC* itaanza utaratibu huu wa kuweka mkalimani kwa ajili ya watu wenye ulemavu?

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vya habari kupokea na kusambaza habari lakini bado wanahabari hawawezi kutekeleza majukumu yao bila kuwepo na sheria ya kuwasimamia. Je, ni lini Muswada wa Habari utaletwa Bungeni?

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nanukuu: "Kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi Ibara hiyo hiyo ya 18 (a) nanukuu "kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake." Kwa makusudi mazima Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo kupitia Waziri wake Mheshimiwa Fenella kuzuia uhuru wa kupata habari kwa wananchi kwa kuendelea na kuzuia ruhusa ya kupewa leseni ya kurusha hewani habari ambazo *TV Imani* imekusudia kuwaelimisha na kutoa habari kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama ambavyo nimeeleza hapo mwanzo. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuititia *TCRA* wametimiza wajibu wao juu ya kupewa leseni kwa *TV Imani* baada ya kujiridhisha kuwa *TV* imetimiza vigezo vyote vya kupewa leseni. Inasikitisha sana kwa mtu mmoja kwa kutumia uwezo aliopewa na wananchi na kwa heshima aliopewa na Rais anatumia fursa hiyo kuzuia wananchi wasipate habari kutoka kwa chombo husika kwao na ambavyo wanavitegemea.

Mheshimiwa Spika, wananchi mbalimbali kwa pamoja walikubali kuchangia karibu bilioni mbili kwa kufanya kila linalowezekana ili wapate habari kuititia *TV Imani* ambayo ndio wanayoiamini kuwa itawapa habari sahihi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri siyo atueleze bali akubali kuruhusu leseni kwa *TV Imani* ili iweze kuwapatia wananchi habari wanazozihitaji.

Mheshimiwa Spika, tunajua Waziri anazo sababu zake za kuzuia *TV Imani* ambazo ni za kidini, sisi hatuoni sababu nyingine kwa sababu *TV Imani* imeasisiwa na Waislamu, ndiyo unatumia madaraka yako kuizua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kuendelea kufanya anavyofanya na sisi tutawaomba Waislamu wa nchi nzima kuandamana ili kumwomba Mheshimiwa Rais amwajibishe kwa kuzuia haki za wananchi kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19(2) nanukuu: "Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu binafsi na shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi." Kumbuka na timiza wajibu wako. Ahsante.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nitoe ushauri kwa baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

- (1) Mheshimiwa Spika, kuhusu usikivu hafifu wa *TBC*, Wilaya ya Kalambo. *TBC* kwa maana ya redio na *television* vimekuwa havisikiki au kuonekana katika maeneo ya Wilaya ya Kalambo na hivyo wananchi kulazimika kusikiliza vyombo vya habari kutoka nchi za jirani na hususani nchi ya Zambia na kwa bahati mbaya sana ikiwa ni habari ya kushawishi namna ya kubadili Serikali iliyo madarakani kama ambavyo wamekuwa wakifanya wao.

Mheshimiwa Spika, habari kama hizi si nzuri kwa mwananchi kuzisikia zikirudiwarudiwa badala ya kupata taarifa ya shughuli zifanywazo na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ihakikishe maeneo ya nchi yetu hususani yaliyo mipakani yanafikiwa na matangazo ili kujenga Utaifa na kuwalishwa wananchi wake nini ambacho kinatoka nchini mwao na kufanya na Serikali yao badala ya kupotoshwa kwa kutopata taarifa sahihi.

- (2) Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwawezesha vijana kwa kuwaweka pamoja. Hivi sasa imezuka kasumba ya kuwaamrisha vijana kama vile wanaweza kupata maisha bora hata bila ya kufanya kazi na kama vile ugumu wa maisha unasababishwa na Serikali yao chini ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri elimu ya ujasiriamali ikatolewa kwa vijana wenu na kuwahamasisha kwa kufanya kazi na wafahamu maisha bora yanakuja kwa kufanya kazi kwa juhudhi na maarifa. Pia pesa zinazotengwa zipelekwe Halmashauri zote ili wimbi la vijana kukimbilia mijini lisiendelee.

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kuititia maandishi nichangie bajeti ya Wizara hii muhimu. Umuhimu wa Wizara hii pamoja na majukumu mengine ni jukumu la kufunda na kuunda rasilimali watu katika utamaduni na maadili mema. Katika kutekeleza jukumu hilo muhimu,

Wizara imepewa kazi ya kuhifadhi na kurithisha utamaduni wetu kwa kizazi hiki na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, ushiriki na msukumo wa Wizara hii katika shughuli za vijana hasa vijijini ni mdogo sana au haupo kabisa. Kweli hii inaweza kutokana na muundo wa Wizara zetu na hofu isiyokuwa na maana ya Wizara au na watendaji kuchelea kuingiliana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara kuongeza jitihada za kuhamasisha na kutekeleza majukumu yake kuititia shule na vyuo vya aina zote. Ni matumaini yangu kuwa shughuli za michezo na maadili mema ya vijana yakisimamiwa kwa nguvu na Wizara zote husika chini ya uongozi wa Wizara hii, kuanzia hatua ya awali tutaweza kupata mafanikio makubwa na kwa haraka. Hili linaweza kutekelezwa kwa mfano, Maofisa wa Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kupanga kwa pamoja na kusimamia shughuli za michezo mashulenii na vijijini. Kuanzisha vituo vya utamaduni hata kama ni chini ya Mwembe ambapo watu maalum watawafunda vijana kwa kulenga maadili mema. Huu ni mkakati wa kujenga vijiwe vyenye maadili mema kwa kuwapa vijana mbadala.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la utamaduni katika malengo mapana ya kujenga maadili mema ya Taifa letu. Kama alivyosema Baba wa Taifa, Mwalimu J. K. Nyerere, "Taifa lisilokuwa na utamaduni ni Taifa mfu na asiyejua atokako hata kule aendako hakujui." Ushauri wangu ni kuwa kwa ngazi angalau ya Tarafa zijengwe hifadhi za mambo ya kale na mambo ya utamaduni. Yapo mambo mengi ya kale ambayo vijana wetu wengi hawajui. Ukienda Mataifa mengine kama China, utashtuka kuwaona Watanzania wakishangaa kuona vitu vya kale vilivyotumika katika nchi hizo ambavyo kimsingi hata kwetu vilikuwepo zama hiso.

Mheshimiwa Spika, wasomi wa historia wanabainisha kuwa miaka 1000 BK, sehemu za Bukoba ziliikuwa mionganoni mwa sehemu chache duniani zilizoweza kufua chuma kwa

ufanisi mkubwa. Nani ajuaye hilo, wapi tunaweza kuona hilo. Hili ni jukumu la Wizara hii kama nilivyoainisha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa ajira zenyetija na zisizolazimisha mtaji mkubwa baada ya kuzianzisha ni michezo. Kijana akifundishwa michezo na shughuli za utamaduni zenyetoko na akamudu na kutambua fursa hiyo, jukumu la Serikali linapungua inabaki mlengwa kujituma na kufaidi. Rai yangu hapa ni Serikali kupitia Wizara hii na nyinginezo kuwekeza zaidi katika kufundisha Walimu na makocha wa michezo na sanaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kupitia michezo kama riadha, soka na sanaa kama nyimbo na ngoma tunaweza kuwawezesha vijana wetu wengi. Pamoja na faida kwa vijana Taifa litapata pato ikiwemo kujenga jina na heshima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. VITA R. M. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza sana Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya kusimamia sekta ya Utamaduni wa Mtanzania, Michezo na Habari.

Mheshimiwa Spika, ni kazi kubwa kulinda utamaduni wetu hasa kwa wakati huu wenye teknolojia ya habari ambayo kila mtu anayo fursa ya kusikia, kuona, kusoma, kuandika kwa uhuru. Hivyo suala hili halina mipaka, lakini linaweza kusimamiwa na kwa kutungiwa sheria za kulinda utamaduni wa Mtanzania, kuheshimu mila na desturi zetu. Lazima tulinde kwa nguvu zetu zote mila na desturi ya Mtanzania. Moja ya changamoto mliyonayo Wizara hii ni kuwa na mkakati tekelevu yaani unaotekelvezeka kusimamia ulinzi wa utamaduni wa Mtanzania ikiwemo lugha yetu ya Kiswahili ambayo ndio imekuwa msingi mkubwa wa usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, leo kukiwa na upotoshaji wowote ambao unataka kuvuruga amani, elimu inatolewa kwa kuelezwaa kwa lugha ya Kiswahili na kueleweka vizuri sana

mpaka vitongojini huko vijiji. Sasa hii ndio lugha inayoeleweka kiraishi kwa Mtanzania, hivyo ushauri wangu lugha ya kiswahili itumike kufundishia shule za sekondari na vyuoni itatusaidia kwa haraka kupata walioelimika kiufasaha. Masomo yao si kwa kuhifadhi kwa ajili ya mtihani, matokeo yake tunapata wasomi ambao mambo mengi hawayajui kiundani.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaweza kutoa maoni yake katika Tume ya Katiba kuwa Katiba mpya ieleze waziwazi kuwa kwa kulinda utamaduni wetu ambapo lugha Kiswahili ni moja ya Utamaduni wetu itumike kufundishia katika sekondari na vyuoni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Sasa nimwite Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Majaliwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru pia kwa kunipa nafasi ili niweze kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu na ili nisje nikasahau, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kwanza, ninataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wake wote wa Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa kazi kubwa wanayoifanya, kutuunganisha Watanzania kuitia shughuli za utamaduni na michezo na hasa kwa vijana na idadi kubwa ya vijana ni hawa ambao bado tuko mashulenii, tunao kwenye shule zetu za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, kuitia programu mbalimbali zilizowekwa na Wizara, tunaweza kufikia malengo ya kuinua vipaji mbalimbali kuitia maeneo haya. Nampongeza pia Mheshimiwa Waziri, kwa ushirikiano mzuri anaoutoa na Wadau kwa maana ya Wizara zingine ambazo pia tunafanya kazi pamoja na hasa kitendo cha Wizara hiyo kuipatia TAMISEMI, Afisa Michezo, Bwana Mohamed Kiganja, kuwa

ndiyo mratibu wa michezo ili kuimarisha Sekta ya Michezo ndani ya TAMISEMI iweze kutoa sura tunayoitarajia.

Mheshimiwa Spika, na hii ndiyo inayotupelekea kuwa michezo ni lazima iendeshwe kitaalamu na iendeshwe na wataalamu waliosomea ili michezo kutoka katika ngazi hii ya chini, iweze kuendeshwa kitaalamu zaidi, tuweze kutoa matunda mazuri na wachezaji ambao pia wameiva kwa utaalamu huo.

Ninataka nianze kuchangia kwa kufafanua hoja kadhaa ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge, zinazogusa Wizara hii, lakini pia zinagusa na Wizara ya TAMISEMI. Moja ni ile ya Mheshimiwa Mturano, alipozungumzia kuwepo kwa kero ya michango mbalimbali ya uendeshaji wa michezo ya shule za msingi na sekondari, ambayo alieleza kwamba wazazi wanapata shida sana. Ninataka nimwambie kuwa, jambo hilo sasa halipo kwa sababu ilipofutwa kwa mara ya mwisho michezo hii, tulipokuja kuirudisha sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tulikuja na mkakati ambao hatuhitaji tena kumbughudhi mzazi kuchangia mchango wowote ule, bali kupitia Halmashauri na mipango yake, lazima itenye fedha kwa ajili ya kuendesha michezo hii.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kuwa, Michezo ya UMITASHUMTA, kwa maana ya Umoja wa Michezo Tanzania kwa SHULE za Msingi pamoja na UMISETA kwa Sekondari imerudishwa na vijana wanashiriki kikamilifu kutoka ngazi ya shule, ngazi ya Kata, Wilaya hadi Taifa. Pia michango hii iliyozungumzwa sasa hivi hatuchangii kwa sababu kule ngazi ya shule, pale wanapata vifaa na kuendesha mashindano ambayo gharama yake siyo kubwa, kwa hiyo, ngazi za shule zenyewe kupitia asilimia 40 ya *capitation* ambayo wanaipata eneo la vifaa, wanaweza kununua mipira mmoja au miwili ya kuendeshea michezo hiyo.

Mheshimiwa Spika, michezo hii inapofikia ngazi ya Wilaya, Halmashauri inaichukua na wanaiendesha ngazi hiyo

mpaka Mkoani na inapokuja ngazi ya Taifa, basi Wizara inagharamia kutoka maeneo yote; vifaa, mavazi, chakula na malazi na vijana wanashiriki. Sasa tuna miaka zaidi ya minne, tunaendelea kuiongoza michezo hiyo na mwezi ujao kuanzia tarehe kumi, tunaanza na michezo ya UMITASHUMTA, ambayo itachezwa Mjini Kibaha na kwa hiyo, niwape mialiko Waheshimiwa Wabunge, mje Kibaha mwone ambavyo vijana wetu wanavyoshiriki kikamilifu kwenye michezo hii. Pia kumekuwa na michango ambayo imetolewa na Wabunge wengine, Mheshimiwa Murtaza Mangungu na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Wote wawili kwa pamoja walizungumzia namna ambavyo tunaweza kuboresha ufundishaji kupitia walimu wake kupata mafunzo mbalimbali. Tumejpanga vizuri kupitia Afisa Michezo ambaye tumeletewa kwa sasa, tumeandaa kozi mbalimbali za walimu, lakini pia TAMISEMI sasa inashirikiana na *association* zote za michezo nchini; *TFF, Basket Ball Association* na *Athletic Association* ili kupata utaalam wa karibu, *specific* kwenye michezo yenye na kuendesha *courses* kwa walimu wetu wa shule za msingi na sekondari ili wapate taaluma hiyo, waanze kuwafundisha watoto kutoka kwenye *ground* wakiwa na utaalam wa kucheza michezo hiyo.

Hivi karibuni tutakuwa na kozi za walimu wa michezo kwenye Chuo chetu cha TAMISEMI pale Hombolo. Chuo ambacho kina Viwanja nya Kimataifa vizuri na Waheshimiwa Wabunge, mlipoenda mmeona viwanja vile vinakidhi viwango. Tumeamua sasa kukitumia Chuo kile kuendeshea kozi za michezo mbalimbali. Sasa hivi *TFF* tumeshirikiana na TAMISEMI, tutaendesha kozi kuanzia tarehe 8 mpaka tarehe 13 Julai ya *Grass Root Level Grade One* ya walimu 35 wa *primary* na *secondary*, ambao wamechukuliwa nchi nzima. Kama haitoshi, tutakuwa na *Grass Root Level Two* ambayo itaendesha Julai hiyo hiyo, baada ya tarehe 13, kwa walimu 274 wanaotoka katika shule zote nchini, ambao watakuja Hombolo kuhudhuria kozi za michezo. Lengo letu ni kuimarisha michezo kwa ngazi ya msingi kutoka kule chini na

kazi hii inafanywa pia kwa ushirikiano na Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru pia kuwaambia kuwa, michezo hatuishii hapo tu, nayo pia tunaifundisha kutoka ngazi ya shule za msingi. Ninataka kutumia nafasi hii pia kulishukuru Shirika la Misaada la Michezo kutoka nchini Finland, ambalo sasa tumeweka makubaliano TAMISEMI kutuendeshea shughuli za mafunzo kwa walimu wetu, tayari walimu wa shule za msingi na sekondari 388 wamepata mafunzo nchi nzima na wamekwishamaliza mwezi wa kumi mwaka jana. Ajira hii mpya, walimu wale wamepangwa kwenye shule na hivi juzi tulikuwa tunawasambaza kwenye shule za sekondari 56 nchini, ambazo tumezichukua kama *model* kwenye Halmashauri zetu ziweze kufundisha somo la *physical education, sports and culture* kwenye shule hizo ili pia kwa vijana wa msingi waweze kupata msingi mzuri. Kwa wale wa sekondari, somo hili pia linasomwa na linafanyiwa mitihani kwenye mitihani yao ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaendelea kufundisha michezo hii kutoka ngazi ya msingi, sekondari na hata vyuo vikuu sasa nako kuna kozi za *physical education*, ambazo zinasomwa pale. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, juu ya walimu tunawaandalia utaratibu gani wa kuwapa mafunzo, tumeanza pia kuwapa mafunzo kwa eneo hilo. Pia siyo hilo tu, hata kwa michezo mmoja mmoja, walimu hawa tunawapeleka kwenye kozi mbalimbali kupitia Afisa Michezo wetu aliyepo pale TAMISEMI, anasimamia uendeshaji wa kozi hizi katika Wilaya zetu kwa walimu wetu ili tuzalishe wachezaji ambao tunataka watakapokwenda kwenye ngazi ya Taifa, vijana hawa waoneshe kipaji cha uchezaji wa michezo hiyo kama tunavyokusudia.

Mheshimiwa Spika, katika hili, ninataka nitoe wito kwa *association* zote za michezo, kuhudhuria mashindano haya ya Kitaifa, lakini pia kutoka ngazi ya Wilaya kuona vijana na vipaji vyao ili vijana wale waanze kuwa *monitored*, waweze kuchangia kuwa wachezaji katika ngazi ya kitaifa. Hasa kwenye eneo la ajira ambalo tumelizungumza sana, eneo la

michezo litatoa ajira ya kutosha sana, leo hii tunaona Kaseja anakataa milioni 300 kutoka Yanga ili aweze kwenda kucheza kule, kwa sababu ni ajira nzuri. Kwa hiyo, sasa tunasisitiza kuwa wachezaji hawa tuwajenge wapate ajira, waweze pia kuweza kupata ajira zao huko baadaye.

SPIKA: Nimekuongezea dakika tano zingine.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Mikidadi, jana alizungumzia juu ya mipira iliyokuwa bandarini; ni kweli tuna mipira 5,328 iliyokuwa bandarini ambayo itatumika na shule za msingi nchini kwa Mikoa ya Lindi na Singida. Huu ni mtiririko wa misaada inayotolewa na Shirika la Michezo la Finland kwa ushirikiano na *AMA Sport*, yenye matawi yake Tanzania, ambako tume-sign mikataba kama nilivyoeleza awali ya kuendesha shughuli za michezo nchini.

Wiki iliyopita tumepokea vifaa vya thamani ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuendesha michezo mbalimbali nchini kwenye shule zetu za msingi na sasa Shirika hili pia limeleta mipira 5,600 lakini katika jitihada ya kutoa mipira hii tayari tumewasiliana na Waizri wa Fedha. Tumeomba ili kupitia vyombo vyake, *TRA* na maeneo mengine, waweze kutoa mipira ile iende kwenye mashule iweze kusaidia kufundishia walimu wetu waweze kusaidia kufundisha michezo katika mashule.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuwahakikisha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba, Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo pamoja na TAMISEMI, tunaendelea kupata ushirikiano mzuri na Wizara hii ili kuendesha michezo kwenye maeneo haya. Suala la bajeti lilzungumzwa na Mheshimiwa Obama, ni kweli na hili tunalipokea, kwa sasa tunatumia bajeti hizo. Tumewasisitiza Wakurugenzi waandae bajeti ili waweze kusimamia michezo kupitia mashule. Jambo hili pia linaweza kuzungumza na Mheshimiwa Waziri, namna ambavyo wanaweza kushusha bajeti kupitia Halmashauri zetu.

Suala la pili, ulizungumzia upatikanaji wa Maafisa Michezo katika Halmashauri. Tulipata kibali kutoka Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili kuwa na Maafisa Michezo katika Halmashauri zote, waweze kusimamia shughuli zote za michezo mashulenzi, lakini pia hata kwa vijana wetu ili tupate usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Spika, tayari Halmashauri tumeelekeza na kwa kuwa tuna walimu wengi wamehudhuria kozi za michezo na wana uwezo wa kuongoza michezo, Halmashauri zimeanza kutekeleza kwa kupata walimu mmoja mmoja katika Halmashauri ili wakae pale ofisini kwa ajili ya kuratibu shughuli za michezo tu. Huo ndiyo utaratibu ambao tumeanza nao, tunayo matumaini sasa Halmashauri zetu zitaendesha shughuli za michezo na walimu ambao wako katika maeneo yale na wana utaalamu wa kutosha kwenye eneo hilli. Msisitizo ambao tumeweka ni kwamba, kwenye michezo yetu hii ambayo tunayo, wasindikizaji wa timu zile sasa tutakuwa ni walimu wenyewe wa michezo ambao wamebobeaa kwenye maeneo hayo ili kulinda *discipline* ya watoto hawa mpaka wanapofikia hatua ya Kitaifa.

Mimi niendelee kuishukuru Wizara hii kwa ushirikiano mzuri ambao mnautoa na tuendelee kushirikiana na tutaaendelea pia kuboresha michezo, pamoja na TAMISEMI ambao ndiyo sasa tuna watoto wadogo wa msingi na sekondari. Kwa kusema hayo, nimeona nimalizie hapo, lakini ninataka kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa, Chuo cha Kibaha ambacho kipo chini ya TAMISEMI na Hombolo ambacho pia ni TAMISEMI, tumekiweka wazi kwa Wananchi wote, Taasisi zote za kimichezo, kuvitumia vyuo vile vyenye *facility* za kimichezo za Kimataifa kuweza kuendeshea michezo mbalimbali, ambayo sasa na sisi tumeanza kuendelea na michezo hii. Mwaka huu tutakuwa Kibaha na mwakani tunafikiria kuandaa utaratibu wa kuhamia Hombolo ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge, mwezi huu wa Juni kwenda kuangalia michezo ya shule za msingi na sekondari, itakapoendeshwa kwenye Chuo chetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wale wote ambao waliomba kuchangia na walikuwemo humu ndani, wamepata nafasi, lakini sasa nitatoa muda huu kusudi Waziri na Naibu wake, wakajipange vizuri, tukiingia mchana waanze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, mlipo muwahi kufika, kwa sababu hapa ataanza kujibu, kwa hiyo, akianza kujibu ninyi hampo siyo mnaanza mshahara wa Waziri kumbe alishasema. Mshahara wa Waziri siku hizi kwa mujibu wa Kanuni, hauchukui watu wengi, kwa hiyo, nawaombeni muwahi kuja, kwa sababu ataanza kujibu.

Baada ya kusema hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka hapo saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.44 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha asubuhi tulikuwa tumemaliza Wabunge wote walioomba kuchangia. Sasa tunaingia kwa Mawaziri wanaojibu hoja zao, tunaanza na Naibu Waziri, dakika 20.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA

MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii, kuchangia Hotuba yetu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Kwa kuanza tu, naunga mkono hoja.

La pili, napenda kutambua michango mbalimbali ya Wabunge, iliyotolewa kuanzia jana mpaka leo na mapendekezo ya Kamati. Nataka niwahakikishie kwamba, ushauri wao na maelekezo yote yaliyotolewa na Kamati, Wizara yetu itayazingatia yote na yale ambayo tuna majibu nayo sasa tutayatoa na kwa yale ambayo kwa bahati mbaya kama muda hautaruhusu, kwangu mimi na kwa Waziri kama

tutashindwa kuyatoa, tutayatoa kwa maandishi kwa kila Wabunge waliochangia.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, naungana na Wabunge wote, naungana na Azimio la Bunge la kututaka sisi Wabunge wote na pia Waandishi wa Habari, kama ambavyo michango imetolewa, kuhakikisha kwamba, nchi yetu inakuwa na amani na utulivu hapa nchini. Itikadi zetu za Vyama ni zaidi ya Tanzania na amani tuliyonayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mambo mbalimbali yameongelewa, lakini nataka niseme kwamba, yapo mambo ambayo ni ya kijinai yanahitaji uchunguzi, basi tuviachie vyombo vinavyohusika ikiwemo Mahakama na vile vinavyochunguza na huo ndiyo Utawala Bora. Serikali ya CCM imeendelea kuchaguliwa madarakani kutohana na kuhestimu Utawala wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, pili, katika kusisitiza amani na utulivu ni kwamba, fitina, ulaghai na hadaa ndiyo ambazo zinaweza zikahatarisha amani na kwamba, iwe katika kupotosha habari, iwe kwetu sisi wenyewe wanasiasa, ni katika kutengeneza fitina ambazo zinaweza kusambaratisha Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nataka niwape hadithi moja ambayo nilisimuliwa na Sheikh mmoja wa Wilaya yangu kule, alisema kwamba; ogopa sana mtu mwenye fitina. Kuna mtu mmoja alikuwa anamwuuza mtumwa wake, lakini wakati anamwuuza yule mtumwa akasema, mtumwa ninayemwuza ana kasoro moja ni mtu fitina. Kwa hiyo, alipofika kwa mfalme, yule mama akaambiwa huyu mtumwa ninayemwuza ni fitina hakuamini, yule mwanamke akashinikiza kwamba, yule mtumwa anunuliwe. Basi baada ya shinikizo la mwanamke, mtumwa alinunuliwa na mtumwa yule alianza kazi yake ya fitina katika nyumba ile ambayo waliishi kwa amani na utulivu.

Siku ya kwanza, akamwambia mwanamke yule kwamba, wewe baba hakupendi; yule mama akajiuliza kwa nini baba hanipendi, akamwambia tutafute dawa, lakini dawa iwe ni kukata ndevu zake yule mzee wetu. Baada ya kukamilisha hiyo kazi, alienda tena kwa baba akamwambia baba, mama anataka kukuua. Kwa hiyo, akamwambia baba leo ukae vizuri kwa sababu mama atakuja usiku kukuua atakuwa na kisu usilale.

Muda ulipofika, akamwambia yule mwanamke sasa nenda baba amekwishalala, tahamaki anakwenda na kisu kutaka kutoa zile ndevu kama dawa, baba akamwonia akamchoma kisu pale pale akafa. Kwa sababu kazi ya mtu fitina ilishakamilika. Baada ya pale, wale ndugu wa mwanamke hawakukubali wakaja wakamwuua baba mtu na wale ndugu tena wakaanza kuuana, hatimaye familia na jamii. Kwa hiyo, tuogope sana watu fitina, wenye hotuba za kuchochea kuligawa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niwahikikishie kwamba, Serikali na sisi kama Wizara ya Habari, tunafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Magazeti yote yaliyofungiwa, yamefungiwa kwa kukiuka Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976 kwamba; mengine yamekuwa yakichochea na kuhtarisha usalama, lakini pia watu wamehoji mamlaka gani ambayo yamempa Waziri kufungia gazeti. Sheria hiyo ya mwaka 1976, Kifungu cha 3(25)(1), kinampa mamlaka Waziri kufungia gazeti lolote anapoona linachochea au kuhtarisha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, niwatake sana kwamba, Serikali imeshakamilisha mchakato na sasa siyo mchakato tu ambao wengi mmechangia kwamba ilikuwa danadana, tayari Baraza la Mawaziri limesharidhia na muda wowote tukitakiwa tutawasilisha Muswada huo hapa Bungeni ili tutengeneze sheria ambayo itatuhakikishia kwamba, tunapata habari safi, maslahi ya Waandishi wa Habari, lakini pia kuona Waandishi wa Habari wanazingatia weledi wao wa kuandika habari.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Mwenge. Tumebezwा sana juu ya Mwenge. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Obama, amechangia vizuri sana kuhusu manufaa ya Mwenge, sina haja ya kuyarudia. Nataka niseme kwamba, Serikali inayoongozwa na CCM, haijawahi kufikiria na haitothubutu kufikiria kuweka Mwenge katika makumbusho bali Mwenge huu utakimbizwa nchi nzima, mwaka hadi mwaka. Narudia tena, Serikali ya CCM haijawahi kuwaza wala kuthubutu tena kuwaza jambo hilo na kwamba, Mwenge utaendelea kukimbizwa, kwa sababu unachangia shughuli za maendeleo, miradi mbalimbali ya maendeleo. Watu wengine wanaangalia tu *quantitative factor*; kwa nini usifikirie pia *qualitative factor*, kwa sababu ule unatupa umoja, kufahamiana na mshikamano kwa Watanzania wote? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, huwezi kwenda kuuliza kengele ya kanisani inanunuliwa shilingi ngapi kwamba milioni mbili halafu ukataka sadaka ndiyo zirudishe gharama ya kengele ile. Zipo sababu zingine za watu kukusanyika na kumwabudu Mwenyezi Mungu, iwe ni spika katika misikiti, huwezi ukauliza gharama hizo na Mwenge nao ni hivyo hivyo kwamba umoja wetu na mshikamano wa Watanzania, huwezi ukauweka katika gharama ya aina yoyote ile. Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba, jambo hili ni la msingi.

Mheshimiwa Spika, Kiongozi mmoja wa China aliwahi kusema, ukiona adui yako anakushabikia jambo fulani, jambo hilo liache ni baya, lakini ukiona adui yako analifurahia jambo unalolifanya, jambo hilo ni baya, lakini ukiona anakukataza jambo hilo lifanye sana. CCM na Serikali yake itaendelea kufanya jambo hili kwa sababu ni jema kwa Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la Baraza la Vijana, ni kweli kwamba Baraza la Vijana limechukua muda mrefu sana, lakini yote haya ilikuwa tu ni kutoa nafasi kwa wadau, vijana washiriki katika mchakato huu. Nataka niseme kwamba, mimi mwenyewe ni mdau mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, humu Bungeni Mheshimiwa Mnyika atakuwa anakumbuka kwamba, mimi Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Lusinde, Mheshimiwa Erasto Tumbo na Mheshimiwa Kitilya Mkumbo, kabla hajaenda CHADEMA ndiyo tulikuwa waasisi wa kutengeneza hili Baraza la Vijana la Taifa. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Vijana wote nchini, wasikubali mashinikizo kwamba watashurutishwa ili kuunda Baraza la Vijana, Baraza la Vijana mimi mwenyewe ni mdau na nimeshapewa dhamana, tutasaidiana na Waziri kuona Baraza la Vijana linaundwa na tutawasilisha Muswada hapa wa kuunda Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo yetu ya michezo; wapo watu waliobeza sana ushiriki wetu wa *Olympic* mwaka jana. Nataka kusema kwamba, michezo hii kuna kushinda na kushindwa, lakini hamuwezi kwenda tu hivi msiambulie kitu chochote, tumejifunza mengi. Kwa sababu kwanza michezo hii safari hii ilioneshwa vizuri, tumeypata uelewa kumbe kuna michezo mingi ambayo Watanzania watapata fursa ya kuweza kushiriki michezo hii itakapofanyika baadaye tena. Tanzania siyo kichwa cha Mwendawazimu kama inavyosemwa tena, katika nchi 205 Duniani zilizoshiriki, zilizopata medali ni nchi 79 tu. Kwa Afrika nchi 50 zilizopata medali ni nchi kumi tu. Kwa hiyo, hata nchi za Ulaya, Amerika na Asia zilizokosa medali ni 86, lakini si kwamba hawa watu hawatashiriki tena, wamejifunza wameona changamoto na watarudi tena kujifunza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutumie fursa hii kuwashakikishia kwamba, tutajitahidi sana kuhakikisha kwa kushirikiana na Baraza la Michezo na Vyama vy'a Michezo vyote, kuona kwamba tunaibua vipaji na tunapata maandalizi ya kutosha ili tukishiriki safari nyingine tuweze kupata medali. Tuepuke kauli ambazo zinaweza zikawakatisha tamaa wanamichezo wetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuweka sawa suala la Tanzania kushiriki katika Kombe la Dunia, maana nimesikia michango mingine inasema tumebakiza mechili mbili tu

tunakwenda Brazil; siyo kweli, bado tuna mechitatu, tarehe 8 mwezi wa sita tutakwenda Morocco tucheze nao, tarehe 16 mwezi wa sita Ivory Coast watakuja Dar es Salaam tutacheza nao, Tarehe 6 mwezi wa tisa tutakwenda Gambia kucheza nao. Tukishinda michezo hii zitatafutwa timu kumi katika Afrika kutakuwa na mtoano zipatikane timu tano kwenda Brazil. Kwa hiyo, Serikali kwa kuelewa umuhimu huu, imeunda Kamati ya kuhamasisha *Taifa Star*, waitafutie fedha na kuangalia namna gani inaweza kushiriki na kushinda mashindano haya.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwahamasisha sana na nawashukuru Wabunge ambao wameendelea kuipongeza *Taifa Star*, lakini pia tunayo kazi na tutajitahidi kuona timu yetu inafanya vizuri. Serikali pia haitaendelea kusema tu itasimamia michezo wa mpira wa miguu, tutaendelea kuimarisha na michezo mingine yote ili kuona kwamba, Tanzania tunapata nafasi katika Dunia kushiriki michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, Serikali hii haina mchango wowote katika kuendeleza *TFF*, mimi nataka niseme siyo kweli. Ningemwomba sana rafiki yangu mpendwa Mheshimiwa Mangungu, *ange-declare interest*, ye ye ni Mjumbe wa Kamati ya Rufaa ya *TFF*, kwa hiyo, kuwasemea *TFF* angesema na mimi nimo mle.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Serikali haina mchango, kwanza *TFF* hawana viwanja, kwa hiyo, viwanja wanashirikiana na Serikali kikiwemo kiwanja kikubwa cha Taifa ambacho ni miundombinu, ambacho timu zote za kimataifa zinautumia zikija ni mchango wa Serikali. Pia na maeneo mengine, viwanja ambavyo vinaendeshwa na wadau mbalimbali ikiwemo Chama cha Mapinduzi na Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia huwezi ukapuuza suala la kulipwa kwa makocha kwamba hakuna mchango wowote. Mimi naaminikabisa kwamba, Serikali ina mchango, lakini pia huwezi kupuuza suala la mashindano mbalimbali

ya Kimataifa, mashindano kama yale ya *All African Games*, *Twiga Star* walienda Msumbiji, Serikali imelipa tiketi, malazi, vifaa na kila kitu kwa *Twiga Star*, kwa hiyo, huwezi kusema kwamba Serikali haijachangia kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuweka sawa hilo kwamba, Serikali muda wowote itaendelea kushirikiana na *TFF* na Sekta Binafsi kuona kwamba, michezo hapa nchini inapiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ilikuwa ni kuhusu mapato ya Uwanja wa Taifa. Kwanza, nataka niseme kwamba, Serikali hii ni sikiu sana, mara ya kwanza uwanja ule unaanza, Serikali ilikuwa inachukua asilimia 20 ya mapato, baadaye ikawa asilimia kumi, lakini katika hayo yapo masuala ya umeme, masuala ya Wachina, masuala ya maandalizi ya uwanja, lakini kwa kusikia kilio cha wadau wa soka, tukakaa vikao na vilabu vyote. Hatimaye kabla ya ligi kuanza mzunguko wa pili, tukakubaliana kwa ridhaa kwamba iwe asilimia 15 na Serikali sasa isitoze masuala ya Wachina wala maandalizi ya uwanja na ndivyo ilivyotokea na vilabu vilipongeza sana. Nataka kusema kwamba, ipo changamoto ya kuona kwamba, tunaendelea kupiga hatua zaidi katika yale ambayo yanaendelea kulalamikiwa, lengo letu ni kuona kwamba vilabu navyo vinaweza kufaidika.

Mheshimiwa Spika, lakini ipo tafsiri, nilikuja hapa tukatoa taarifa ya mapato ya Uwanja wa Taifa, ikaonekana ni fedha ndogo, ndiyo, lakini ni ule uelewa kwamba, tulikuwa tunamaanisha nini. Tulichomaanisha ni zile hela zinazokwenda Serikalini. Kwa mfano, milioni mia tano zilizopatikana juzi, yale ni mapato kwa ujumla wake, lakini Serikali kwa asilimia 15 ilipata milioni 63. Kwa hiyo, hapo itagharamia umeme, maji, Wachina na kila kitu. Fedha hizi zingine yapo makato, wamepewa mgawo vilabu, ipo VAT, Kamati ya Ligi, DRFA, gharama za mechi, gharama za tiketi, hayo yote hayahusiani na Serikali. Serikali inachukua asilimia 15 tu.

Mimi ninaamini kabisa, ipo hatua lazima twende mbele na taasisi zingine ikiwemo *TFF* na wengine, tukae

pamoja kuona Serikali imetekeleza wajibu wake na wenyewe waanze kuona ni namna gani wanawenza wakavisaidia vilabu badala ya kuendelea kuwa na makato hayo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naelewa kwamba, lipo tatizo la kudhibiti mapato ikiwemo mambo ya tiketi. Ninayo furaha kuwafahamisha kwamba, tayari maandalizi ya kuanza kutumika tiketi za kielektroniki yamekamilika na kwa kuwa ligi imeisha, sasa hivi tunaandaa mechi za majaribio. Kwa hiyo, unakata tiketi ya kielektroniki, lakini kutakuwa na vizuizi nya ku-sense ile tiketi. Naamini kabisa, hatua hiyo itaisaidia sana Serikali kuweza kudhibiti mapato ya Uwanja wa Taifa. Maandalizi hayo yameshakamilika, kwa hiyo, tutataka kuwa na majaribio katika mechi za majaribio. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nigosie suala la Sera ya Michezo, alilisema Mheshimiwa Iddi Azzan. Nataka niseme kwamba, jamani mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Tumejitahidi katika mwaka mmoja kuhakikisha tunashinikiza, tumeifanya hii kazi, Sera ya Michezo haijatajwa kwa miaka yote ya nyuma lakini safari hii ipo katika ngazi ya juu kabisa ya maamuzi na hatimaye ikikamilika, tunaahidi tutaileta Bungeni. Naomba tuwe na imani hiyo, haya tutayafanya kwa nia njema tu kuona kwamba, tunakuwa na Sera inayoendana na wakati, lakini pia ni Sera ambayo itazaa Sheria za Michezo zinazoendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, nigosie pia suala la wizi wa kazi za wasanii, tuliambiwa kwamba, inawezekana ilikuwa ni nguvu ya soda, Serikali inataku kuhakikisha suala la wizi wa kazi za wasanii tutaendelea kushirikiana na wasanii kote nchini, kuhakikisha kwamba kazi za wasanii haziibiwi na wale wote watakaofanya jambo hili, hatua kali za kisheria zitachukuliwa. Baada ya Bunge lile, tumefanya operesheni Mwanza, Msama alifanya kazi kubwa, tulimpa ushirikiano kama Serikali na vyombo nya ulinzi, lakini pia *TAFU* wamefanya kazi kubwa sana, akina Mwakifamba nimewapa ushirikiano na Wizara imewapa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumefanya Mkutano wa pamoa na wasanii wa vikundi vyote kutueleza matatizo yao na tumeelewa na hatimaye kuna mambo mengi tumeyaboresha hata katika urasimishaji wa kazi za wasanii. Nataka niseme tu ni hatua moja kubwa tumeipata hiyo. Tuachieni haya mengine tutaendelea kuyashughulikia kadiri tunavyoendelea. Pia zoezi hili la urasimishaji hizi kazi za wasanii, malengo yake hasa si kwamba Serikali ipate tu mapato. Lengo la kwanza ni kuhakikisha kwamba, tunalinda kazi za wasanii. Hili la mapato siyo kwamba, tumekusudia sana kwamba ndio hilo, lengo letu ni kuhakikisha wasanii wetu wanapata mapato na haki na Serikali itaendelea kulisimamia jambo hilo. (*Makof!*)

Sasa kuna michango mbalimbali hapa ya Waheshimiwa Wabunge wengine. Hili la Mheshimiwa Juma Nkamia amelisema, la makato nimeshaliongelea na suala la kodi ya makocha. Ni kweli, lilikuwepo tatizo mara ya kwanza la makocha wetu kuanzia Maximo, akaja mwingine na huyu wa sasa. Tumeshakaa kati ya Uongozi wa *TFF* na Serikali na *TRA*, kuona kwamba yale malimbikizo Serikali inayashughulikia na jambo hili halitajirudia tena, kwa sababu tumeshaelewa tatizo lilikuwa wapi. Kwa hiyo, ninawaahidi tu kuwa jambo hili halitaweza kujirudia.

Ipo michango ya kwamba, *TFF* washirikiane na *ZFA* ya Zanzibar na suala lile la kocha kutokwenda Zanzibar anaangalia *Vodacom* hii ligi ya huku. Matokeo yake anapata wachezaji ambao ni Wazanzibari, lakini wanacheza wanaocheza huku. Hili tumelipokea na tutawaelekeza *TFF* kufanya hivyo; kwamba, kocha afike kule Zanzibar, awaone wachezaji, awateue. Pia na hili la mashirikiano kati ya *TFF* na *ZFA* nalo tunawaelekeza *TFF* kuchukua hatua za haraka sana. (*Makof!*)

Kulikuwa na suala ambalo lilisemwa na hasa Mheshimiwa Paresso na wengine walisema kwa nini Serikali inaendelea kutegemea makocha wa kigeni na haina mpango wowote wa kuzalisha makocha hapa nchini. Mimi nataka niseme tu kwamba, hali ya michezo inabadilika,

twende na wakati. Nchi nyingi tu zinatumia makocha wa nje, lakini pia makocha wa nje hao wanawafundisha. Wanapokuwa hapa lazima wanakuwa na wasaidizi wazawa wa hapa. Mimi nataka niseme tu kwamba, tutaendelea kuwatumia makocha wa nje na wa ndani. Pia siyo kwamba, Serikali imekaa tu. Tayari Serikali kupitia Chuo cha Malya tunazalisha makocha wazuri sana. Wanakwenda katika Halmashauri zetu. Wanakuwa walimu katika michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele yenu siku hii ya leo. Pili, napenda nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa dhati kwa kuongoza kwa umakini mkubwa majadiliano ya Hotuba ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Napenda pia kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Wajumbe wa Kamati hii, kwa michango yao makini ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu na asasi zake. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa maoni na mapendeleko aliyotoa katika kufanikisha utekelezaji na majukumu ya Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia ama kwa kuongea au kwa maandishi. Michango yao imewezesha kwa kiasi kikubwa, Wizara yangu kutambua maeneo ambayo kama Wizara tumefanikiwa na yale ambayo bado tunahitaji kuyafanya kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, katika mjadala huu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 102 walipata fursa ya kuchangia. Kati yao; Waheshimiwa Wabunge 33 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja na Waheshimiwa Wabunge 69 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizi kwa wachangiajai, naomba sasa nianze kujibu na kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Nitaanza kwa kujibu hoja chache kwa ujumla wake, halafu nitajikita katika hoja mbalimbali kama muda utakavyoniruhusu. Kwa yale ambayo sitaweza kuya-cover, basi ninaahidi kwamba, tutayafanya kazi bila kusita.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu maadili ya vyombo vya habari. Kwanza, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia kuwaombea Waandishi wa Habari mbalimbali ambao wamepoteza maisha yao katika nafasi zao za kazi. Pia wale wachache ambao wameumizwa wakiwa katika kazi zao. Tumwombe Mwenyezi Mungu, awasadie waweze kupona haraka waweze kurudi katika utekelezaji wa kazi zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika hii hoja ya maadili ya vyombo vya habari, michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi imezungumzia suala la maadili ya vyombo vya habari. Suala hili pia limegusiwa sana na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Ningependa nilitolee ufanuzi kwa maelezo mafupi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuwapongeza kwa dhati Waandishi wote wa vyombo vya habari hapa nchini, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha jamii yetu. Nataka niliseme vizuri kwamba, Serikali inathamini sana mchango wao katika

maendeleo ya nchi yetu. Aidha, Serikali itaendelea kuwajengea mazingira mazuri, yatakayowawezesha kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na tija. Ni kwa sababu hiyo, tunaleta Sheria yetu hii ya Vyombo vy'a Habari mwaka huu, itakayotuwezesha kusimamia vyombo vy'a habari na kuhakikisha maadili ya masuala ya habari pamoja na vyombo vy'a habari inafuatwa.

Mheshimiwa Spika, uandishi wa habari popote duniani ni taaluma. Ina msingi yake na maadili yake. Moja ya maadili muhimu ya taaluma hii ni kuandika na kutangaza habari zenye ukweli na uhakika. Hivyo, magazeti na vyombo vy'a utangazaji ikiwemo redio na *television*, vyote vinawajibika kuandika na kutangaza habari za ukweli, uhakika na siyo habari za uwongo, uzushi na uchochezi. (*Makofii*)

Kwa msingi huo basi, siyo kila habari ni habari na katika hili namshukuru sana Mbunge Kijana, Mheshimiwa Ester Bulaya, alioneshaa wazi si kila habari ni habari. Nimekuwa narudia hii kila mara, si kila habari ni habari. Hata *definition* ya habari inasema wazi, habari ni taarifa zilizochambuliwa kwa maana ya *processed data*. Ina maana kabla hujachambua habari yako mwanahabari, chombo cha habari huna haki ya kutangaza hiyo habari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa chombo cha habari kinachoandika au kutangaza habari za uongo kwa kusudi au kukusudia kwenda kinyume cha maadili ya taaluma ya habari, kwa kufanya hivyo kinaipotosha jamii na madhara yake kwa jamii ni makubwa sana. Tunafahamu mara nyingi waandishi wa habari wanazungumza, wanafanya vitu vizuri, wao ndiyo wenye kuhabarisha jamii, lakini pia ndiyo wao wenye kubeba jukumu kwa jamii kwa kuweza kuwaelimisha. Sasa ni muhimu waelimishe vizuri na maadili mengine katika masuala ya habari ni pamoja na kutoonesha picha zinazodhalilisha utu wa mtu, kutokuonesha picha za maiti au watu waliojeruhiwa vibaya sana na picha za watoto walio chini ya umri usioruhusu kisheria.

Mheshimiwa Spika, nadhani haya tumekuwa tunayaona, ndiyo maana tunalalamikia kuhusu kuperomoka kwa maadili ya vyombo vyahabari. Aidha, katika kutekeleza wajibu wao, waandishi wa habari pia wanatakiwa kuzingatia uzalendo. Kila wakati wanatakiwa kupima ni kwa kiasi gani kile wanachokiandika na kikitangaza, kinahatarisha usalama na amani ya nchi yao. Jambo hili la waandishi wa habari kuzingatia uzalendo linafanyika katika nchi zote duniani, zikiwemo zilizoendelea kama Marekani na Uingereza na nimezitaja hizi, kwa sababu wengi tikitangaza mifano yetu, tunajipima katika Marekani na Uingereza.

Mheshimiwa Spika, Iakini kwa kiasi kikubwa pia tunasahau, sijui hao Marekani na Uingereza walipokuwa na miaka 50 ya kwao ya Uhuru walikuwa katika *level/gani*. Kwa hiyo ni kiasi kikubwa kabisa kuweza kujipima tuangalie au huu uhuru ambao tunauruhusu sasa sisi *enabling environment* tumeshaiweka. Kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii nieleze kwamba, aidha, katika utekelezaji wa wajibu wao, waandishi wa habari pia wanatakiwa kuzingatia huo uzalendo. Pia wanatakiwa kuhakikisha kwamba, wanatoa zile habari za ukweli na uhakika. Hivyo, Serikali inawatarajia waandishi wa habari wote hapa nchini, kuzingatia uzalendo wakati wote wanapotekeliza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, hatuwatarajii wajihushe na kutangaza habari za uchochezi, zinazohatarisha usalama wa nchi yetu, kwa kisingizio chochote kile ikiwemo kisingizio cha uhuru wa habari. Hakuna uhuru usiyo na mipaka. Aidha, hakuna uhuru wa habari wa kuibomoa nchi. Katiba yetu ya nchi iko wazi katika suala la uhuru na haki ya habari na tuzingatie hilo. Suala hili la maadili litazingatiwa zaidi kwenye Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vyahabari itakapowasilishwa hapa Bungeni baadaye mwaka huu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuomba tu uongozi na waandishi kwa ujumla, kushiriki katika mijadala ya kujenga taifa na jamii kwa ujumla. Vyombo vyahabari vilivyo kinyume kabisa na Serikali yetu, siyo kipaumbele chetu

sisi kama Serikali. Serikali iliyopo madarakani ina vipaumbele vyake. Serikali itaendelea kusimamia vyombo vy ya habari, kuwatendea haki Wananchi kwa kuhimiza na kuwashirikisha katika mijadala na shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyngine ambayo imejitokeza kwa kiasi kikubwa ni kuhusu ufinyu wa bajeti ya Wizara. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia hili. Nataka nichukue nafasi hii niwashukuru kwa maoni na ushauri wao. Naishukuru kipekee, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mheshimiwa Jenista Mhagama. Napenda kuihakikishia Kamati kuwa, ushauri na maelekezo yake tutayazingatia na kuyafanya kazi. Niseme tu kwamba, Wizara itaendelea kutumia vizuri fursa zilizopo katika kufanikisha utekelezaji na majukumu yake. Katika hili, tutazidi kushirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali zikiwemo asasi za kiserikali, za kibenki, washirika wa maendeleo na sekta binafsi. Aidha, tutaimarisha zaidi moyo wa kujitolea mionganoni mwa vijana ili yale yanayoweza kutekelezeka bila kuhitaji fedha, yaweze kufanyika kwa faida ya vijana wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hoja nyngine ambayo imejitokeza ni mchango kuhusu *TBC*. Idadi kubwa wamezungumzia umuhimu wa kuimarisha Shirika letu la Utangazaji *TBC* ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Tunawashukuru wote na tunaahidi kutekeleza ushauri mliotupatia. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kuchukua hatua za makusudi za kuimarisha *TBC* ili matangazo yake yaweze kuwafikia Wananchi katika pembe zote za nchi yetu. Kwanza, tutahakikisha kuwa, *TBC* inajengewa uwezo wa kuandaa vipindi vingi, vizuri, vinavyoelezea jitihada za Wananchi wetu kujilettea maendeleo. Hili litaihusisha kuipatia *TBC* vitendea kazi vya kisasa na kuwapatia watumishi wake ujuzi zaidi na kutengeneza vipindi vinavyovutia watangazaji na wasikilizaji. Tutaendelea pia kujenga mazingira mazuri, yatakayoiwezesha *TBC* kuvutia watangazaji wengi zaidi na hivyo kuiongezea mapato. Wizara itaendelea kushawishi washiriki wetu wa maendeleo wakiwemo Mashirika ya

Kimataifa kama vile UNESCO, kuisaidia TBC katika jitihada zake za kuimarisha kama chombo cha utangazaji wa umma.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine kubwa ambayo imejitokeza ni ya ukosefu wa ajira kwa vijana. Katika Bunge la Bajeti lililopita, hoja hii ya ukosefu wa ajira kwa vijana na mikakati gani Wizara imejipanga kuweza kutekeleza na kutatua tatizo hili ilijitokeza na kwa kiasi kikubwa nilielezea kwa kirefu mikakati mtambuka mbalimbali inayotekelawa na Wizara yangu, lakini pia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutatua changamoto hii inayowakabili vijana wetu. Suala hili limejitokeza tena jana na leo, kwa mitazamo, hisia na ushauri mbalimbali wakati Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wakichangia bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, suala la ukuzaji wa ajira nchini siyo suala la sekta moja bali ni la sekta zote. Kila Wizara, Idara ya Serikali, Wakala na Sekta Binafsi kwa ujumla, zina wajibu wa kupanua fursa za ajira kwa Wananchi wetu hususan vijana katika mipango na mikakati inayojiwekea.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo la ajira kwa vijana ni kero kubwa siyo tu kwa vijana wetu hapa nchini, lakini pia duniani. Ukosefu wa ajira kufikia mwezi Machi, 2013 ilikuwa asilimia 12, sawa na vijana 73.4 milioni. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4.5, ukilinganisha na hali ya ukosefu wa ajira ya vijana duniani kwa mwaka 2007. Kwa hiyo, ina maana ukosefu wa ajira unapanda huko duniani na sisi siyo kisiwa. Sisi pia inatuathiri hapa kwetu Tanzania, tatizo la ajira kwa vijana limekuwa ni changamoto kubwa kwa Wananchi wetu, kwa mujibu wa takwimu ya Taarifa ya Takwimu Tanzania ya Januari, 2012, ukosefu wa ajira nchini ulifikia asilimia 10.7. Waathirika wakubwa wa tatizo hili ni vijana, kwani vijana ni zaidi ya asilimia 68 ya nguvu kazi ya Taifa. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu wa Makazi ya Mwaka 2012 vijana ni takriban milioni 16 plus na ni asilimia 35 ya Watanzania wote.

Wizara yangu ina jukumu la kisera, kimkakati na kimuundo la kushughulikia maendeleo ya vijana nchini. Maendeleo ya vijana yanagusa malezi yao, makuzi yao, afya

zao, utamaduni wao, uzalendo na uwajibikaji wao kwa Taifa, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha nguvu kazi yao inatumika ipasavyo kwa maendeleo yao, familia zao na Taifa lao kwa ujumla. Idara ya Sekta ya Maendeleo ya Vijana katika Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ina hili jukumu na inalitekeleza kuititia Vitengo vyake vitatu, ina Vitengo Maalum. Kwa hiyo, masuala mbalimbali ambayo yamekuwa yanajitokeza katika majumuisho mbalimbali na michango mbalimbali kuhusu nini kinatakiwa kifanyike ili kiweze kuwafikia vijana.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali imejipanga, inayo Idara nzima inayoshughulikia hiyo na ikishirikiana na TAMISEMI, lakini ikishirikiana na Wizara mbalimbali kuweza kushughulikia ukosefu wa ajira kwa vijana. Sasa Kitengo kimoja kikubwa ambacho kinashughulikia masuala ya vijana ni kitengo ambacho kinashughulikia maendeleo ya uchumi na uhamasishaji kwa vijana na kingine kinashughulikia makuzi, ushauri nasaha na maongozi kwa vijana. Kingine kinashughulikia mafunzo na maendeleo ya ujuzi, kwa maana ya kushughulikia masuala ya kuratibu na kutoa mafunzo ya ujasiriamali na stadi za kazi kwa vijana kuititia vituo mbalimbali vya mafunzo ya vijana vilivyopo hapa Tanzania katika sehemu tofauti, kingine kipo Mbozi, kingine kipo Morogoro na kingine kipo Kilimanjaro Marangu.

Wizara kuititia Kurugenzi ya Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Maafisa Vijana walio katika Sekretarieti ya Mikoa na Halmashauri za Wilaya, tunawatayarisha vijana kwa kuwapa mafunzo ya ujasiriamali. Kwa hiyo, hii ninapozungumza katika *level* ya Wizara, haina maana kwamba, hatufikii katika Halmashauri kama alivyotoka kuzungumza mchangiaji mmoja. Wizara imefanya juhudzi za makusudi za kutambua kwamba sekta tunazoshughulika nazo ni sekta mtambuka na watekelezaji na walengwa muhimu wako katika Halmashauri. Kwa hiyo, tumefanya juhudzi ya makusudi ya kuhakikisha kwamba, tumeweka kigezo na mlengo wa kuhakikisha tunawafikia vijana kule kule katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu mkakati wa maendeleo ya ajira kwa vijana, kama upo au haupo. Kama nilivyoeleza hapo awali, mkakati unaosimamiwa na Wizara yangu unabeba dhana nzima ya maendeleo ya vijana na unalenga pia kwa kiasi kikubwa kushughulikia suala la kuwatayarisha vijana kuweza kujajiri na kuweza kuajiri wengine. Hili nataka nirudie tena, ni jukumu la Idara ya Sekta ya Vijana ndani ya Wizara yangu na tumejipanga bila kusita, kuhakikisha kwamba, lile jukumu tulilopewa tunalitekeleza kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyokwisha zungumza, tuna hivyo vitengo vitatu ambavyo vinajielekeza nguvu kabisa katika utekelezaji wa mpango wa kuwatayarisha vijana kupitia stadi za kazi na stadi za maisha. Kuwatambua vijana walipo, wako wangapi na mahitaji yao ni nini. Kazi hili tunaifanya, kama nilivyosema hapo mwanzo, kwa vijana wote walio katika Vyuo Vikuu na vijana walio nje ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara inaboresha mahusiano ya moja kwa moja, kama nilivyozungumza, kwa kutekeleza majukumu yetu na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini. Tumekubaliana kuwa kila Mkoa, uwe na Afisa Vijana katika Sekretarieti za Mkoa, kila Halmashauri iwe na Afisa Vijana kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na Mikakati mbalimbali inayotolewa na Serikali Kuu kwenda TAMISEMI, kwa lengo la kuendeleza vijana nchini, inatekelezeka na kwa kiasi kikubwa tupo katika ngazi tofauti tofauti za kutekeleza hiyo mikakati. Kwa makubaliano na TAMISEMI, tayari Wizara inaye Afisa ndani ya TAMISEMI, anayeshughulikia moja kwa moja masuala ya Wizara yetu yanayohusu Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie hapo; tumeona wazi kabisa hapa Waziri mwenzangu wa kutoka TAMISEMI, anazungumzia masuala ya michezo yako katika *finger tips*. Ile ni mwonekano kabisa ambao tunavyofanya kazi kwa karibu kwa kushirikiana na kuhakikisha kwamba, masuala

yanayowagusa wale vijana huko katika Halmashauri mbalimbali yanawafikia na sisi tumechukua. Tumeiona hiyo *gap* na kuhakikisha kwamba, tunaizuwia hiyo isiwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia ilikwishaomba kila Mkuu wa Mkoa, kuhakikisha kila Halmashauri ya Wilaya nchini inatenga maeneo muhimu ya kushughulikia vijana. Kama nilivyosema na hao vijana wapo, hivi sasa wengine wanashughulika na kilimo, ufugaji wa nyuki, biashara ndogondogo na shughuli nyininge za maendeleo ya vijana na jukumu kubwa ambalo tumeliweka ni kushughulikia masuala zaidi yale ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, tatu, tumejikita katika kuwajengea mahusiano chanya baina ya vijana na sekta binafsi, kama kiungo muhimu kwa maendeleo ya vijana. Katika hili, nguvu ya makusudi imewekwa katika kuhakikisha vijana wa ngazi zote, hasa wa Vyuo Vikuu, wamejengewa mitazamo yenye fikra chanya ya misingi ya ujasiriamali na biashara na kuwahamasisha kujunga katika vikundi na kutengeneza kampuni zao zinazolenga kutatua kero mbalimbali zinazowazunguka na kuzigeuza kuwa fursa za kujajiri na kuwaajiri wengine tangu wakiwa vyuoni.

Mheshimiwa Spika, katika hili, Wizara imeshawasiliana na Wakuu wa Vyuo Vikuu kutekeleza mkakati huu na kazi inaendelea. Hivi ninavyozungumza, sasa hivi Mkoa wa Pwani, wamekwishawasiliana na Vyuo Vikuu, kwa kiasi kikubwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na baada ya muda mfupi pale Kibaha, wataweza kuona mambo ya ajabu kabisa yanayotokana na vijana ambao wameitikia wito kwa nguvu zote. Katika kufanikisha hili, Wizara pia imewafikia wafanyabiashara mbalimbali na kufanya nao mazungumzo moja kwa moja na wengine kwa makundi, lengo likiwa ni kuwapa picha kamili ya umuhimu wa vijana na nafasi ya vijana katika kufanikisha shughuli mbalimbali za maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilijitokeza kwa kiasi kikubwa ni hoja ya mikakati na kazi mbalimbali. Nimeizungumzia na kusema kwamba, mikakati mbalimbali inatekelezeka, Wizara mbalimbali zinatakiwa kutekeleza kazi mbalimbali kwa kuhakikisha wanawa-covervijana. Sasa kwa upande wa Wizara yangu kama Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, nayo nataka nizungumzie tu hapa fursa mbalimbali za kazi ambazo zinaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Habari, mtu ukiiangalia, unaweza ukaiangalia tu juu juu ukadhani hapa ni masuala tu ya *journalism*, lakini katika upande wa habari kuna habari, masuala mbalimbali, unaweza ukagusia masuala ya upangaji wa habari, kusimamia, kushughulikia habari. Unapoangalia rasilimali za habari, kwa maana ya *information resources*, watu wenyewe ustadi wa habari (*Information related skills individuals*), teknolojia ya habari (*Information technology*) kwa maana ya mkonga, nakala mango, masuala ya *hardware*, nakala tepe, masuala ya *software*, masuala ya *programme za computer*, vyanzo na vifaa viwezesho vya mtu kupata, kujituma na kutunza mwenyewe habari, *information facilities* mbalimbali kwa maana ya Maktaba, kwa maana ya Vituo vya Habari mbalimbali, vyote hivi ni vyanzo ambavyo fursa za kazi zinaweza kupatikana na watu wakaweza kujikita.

Mheshimiwa Spika, tunajitahidi kuhakikisha tunawahimiza wasomi mbalimbali wa Vyuo Vikuu na wale ambao wametoka nje ya Vyuo Vikuu kwamba, katika hizi nafasi zipo ngazi mbalimbali za kuweza kupata kazi. Vyanzo vya Habari (*Information Resources*), Huduma za Habari (*Information Services*), Mifumo ya Habari (*Information Systems*), vyote hivi ni nafasi ambazo kazi mbalimbali zinaweza zikatekelezeka. Vijana wa Vyuo Vikuu nataka niwaambie kabisa, masuala ya habari yanatoa fursa mbalimbali za kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa filamu, upande wa utamaduni, ukiacha masuala ya sanaa tu, filamu pamoja na muziki, kuna nafasi tofauti tofauti za kazi. Zipo nafasi zaidi

ya 20, kama ukitaja unaamua sasa hivi kutengeneza filamu. Siwezi kuzitaja hapa kwa sababu ya ufinyu wa muda, lakini nafasi zipo nyingi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya maadili kuporomoka kwa ujumla katika jamii ikihusishwa na vyombo vyahabari na sanaa imejitokeza na hili tumelizungumzia kwa kiasi kikubwa. Tumesema muda wote kwamba, Mtanzania ni mtu mwenye utii, mwenye amani, upendo, ushirikiano, umoja na uvumilivu, kwa hiyo basi, tujitahidi kwa kiasi kikubwa, kuhakikisha tunasimamia hayo maadili yetu na vyombo vyahabari visitusaidie kuporomosha hiyo na watu tusichangie, hasa viongozi, kuhakikisha tunatumia vyombo vyahabari kuendelea kuporomosha maadili yetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, walochangia katika suala hili la maadili, kwa kuona tabia hii mbaya inayojenengeka ndani ya jamii yetu. Nawaomba kwa pamoja tujitahidi kupiga vita kwa nguvu zetu zote, kila tunapopata fursa ya kuongea na Watanzania wenzetu, tuwaambie wazi kabisa vurugu siyo maadili yetu, kama Serikali, tutaendelea kufanya kazi na kila tunaloweza, kuzuwia vurugu na viashiria mbalimbali vyahurugu vinavyoweza kujitokeza vitakavyoendeleza kuporomosha maadili yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ya jumla, napenda sasa nichukue nafasi hii, nizungumzie pia kwa ujumla Sekta ya Utamaduni. Sekta ya Utamaduni ilichangiwa na Wabunge zaidi ya 80 na hoja zao zipo mbalimbali, nikipata muda ninaweza kuzipitia. Kwa kiasi kikubwa yapo maeneo kama matano, ambayo wameyazungumzia. Moja la uzingatiaji wa maadili ya Mtanzania, hasa katika maleba na uchezaji wa muziki wenye staha na hii imezungumziwa na wachangiaji kama wanane.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme tu kwamba, Wizara inaendelea kuvifutilia kwa karibu vikundi vinavyofanya maonesho haya na kuvichukulia hatua kali, hususan vikundi na kumbi zinazoonesha maonesho hayo. Kwa

kiasi kikubwa, wamepewa onyo tayari na hatua itakayofuata kama havitajirekebisha, kwa bahati mbaya itabidi nifanye yaleyale ambayo wengi wakati mwingine huwa mnahangaika nayo; Wizara yangu itavifungia kuendelea na shughuli za kutoa burudani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu imekuwa ikielimisha jamii kuititia vyombo vya habari kuhusiana na masuala mbalimbali ya kiimaadili katika jamii, yakiwemo mavazi ya staha, kuheshimu na kuthamini mila na desturi zetu za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hoja nydingine ambayo imejitokeza na imechangiwa na wachangiaji kumi ni mchakato wa Vazi la Taifa na mahali ulipofikia.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, nizungumzie kwamba, Wizara imekamilisha mchakato wa mapendekezo ya Vazi la Taifa, baada ya kushirikiana na kupokea maoni ya wadau. Hivi sasa mapendekezo yameshafikishwa ngazi ya *MTC*; matarajio ya Wizara ni kwamba, hatua zote zitakamilika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu, kulindwa kwa haki na maslahi ya wasanii. Hili tayari mwenzangu ameshalizungumzia na lilichangiwa na wachangiaji kumi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni usimamizi wa haki za wasanii na hilo pia tayari limekwisha; hapana, hili katika uuzaji wa miito ya simu, hili limechangiwa na wachangiaji kumi.

Kimsingi, niseme tu kwamba, Wizara yenze dhamana ya kufuatilia biashara ya milio ya simu ni Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wizara yangu ikiwa msimamizi wa wasanii, kazi zao na wadau wa sanaa, inashirikiana na Wizara hiyo ili kuona wasanii wanapata haki zao.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa kwa makini na kwa ushauri mzito mwingine kutoka kwa

Profesa ni maendeleo na mwendelezo wa Lugha ya Kiswahili na kuthamini Lugha yetu ya Kiswahili. Hii imechangiwa na Wabunge 12.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuratibu, kuimarisha uimarishaji wa Lugha ya Taifa kwa kuhimiza matumizi yake katika mawasiliano yote rasmi ya Serikali katika kuifundisha hadi ngazi ya Vyuo Vikuu pamoja na kuifundisha kama lugha ya kigeni katika vyuo mbalimbali nje ya nchi. Hivyo, natoa wito Watanzania wote tuendelee kukienzi Kiswahili kwa vile ndiyo utambulisho wetu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi walichangia pia masuala mbalimbali kutokana na yale niliyozungumzia kwa ujumla kuhusu kero ya vijana. Pia, wameuliza kuhusu mpango maalum wa makusudi wa kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri huu wa Kamati. Hata hivyo, tumeshaanza kufanya matayarisho, kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana, kama nilivyokwisha kuelezea; Wizara, imehamasisha Mikoa na Wilaya, kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli zao za uzalishaji mali. Mikoa na Wilaya mbalimbali tayari wameitikia wito huu. Aidha, Wizara, imeshirikiana na Taasisi za Fedha kama vile *NMB* na *Exim* ili kutoa elimu ya ujasiri amali na mikopo rafiki kwa vikundi vya vijana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hoja nyiningine ambayo imejitokeza katika *section* ya vijana; Baraza la Vijana tayari limeshazungumziwa.

Mheshimiwa Spika, fedha ya Mfuko wa Vijana kugharamia pia uundwaji wa Baraza la Vijana. Fedha ya Mfuko wa Vijana wa Maendeleo, zimetengwa maalum kwa ajili ya kuwawezesha vijana kupata mikopo nafuu. Shughuli za Baraza la Vijana zitakuwa na vyanzo vya mapato tofauti na shughuli nyiningine za maendeleo ya vijana. Nina maana fedha zitakazowenza kuendesha Baraza la Vijana litakapokuwa tayari, hazitatokana na Mfuko wa Vijana.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Afrika wa Vijana, umeulizwa hapa umefikia wapi. Kazi ya kuandaa Muswada wa Sheria ya Utekelezaji wa Mkataba huo tayari imeanza kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Muswada huo utakamilishwa mapema iwezekanavyo ili uweze kuletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lakini pia masuala ya mwenge yameshazungumziwa.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana kwa ujumla imezungumziwa na watu 16; nayo tayari nimeshaigusia.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge 15; nao tayari nimeshauzungumzia.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya shughuli za ujasiriamali na stadi za vijana; nimeshazungumzia kwa ujumla nayo imechangiwa *specifically* na watu watatu.

Mheshimiwa Spika, suala la madawa ya kulevyta nalo limechangiwa na mtu mmoja, ingawa hili ni suala ambalo linatupa shida kwa upande wa vijana. Ni tatizo, lakini kama nilivyosema, katika Wizara yangu kuna sekta ambayo kuna Kitengo cha *Guidance and Counselling* ambacho kinashughulika na masuala haya moja kwa moja, tukisaidiana na wadau mbalimbali pamoja na Serikali, kwa ujumla. Wizara, inayo hii katika stadi za maisha na stadi za kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia usimamizi wa Mfuko wa Vijana wa Wanawake wa Halmashauri, wameuliza wajumbe watano.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba, jukumu zima la kutenga na kusimamia matumizi ya fedha za vijana zinazotengwa kutokana na mapato yao, Halmashauri inalisimamia. Vijana na Wamachinga wanaweza kunufaika na mpango wa Halmashauri wa kutenga maeneo ya kazi kwa vijana na

kuepuka adha ya maaskari wa mijini kuendelea kushirikiana na TAMISEMI, waendelee kushirikiana na TAMISEMI, kuhakikisha kwamba, wanafanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, suala la Mwenge wa Uhuru, limezungumzwa na watu wanne, lakini Mheshimiwa Makala, tayari amekwishalizungumzia.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo wamegusia kubwa ambalo ningependa nisije nikalisahau au nikakosa muda wa kulizungumzia ni suala la *TV Imani*.

Mheshimiwa Spika, hili limezungumziwa na wachangiaji wengi kwa kiasi, wachangiaji kama wanane; *Television* ya Imani kutopatiwa kibali cha kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nichukue nafasi hii niseme, hili suala lipo linafanyiwa kazi. Serikali, inatambua kwamba, *Radio Imani* au *TV Imani* wameomba kituo cha *television*, kupatiwa kwanza kibali cha kujenga kituo. Sheria ya *Electronic* na Posta ya Mwaka 2010, pamoja na Kanuni zake, imeainisha kwa kina utaratibu wa kituo cha *television* kupatiwa kwanza kibali cha kujenga kituo baada ya kuwasilisha maombi ya kutoa matangazo ya *television*.

Mheshimiwa Spika, *Television Imani*, ilienda kinyume na utaratibu huo kwa kuanza kutangaza kabla hata ya kupata kibali cha kurusha matangazo hewani kwa majaribio. Hii kidogo ikaleta shida, kwa hiyo, *Television Imani* inapaswa kufuata utaratibu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utangazaji. Pamoja na *Television Imani*/kukamilisha utaratibu wa kupatiwa leseni, kinachofanyika hivi sasa ni uhakiki wa kina (*Vetting*) ili kujiridhisha kama wamekidhi matakwa. Kwa hiyo, hili la kusema liko Wizarani kwangu au haliko Wizarani kwangu, hiyo ni *relative*, liko katika Vyombo ambako linatakiwa kufanyiwa kazi na linafanyiwa kazi kwa karibu kwa kuangalia umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, hoja mbalimbali zilitoka kwa Wabunge mbalimbali, wengine wanaauliza Serikali ina

mpango gani kuboresha vitendea kazi nya *TBC*; Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Nassib Suleiman, pia amezungumza hilo.

Mheshimiwa Spika, hilo nimekwishalielezea na kama tukiweza kuongezewa hizi pesa ambazo nashukuru Waheshimiwa Wabunge, tunaweza pia kuhakikisha na kuisimamia vizuri *TBC* kuhakikisha inajijenga kama inavyotakiwa kama *Television* ya Taifa. Kwa kiasi kikubwa vifaa vingine vitaendelea kununuliwa kadiri hali ya kifedha itakavyoendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kuna Mbunge ambaye ameomba kwamba, *TBC* irudishe nyuma muda wa kipindi cha Bunge cha usiku badala ya saa nne.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme tu, *TBC* imepokea ushauri huu na itaona uwezekano wa Kitaalamu wa kuweza kulifanya kazi, bila kuathiri mtiririko wa vipindi, hasa Taarifa ya Habari, ambayo ni lazima iwe saa mbili kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna wachangiaji wengi ambaao wamezungumzia hoja ya kutosikika kwa redio za *TBC* Wilayani Nkasi, Mwambao na Ziwa Tanganyika na maeneo mengine ya nchi. Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Injinia Lwenge, Mheshimiwa John Mipata, Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari na Mheshimiwa John Paul Lwanji, wote wamezungumzia masuala haya.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii njibu kwamba, azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa, matangazo ya *TBC* yanamfikia kila Mtanzania. *TBC* inaendelea na mpango wa kufunga mitambo ya redio maeneo ambayo hayana usikivu mzuri au *TBC* haifiki kabisa. Mpango huu utaendelezwa kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika hili niseme, ndiyo maana nilichukua nafasi ya kuzungumzia masuala ya *TBC* kwamba, yamezungumziwa kama hoja thabiti kutoka kwa watu wengi,

ambayo imetupa nguvu na kuonesha kwamba, wana hamu kabisa *TBC* iweze kufanya kazi na wanaiamini. Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Kitandula na yeye pia amezungumzia hayo hayo.

Waheshimiwa wengine wameomba *TBC* iangaliwe kwa jicho la huruma, ipewe fedha za kuweza kuiendesha. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Abdallah Ameir, Mheshimiwa Mipata na Mheshimiwa Diana Chilolo, wote hawa wamejitalidi kuitetea *TBC*.

Nataka nichukue nafasi hii nielezee kuwa, Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na *TBC* katika kuelimisha jamii. Hivyo, itaendelea kutatua matatizo ya *TBC* kwa kadiri fedha inavyopatikana. Kuhusu Jengo la *TBC*; Serikali, inaendelea na juhudzi za kutafuta fedha ili kulimalizia Jengo hilo. Katika juhudzi hizo, *TBC* iliomba mkopo wa *NNSS*, kwa hiyo, nategemea labda huko tunakoelekea, *NNSS* nao watatuangalia kwa jicho la huruma, kwa kutambua kwamba, *TBC* nayo ni Chombo cha Taifa, ambacho itakuwa ni vizuri kiweze kufaidika pia na pesa hizi ambazo zinakatwa kila siku.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi akina Mheshimiwa Agness Mkanga, wote wamezungumzia haya masuala. Mheshimiwa Ritta Kabati, ameyazungumzia hayo na Mheshimiwa Obama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, amezungumzia kuhusu bajeti ndogo. Wanaodaiwa wa *TBC*; nataka niseme tu kwamba, tumepokea ushauri na tutauzingatia.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya *TBC* iwe *creative* na *innovative*, ili iweze kuhimili ushidani. Maslahi ya Watumishi yaongezwe, watumishi wasomeshwe vizuri; yote haya nasema tutayazingatia.

Mheshimiwa Spika, labda nigusie pia kidogo wazungumzaji mbalimbali waliozungumzia utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, nizungumzie kidogo suala la Twiga *Stars*. Twiga *Stars* na yenyewe pia inafanyiwa mipango maalum na *TFF*, lakini pia na Serikali kuhakikisha kwamba tunawa-*support* na ninategemea kwa kushirikiana na Wizara ya Jinsia na Watoto hata katika wale makocha mbalimbali tunajaribu kutafuta uwezekano wa kuhakikisha kwamba Twiga *Stars* inakuwa katika mstari wa mbele lakini inaonekana na kuendeleza mwendelezo wake ambao umekwishaanza siku zote.

Mheshimiwa Spika, lakini katika upande wa utamaduni, napenda pia niendeleze kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilizungumzia masuala ya BAKITA. Wizara tayari imekamilisha kuandaa mapendekezo mbalimbali ya marekebisho ya sera ya utamaduni na hivi karibuni nitawasilisha mapendekezo hayo ya sera katika ngazi ya juu ya maamuzi ya Serikali. Sera ya Utamaduni mpya itafanyiwa marekebisho na itakapokuwa tayari, marekebisho ya Sheria ya BAKITA ili kulipa uwezo wa mamlaka ya kudhibiti, kusajili na kutoa ada na pia kutoa adhabu kama Kamati ilivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Kamati ilishauri kwa upande wa utamaduni kutengea BAKITA fedha ya kutosha. Hili na sisi tumeliona kama Serikali, lakini pia tunajitahidi kuwajengea BAKITA uwezo wa wao kama chombo ambacho kinaweza kujitegemea kuweza kuandika maandiko mbalimbali na kuwakutanisha na wafadhili mbalimbali kufanya kazi na kujimudu kwa kiasi kikubwa pamoja kuongezea na hiyo ruzuku ya kutoka kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja mbalimbali za utamaduni kama kumi kutoka Kambi ya Upinzani na zenyewe ni hiyo ya madai ya Viongozi kutumia lugha ya Kiswahili. Wizara itaendelea kuhimiza hiyo, lakini pia Serikali imefanya nini kwa tasnia kuingiza kiasi gani cha kipato? Serikali inachukua hatua mahususi kuhakikisha kuwa tunafuatilia mapato yatokanayo na tasnia ya filamu na kiasi kikubwa kwa hali ya sasa, tasnia hii inachangia *percent* mbili ya pato la Taifa kwa wastani kwa kipindi cha mwaka 2006 mpaka 2010/

2011. Filamu zinazoingia sokoni kila mwezi hazipungui *master 20*, yaani nakala mama. Kila nakala mama huzalisha siyo chini ya nakala 20,000. Kila nakala huuzwa Sh. 1,800/= kwa bei ya jumla kwa bei ya reja reja ni Sh. 2,500/= hadi Sh. 3,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa mahesabu haya, kila nakala ikiuzwa kwa Sh. 2,500/= kwa makisio, jumla ya Sh. 50,000,000/= hupatikana kwa kila nakala mama. Haya ni mahesabu ya wastani kuitipitana na kipato cha tasnia hii kuimarika na wasanii mbalimbali kuweza kunufaika kwa hakika, lakini pia kuwajengea pamoja na vijana mbalimbali umuhimu wa kuhakikisha kwamba vijana tunawajengea masuala ya ujasiriamali lakini pia tunawajengea utamaduni wa kuweza kulipa kodi. Kuheshimu kazi mbalimbali unayofanya, kipato chochote unachokipata, basi kodi ni lazima ulipe kuhakikisha kwamba *services* mbalimbali ambazo zinatekelezeka ambazo pia na vijana wanazitumia na wananchi mbalimbali, ni lazima kodi ambayo inahitajika kufanya basi ifanyike.

Mheshimiwa Spika, pia hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imeuliza, Serikali inafanya nini kuhakikisha Tanzania inakuwa *film destination?* Nakubali kuwa tasnia ya filamu inaweza kuitangaza Tanzania na kuifanya kuwa sehemu ya utalii wa kupiga picha. Wizara yangu inachukua hatua ya dhati kwa kuwahamasisha na kuwajengea uelewa wadau wa filamu kuhusu umuhimu wa matumizi ya mandhari asilia ya Tanzania katika *film* zao ili kutangaza utambulisho wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa wadau wa filamu wapanue wigo katika matumizi ya mandhari hiyo. Lakini pia wakati ninazungumza kwa ujumla, nimezungumzia kwamba masuala ya filamu na masuala haya ni ajira tosha. Mpaka filamu itoke, ina *section* zaidi ya 20. Hata ile wazo tu lenyewe peke yake linatosha. Hata ile kuweza kukusanya tu avae nguo gani, peke yake, wako watu ambaao ni *trained* wa kuweza kuamua wazo lako hili bwana *scenery* yake iwe namna hii. Kwa hiyo, ndiyo ninachotaka kusisitiza kabisa kwamba

pamoja na Kambi ya Upinzani kukumbusha hili, sisi tuko tayari, tunalfanya kazi, na wewe kama msanii rasmi, basi tuungane mkono kuhakkisha kwamba tunafanya vitu sawasawa na tunapochukua filamu mbalimbali zisiwe kuuza *lines* za ISO huko nje. Maana ukiangalia *films* za wenzetu unazikuta zimejipanga vizuri, siyo mambo ya kufanya kiutani utani. Masuala ya *lightening* yamejiweka vizuri. Kwa hiyo, hayo yote ni masuala ambayo Serikali inayasmamia na inayafuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani pia imetaka kujua kwa nini Bodi ya *COSOTA* haina mwakilishi wa wasanii kama Sheria inavyotaka? Sheria ya Hati Miliki ilikuwa na upungufu na iko kama nilliyosema, iko katika mchakato ambao tumesema ziko Sheria ambazo tumezi - *pin point* kwamba hizi Sheria fulani ili kuweza kufanikisha hili lengo ni lazima zifanyiwe kazi. Kwa hiyo, hiyo ni mojawapo ya Sheria ambazo zitaletwa na hata katika wakati wa kuboresha kanuni mbalimbali ili kuweza kushughulikia ule mtando ambao tunautengeneza wa kuhakkisha kazi za wasanii haziibwi na kuweza wao wenyewe kujua kwamba ni kazi gani ambazo ziko katika *market* na ni kazi gani wamezitengeneza, ni wao wenyewe watakuwa katika *control*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii niwaombe wasanii, basi kwa vile Sheria zikitengenezwa ni muhimu pia kuwa na nidhamu ya kuzifuatilia, au kanuni mbalimbali, au maelekezo mbalimbali ambayo yanapelekea kuwasaidia wao kuimarisha nafasi zao, basi wazingatie na ndiyo msimamo mzuri wa maadili mazuri ambayo tunawategemea vijana wetu na hasa hawa kioo cha jamii ambacho tunasema ndio wanakionesha huko nje pamoja na ndani. Lakini baada ya kuzungumza hayo, niseme pia hata katika nafasi ya muziki zipo nafasi mbalimbali za kazi waandishi, wale ma-producers mbalimbali, wote ni hao ni nafasi mbalimbali za kazi ambazo tungeomba vijana wazitumie vizuri na ikiwezekana kwa kutumia sanaa mbalimbali za vyombo mbalimbali vya muziki, kila mwanasanaa asiwe wa ku-*rap* tu, apige na chombo kimoja au viwili. Ukiangalia wote walijitokeza, hata kule Marekani

hawa-*rap* tu. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema ni lazima tujihakikishie kwamba wanabeba zile ala zenyewe za muziki.

Mheshimiwa Spika, nilisema hotuba ya Kambi ya Upinzani ina *itemskumi* na hizo zote nadhani nimeshazi-*cover* haki za wasanii, tayari na miito ya simu nimekwisha izungumzia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maendeleo ya Jamii pia imezungumzia masuala hayo hayo, haja ya kuiongezea mtaji wa fedha *TBC*, hili nimeshalizungumzia. Serikali kutekeleza mapendekezo ya utafiti uliofanywa na mamlaka ya mawasiliano *TCRA* kuhusu jinsi ya kugharamia na kuendesha vyombo vya utangazaji vya umma. Hili napenda nilielezee tu kwamba ni kweli tunakubaliana na Kamati na kwa kweli utafiti ule ambao umefanyika, katika nchi nane, umetunufalsha kama Wizara, lakini pia kwa *TBC* kupata hata nguvu ya kuweza kuendelea kusukuma mtazamo wa kuhakikisha kwamba Serikali tunaisimamia na *TBC* na kuhakikisha kwamba inafanya yale majukumu yake ambayo yanahitajika.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, ule utafiti ulionyesha wazi kabisa vyombo vingine vya Serikali kama *TBC* ilivyo, vinafanya biashara, kwa hiyo, ile dhana ya hapa ya kujaribu ku-*pushile element* ya kwamba *TBC* isifanye biashara, tunataka tuongezee wazi kabisa kwamba *TBC* kwa misingi iliyojenjeka katika nchi nyingine za Afrika pamoja na nchi nyingine zilizoendelea, zinafanya biashara. Lakini pia Serikali inavipa *support*, na inapata majukumu ambayo wengine ambao ni *private* hawana hayo majukumu. Kama tulivyosema, hivi leo *TBC* watatakiwa wa-*cover* vitu nchi nzima, waonyeshe masuala mbalimbali ya Kitaifa, lakini vyombo vingine havina hilo jukumu. Wakiamua kuzima, wanaweza kuzima tu pamoja, wakijua kwamba siyo maadili ambayo tunawajengea.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya jamii wamezungumzia ni kutaka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNU NA
MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Vijana,
Utamaduni na Michezo**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management...*
Tshs. 3,271,464,000/=

MWENYEKITI: Mshahara wa Waziri. Mmesema hela hazitoshi, bado mnautaka mshahara wake. Haya, tunaanza na Mheshimiwa Soni, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Jenitsta na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi. Haya, tunazo dakika 25 kama zitakuwa bado, wengine hawataitwa.

MHE. JITU VRAJLAL SONI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi katika mchango wangu niliomba kupata tamko la Serikali na sikupata jibu wakati Mheshimiwa Waziri anajibu maswali wala Naibu Waziri, juu ya kufuatilia mashindano ya mpira kanda, Mkoa na Wilaya. Kumekuwa na uzembe mkubwa kwa Vyama vya Michezo na Vyama vya Mpira katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Kanda kutokuzingatia utaratibu wa namna ya kuendesha yale mashindano na pia kuondoa baadhi ya timu, ikiwemo timu ya Magugu *Rangers* ambayo imekuwa bingwa wa Mkoa wa Manyara bila wao kupata utaratibu wowote. Baada ya kutoa malalamiko, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kufuatilia Mikoa yote ya Tanzania Bara mahali ligi imechezeshwa ili kujua

namna hizi ligi zinavyochezeshwa na mahali ambapo wamekosea hizo timu zote ziondolewe katika ligi na viongozi wale wazembe wachukuliwe hatua za kinidhamu? Je, Serikali inatuhakishiaje ili watu wawe na imani na masuala ya michezo? Kwa wale wote waliochangia wameshaanza kukosa imani ya namna ligi hizi zinavyochezeshwa na kuna malalamiko kuwa baadhi ya Mikoa imechezesha timu chache tu na kuzipendelea na kuzipeleka katika ngazi ya Kanda. Mimi naomba tupate tamko la Mheshimiwa Waziri ili nikubali kwamba nitaunga mkono hoja. La sivyo, nitaondoa Shilingi.

MWENYEKITI: Hapa ni ufanuzi. Matamko yanatokea wapi? Matamko huwa Mawaziri wanaleta hapa? Ufanuzi! Waheshimiwa Mawaziri, naomba mwandike kila anayezungumza, maana yake mtajibu pamoja.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri naomba maelezo ya kina kidogo katika hili kwa sababu nisiporidhika nitaondoa Shilingi. Katika kitabu chako, toka ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho hujazungumzia kabisa majanga yanayowakuta wanahabari ikiwemo kutekwa na kung'olewa kucha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, tusitafutane hapa, hebu kaa chini! Uamuzi wangu wa jana ni *standing*. Kama mnarudia, basi unakaa chini na nilikuwa nachelea kusema. Tunaendelea. Mheshimiwa Kabati, hatuna muda wa kupoteza. Mheshimiwa Kabati, hayupo, *okay*, Mheshimiwa Iddi Azzan.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Miongoni mwa mambo ambayo yalikuwa yanaleta mkanganyiko na vurugu kubwa sana katika michezo ni suala la kuitwa kwa wakati kwa sera za michezo. Lakini kwa maelezo ambayo leo yametolewa na Mheshimiwa Waziri na nilikuwa nikilipigia kelele miaka mingi, tuna matumaini makubwa sasa kwamba suala hili litakamilika. Kwa sababu kama ambavyo wamesema kwenye hotuba yao na katika maelezo yao ya majumuisho,

kwamba suala hilo lipo kwenye ngazi za juu na ni matarajio yangu kwamba hizo ngazi za juu na zenyewe zitatimiza wajibu wao haraka ili tupate sera ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kupitia Wizara hii kwa kuchukua hatua hizo na niwatake tu sasa Mheshimiwa Waziri atakaposimama atuambie kwamba huko ngazi za juu kazi zikienda huwa zinachukua miaka ama ni miezi kadhaa tu zitakuwa tayari ili tuwe na sera nzuri ya michezo? Naomba sana hili lifanyike haraka kwa sababu tunachotaka ni kuwa na sera nzuri ya michezo itakayoleta maendeleo kwa wananchi wetu. Hatutaki mambo ya haraka haraka kama yaliyotokea juzi ya Yanga kumfunga Simba wakati Simba walikuwa na wachezaji nane tu kiwanjani. Ahsante.

MWENYEKITI: Ah! Mh! Mheshimiwa Clara Mwatuka.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kueleza kutokana na jinsi nilivyochangia wakati ule, nafikiri uliona ni jinsi gani nilizungumza kwa uchungu kulingana na hali ambayo vijana wetu wanaiga mitindo mbalimbali ya mavazi ambayo haiendani na mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri pale amejibu vizuri, amejitahidi, lakini naona bado na imezoeleka kwamba mara nyingi wanasema tu hili tutafuatilia, hili nitalifuatilia kwa karibu. Lakini utakuta miaka inapita, utekelezaji haupo. Sasa kulingana na hali inayokuwepo ni kwamba siyo wale wanaaibika wenyewe tu, ni kwa Taifa na hasa ukichukulia kwa sisi akina mama unavyomwona mtoto au watazamaji wanaojiheshimu wanapoona mavazi yale sijui wanajisikiae. Kwa vyovyote hii inakuwa inafedhehesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutokana na hilo, naomba kauli ya Serikali inasema nini juu ya hili? Maana isiwe maneno tu, nataka hasa vitendo. Siyo nadharia, hapana.

Kwa hiyo, naomba ueleze hapa ni jinsi gani utaondoa kabisa au angalau utapunguza? Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imezungumza na kuweka bayana nia ya Serikali ya kushughulikia tatizo la ajira. Ni bahati nzuri sana sensa ya idadi ya watu na makazi kama nilivyokuwa nachangia imeweka bayana kwamba asilimia siyo chini ya 70 ya Watanzania wote ni vijana chini ya miaka 35 na takribani vijana sio chini ya milioni 16 hawana ajira katika nchi yetu ya Tanzania. Tunayo idadi ya wasomi takribani 1,200,000, wamesoma lakini ni 200,000 tu ndiyo wameingia kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu ya Serikali imekuwa ikitenga fedha katika maeneo mbalimbali. Leo tunaishukuru Serikali kwa kusikiliza kilio cha Kamati na Wabunge, kuongeza fedha ya Mfuko wa Vijana, kutoka Shilingi bilioni tatu kwenda Shilingi bilioni sita. Lakini nilichokuwa nataka kujua kutoka kwa Serikali, kwa kuwa, Sekta ya Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano ina fedha nyingi tu kwenye kilimo, madini, uwekezaji, maji na kadhalika, itahitaji wataalam wasomi na wale ambao sio wasomi; na kwa kuwa tayari tunaelewa idadi ya vijana wetu waliosoma na wasiosoma ambao wako vijiji: Je, Serikali inatueleza nini na inajipanga namna gani ili sasa hii mipango yote ambayo ina fedha za bajeti iweze kuwa *coordinated* mahali pamoja na kujua idadi ya vijana watakaochukuliwa katika sekta mbalimbali katika kila fedha inayotengwa na Serikali ya nchi yetu, kuweza kujibu tatizo hili la ajira kwa hatua na hizo *level* mbalimbali kwa vijana wetu wa nchi hii ya Tanzania?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kupata maelezo kutoka kwa Waziri, kwamba Shirika la Magazeti ya Serikali (*TSN*) limekuwa na Wakurugenzi wanaokaimu. Mkumbo amekaimu kwa miaka minne na hivi sasa Nderumaki naye anaendelea kikaimu baada ya Mkumbo kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali hajjateua Mkurugenzi ambaye atakuwa nafanya kazi bila wasiwasi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi na katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ukurasa wa 29, Kambi Rasmi ilihoji kuhusiana na uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa, na ikawa imeeleza kwamba kuna Muswada binafsi uliowasilishwa wa kuunda Baraza la Vijana ambao Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa ushauri kwa Serikali kwamba, Muswada huo hautaingia Bungeni kwa madai ya kwamba umekiuka Ibara ya 99 ya Katiba ya nchi. Sababu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa ushauri huo, ni Muswada huo kuwa na kifungu cha 31 ambacho kinataka kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, kwa sababu mfuko tulionao sasa wa Maendeleo ya Vijana haujaanzishwa kwa mujibu wa sheria, na ni kitengo tu ndani ya Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Kambi Rasmi ya Upinzani imehoji hapa kwamba Muswada wenyewe ulianzisha huo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa kutumia Ibara ya 135 ya Katiba ya nchi ambayo imetoa mwanya kwa kuanzishwa kwa mifuko mingine bila kutoa pesa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, jambo ambalo halikuwa na sababu yoyote ya kuzuia ule Muswada kuwasilishwa Bungeni.

Kwa hiyo, ningependa kupata ufanuzi kutoka kwa Serikali, aidha, kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali au kutoka kwa Wizara inayohusika na Masuala ya vijana. Ni kwa nini Serikali imetoa ushauri wa kuzuia huu Muswada usiletwe Bungeni, wakati Serikali yenyewe imeahidi kwa miaka 17 kuleta Muswada bila Mheshimiwa Rais au Mheshimiwa Waziri kuagiza huu Muswada kuja Bungeni? Ni kwa nini Serikali imezuia huu Muswada? Kama sitaridhika na ufanuzi, nitaomba nitoe Shilingi hili jambo ili lijadiliwe kwa ajili ya kuisimamia Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa, nami napenda kuipongeza Serikali kwamba kwa mara ya kwanza imeweza kutenga Shilingi bilioni sita katika Mfuko wa Vijana. Kwa sababu kimekuwa ni kilio chetu miaka nenda rudi, kwamba tumekuwa tukitengewa fedha ndogo. Hata zile ndogo ambazo zilikuwa zikitengwa kwenye Halmashauri zetu zilikuwa haziwafikii walengwa. Hapa napata shaka, isije ikatokea kama ilivyotokea kwenye mabilioni ya JK, zile fedha hazikuwfikia walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 15 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba tuna tatizo kubwa la wasimamizi. Amesema kati ya Mikoa yote, Mikoa 14 tu ndiyo ina Maafisa Vijana na kati ya Wilaya zaidi ya 120 ni Wilaya 30 tu. Sasa leo hihi tuna hizi Shilingi bilioni sita, wakati bado hatujakamilisha mchakato wa kuhakikisha tuna wasimamizi ambao ni vijana. Tayari tumeshaona tatizo kwa hawa waliopo, na fedha zile kidogo zilizokuwa zikienda zimekuwa haziwafikii vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kuanzia, wana mikakati gani kuhakikisha bilioni hizi zitakwenda kuwanufaisha vijana wenye, huku tukijua katika Halmashauri zetu kuna watu wenye uchu, ambao wakiona fedha kidogo tayari wanashindwa kutimiza wajibu wao? Sasa nataka kupata majibu sahihi, wamejipangaje kuhakikisha hizi Shilingi bilioni sita zinawanufaisha vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Ritta Kabati, nilikuita.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Hoja ya ajira kwa vijana ni ilani ya Chama cha Mapinduzi. Naishukuru Kamati yako kwa kuweza kuleta hoja ya kuweza kuongezea pesa katika mfuko

wa maendeleo. Je, Serikali imeweka mkakati gani, wa kuuboresha mwongozo uliokuwepo ili kuongeza tija na kuleta ufanisi wa mfuko huo huko, pamoja na kujenga *economic zones* ili vijana waweze kufaidika zaidi?

MHE. LETICIA M. NYARERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taifa letu limekumbwa na tatizo kubwa sana hasa kwa vijana wetu, wamekuwa na tabia ya kuiga mambo kutoka Mataifa makubwa ikiwemo Marekani na Ulaya, hata kama mambo hayo wanayoiga hayafai kwenye jamii, hata ndani ya mataifa hayo. Sasa ningeomba kujua, Mheshimiwa Waziri husika, tatizo hili atalitatua vipi ili vijana wetu wapewe elimu ya kueleweka, waelewe kwamba hata Marekani na Ulaya kuna watu wenyе tabia nzuri na mbaya, sio unaiga tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wamekuwa hata wakiimba Kiswahili lakini wanaweka sauti ya Kiingereza au Kimarekani. Vijana wetu wamekuwa wakitumia maneno ambayo hata katika hizo jamii hayakubaliki. Lakini wamekuwa wakifanya hivyo kwa sababu tu ya kukosa uelewa. Namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii atuambie leo, ni jinsi gani atatutalia tatizo ambalo limewakumba vijana wengi sana Tanzania? Siyo makosa yao, ni kwa sababu ya kutokupewa elimu ya kutosha. Ahsante sana.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, niliongea kuhusu suala la kuanzisha mfuko wa kuimarisha michezo kwenye Halmashauri zetu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI wakati anajibu asubuhi alisema kwamba, michezo ya UMISHUMITA na UMISETA itaendeshwa kwa fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Halmashauri zote zenye uwezo wa kifedha, Halmashauri nyingine hazina fedha kabisa kupitia vyanzo vyake vyenyewe. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mifuko hii kwenye Halmashauri ili Halmashauri iweze kushirikiana na Serikali Kuu kwa lengo la

kuimarisha michezo kwenye Halmashauri zetu ili kuwasaidia vijana hawa kuibua vipaji vyao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu! Unakwenda hatua moja, baada ya nyingine.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja alioitoa Mheshimiwa Jitu Soni kuhusu uzembe unaofanywa na Vyama vya Mikoa na Wilaya hatimaye timu ya Magungu *Rangers* kutokushiriki katika ligi ambayo wao walikuwa washindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, natumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Jitu kwa namna ambavyo amefuatilia jambo hili. Alinipigia simu, tukawasiliana halafu nikamuunganisha na *TFF*, na *TFF* walitoa tamko juu ya timu siyo hii tu ya Manyara, bali hata timu ya Mkoa wa Pwani ambayo walikuwa wanatakiwa kuwasilisha majina ya timu za Mikoa tarehe 9 ili ligi ianze tarehe 13. Mpaka kufika jioni, kwa taarifa ambazo nilikuwa nimepata ni kwamba, Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Pwani ulikuwa bado haujafanya hivyo. Hata hivyo, nimwahidi tu kwamba nitashughulikia suala hili ili niweze kupata hatima ya Timu za Mkoa wa Manyara.

Suala la Mheshimiwa Iddi M. Azzan kuhusu Sera ya Michezo, kwanza, namshukuru kwa kutambua kwamba tumejitahidi mwaka huu kuja na taarifa kwamba, Sera ya Michezo sasa iko katika ngazi ya juu ya maamuzi. Nataka nimhakikishie tu kwamba, mimi kama mdau wa michezo na ye ye mwenyewe, nitahakikisha tunalishughulikia suala hili na kulisukuma kuona kwamba tunapata Sera ya Michezo ambayo italeta tafsri ya kuwa na sheria nzuri ya michezo inayoendana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mama yangu Mheshimiwa Clara, amesema kwa uchungu suala la mavazi na kwamba Mheshimiwa Waziri alishatoa maelekezo kwamba Serikali itachukua hatua. Nataka nimthibitishie siyo nadharia; tutakuwa wakali kwa wamiliki wa bendi na watu wengine ambao watakiuka maelekezo ya Serikali na

kuwatumia wasichana hawa kuwalisha nguo ambazo
haziendani na staha. (*Makofi*)

Swali la Mheshimiwa Juma Nkamia, nakubaliana naye, kwamba ni kweli kumekuwa na Kaimu Mkurugenzi wa TSN akiwepo Ali Mkumbwa na sasa hivi ni Nderumaki. Nataka nimhakikishie tu kwamba, kwa sababu uteuzi wa Mkurungezi hufanywa na Mheshimiwa Rais, tayari sisi kama Wizara tumeshakamilisha wajibu wetu na kufanya mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, wakati wowote atateuliwa Mkurugenzi wa TSN.

Suala la Mheshimiwa Jenista Mhagama kuhusu mpango wa Serikali na hasa kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la ajira na hizi fedha ambazo tumeweza kuzipata, lakini pia kutokana na Wizara mbalimbali ambapo zitachochea ajira kwa vijana; mimi nataka nimhakikishie tu kwamba, fedha hizi tutahakikisha zinawafikia walengwa, lakini pia tayari tumeshaziwekea mpango mkakati wa kuona kwamba matokeo ya fedha hizi yanaonekana. Tukija katika bajeti ya mwaka kesho kuwe na kitu cha kusema kwamba kuna maeneo, kama maeneo yalitengwa na Wakuu wa Mikoa kwa Mikoa mbalimbali; fedha hizi ziwakute vijana huko vijijini, waonekane kama ni katika kilimo au biashara ndogo ndogo, tutakuja na takwimu. Namhakikishia Mheshimiwa Jenista kwamba Mpango upo tayari na tutashirikiana na Wizara nyingine. Lengo ni kuona kwamba tunapunguza tatizo la ajira. Kwa hiyo, hilo nilitaka tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Leticia Nyerere, aliuliza kuhusu suala la vijana kuiga tamaduni za nje. Nakubaliana naye, ni wajibu wa Serikali, Wabunge na wazazi kuona kwamba vijana wetu wanalinda maadili yetu ya Kitanzania. Nataka niseme kwamba hili siyo suala la Serikali tu, sisi kama Serikali tunawaasa na tutaendelea kuelimisha vijana kuzingatia maadili na wasiige kila kitu kutoka nje ya nchi, bali wazingatia utamaduni wa Kitanzania. Nakubaliana naye kwamba tutaendelea kufanya kazi hiyo kama Serikali, lakini na sisi kama Wabunge na wazazi kuhakikisha kwamba tunakuwa Walimu wazuri wa kuelimisha watoto wetu. Kwa sababu mtoto

anaanza kukua katika ngazi ya familia kabla hajawa kijana anayeweza kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Diana Chilolo, amesema kuhusu mfuko wa michezo. Kwanza, namshukuru kwamba maelezo aliyokuwa ameyatoa Naibu Waziri wa TAMISEMI yalikuwa yanajitosheleza. Lakini nataka niseme kwamba sisi ndani ya Serikali tutaliangalia suala hili na Wizara ya TAMISEMI nao wanasielia, hivyo tutashirikiana kuona kwamba tunaendeleza michezo. Naye kama Diwani katika Halmashauri husika, basi tushirikiane kuona kwamba mifuko hii ya michezo inaweza kuanzishwa.

Suala la Mheshimiwa Ritta Kabati ambalo linafanana sana na suala la Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Ester Bulaya kuhusu fedha hizi na maeneo ambayo yametengwa, mimi nataka tu niwahakikishie kwamba, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya awali, tuhakikishe kwamba fedha hizi zinawafikia walengwa, vijana, bila kujali itikadi ya Chama. Lakini pia kwa uwiano sahihi katika Mikoa yetu na katika maeneo ya Mjini na Vijiji kwa maana ya kuwalenga vijana wajasiriamali wa kilimo na viwanda vidogo vidogo.

Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo. Kwa maana hiyo, nitakuwa nimemjibu pia mdogo wangu Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba Wizara imejipanga kuona kwamba matokeo ya fedha hizi yanakuwa chanya, ili tukija mwakani tuwe na kitu cha kuonyesha kwamba fedha hizi zimetumikaje. Nataka niwahakikishie tu kwamba Wizara imejipanga na ina mpango mzuri zaidi wa kuona kwamba fedha hizi zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Mnyika, nataka niseme tu kwamba, sisi kama Wizara siyo kazi yetu kuzuia Muswada binafsi wala kuzuia hoja binafsi ya Mheshimiwa Mnyika kuwasilisha Muswada wa Kuundwa Baraza la Vijana. Kazi yetu, nimetoa maelezo na nimesema hapa, namshukuru Mheshimiwa Mnyika kwamba yeze ni Mwasisi wa Baraza la Vijana. Katika Bunge hili tupo mimi, Mheshimiwa Nchimbi, yeze na Mheshimiwa Lusinde, tulikuwa

wanaharakati wa kuona kwamba kunaundwa Baraza la Vijana. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba sisi kama Serikali na mimi kama mdau tutahakikisha sheria hii inafikishwa Bungeni ili tuunde Baraza la Vijana. Lakini suala la kukataliwa kwa hoja binafsi halihusiani sana na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo yetu.

MWENYEKITI: Bado wengine, Mheshimiwa Majaliwa kwa hoja ya Diana Chilolo, Mheshimiwa Naibu Waziri, hasikii!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, naomba nitoe ufanuzi zaidi juu ya swali loulizwa na Mheshimiwa Diana Chilolo linazongumzia bajeti katika Halmashauri.

Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Halmashauri zetu zote nchini zina fungu la shughuli za michezo na burudani ndani ya Halmashauri zenyewe, ambazo wanazitenga kila mwaka wa fedha kwa shughuli hiyo. Shule za Msingi na Sekondari zote ziko kwenye Halmashauri hizo hizo. Nasi kwa sababu tunatambua hilo, tumewaelekeza sasa fungu hilo lisaidie uendeshaji wa shule katika ngazi za Kata na Wilaya ili kuandaa timu zetu za Shule za Msingi na Sekondari.

Hata hivyo, Halmashauri nazo hushiriki mashindano ya Shirikisho la TAMISEMI, linaitwa SHIMISEMITA. Kupitia fungu hilo wanafanya maandalizi, lakini wanapofika kwenye ngazi ya Wizara, ngazi za shule zote na Halmashauri zenyewe, Wizara ndiyo inagharamia huko katika ngazi ya juu. Kwa hiyo, hatuna mashaka tunaposema kwamba Halmashauri zinapanga bajeti. Tunachosema sasa, watunishe bajeti hizo ili ziweze kuendesha shughuli za michezo nchini kuunga mkono jitihada za ufufuaji wa michezo na kuendeleza michezo nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa John Mnyika, maana sasa unatoa Shilingi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kuondoa Shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Ondoa Shilingi tu, ndiyo hoja yenyewe!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sijaridhika na ufanuzi uliotolewa, nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, mimi ni kati ya watu ambao kwa miaka mingi sana toka miaka ya 1990 tulikuwa kwenye harakati za kutaka Baraza la Vijana lianzishwe, ambalo lilikuwa ni ahadi ya nchi kwenye Sera ya Maendeleo ya Vijana. Sasa ni miaka 17 Baraza hilo halijaanzishwa. Ninachokisema, na hapa Serikali siyo Wizara ya Vijana peke yake, Serikali yote iko hapa, na Kambi Rasmi ya Upinzani iliihoji Serikali kwenye ukurasa wa 30 wa hotuba ya Kambi. Kambi Rasmi ya Upinzani ilitaka ufanuzi kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yeye ndiye ambaye kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, inaeleza kwamba Mheshimiwa Freeman Mbowe, alipoulima kwenye hotuba ya upinzani kwa Waziri Mkuu, kwa nini Miswada ya Wabunge hajji Bungeni? Ofisi ya Waziri Mkuu ikajibu kwenye ukurasa wa 28, imenukuliwa Ofisi ya Waziri Mkuu ikijibu kwenye majibu yake kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu imepeleka Muswada huu kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutoa ushauri.

Sasa kwa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inazo, ambazo ziko kwenye ukurasa wa 29, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetoea ushauri kwamba, Muswada huu hauwezi kuletwaha hapa Bungeni, kwa sababu eti unakwenda kinyume na masharti ya Ibara ya 99 ya Katiba ya nchi. Sasa masharti hayo ya Ibara ya 99 ya Katiba ya nchi, yanachokisema ni kwamba, Muswada; na yanazungumzia zaidi masharti yanayohusiana na Miswada ya utungaji wa sheria za fedha na mgawanyo wa fedha, kwamba Bunge halitaruhusiwa kupitia Muswada kama hautaletwa Bungeni na Mheshimiwa Rais kupitia Mheshimiwa Waziri, kama

Muswada huo unalenga kuagiza kuwa malipo ya matumizi yafanyike kwenye Mfuko wa Serikali au mfuko mwingine na kadhalika. Inaendelea hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye Muswada binafsi ambao Mwanasheria Mkuu wa Serikali anao na Serikali inao, kwa sababu iliombwa ushauri, kifungu hiki hakikutumika. Muswada umetumia kifungu cha 135 (2) cha Katiba ya nchi, kinachoruhusu Bunge kutunga sheria ya kutengeneza mifuko mingine. *In this case*, Bunge litunge sheria ya kutengeneza Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sasa hivi tunatenga fedha Shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao kimsingi haupo kisheria na haupo kitaasisi. Tumekuwa na tatizo toka mwaka 1993, fedha za maendeleo ya vijana zilikuwa zinatengwa kwenye Halmashauri, sehemu kubwa zinaliwa na wajanja. Hata hizi fedha ambazo zilikuwa kwenye Wizara, mwaka 2012 Wizara hii ilitengewa Shilingi milioni 100 kwa ajili ya kinachoitwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, lakini hizo Shilingi milioni 100 hazijafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ninayoitoa...

SPIKA: Enhee, nilitaka nipate hoja kusudi tuwe pamoja na wewe.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema hapa ni kwamba, ili vijana waweze kupata fursa ya kuunganishwa bila kujali vyama, bila kujali itikadi, na waweze kupata fursa wenye, kusimamia huu mfuko wa maendeleo ya vijana. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atoe kauli ya kubatilisha ushauri ambao ulitolewa na *junior officers* wa ofisi yake, ili ule Muswada binafsi wa sheria uweze kuwasilishwa Bungeni, ujadiliwe upitishwe na pande zote tupate mfumo wa kuliunda Baraza la Vijana ambalo vilevile ndilo litasimamia mfuko wa maendeelo ya vijana. Hiiyo ndiyo hoja ambayo naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waiunge mkono ijadiliwe ili Bunge litimize wajibu wake kwa jambo ambalo miaka 17 halijafanya.

SPIKA: Kwa hiyo hoja, inasemaje?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inasema kwamba, Muswada binafsi wa Sheria wa kuunda Baraza la Vijana, uruhusiwe uendelee na zile taratibu zake nyingine ili uje Bungeni, kwa sababu Muswada huu umeshatangulia na umeshaingia kwenye *system* ya kibunge.

SPIKA: Mheshimiwa, mimi nimeshindwa kusema kwa sababu niliuona Ofisini kwangu, ulikuwa sawa, sasa sijaelewa kingine. Mwanasheria hebu tufafanulie, *what is happening?* Maana yake nakuwa *accused* hapa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa ambao Mheshimiwa Mnyika anazungumza, nafikiri amekuwa *technical*, nafikiri na sisi tuwe *technical*. Anasema Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa, wewe hizi taarifa umezipata wapi? Kwa sababu, na Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba ataleta Muswada kwa ajili ya kuunda Baraza la Vijana, na *sources of fund* kwenye Baraza hilo zitakuwa ni za hakika zaidi kuliko zile ambazo umeona kwamba ulikuwa umeweka kwenye Muswada wako. Hilo ndilo jibu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa tu, nimeandikiwa barua rasmi na Ofisi ya Bunge kwamba Ofisi ya Bunge imepokea ushauri kutoka kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Bunge lina mkondo wake, Serikali ina mkondo wake. Serikali bado hajalaeta Muswada, kwa sababu Muswada upo, kwa nini usiletwe Serikali ikaufanyia hayo marekebisho sasa kama inataka *source* nyingine na kadhalika? Lakini ulivyo ule Muswada unaweza bado kutimiza malengo. Sasa kwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inaonyesha ye ye hajaandika hiyo barua, basi taratibu nyingine ziruhusiwe, kama ilikuwa ni *junior officers* wametoa ushauri tofauti, taratibu nyingine ziendelee, Muswada huo uendeleee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, ili tuweze kuwahi, tunapitisha Shilingi billioni 6.1 za Mfuko wa Maendeleo ya vijana, hatuna chombo cha vijana cha kufuatilia jambo hili. Ili tuweze kuwahi jambo hili, huu Muswada uendelee na taratibu zake ili mfumo huu uweze kutengenezwa, na Serikali kama ina *amendments*, iletu tuweze kutengeneza Baraza la Vijana.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mnyika kwamba sisi vijana wote tunaona umuhimu wa kuwepo kwa Baraza la Vijana, bila kujali itikadi za Vyama vyetu. Lakini naona sasa tunataka kurudi nyuma, tunataka kukurupuka, wakati tayari Serikali imeshaji-*commit* kwamba inaandaa walete Muswada, Wabunge wote tushiriki kwa ajili ya kuhakikisha tunapata chombo bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hatuwezi kufanya maamuzi ya haraka haraka kwa zaidi ya vijana asilimia 60 ambaao wapo wanatuangalia. Sawa tumeimba miaka 17, nami nakupongeza wewe kwa kuwa Mwasisi, lakini leo hii haitoshi, kwa dakika hizi, kuanza kujadili chombo cha msingi kama hicho wakati tayari Serikali imeshasikia kilio cha Vijana; tayari Serikali imeshaona umuhimu na sisi Wabunge wote vijana wa pande zote mbili tunaona umuhimu wa kuwepo kwa hili Baraza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja ya Serikali kwamba, wafanye huo mchakato haraka, waweze kuleta, tuweze kushughulikia kwa mapana yake. Siku hii moja haitoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. (*Makofii*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika anaongea vitu viwili tofauti. Cha kwanza anachosema, ni kuwa na Baraza la Vijana, kwamba Sheria ije Bungeni. Hakuna anayepinga hilo jambo hata mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa kuna suala la Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Kama ulivyo mfuko wa akina mama, na sisi wenyewe Bunge hili tunasisitiza *D by D*, kwamba tupeleke maendeleo kule kwenye Halmashauri zetu. Ni jukumu letu sisi Wabunge kuhakikisha fedha hizo kwenye Halmashauri zetu, vijana wengi wanazipata fedha hizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemheshimu sana Mheshimiwa Mnyika kama angesema fedha hizo ni kidogo. Mimi ningependa mfuko huu uongezeke ili kwenye Halmashauri zetu tupeleke fedha nyingi sana kwa ajili ya kuwasaidia vijana na akina mama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuleta Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuanzisha Baraza la Vijana, Muswada huu uendeleee. Halwezekani kwamba barua aliyopewa yeye, ndio Bunge hili lifanyie kazi, barua aliyopewa yeye ambayo mimi sijaiona, Mbunge mwengine hajaiona. Mimi ninachoomba Serikali, naunga mkono hoja ya Serikali, kuongeza fedha kwa ajili ya maendeleo ya vijana. Lakini pia naionba Serikali ilete Muswada ili tuunde Baraza la Vijana. (*Makof!*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hapa watu tuna tabia labda ya kusahau mambo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, tulilizungumza hili. Tulisema tunaitaka Serikali ilete Muswada. Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri, mwaka 2012 ikaahidi kuleta kwenye Bunge linalofuatia ambalo ndilo la leo, yaani Bunge hili la Bajeti ya sasa. Sasa leo majibu ya mwaka 2012 yanajirudia tena kwamba tutaleta, tutaleta, tutaleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri ikaeleweka wazi kwamba miaka 17 inatosha, na inawezekana kabisa kwa sababu kila mmoja anaelewa, hoja ya Muswada ipo, inawezekana kuleta ndani ya Bunge hili kabla Bunge hatujaahirisha, inawezekana. Lengo na nia ni nini? Ni kwa

sababu fedha tunazopitisha zimekuwa zikitoka kwa miaka yote na vijana wamekuwa wakilalamika haziwafikii walengwa kama inavyokuwa inatajwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi fedha nyingi zinaishia tu kutumika vibaya, na ndiyo maana sasa tunataka Baraza lenyewe litakalouniganisha vijana wote kitaifa na litakalosimamia mfuko huu kwa ajili ya maendelo yao. Kwa hiyo, hoja yetu iko pale pale, Serikali ituhakikishie kwamba inaweza kuleta hoja na kabla ya Bunge kwisha kwa sababu hoja ipo, tutairekebisha ndani ya Bunge kwa sababu sisi ndiyo tunaotunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Naibu Waziri, naomba Waziri Mkuu abakie asikillize hili swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu aachwe tumalize hili swali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachozungumzwa hapa wala hakina *controversy* ya kusababisha Bunge lako likapoteza muda mwingu kwa hoja ambazo tayari majibu yake yalikwishatolewa. Nilipokuwa nasikiliza pande zote, na hasa majibu ya Naibu Waziri, na hoja anayoitoa Mheshimiwa Mnyika ni kama kimsingi wamekubaliana. Yule anasema liundwe Baraza, huyu anasema ndiyo tutaunda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka hapo, unahamia sasa kwenye hoja ya Mheshimiwa Mnyika. Anasema, Mfuko wa Vijana, hawa wanasesma likiundwa Baraza na Mfuko ndiyo utapata sura nzuri zaidi, maana yake litakuwa na vyanzo vya mapato na namna ya kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wasemaji wengine wanasesma, jambo hili hatuwezi kulisema kwa sasa hivi tukalimaliza. Hata kama ye ye Mheshimiwa Mnyika anazo hizo taarifa, lakini sisi wengine hapa hatuna. Mimi nadhani jambo

hili ni kama limekwisha, labda kama kuna zaidi ya hapo, tuseme ndiyo na hapana tumalize. (*Makofî*)

MBUNGE FULANI: Eeeh!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni la Bajeti, sasa kama kuna Muswada ulikuwa uletwe, pengine utaletwa kwa wakati mwingine wa Bunge kwa ajili ya shughuli hizo, lakini siyo Bunge hili la Bajeti. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nirudie tu kwamba, sisi kama Serikali, kuchelewa kwa Muswada huu, kwanza imetupa nafasi ya kuweza kupata maoni mengi zaidi na kuwashirikisha vijana kwa wingi zaidi na kwamba tunakusudia kuleta kitu ambacho kwa kweli kimekamilika. Nataka niseme tu kwamba, nia ya Serikali ni kuona kwamba jambo hili tunalifanya kwa haraka, lakini pia izingatiwe kwamba ratiba za Bunge letu imebadilika. Kwa hiyo, hili ni Bunge la Bajeti, lakini pia kuna mihimili mitatu; Mahakama, Bunge na Serikali. Sasa ndani ya Serikali, taratibu zake ni mpaka lipite Baraza la Mawaziri.

Kwa hiyo, watupe nafasi, Serikali ikamilishe kazi zake, hatimaye tutaleta Bungeni Muswada huu. Ni kwa lengo lile lile ambalo Mheshimiwa Mnyika analisema, ambalo nimesema kabisa na yeye alikuwa ni Mwasisi na tulikuwa wote na awe na hakika tu kwamba, upele umepata mkunaji. Kama na mimi nilikuwa Mwasisi, tutalifanya haraka zaidi hili jambo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja kwa ufupisana. Mheshimiwa Ester Bulaya, haikuwa dhamira yangu kwamba Baraza liundwe leo kwa siku moja. Muswada wa Sheria una taratibu zake, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 80 mpaka 93, na Muswada binafsi nilioupeleka, nimeupeleka siyo kwa hati ya dharura.

Tungeweza kuleta ule Muswada kwa hati ya dharura ya saini za Wabunge 10, na ungekuja Bungeni moja kwa moja.

Tumesema, Muswada uchapwe kwenye gazeti la Serikali. Ukichapwa, maana yake sasa unakuwa wazi, hauwezi kujadiliwa Mkutano huu wa Bunge, utajadiliwa kwenye Mkutano ujao wa Bunge, na kutakuwa na fursa ya kukusanya maoni, watu kuujadili kuona kipengele kwa kipengele.

Sasa suala la msingi la kujiuliza, hivi ni kwa nini Serikali inaona uzito sana, Muswada ambao uko tayari kuuruhusu uchapwe kwenye gazeti kwa mara ya kwanza ili ujadiliwe kwenye Bunge lijalo na hapo katikati kuna muda wa kazi, muda wa marekebisho na kila kitu? Hilo ndilo jambo la kujiuliza.

Sasa kwa ufupi sana, Mheshimiwa Serukamba, huu Muswada una kifungu kinachohusu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, na ndiyo msingi wa ubishani. Muswada huu utasaidia ufanisi kwenye uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana siyo Wizarani tu, bali ni mpaka kwenye ngazi ya Halmashauri. Muswada umeweeka kipengele kwa kipengele, hatua kwa hatua. Sasa kinachokosekana hapa ni dhamira ya kuruhusu tu Muswada kwanza uchapwe tu kwenye gazeti la Serikali, usomwe kwa mara ya kwanza, ili uanze kuangaliwa na kutafakariwa. Ni jambo ambalo linaweza kufanyika kabisa na ikasaidia nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Silinde nimwongezee tu kidogo. Ahadi ya Serikali ukiondoa ya mwaka 2012, aliyekuwa Waziri wa Vijana - Mheshimiwa Nchimbi, ambaye naye tulikuwa naye kwenye hizi harakati za vijana miaka ya 1990, alikuwa Waziri mwaka 2011 akaahidi kwamba mwaka huu upele umepata mkunaji, hivyo hivyo kama Mheshimiwa Makalla. Baraza litajengwa, Baraza litaundwa na halikuundwa. Kwa sababu hiyo ya kutolewa kauli ambazo hazijatekelezwa, mimi ndiyo maana nikaamua kuleta Muswada binafsi. Sasa siwezi kuamini moja kwa moja hiyo kauli, *unless Serikali iji-commit* na *time frame* ya kwamba Muswada huu unakuja lini? Lakini

kama ni kauli tu, haiwezekani kwa sababu kauli zimeshatolewa kwa miaka 17 bila utekelezaji. (*Makofi*)

Kwa ufupi sana, Mheshimiwa Simbachawene, hili ni Bunge la Bajeti, lakini Bunge hili la Bajeti lina siku tano ambazo hakuna shughuli za Serikali za Bajeti. Kuna shughuli za Wabunge, kwa hiyo, tukitaka ule Muswada usomwe, unaweza kabisa kusomwa katika zile siku ambazo siyo za Bajeti. Hata kusingekuwa na hizo siku, Muswada haujadiliwi Bunge hili, unajadiliwa Bunge ijalo. Sasa unasomwa mara ya kwanza peke yake. Jambo hili linawezekana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize na Mheshimwa Makalla. Nakubaliana na wewe kabisa katika maelezo yako. Dhamira yangu ni kuona Baraza linaundwa na ni dhamira ya Waheshimiwa Wabunge wengi sana ambao wamekuwepo wakitaka Baraza hili liundwe. Sasa ili hii dhamira ionekane kwa vitendo, mkubali tu Serikali Muswada huu uchapwe kwenye Gazeti la Serikali. Kunaweza kufanyika *negotiation*. Kama mnataka ninyi Serikali ndiyo muulete, kwanza Bunge litimiza masharti yake ya kikanuni, kwa sababu ni suala la Kanuni za Bunge kwa Muswada kuchapwa kwenye gazeti la Serikali. Sasa hata hilo tu! Hata hilo tu! Mimi hilo ndilo ninaloliomba. Muswada uchapwe kwenye Gazeti la Serikali, taratibu nyinezi ziendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa naomba tufanye uamuzi wa hoja hii.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kukataliwa*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - *Finance And Accounts*.....Tshs. 276,746,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*.....Tshs. 461,426,000/=
Kif. 1004 - *Government Comm. Unit*.....Tshs. 113, 350,000/=
Kif. 1005 - *Procurement Mgt Unit*.....Tshs. 184, 742,000/=

Kif. 1006 - *Internal Audit Unit*.....Tshs.183, 088,000/=
Kif. 1007 - *Inform. & Comm. Techn. Unit*....Tshs. 90, 086,000/=
Kif. 1008 - *Legal Services Unit*Tshs. 81,334,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 6001- *Culture Development Division*..Tshs. 2,626,666,000/=

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 270800 - Ruzuku kwa Taasisi. Mwaka wa fedha uliopita tulitenga Shilingi bilioni 1.2, mwaka huu zimeshuka mpaka Shilingi bilioni 1.1, hapa ndipo zilipo Taasisi muhimu kama Baraza la Sanaa la Taifa na Baraza la Kiswahili la Taifa. Taasisi ambazo ukikutana nazo malalamiko yao makubwa ili kuweza kufanya kazi ya kulinda masuala ya Wasanii na kuendeleza Kiswahili ni kwamba, wanapewa tu fedha za mishahara, fedha za mafungu mengine hata ya kawaida tu ya kiutendaji *OC*, hawapewi.

Sasa ningependa kupata ufanuzi toka kwa Serikali, ni kwa nini kiwango cha fedha kimeshuka kutoka Shilingi bilioni 1.2 mpaka Shilingi bilioni 1.1 pamoja na umuhimu wa hivi vyombo kwenye malengo yake?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwa umuhimu wa hayo maelezo aliyotoa kwa ajili ya Taasisi hizi. Lakini kifungu hiki kimepungua kutokana tu na ufinyu wa Bajeti.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 6002 - *Youth Development Division*... Tshs. 7,130,887,000/=

MWENYEKITI: Ataanza Mheshimiwa Leticia, atafuatia Mheshimiwa Zitto halafu Mheshimiwa Mnyika.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6002 – *Youth Development Division*, Kasma 22100 – *Travel Out of Country*. Swali langu hapa, ningependa tu kufahamu kwamba, hii Kasma ita-include *educational exchange programme* wanaposafiri?

MWENYEKITI: Ah, hiyo *Development*, Soma pale juu, *Youth Development Division*.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante Kifungu 6002 – *Youth Development Division*, halafu kwenye Kasma 221000 – *Travell Out of Country*. Ninaelewa kwamba *Youth* ndiyo watakaohusika kwenye hiki Kifungu. Nililitaka kujua kwamba *does it include educational exchange programme* wanaposafiri?

MWENYEKITI: Sawa. Maelezo!

NAIBU WAIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hiki hakihusiani na mambo ya *training*, bali ni kwa ajili ya *ticket* za ndege. Lakini wakienda huko pia watajifunza mambo mengi kwa ajili ya Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Soni.

MHE. JITU VRAJLAL SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika sub vote 6002, kasma ya 271200, mwaka 2012/2013 ilipitishwa Shilingi milioni 100 na mwaka huu kuna Sh. 3,100,000,000/=. Nilikuwa ninaomba ufanuzi hapo.

MWENYEKITI: Nimeiona. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndiyo fedha za Mfuko wa Vijana kutoka Sh.100,000,000/= kwenda

Sh. 3,100,000,000/= na sasa itakuwa ni Sh. 6,000,000,000/=. Kwa hiyo, ni kwa ajili ya Mfuko wa Vijana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka ufanuzi tu. Ni kwamba Sh.100,000,000/= hazikutolewa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Nini *commitment* ya Serikali kwamba Sh. 6,100,000,000/= zitatalewa kama Sh.100,000,000/= peke yake hazikutolewa?

MWENYEKITI: Ah, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu *concern* ya huyu Mheshimiwa Mnyika kwamba, kwa msisitizo tuliuweka safari hii, nina hakika pesa hili itapatikana bila kusita.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kiliptishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)

Kif. 6004 – *Sports Development*..... Sh. 2,504,039,000/=

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika Kifungu 6004, kipengele cha 270800; nilitaka kujuahapa pesa zimeongezeka *almost* kwa asilimia 100, kutoka kwenye Sh. 863,000,000/= kwenda kwenye Shilingi billioni 1.56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujuahizi *None Financial Public Unit* ni zipi, ambazo zimeainishwa hapa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, nimekuona.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizozinahusu ongezeko la Baraza la Michezo kwa ajili ya kuwalipa Makocha wa Kigeni. Tumepata kocha mwingine zaidi wa *Basket Ball*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musa Haji Kombo.

MHE. MUSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki 6004 – *Sport Development*. Tukiangalia Item 221200 – *Communication Information*, ambayo ni michezo hakuna pesa hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa michezo hii ambayo itakuwa haina matangazo, mawasiliano, kweli kutakuwa kuna maendeleo? Je, kuna maelezo gani Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri angerudia.

MWENYEKITI: Hata na mimi pia sijasikia vizuri, uongo mbaya. Naomba urudie tu. Rudia hatujasikia vizuri. Anza tu.

MHE. MUSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki...

MWENYEKITI: Anza toka mwanzo. Kifungu gani?

MHE. MUSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kifungu, *Sub Vote 12200 – Communication and Information*, hakikutengewa...

MWENYEKITI: Ni Kifungu gani, wenzio tunahangaika? Lazima tukione ili tukujibu. Ishirini na ngapi?

MHE. MUSA HAJI KOMBO: Kifungu cha 221200.

MWENYEKITI: 221200, umekiona Mheshimiwa Waziri? Majibu!

NAIBU WAZIRI HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki, hapa kinaonekana hakijatengewa fedha, lakini kiko katika Utawala.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 7003 – *Information Services* Sh.6,804,217,000/=

MWENYEKITI: Samahani sana, nilimwita Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Kama tumekipita, bahati mbaya.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Bado hutujakipita Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Haya.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Kifungu hicho, hicho cha 270800, kwenye eneo hilli kimepangiwa...

MWENYEKITI: Soma vizuri, ni kifungu gani? Tuko katika...

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Ni katika *Sub-Vote* 7003, kifungu kidogo cha 270800. Hapa kimetengewa Shilingi bilioni 6.2. Pesa hizi zimetengwa katika matumizi yapi?

MWENYEKITI: Ehe, Mheshimiwa Waziri, maelezo.

NAIBU WAZIRI HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya *TBC*, ni mishahara ya wafanyakazi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MATUMIZI YA MAENDELEO

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Vijana,
Utamaduni na Michezo**

Kif. 6001 – *Culture Development Div.*..... Sh. 600,000,000/=

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Suzan Lyimo halafu Mheshimiwa Mnyika.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, *Sub-Vote 6001, 6246 – Construction of Open-BAKITA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, tuna tatizo kubwa sana la lugha yetu ya Kiswahili kuieneza nchi za nje. Hili limeongelewa kwa muda mrefu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilitaka Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri atuambie, hili jengo linategemewa kukamilika lini? Kwa sababu naamini kabisa jengo hili litakapokamilika tutapata *translators* wazuri ili waweze kutusaidia katika kutafsiri wakati Watanzania wanapokuwa nje ya nchi hasa kwenye Mikutano?

NAIBU WAZIRI HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakipitisha bajeti hii, litakamilika hilo jengo la BAKITA.

MWENYEKITI: Sasa hapa hakuna pesa. Sawa iko katika *Addendum*. Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka uhakika tu, kwa sababu mwaka 2012/2013 tulitenga Sh.300,000,000/= zikatolewa Sh.150,000,000/=. Sasa sijui kwa vipi niamini zitatolewa?

MWENYEKITI: Kama ni Kifungu hicho hicho, hakuna kujibu hapa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kiliptishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 7003 - *Information Services* Sh.6,000,000,000/=

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila marekebisho yake)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Tunaendelea, tumeshasema Ndiyo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vifungu vimerukwa, 6002, na 6004.

MWENYEKITI: Tumeshapitisha hicho.

(Bunge ilirudia)

TAARIFA

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi baada ya kujadili Taarifa ya Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014, kifungu kwa kifungu, pamoja na marekebisho yaliyoletwa na Waziri wa Fedha, hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari,
Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka
2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa mjadala mliokuwa nao. Lakini kama ilivyo ada, tunategemea kabisa maoni ya Waheshimiwa Wabunge yaliyotolewa katika siku hizi mbili yanafanyiwa kazi kipindi kingine. Kwa sababu kama msipofanya hivyo, itakuwa hali ngumu sana kipindi kijacho kuliko ilivyo leo. Kwa hiyo, ni vizuri mkayafanya kazi vizuri. Lakini tunawapongeza wewe na

Naibu wako na Wataalam wenu wote kwa kazi nzuri, na wote tuendelee kulijenga Taifa letu kwa sababu linatuhitaji sisi.

Waheshimiwa Wabunge, lakini ni kweli kabisa, lazima tudumishe amani. Mimi ninaona watu wanachezea amani kwenye kikaango cha mafuta. Jamani, hatapona Mwandishi wa Habari, hatapona Mbunge wala mwингine ye yole. Kama ni uhuru sawa sawa wa Waandishi wa Habari, kama amani haipo, utakuwa haupo kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni kabisa, kila mmoja kwa dhati kwa dhamira yake, tujenge nchi moja na tufanye vituko vyetu, lakini tukijua tunataka amani ya nchi ibakie. Hili ninawaombeni sana. (*Makofii*)

Tangazo lingine dogo, kuna tangazo la Mheshimiwa Idd Azan, kuhusu mchezo wa *Basket Ball* unataka kuanzishwa. Kwa hiyo, wanaotaka waende kwake mwenyewe wajiaandikishe kusudi muweze kushiriki.

Nadhani kuna mafunzo yanafanyika hapo *CBE* kila siku kuanzia asubuhi saa 12.00 mpaka saa 1.30 asubuhi. Kwa hiyo, itakuwa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia naomba niwakumbushe, tukiwa kwenye Kamati ya Matumizi, Mheshimiwa Mbunge ukiniandikia barua ya ukurasa mzima, kweli sitaisoma. Nanaiweka kwenye faili, nitaisoma ofisini. wakati wa Kamati ya Matumizi unasoma barua *page nzima!* Haiwezekani! Yaani haiwezekani. Kuna barua za namna hiyo nimeziweka kwenye faili nitakwenda kuzisoma ofisini.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo hivyo wakati wa kipindi cha Maswali. Katika kipindi cha Maswali, unaweza kumwandikia Spika, mimi nataka niulize swali fulani nambari fulani. Mistari mitatu tu, nilione kabisa jina lako unayetaka kusema na jina la yule aliyetaka kuuliza swali. Hii inakuwa rahisi. Lakini unaanza kusoma ukurasa mzima, utaharibu kabisa fikra za humu ndani, utakuta Spika anaanza kuzungumza habari nyingine wakati mwингine siyo zenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sana tushirikiane. Mwelewe kukaa hapa ni pamoja na kufikiri, akili zote ni lazima ziwe kichwani mwako. Siyo unakaa tena hapa unapewa barua ndefu kabisa, Salaam Mheshimiwa Spika, haiwezikani! Pelekeni ofisini.

La tatu, naomba fikirieni, tunafanya maamuzi, kipindi peke yake *quorum* inatakiwa iwepo asilimia 100 kwa mia 100 tufanye maamuzi. Siyo vizuri Waheshimiwa Wabunge kwenda kuzungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Siyo vizuri kabisa kabisa, yaani inaonekana kabisa sura yake haipendezi, kwa sababu Waziri Mkuu hajali haya tunayofanya sisi. Hajali! Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge msaidieni. Yeye ni mtu mmoja *polite* sana, anashindwa kukwambia ondoka. Ningelikuwa mimi, ningekwambia ondoka hapa! Kwa hiyo, namsemea sasa. Nitawaondoa mimi, kwa sababu nisingependaji jambo hilli. (*Kicheko/Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa mjadala mlioufanya katika siku hizi mbili, naomba niwatakie jioni njema. Ninaahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.15 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 22 Mei, 2013 Saa Tatoo Asubuhi)